# TATHMINI YA MCHANGO WA SWAHILIHUB KATIKA UKUZAJI KISWAHILI NCHINI KENYA

**OWINO ANTHONEY OLOO**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA MINAJILI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMIVU KATIKA ELIMU YA KISWAHILI**

**CHUO KIKUU CHA SAYANSI NA TEKNOLOJIA CHA MASINDE MULIRO**

**APRILI, 2024**

## IKIRARI

Tasnifu hii ni yangu na haijawahi kuwasilishwa popote na yeyote kwa minajili ya shahada yoyote au jambo lingine lolote lile na hairuhusiwi kutoleshwa kwa njia yo yote tasnifu nzima au sehemu yake bila kibali changu au cha Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro.

**Sahihi………………………………    Tarehe……………………………**

**Owino Anthoney Oloo.**

EDK/H/03/13

**Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro**

**Kakamega, Kenya.**

Tasnifu hii imeidhinishwa kwa kibali chetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro.

**Sahihi………………………………    Tarehe……………………………**

**Prof. Kenneth I. Simala.**

**Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro S.L.P. 190-50100**

**Kakamega, Kenya.**

**Sahihi………………………………    Tarehe……………………………**

**Prof. John Habwe.**

**Chuo Kikuu cha Nairobi S.L.P. 30197-00100**

**Nairobi, Kenya.**

## HATILINZI

Tasnifu hii ni hakimiliki kwa mujibu wa mkataba wa Berne, kifungu cha sheria cha hakimiliki cha mwaka wa 2001, kulingana na sheria za hati za kimataifa na kitaifa. Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kuhifadhi kwa mfumo wowote ule au kutoa hata sehemu ndogo ya tasnifu hii kwa njia yoyote ile bila idhini ya mwandishi na/au Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro.

## YALIYOMO

IKIRARI.......... ii
HATILINZI.......... iii
YALIYOMO.......... iv
TABARUKU.......... ix
SHUKURANI.......... x
IKISIRI.......... xi
ABSTRACT.......... xii
ORODHA YA MAJEDWALI.......... xiii
ORODHA YA CHATI.......... xiv
ORODHA YA PICHA.......... xv
ORODHA YA MICHORO.......... xvii
VIFUPISHO NA AKRONIMU.......... xviii
DHANA ZILIZOTUMIKA.......... xix

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI.......... 1**
1.1 Usuli wa Utafiti.......... 1
1.2 Suala la Utafiti.......... 6
1.3 Madhumuni ya Utafiti.......... 7
1.4 Maswali ya Utafiti.......... 7
1.5 Misingi ya Uteuzi wa Mada ya Utafiti.......... 7
1.6 Umuhimu wa Utafiti.......... 8
1.7 Tahadhania ya Utafiti.......... 10
1.8 Nadharia ya Utafiti.......... 10
1.8.1 Mihimili ya nadharia ya Uvumbuzi wa Mawasiliano.......... 12

1.8.2 Nadharia katika Utafiti na Ukuzaji wa Kiswahili........................................23
1.9 Upeo na Mipaka ya Utafiti..................................................................................28
1.10 Hitimisho..............................................................................................................29

**SURA YA PILI: UHAKIKI WA MAANDISHI..........................................................30**
2.1 Utangulizi...............................................................................................................30
2.2 Malengo ya Tovuti ya Swahilihub....................................................................30
2.3 TEHAMA katika Ukuzaji Lugha.......................................................................34
2.4 Ukuzaji wa Kiswahili kwenye Tovuti Swahilihub...........................................45
2.5 Maendeleo ya Tovuti ya Swahilihub katika Ukuzaji Kiswahili.......................54
2.6 Umuhimu wa Swahilihub na Mafanikio yake katika Ukuzaji Kiswahili..........59
2.7 Hitimisho..............................................................................................................66

**SURA YA TATU: MUUNDO WA UTAFITI...............................................................68**
3.1 Utangulizi...............................................................................................................68
3.2 Mwelekeo Mseto wa Utafiti.................................................................................68
3.3 Eneo la utafiti......................................................................................................... 78
3.4 Sampuli ya Utafiti..................................................................................................78
3.5 Njia za Utafiti........................................................................................................85
3.5.1 Mahojiano..........................................................................................................85
3.5.2 Hojaji..................................................................................................................86
3.5.3 Uchunzaji Mtandaoni.........................................................................................87
3.5.4 Mijadala ya Makundi.........................................................................................88

3.6 Mbinu za Utafiti....89
3.6.1 Usaili....89
3.6.2 Hojaji....90
3.6.3 Uchunzaji Shiriki....91
3.6.4 Mijadala ya Kimakundi....92
3.7 Vifaa vya Utafiti....93
3.7.1 Dodoso....93
3.7.2 Hojaji za Ukuzaji wa Kiswahili kwenye Tovuti ya Swahilihub....93
3.7.3 Mwongozo wa Uchunzaji kwa Msaada wa ARhefs....95
3.7.4 Picha na Video....96
3.7.5 Mwongozo wa Mijadala ya Makundi....97
3.8 Utegemezi na Uaminifu wa Vifaa vya Utafiti....97
3.9 Utaratibu wa Uchunguzi, Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data....101
3.10 Maadili katika Utafiti....103
3.11 Hitimisho....103

**SURA YA NNE: MCHANGO WA SWAHILIHUB KATIKA UKUZAJI WA KISWAHILI....105**

4.1 Utangulizi....105
4.2 Mfumo wa Swahilihub na Ukuzaji wa Kiswahili Nchini Kenya....106
4.3 Swahilihub na Ukuzaji wa Kiswahili Nchini Kenya....208
4.4 Tathmini ya Swahilihub katika Ukuzaji wa Kiswahili Nchini Kenya....215
4.4.1 Kitambulisho Mahususi cha Tovuti ya Swahilihub....217

4.4.2 Ushindani wa Tovuti ya Swahilihub Mtandaoni........................................220

4.4.3 Nafasi ya Swahilihub katika uchunguzi wa pili miezi mitatu baadaye.......227

4.4.4 Uhariri wa matini ya Tovuti ya Swahilihub...............................................235

4.5 Changamoto za Matumizi ya Swahilihub katika Ukuzaji wa Kiswahili........252

4.5.1 Gharama na miundombinu.........................................................................254

4.5.2 Matumizi ya istilahi....................................................................................256

4.5.3 Uchache wa wataalamu..............................................................................257

4.5.4 Ukosefu wa Lugha-Ishara na tafsiri...........................................................258

4.5.5. Uchangamano wa Kimuundo wa Swahilihub..................................................258

4.5.6. Tovuti nyingine na Lugha ya mawasiliano......................................................260

4.6 Mustakabali wa Swahilihub katika Ukuzaji wa Kiswahili............................261

4.7 Mustakabali wa Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili..............................264

4.7.1 Matumizi duni ya matini ya tovuti ya Swahilihub.....................................265

4.7.2 Mkabala wa tathmini ya tovuti za ukuzaji wa lugha..................................266

4.7.3 Hitimisho....................................................................................................273

**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO................275**

5.1 Muhtasari...........................................................................................275

5.2 Hitimisho...........................................................................................279

5.3 Mapendekezo.....................................................................................288

MAREJELEO....................................................................................................291

VIAMBATISHO..............................................................................................311

A. Kiambatisho I: Mwongozo wa Dodoso.....................................................................311

B. Kiambatisho II: Hojaji kwa wahadhiri wa Taaluma ya Kiswahili.............................312

C. Kiambatisho III: Hojaji kwa wanafunzi wa Taaluma ya Kiswahili...........................315

D. Kiambatisho IV: Hojaji kwa watumiaji wengine Swahilihub...................................317

E. Kiambatisho V: Dodoso kwa mahojiano kwa Meneja wa Swahilihub......................320

F. Kiambatisho VI: Dodoso kwa mahojiano kwa Wahudumu wa Nation Media...........321

G. Kiambatisho VII: Kielelezo cha Uchunzaji...............................................................321

H. Kiambatisho VIII: Idhini ya Utafiti...........................................................................323

I. Kiambatisho IX: Plagiarism Statement........................................................................324

K. Kiambatisho XI: Machapisho.....................................................................................325

L. Kiambatisho XII: Makongamano na Semina.............................................................326

# TABARUKU

Kwa wazazi wangu Patrick Owino Agalla na Roseline Owino Adhiambo.

# SHUKURANI

Namshukuru Mungu Muumba kwa kunipa neema zake katika kiwango hiki cha masomo yangu na kuniwezesha kuimaliza kazi hii. Natoa shukurani za dhati pia kwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro kwa kufadhili utafiti huu. Shukurani maalum kwa wasimamizi wangu Prof.Kenneth Inyani Simala na Prof. John Habwe kwa kuniongoza kwa kila hatua katika kazi hii. Shukurani zangu nyingine ziwaendee wote waliohusika kwa namna mbalimbali katika kutoa msaada anuai nilipokuwa nikitafiti na kuitayarisha tasnifu hii.

# IKISIRI

Swahilihub ni tovuti iliyozinduliwa katika mwaka wa 2012 kwa lengo la kukuza Kiswahili mtandaoni. Swahilihub ni miongoni mwa tovuti kuu za Kiswahili ambayo matumizi yake yanazidi kuenea na kuimarika kwa sababu ya maendeleo ya kiteknolojia. Ujio wa mitandao umebadili mikondo ya utangamano na kwa sasa majukwaa ya kidijitali ndiyo maeneo makuu ya ukuzaji wa lugha. Kwa takriban mwongo mmoja, Swahilihub imekuwa ikitumika katika sehemu mbalimbali za ulimwengu. Aidha, katika kipindi hiki, teknolojia imekua kwa kasi kubwa mno na kuathiri Kiswahili. Licha ya maendeleo ya teknolojia na athari zake, hakuna utafiti ambao umetathmini namna mradi wa Swahilihub unavyochangia ukuzaji Kiswahili. Ni kutokana na msingi huu ambapo utafiti huu ulilenga kutathmini mradi wa Swahilihub katika ukuzaji Kiswahili. Ili kulifikia lengo hili, utafiti huu ulikusudia kubaini namna mfumo wa Swahilihub unavyochangia katika ukuzaji Kiswahili nchini Kenya, kuchunguza matumizi ya Swahilihub katika ukuzaji Kiswahili, kupambanua changamoto za matumizi yake pamoja na kujadili mikakati ya kuimarisha matumizi ya Swahilihub katika ukuzaji Kiswahili nchini Kenya. Tathmini hii ilitumika kutoa mapendekezo ya mikakati ya kuimarisha mfumo wa tovuti ya Swahilihub. Mwelekeo mseto wa utafiti unaohusu matumizi ya mbinu za kimaelezo na kijarabati kwa pamoja ulitumika katika utafiti huu. Data ya utafiti huu ilikusanywa kwa kutumia uchanganuzi wa matini mtandaoni, mahojiano nyanjani pamoja na hojaji na mijadala miongoni mwa watumiaji wa Swahilihub katika baadhi ya vyuo vikuu nchini Kenya. Utafiti huu ulitumia mahojiano kwa wasimamizi 5 wa Swahilihub na wahadhiri 15, huku hojaji ya matumizi na ukuzaji Kiswahili pamoja na mijadala ya kimakundi ikitumiwa ili kubaini matumizi na ukuzaji Kiswahili miongoni mwa watumiaji wake 320 katika vyuo vikuu nchini Kenya. Jumla watafitiwa 340 walishiriki katika utafiti huu. Aidha utafiti huu ulitumia ARhefs na Similarweb ambavyo ni vifaa vya tathmini ya tovuti ili kutathmini viwango vya ukubalifu na ustahilifu wa Swahilihub miongoni mwa watumiaji wake. Data ya utafiti huu ilichanganuliwa kutokana na malengo ya utafiti na kuongozwa na mihimili ya Nadharia ya Msambao wa Uvumbuzi ya Rodgers (2003). Matokeo ya utafiti huu yaliwasilishwa kwa njia za maelezo, majedwali, picha, michoro na chati. Utafiti huu ulibaini kwamba viwango vya ukubalifu na ustahilifu wa Swahilihub vilikuwa asilimia 45. Aidha matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha kwamba Swahilihub inastahimili ushindani miongoni mwa tovuti zote mtandaoni kwa kiwango cha asilimia 0.13. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kwamba kulikuwa na changamoto anuai zilizokabili Swahilihub. Utafiti huu pia ulijadili mustakabali wa Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Aidha utafiti huu ulizua tasnifu kuwa utanuzi wa teknolojia pamoja na ustawi wa Swahilihub ni nafasi nzuri ya uundaji wa dira ya ukuzaji endelevu wa lugha ya Kiswahili mtandaoni.

## ABSTRACT

Swahilihub is a website launched in the year 2012 with the aim of developing Kiswahili online. Swahilihub is among the main websites whose use is steadily growing as a result of technological advancements. The emergence of the internet has changed the mode of interactions and digital platforms are the key players in language development. For about one decade, Swahilhub has been in use among Swahili users in various places globally. During this period, technology has advanced greatly thus affecting Kiswahili. However, despite these technological advancemts, little study has been done to evaluate its achievements and prospects in developing Kiswahili. As a result, this study sought to find out how the structure of Swahilihub enhances the development of Kiswahili, to determine the use of Swahilihub in the development of Kiswahili, to find out the challenges facing Swahilihub and to discuss the various interventions to the use Swahilihub in the development of Kiswahili in Kenya. This evaluation was used in making recommendations on the ways of improving the functionality of Swahilihub. This study also discussed the challenges and prospects of Swahilihub in the development of Kiswahili online. Mixed reseach approach which integrates both descriptive and experimental designs was used in this study. Data in this study was collected through online document analysis, interviews in the field, questionnaires, and focused group discussions in some universities in Kenya. In this study interview was administered among 5 Swahilihub administrators and 15 lecturers, while questionnaires and focused group discussions were used among 320 Swahilihub users in Kenya. Thus a total of 340 respondents were used in this study. Moreover, ARehfs and Similarweb which are online website evaluation tools were used to establish the levels of adoption and relevance of Swahilihub among its users. Data in this study was analysed based on its objectives and the Diffusion of Innovation Theory by Rodgers (2003). Results of this study were presented descriptively through tables, charts, drawings and pictures. The findings of this study placed the level of adoption of Swahilhub at the rate of 45%. Additionally, the study found out that Swahilihub competed with other websites online at the rate of 0.13%. The findings of this study found out salient challenges of Swahilihub. The study also discussed the prospects of Swahilihub in the development of Kiswahili. This study argues that the technological affordances coupled with the advancement of Swahilihub raises sufficient impetus for sustainable digital development of Kiswahili online.

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 3.1: Jumuiya finyu ya utafiti.................................................................................84
Jedwali 4.1 Matumizi ya Vitengo mbalimbali vya tovuti ya Swahilihub........................108
Jedwali 4.2: Njia za Ukuzaji wa Kiswahili kwenye Swahilihub.....................................212
Jedwali 4.3: Njia mbalimbali za matumizi ya Swahilihub..............................................213
Jedwali 4.4: Baadhi ya Istilahi za Kiswahili kwenye Jukwaa la Facebook....................222
Jedwali 4.5: Changamoto katika matumizi ya Swahilihub.............................................254

## ORODHA YA CHATI

Chati 4.1: Kategoria za Watafitiwa....................................................................106

Chati 4.2: Matokeo ya Matumizi ya Mwanzo................................................................109

Chati 4.3: Matokeo ya Matumizi ya Habari....................................................................112

Chati 4.4: Matokeo ya matumizi ya Jifunze Kiswahili..................................................113

Chati 4.5: Matokeo ya matumizi ya picha......................................................................114

Chati 4.6: Matokeo ya Matumizi ya Blogu na Ukumbi..................................................117

Chati 4.7: Matokeo ya  matumizi ya video.....................................................................122

Chati 4.8: Matumizi chini ya  miaka  mitano.................................................................216

Chati 4.9: Matumizi ya zaidi ya  miaka  mitano.............................................................217

Chati 4.10: Mikakati ya  Ukuzaji wa Kiswahili kwenye Swahilihub.............................263

Chati 4.11: Swahilihub katika Ukuzaji wa Kiswahili.....................................................265

Chati 4.12: Mustakabali wa Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili............................266

## ORODHA YA PICHA

Picha 4.1: Kitengo cha Habari....................................................................................111
Picha 4.2: Kitengo cha Blogu na Ukumbi......................................................................115
Picha 4.3: Kitengo cha Maktabani Jisomee....................................................................118
Picha 4.4: Kitengo cha Video..........................................................................................119
Picha 4.5: Mikakati mbalimbali ya matumizi ya Video..................................................123
Picha 4.6: Kitengo cha Makala........................................................................................125
Picha 4.7: Vitengo mbali mbali vya Tovuti ya Swahilihub............................................128
Picha 4.8: Mifano ya misemo katika ujenzi wa msamiati kwenye kitengo cha Jifunze Kiswahili...........................................................................................................................132
Picha 4.9: Makala za tafiti mbalimbali kwenye kitengo cha Jifunze Kiswahili.............134
Picha 4.10: Ujenzi wa lugha kupitia nahau kwenye kitengo cha Jifunze Kiswahili......136
Picha 4.11: Umuhimu wa Kitengo cha Jifunze Kiswahili..............................................138
Picha 4.12: Mitagusano kwenye Blogu na ukumbi katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili141
Picha 4.13: Mifano ya vitabu katika kitengo cha Maktabani Jisomee............................143
Picha 4.14: Michakato ya ukuzaji wa lugha ya Kiswahili..............................................145
Picha 4.15: Magazeti mbalimbali katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili.......................147
Picha 4.16: Ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kupitia ushari na tenzi...............................149
Picha 4.17: Kitengo cha Picha........................................................................................151
Picha 4.18: Vitendawili katika Kitengo cha Picha..........................................................153
Picha 4.19: Picha katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili.................................................155
Picha 4.20: Mifano ya Video iliyochangia ujenzi wa msamiati wa Kiswahili................157
Picha 4.21: Vitendawili katika ujenzi wa misamiati kwenye Kitengo cha Mwanzo……160
Picha 4.22: Mchango wa vitendawili katika ukuzaji wa kiswahili................................162
Picha 4.23: Nafasi ya Kitengo cha Habari......................................................................165
Picha 4.24: Nafasi ya vyombo vya Habari katika Kitengo cha Habari...........................166
Picha 4.25: Nahau katika ukuzaji wa Kiswahili kwenye Kitengo cha Jifunze Kiswahili.169
Picha 4.26: Prof Mosha katika ujenzi wa msamiati kupitia ufundishaji kwenye kitengo cha Jifunze Kiswahili..........................................................................................................172
Picha 4.27: Mifano ya vitabu vilivyochangia usambaaji wa Kiswahili..........................174
Picha 4.28: Kitengo cha Jifunze Kiswahili.....................................................................176
Picha 4.29: Mifano ya Makala katika Kitengo cha Jifunze Kiswahili.......................178
Picha 4.30: Nafasi ya Blogu na ukumbi katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili.............180
Picha 4.31: Ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kupitia Hadithi...........................................182
Picha 4.32: Mifano ya Video iliyochangia usambaaji wa Kiswahili..............................185
Picha 4.33: Mifano ya misemo ya lugha ya Kiswahili....................................................187
Picha 4.34: Ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kupitia Mashairi.........................................189
Picha 4.35: Matini muhimu katika kitengo cha mwanzo................................................192
Picha 4.36: Kitengo cha Mwanzo....................................................................................194
Picha 4.37: Ushawishi wa viongozi mbalimbali kote ulimwenguni katika Kitengo cha Jifunze Kiswahili..........................................................................................................196

Picha 4.38: Hifadhi ya utafiti wa lugha ya Kiswahili....................................................199
Picha 4.39: Hifadhi ya Makala za utafiti wa lugha ya Kiswahili...................................201
Picha 4.41: Mifano ya ushawishi wa viongozi uliochangia usambaaji wa Kiswahili.....204
Picha 4.42: Vitendawili kwenye Kitengo cha Makala...................................................207
Picha 4.43: Kitambulisho maalum cha tovuti ya Swahilihub kwa mujibu wa AHREFS219
Picha 4.44: Nafasi ya Swahilihub katika uchunguzi wa pili miezi mitatu baadaye........227
Picha 4.45: Kuimarika kwa Nafasi ya Swahilihub kwa Muda wa miezi mitatu.............229
Picha 4.46: Tovuti Nyingine zinazoshughulikia lugha ya Kiswahili..............................233
Picha 4.47: Kurasa za matini zilizorejelewa na watumiaji wa tovuti ya Swahilihub......237
Picha 4.48: Ruwaza ya Tovuti mpya na za kale zilizorejelea tovuti ya  Swahilihub……238
Picha 4.49: Tovuti Zilizorejelea tovuti ya Swahilihub...................................................242
Picha 4.50: Urejeleaji wa Matini ya tovuti ya Swahilihub Kimaeneo............................248
Picha 4.51: Urejeleaji zaidi wa Matini ya Swahilihub Kimaeneo..................................250
Picha 4.52: Matumizi ya tovuti ya Swahilihub..............................................................251

## ORODHA YA MICHORO

Mchoro 1.1: Mchakato wa Msambao wa uvumbuzi........................................................21

Mchoro 3.1: Mpangilio Sambamba wa Mwelekeo Mseto wa Utafiti...............................72

Mchoro 4.1: Mkabala wa Rodgers(2003)......................................................................270

Mchoro 4.2: Mkabala Mpya (2023)...............................................................................271

## VIFUPISHO NA AKRONIMU

| | |
|---|---|
| **CCTV** | Closed Circiut Television |
| **HCS** | Helsinki Corpus of Swahili |
| **ICT** | Information Communication Technology |
| **KIE** | Kenya Institute of Education |
| **KIKO** | Kiswahili katika Kompyuta |
| **KNEC** | Kenya National Examinations Council |
| **NMG n.w.** | Nation Media Group na wengine |
| **RoK** | Republic of Kenya |
| **SALAMA** | Swahili Language Manager |
| **SPSS** | Statistical Package for Social Sciences |
| **TATAKI** | Taasisi ya Taaluma za Kiswahili |
| **TEHAMA** | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| **UNESCO** | United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization |

## DHANA ZILIZOTUMIKA

**ARhefs:** Programu ya tarakilishi inayokusanya na kuchanganua data kwenye tovuti.

**Heterofilia:** Mitagusano inayotokea miongoni mwa wanajamii walio na imani, itikadi, elimu, hali ya kiuchumi na sifa zinazotofautiana.

**Homofilia:** Mitagusano inayotokea miongoni mwa wanajamii walio na imani, itikadi, elimu, hali ya kiuchumi na sifa zinazofanana.

**Mawasiliano:** Mchakato unaowawezesha wanajamii kubuni, kushiriki na kusambaza habari miongoni mwao ili kuyafikia malengo fulani mahususi.

**Mbwiaji:** Mwanajamii anayehiari kuukubali uvumbuzi mapema kabla ya wanajamii wengine.

**Msambao:** Mchakato wa kuwasilisha uvumbuzi kupitia vyombo fulani katika mfumo wa wanajamii mahususi kwa muda fulani.

**Swahilihub:** Tovuti inayokuza taaluma ya Kiswahili mtandaoni .

**Ubwiaji:** Hali ya mwanajamii kuhiari kuukubali uvumbuzi mapema zaidi kuliko wanajamii wengine.

**Udhibitishaji:** Hatua ambapo maamuzi ya matumizi na utekelezaji yametokea lakini msisitizo hapa ni kwamba kuna haja ya wanajamii

wengine kutiana moyo kuhusu maamuzi ya kuukubali uvumbuzi husika.

**Uhamisho:** Hatua ya tatu kwenye mchakato wa msambao wa uvumbuzi inayohusu mwanajamii kutambua uwepo wa uvumbuzi na kujitahidi kuuelewa zaidi..

**Ukuzaji wa Kiswahili:** Hatua mbalimbali zinazochukuliwa ili lugha ya Kiswahili iweze kutumiwa na watu wengi zaidi na kuihusisha katika shughuli za kila siku za wanajamii.

**Uvumbuzi:** Upya wa jambo hali au dhana kwa mujibu wa mtu binafsi au asasi fulani.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Utafiti

Dhana ya ukuzaji wa Kiswahili imesheheni jitihada mbalimbali za ukuaji na ueneaji wake miongoni mwa watumiaji wake (Clement, 2010). Ukuzaji Kiswahili ni jumla ya juhudi na hatua mbalimbali zinazochangia katika upanuzi wa wigo wa matumizi ya Kiswahili miongoni mwa wanajamii. Ukuzaji Kiswahili umejengwa kwa nguzo kuu tatu: ujenzi wa lugha ya Kiswahili kwa misingi ya maandishi yake mapana, uundaji wa istilahi zake, ufafanuzi wa sarufi yake na uundaji wa makamusi, usambaaji wa Kiswahili kulingana na mahitaji ya walengwa mtandaoni pamoja na udumishaji wa hadhi yake katika jamii (Cooper na Robert, 1990). Hivyo basi, ukuzaji Kiswahili ni mchakato na mikakati ambayo hutokea kwa namna mbalimbali na kupitia asasi na vyombo tofautitofauti.

Kwa muda mrefu sasa, lugha ya Kiingereza imeendelea kutumika zaidi na kutawala shughuli na mitagusano mitandaoni. Hata hivyo, mnamo mwaka wa 2010, zaidi ya 60% ya idadi ya watu walitumia lugha nyinginezo zisizo Kiingereza hivyo kuthibitisha kwamba kuna mabadiliko katika mkondo wa takwimu za wanaotumia lugha mbalimbali mtandaoni (King 2010). Hali hii inaendelea kubadilika kwani lugha nyingine zimeanza kutumika zaidi mtandaoni kutokana na ongezeko kubwa la idadi ya tovuti pamoja na watumiaji wa tovuti hizi kote ulimwenguni. Hali hiyo ya wingi lugha na tofauti za kitamaduni katika mtandao imesababisha kuwepo kwa vyombo vya habari vya kijamii vyenye wingi lugha, vikiwa na matumizi ya kipekee ulimwenguni (King, 2010).

Lugha ya Kichina ilikuwa ya pili iliyopendwa na kutumika katika mtandao baada ya

Kiingereza (internetworldstates.com). Kwa sasa, mbali na lugha ya Kiingereza na Kichina, lugha ya Kiswahili inatumika katika mitandao mbalimbali kuandika habari na kutoa maoni kuhusu maswala ya kijamii. Isitoshe lugha ya Kiswahili ina nafasi muhimu ya kubuni na kusambaza dhana anuai mtandaoni, hali ambayo imezua changamoto kubwa ya kubuni sera na mikakati maalum ya matumizi ya tovuti ya Swahilihub.

Hivyo basi, ukuzaji wa lugha ya Kiswahili katika tovuti ya Swahilihub hauwezi kupuuzwa. Lugha ya Kiswahili, kama zilivyo lugha zote duniani, iliinukia, ikakua, na inaendelea kukua katika maana halisi ya neno 'kua' – "kitendo cha kuongezeka kimo, ukubwa au uwezo" (*Kamusi ya Kiswahili Fasaha* – BAKIZA, 2010:167). Ukuzaji Kiswahili ni suala muhimu kwa kuwa Kiswahili ndiyo lugha ya kipekee ya Kiafrika iliyo na hadhi ya nafasi ya sita kimataifa kikitanguliwa na Kiingereza, Kifaransa, Kihispania, Kiarabu na Kireno (Jagero, 2013). Kiswahili kinazungumzwa na watu takriban milioni 160 kote ulimwenguni (Mutiso, 2014). Licha ya kuwa tayari Ukanda wa Afrika Mashariki umeanza kuweka mikakati ya kukuza ushirikiano na utangamano wa mataifa ya ukanda huu, ni muhimu kusisitiza suala la teknolojia na Lugha ya Kiswahili kwani lugha hii tayari imekubaliwa kuwa ya mawasiliano mapana katika ukanda wa Afrika Mashariki. Kizazi cha sasa na vile vya siku zijazo vinatumikiza TEHAMA kwa wingi kutokana na kasi ya uvumbuzi na usambaaji wake. Matokeo ya utafiti anuai kuhusu historia na maendeleo ya Kiswahili yanathibitisha jambo moja muhimu kwamba lugha ya Kiswahili na matumizi yake yamekuwa yakipanuka tena kwa kasi kubwa ikiwa ni pamoja na msamiati na istilahi zake kuongezeka, nyanja za matumizi yake kupanuka, idadi ya watumiaji na wazungumzaji wake kuongezeka pamoja na hadhi na dhima yake kupaa juu. Mintarafu ya ukweli huu, tunaweza kudai kuwa kukua kwa Kiswahili hususan katika Ukanda wa Afrika ya Mashariki na Kati ni ushahidi kuntu wa kuendelea kwa jamii ya wazungumzaji wa Kiswahili katika janibu

hizi. Nchini Kenya kumekuwa na juhudi mbalimbali za ukuzaji Kiswahili. Baadhi ya hizo juhudi ni vipindi vya redio na televisheni vinavyochangia katika ufundishaji wa Kiswahili shuleni. Pia kuna mchango wa vyama vya Kiswahili humo nchini kama vile CHAKITA ambavyo huchangia pakubwa katika kuimarisha utafiti wa Kiswahili miongoni mwa wataalamu shuleni na vyuoni. Aidha kumekuwa na juhudi mahususi kwenye televisheni ya NTV za kusambaza Kiswahili mtandaoni kupitia kwa jukwaa la Swahilihub hasa katika vitengo vyake nane. Nchini Kenya, katika kampuni ya Nation Media Group kulikuwa na kitengo cha Swahilihub ambacho kilitumia gazeti la *Taifa Leo* kukuza taaluma ya Kiswahili.

Miongoni mwa masuala ibuka katika mchakato wa ukuzaji wa Kiswahili ni uvumbuzi wa tovuti uliotokea katika mwaka wa 1989. Tangu kubuniwa kwa tovuti hadi sasa, maendeleo ya kiteknolojia mtandaoni yamechangia kubuniwa kwa tovuti anuwai, Swahilihub ikiwa mojawapo (Aghaei, Nematbakhsh, na Farsani, 2012). Kwa takriban miaka kumi sasa, TEHAMA imekuwa ikichangia ukuzaji wa Kiswahili kupitia tovuti ya Swahilihub. Swahilihub ni tovuti iliyovumbuliwa katika mwaka wa 2012 na Kituo cha utangazaji cha Nation kwa ajili ya ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili kwenye mtandao. Swahilihub ni miongoni mwa mitandao mikuu ya Kiswahili ambayo matumizi yake yanazidi kuenea na kuimarika kwa sababu ya maendeleo ya kiteknolojia. Kwa kuwa utendakazi wa tovuti ya Swahilihub huchangiwa pakubwa na urahisi wake kimatumizi na uamilifu wake kimatini, utafiti huu ulitokana na miongoni mwa mambo mengine, haja ya kuichunguza tovuti ya Swahilihub kimatini ili kubaini iwapo Swahilihub ina matini na kongoo inayokidhi mahitaji ya watumiaji wake na kutimiza lengo la ukuzaji wa Kiswahili mtandaoni au la.

Uwezo wa tovuti ya Swahilihub kukusanya, kuhifadhi na kuimarisha upatikanaji wa matini za Kiswahili mtandaoni umeimarishwa kutokana na maendeleo yanayojiri

mtandaoni. Maendeleo haya yamechangia pakubwa katika juhudi za ukuzaji wa Kiswahili kwenye tovuti ya Swahilihub. Mabadiliko makubwa mtandaoni yamefanikisha utendakazi wa Swahilihub na kuchangia manufaa mengi kwa watumiaji wake. Ingawa mabadiliko haya ya kiteknolojia hutokea kila uchao, utafiti wa kina haujafanywa ili kutathmini mchango wa tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Miundo ya kiteknolojia ya tovuti anuai imeshuhudia maendeleo mengi katika miaka michache iliyopita. Maendeleo haya yanajitokeza kwenye vigezo vipya vya tovuti kama vile injini pekuzi za kisemantiki na mitandao ya kijamii (Stringam na Gerdes, 2010). Maendeleo haya ya kiteknolojia ni msukumo wa kipekee unaolazimu tathmini ya kila mara ya tovuti husika ili kuifanya kuyafikia malengo yake.

Licha ya maendeleo haya ya kiteknolojia kushuhudiwa, tovuti ya Swahilihub haijafanyiwa uchunguzi wa kina ili kupambanua changamoto zinazowakabili watumiaji wake katika ujenzi wa Kiswahili, usambaaji wake na udumishaji wa hadhi na dhima yake. Hali hii ilizua haja kubwa ya kufanya utafiti huu kwa lengo la kupambanua mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili miongoni mwa watumiaji wake mtandaoni. Isitoshe, licha ya kuwa na utafiti wa awali kuhusu mradi wa Swahilihub, ni adimu kupata utafiti ulioweka wazi vipengele mahususi vya tathmini ya utendakazi wake kimatumizi na uamilifu wake kimatini kama msingi wa ujenzi wa Kiswahili, usambaaji wake na udumishaji wa hadhi na dhima yake mtandaoni. Hali hii ilichochea utafiti huu kuhusu tathmini ya Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa watumiaji wake.

Miongoni mwa manufaa ya tovuti ya Swahilihub ni pamoja na ongezeko kubwa la idadi ya watumiaji wake kutokana na kuimarishwa kwa mitagusano ya kidijitali mtandaoni. Mitagusano hii ya kidijitali huchangia pakubwa katika kupunguza maingiliano ya moja kwa moja miongoni mwa watumiaji wake mitandaoni. Kutokana na ongezeko hili la

idadi ya watumiaji pamoja na maingiliano ya kidijitali, Swahilihub imechangia pakubwa usambaaji wa Kiswahili na udumishaji wa hadhi na dhima yake miongoni mwa watumiaji wake kote ulimwenguni. Swahilihub ni mtandao wenye upekee mkubwa katika kuimarisha michakato ya kitaaluma mitandaoni.

Hata hviyo, tovuti hii haijafanyiwa uchunguzi wa kina ili kubaini mchango wake wa kinadharia katika kuboresha mkabala wa tathmini ya tovuti na kujadili mustakabali wake katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Mazoea yamekuwa kuviangalia vyombo vya habari, asasi anuai na serikali kwa ujumla kama ndivyo vyombo pekee vyenye wajibu wa kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili. Kando na serikali na asasi mbalimbali, yapo maeneo mengine yanayoweza kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili ambayo ama hayajaangaliwa kwa kiasi cha kutosha au yamesahaulika. Mojawapo ya maeneo hayo ya ukuzaji wa lugha ya Kiswahili ni maingiliano yanayojiri mitandaoni kwenye tovuti ya Swahilihub. Utafiti huu unadahili kuwa Swahilihub inapaswa kuchukua jukumu muhimu sana katika ukuzaji Kiswahili kwani ndicho chombo kilicho na nafasi ya kikati katika kukusanya, kuhifadhi na kuhariri matini katika hali mbalimbali kwa wadau wa Kiswahili mitandaoni.

## 1.2 Suala la Utafiti

Ingawa Swahilihub ilizinduliwa katika mwaka wa 2012 kwa lengo la kuhifadhi, kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili, ni utafiti mchache umefanywa tangu uzinduzi wake kubaini mafanikio yake. Kumekuwa na juhudi nyingi za kukuza Kiswahili, zikiwa pamoja na ufundishaji wake katika asasi kama vile BAKITA na TATAKI katika ukanda wa Afrika Mashariki na kote ulimwenguni. Ujio wa mitandao umebadili mikondo ya utangamano na kwa sasa majukwaa ya kidijitali ndiyo maeneo makuu ya maenezi na ukuzaji wa lugha. Licha ya Swahilihub kufanya kazi kwa takriban mwongo mmoja sasa, hapana tathmini ambayo imefanywa ili kubaini jinsi inavyofanya kazi. Utanuzi wa teknolojia na taaluma umechangia pakubwa kutoa msukumo wa kufanya utafiti huu. Katika kipindi hiki, TEHAMA imekua kwa kasi kubwa mno na kuathiri mikakati ya ukuzaji Kiswahili kwenye tovuti ya Swahilihub. Msukumo mkubwa wa kufanya utafiti huu, ulitokana na hali hii ya maendeleo ya TEHAMA na athari zake pamoja na Swahilihub kuendelea kutumika katika sehemu nyingi kote ulimwenguni bila utafiti wa kutosha kuhusu hali, ufanisi, changamoto na mustakabali wake katika ukuzaji wa Kiswahili. Licha ya Swahilihub kuwa na nafasi hii muhimu katika ukuzaji wa Kiswahili, tathmini yake inahitaji kutolewa kwa lengo la kuielewa, kuitolea michango na mapendekezo ya kuiboresha kama chombo cha ukuzaji wa Kiswahili. Mfumo wa ukuzaji wa Kiswahili mtandaoni umekosa muumano, umechanganyika, unakinzana na unaweza kuleta madhara tukizingatia kwamba mitandao mbalimbali ni majukwaa muhimu sana katika mawasiliano mapana miongoni mwa wadau wa Kiswahili. Hilo pamoja na hoja kwamba TEHAMA na ukuzaji wa Kiswahili kwenye tovuti ya Swahilihub ni masuala ibuka yanayozua mijadala mingi ulimwenguni, ndicho kichocheo cha kufanya utafiti huu ili kutathmini mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili.

## 1.3 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu uliazimia kutathmini mradi wa Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili nchini Kenya. Lengo kuu la utafiti lilikuwa kupambanua mchango wa Swahilihub katika ukuzaji Kiswahili. Ili kulifikia lengo hilo, madhumuni mahsusi yafuatayo yalizingatiwa:

i) Kubaini namna mfumo wa Swahilihub unavyochangia katika ukuzaji Kiswahili nchini Kenya.

ii) Kuchunguza matumizi ya Swahilihub katika ukuzaji Kiswahili nchini Kenya.

iii) Kupambanua changamoto za matumizi ya Swahilihub katika ukuzaji Kiswahili nchini Kenya.

iv) Kujadili mikakati ya kuimarisha matumizi ya Swahilihub katika ukuzaji Kiswahili nchini Kenya.

## 1.4 Maswali ya Utafiti

Ili kulifikia lengo lake, utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

i) Je, mfumo wa Swahilihub unaathiri vipi ukuzaji Kiswahili nchini Kenya?

ii) Ni kwa namna gani Swahilihub inatumiwa katika ukuzaji Kiswahili nchini Kenya?

iii) Nini changamoto za matumizi ya Swahilihub katika ukuzaji Kiswahili nchini Kenya?

iv) Nini mustakabali wa mradi Swahilihub katika ukuzaji Kiswahili nchini Kenya?

## 1.5 Misingi ya Uteuzi wa Mada ya Utafiti

Mada ya utafiti iliteuliwa kwa misingi ifuatayo: Kwanza, mada hii ilitokana na haja ya kuchunguza namna mfumo wa Swahilihub unavyochangia katika ukuzaji Kiswahili nchini Kenya. Kuzuka kwa teknolojia ya mawasiliano ya kimtandao ambayo imekuwa maarufu sana miongoni mwa watumiaji wa Swahilihub kote ulimwenguni kumechangia pakubwa katika ukuzaji Kiswahili. Hivyo basi utafiti huu ulichochewa na haja ya

kuchunguza namna mfumo wa tovuti ya Swahilihub unavyochangia katika ujenzi wa Kiswahili, udumishaji wa hadhi na dhima ya Kiswahili pamoja na usambaaji wake mtandaoni nchini Kenya. Pili, mada ya utafiti huu iliteuliwa kutokana na haja ya kutathmini kiwango cha ukuzaji Kiswahili kwenye tovuti ya Swahilihub miongoni mwa watumiaji wake mtandaoni. Tathmini ya utendakazi wa tovuti ya Swahilihub ni suala muhimu katika makadirio ya manufaa yake kwa watumiaji wake katika ukuzaji Kiswahili. Msingi wa tatu ulitokana na haja ya kujadili changamoto za matumizi ya Swahilihub katika ukuzaji Kiswahili. Changamoto hizi huathiri pakubwa uwezo wa Swahilihub kukusanya, kuhifadhi na kuimarisha upatikanaji wa matini ya Kiswahili kutokana na mabadiliko na maendeleo yanayojiri mtandaoni. Hatimaye uteuzi wa mada ya utafiti huu ulitokana na haja ya kubaini mikakati ya kuimraisha matumizi ya Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili. Hivyo basi, utafiti huu ni wa msingi katika kutathmini mchango wa tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili mitandaoni.

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu ni chimbuko na kichocheo kwa wadau wa Kiswahili cha kuanza kutafakari juu ya uundaji wa dira ya ukuzaji endelevu wa Kiswahili mitandaoni na ustawi endelevu wa Swahilihub katika karne ya 21. Kwa kuwa ukuzaji Kiswahili ni mchakato muhimu unaohusisha hatua zinazochukuliwa ili lugha ya Kiswahili iweze kutumiwa na watu wengi zaidi, na watu hao waweze kuihusisha lugha ya Kiswahili katika shughuli zao mbalimbali za kila siku, mikakati mbalimbali ikiwemo utafiti huu ni miongoni mwa juhudi mwafaka za kupanua wigo wa matumizi yake. Juhudi hizi huchangia katika shughuli mbalimbali za jamii za kuingizwa kwa Kiswahili katika harakati mbalimbali kama vile katika siasa, uchumi, elimu na pia nyumbani mwa watumiaji wake kama njia ya ukuaji na ueneaji wake.

Utafiti huu ulibaini namna mfumo wa Swahilihub unavyochangia katika ukuzaji Kiswahili nchini Kenya. Mchango huu ulionyesha nafasi ya mfumo wa Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili kama teknolojia ya mawasiliano ya kimtandao ambayo imekuwa maarufu sana miongoni mwa watumiaji wake kote ulimwenguni. Kama ilivyo mtindo wa uimarishaji ubora katika tovuti anuwai kote ulimwenguni, hapa nchini Kenya, tathmini ya Swahilihub ni hatua muhimu katika kuimarisha ukuzaji wa lugha ya Kiswahili mitandaoni. Utafiti huu ulieleza mchango wa Swahilihub kwa kutoa maelezo kuhusu umbo na mwonekano wake, urahisi wake kimatumizi, ufikiaji wa habari zake miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub. Maelezo hayo yalikuwa ya maana kwa wataalamu wote wa Kiswahili katika kuimarisha ukuzaji wa Kiswahili mtandaoni.

Utafiti huu pia ulitathmini kiwango cha ukuzaji wa Kiswahili miongoni mwa watumiaji wa Swahilihub. Tathmini ya utendakazi wa tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili, ilitoa mchango katika kudhihirisha ushindani wake, utambulisho wake, maingiliano na ushirikiano wake na tovuti nyingine, maenezi ya matumizi yake kimaeneo pamoja na maendeleo ya kiteknolojia yanayochangia mageuzi makubwa yanayoendana na urahisi wake kimatumizi na uamilifu wake kimatini.

Aidha utafiti huu ulijadili changamoto za matumizi ya Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili na kudhihirisha athari zake katika utendakazi wa Swahilihub katika kukusanya, kuhifadhi na kuimarisha upatikanaji wa matini ya Kiswahili mtandaoni Aidha mapendekezo yaliyotokana na utafiti huu yalichangia kuzua suluhisho kwa changamoto hizo na kuwanufaisha washikadau katika kubuni na kuboresha tovuti shindani za Kiswahili.

Hatimaye utafiti huu ulikuwa muhimu katika kubaini mikakati mbalimbali ya kuimarisha ukuzaji Kiswahili kwenye tovuti ya Swahilihub nchini Kenya. Kwa njia hii, utafiti huu uliibua data muhimu kwa mustakabali wa tovuti ya Swahilihub. Hii ni data

ambayo itaweza kutumiwa na wataalamu na wadau wa lugha ya Kiswahili katika kuimarisha na kuboresha namna ambavyo Swahilihub itakavyotumika kwa manufaa ya watumiaji wake katika siku za usoni. Ugunduzi wa utafiti huu ni muhimu kwa wataalam wa Kiswahili katika kuitumia Swahilihub kukuza taaluma za Kiswahili. Hivyo basi, utafiti huu ulikuwa wa msingi katika kutathmini mchango wa tovuti ya Swahilihub kwa kujadili mustakabali wake katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili.

Utafiti huu pia una mchango mwafaka katika kupanua wigo wa matumizi ya lugha ya Kiswahili mitandaoni kufikia viwango vya lugha zingine za kimataifa kama vile Kiingereza na Kifaransa. Mvumko wa mitandao mbalimbali umebadili namna asasi mbalimbali zinavyoendeleza mawasiliano yao na mitagusano yao katika kuyafikia malengo yao. Njia moja ya kufikia hadhira kubwa ni kupitia majukwaa ya kimtandao kama vile barua pepe, injini pekuzi ya Google, mitandao ya kijamii na tovuti anuwai. Utafiti huu ni muhimu kwa sababu unatathmini mchango wa tovuti ya Swahilihub mtandaoni katika ukuzaji wa Kiswahili miongoni mwa watumiaji wake. Kwa jumla, utafiti huu ulikuwa wa manufaa kwa wakuza mitaala na wataalamu mbalimbali katika kuandaa semina, warsha na simposia kwa madhumuni ya kuimarisha matumizi na makuzi ya lugha ya Kiswahili mitandaoni.

## 1.7 Tahadhania ya Utafiti

Licha ya changamoto mbalimbali zinazoikumba Swahilihub, tovuti hii inatoa mchango mkubwa katika ukuzaji wa lugha ya Kiswhaili na mustakabali wake unatia moyo miongoni mwa watumiaji wake kote ulimwenguni.

## 1.8 Nadharia ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Msambao wa Uvumbuzi ya Rodgers, (2003). Kwa mujibu wa Rodgers, nadharia ya Msambao wa Uvumbuzi ilibuniwa kutokana na juhudi mbalimbali za awali katika nyanja za soshiolojia, anthropolojia, elimu, afya, na

mawasiliano. Raslimali muhimu sana ya nadharia hii ni wanajamii ambao wana uwezo wa kuukubali ama kuukataa uvumbuzi wo wote. Ili uvumbuzi wo wote ufanikiwe, ni lazima ukubalike na hatimaye kufikia kilele chake cha ukubalifu miongoni mwa wanajamii.

Dhana ya uvumbuzi iliangaziwa mara ya kwanza na mwanasoshiolojia wa Kifaransa, Gabriel Tarde mwishoni mwa karne ya 19 pamoja na wanaanthropolojia wa Kijerumani na wanajiografia kama Ratzel na Leo (Spier, 1929). Uvumbuzi ni dhana inayoelezea kutokea kwa teknolojia au mawazo mapya na kusambaa kwake kupitia kwa mchakato unaotumia vyombo vya mawasiliano kwa muda mahsusi miongoni mwa jamii (Rodgers, 2003). Uvumbuzi ulishughulikiwa mwanzoni kama kipera cha sosholojia kule Marekani katika miaka ya 1920. Katika kipindi hiki, matumizi ya teknolojia katika sekta ya kilimo yalianza kuenea na watafiti wengi walianza kuchunguza namna wakulima walivyokuwa wakitumia teknolojia iliyojengwa kwenye usetaji wa mbegu, mashine na mbinu mpya za kilimo (Valente na Rodgers 1995). Juhudi hizi zilichangia pakubwa hatua ya Everett Rodgers mnamo mwaka wa 1962 kuchanganua takribani kazi 508 za utafiti kuhusu msambao wa uvumbuzi. Hata hivyo, ni michango ya utafiti wa awali kuhusu matumizi ya mbegu mseto kule Iowa uliojenga msingi wa msambao kama uliorejelewa mwanzoni na wataalam wengi.

Tangu kuasisiwa kwake katika soshiolojia, Msambao wa Uvumbuzi umetumiwa katika miktadha mbalimbali ikiwemo: mawasiliano, maswala ya kimaendeleo, kiafya na maswala ya kiutawala. Mchango mkubwa wa nadharia ya Msambao wa Uvumbuzi ulidhihirika katika ukubalifu na matumizi faafu ya madawa mapya, mbinu mpya za kimatibabu na mawasiliano (Berwick, 2003).

Nadharia ya awali ya Msambao wa Uvumbuzi (1995) ilijengwa kwenye misingi mikuu mitatu: uvumbuzi wenyewe, vyombo vya mawasiliano na mfumo wa kijamii. Hata

hivyo nadharia hiyo ya awali ilipungukiwa kwa kutozingatia na kuangazia kipengee muhimu cha muda unaohitajika kukamilisha mchakato mzima wa msambao wa uvumbuzi husika. Kutokana na upungufu wa nadharia ya awali, Rodgers aliifanyia mabadiliko nadharia hii katika mwaka wa 2003. Mabadiliko hayo yalizingatia kipengele cha muda unaohitajika ili kusambaza uvumbuzi. Rodgers, (2003) anaeleza kwamba uvumbuzi una uwezo wa kubadilikabadilika kiasi kwamba dhana za teknolojia na uvumbuzi zikawa na sifa za kiusawe.

### 1.8.1 Mihimili ya nadharia ya Uvumbuzi wa Mawasiliano

Mihimili mikuu minne ya Nadharia ya Msambao wa Uvumbuzi iliyopendekezwa na Rodgers (2003) ni ifuatayo:

a) Uvumbuzi
b) Vyombo vya mawasiliano na mitagusano ya kijamii.
c) Muda wa msambao wa uvumbuzi katika mfumo mahususi wa kijamii.
d) Michakato na hatua mbalimbali za msambao wa uvumbuzi.

**a) Uvumbuzi**

Uvumbuzi unafafanuliwa na Rodgers (2003) kuwa mradi, jambo au dhana inayochukuliwa kuwa mpya na mtu binafsi au asasi fulani. Mhimili huu una sifa mahususi tano zilizotokana na Rodgers kuangazia upya nadharia hii katika mwaka wa 2003. Miongoni mwa sifa hizo tano, zinazochangia pakubwa msambao wa uvumbuzi katika mfumo mahsusi wa kijamii ni pamoja na: manufaa ya uvumbuzi, uwiano wake, uchangamano wake, majaribio ya uvumbuzi na uchunzaji wa uvumbuzi. Suala la kimsingi katika nadharia hii ni ukadiriaji wa kiwango cha ukubalifu na ubwiaji wa uvumbuzi mpya miongoni mwa watumiaji wake katika jamii. Rodgers (2003), anafafanua viwango vya ubwiaji kama kasi ambayo kwayo uvumbuzi unakubaliwa na wanajamii. Kwa mfano idadi ya watu walioubwia uvumbuzi katika kipindi fulani

mahususi inaweza kutumika kupimia kiasi cha ukubalifu na ubwiaji wa uvumbuzi husika (Rodgers, 2003). Kiwango cha ukuzaji wa Kiswahili kwenye tovuti ya Swahilihub kinaweza kukadiriwa kwa kupima idadi ya watumiaji wa Swahilihub. Ukuzaji wa Kiswahili hupimwa kwa kubaini kiwango cha ujenzi wake, usambaaji wake na udumishaji hadhi na dhima yake mtandaoni (Cooper, 1990).

Hata hivyo sifa ya kimsingi katika ubwiaji wa uvumbuzi ni uwazi kuhusu manufaa yake na kwa kiwango gani uvumbuzi huo unavyochukuliwa kuwa wa manufaa kwa wabwiaji wake. Kwa mfano, wavumbuzi, wabwiaji wa awali na wabwiaji wengi wa awali hukubali na kutumia uvumbuzi kwa sababu ya hadhi yao katika jamii. Ili kuboresha uvumbuzi na kufanya manufaa yake kudhihirika, msaada wa kifedha unaweza kutolewa kwa watumiaji wake ili kuwahimiza wengine katika jamii kuukubali uvumbuzi husika (Sherry, 1997). Isitoshe, mchango wa wanajamii ulitambuliwa na kubainishwa katika viwango vifuatavyo: wavumbuzi, wabwiaji wa awali, wabwiaji wengi, wabwiaji wa baadaye, na wasiobwia (Rodgers, 2003). Wavumbuzi na wavumbuzi awali ni wale watumiaji wa tovuti ya Swahilihub waliofanya uamuzi wa kuitumia mapema mbele ya wenzao huku wabwiaji wengi na wabwiaji wa baadaye wakifanya uamuzi huo baadaye. Wasiobwia kabisa wakiwa wanajamii waliokataa kabisa kuitumia tovuti ya Swahilihub katika shughuli zao mitandaoni.

Sifa ya pili ni uwiano ambao umefafanuliwa na Rodgers (2003) kama namna uvumbuzi unavyochukuliwa kuingiliana na hali, maadili na mazoea ya awali ya wabwiaji wa uvumbuzi fulani. Ili kufanikisha msambao wa uvumbuzi, uwiano huchangia pakubwa. Isitoshe, kwa msingi huu Hoerup, (2001) anadai kuwa kila uvumbuzi huathiri mielekeo, imani, maadili, na maoni ya walimu kuhusu ufundishaji na utendakazi wao. Iwapo matumizi ya uvumbuzi yanawiana na imani, maadili na mahitaji ya wabwiaji basi uvumbuzi huo hukubalika haraka na kwa urahisi.

Uchangamano ni sifa ya uvumbuzi inayofafanuliwa kama kiasi cha ugumu wa kuelewa matumizi ya uvumbuzi husika. Uvumbuzi wowote unapochukuliwa kuwa changamano unakuwa vigumu kukubaliwa na kutumiwa na wanajamii Rodgers (2003). Ni rahisi kuimarisha ukubalifu na msambao wa uvumbuzi miongoni mwa wabwiaji wengi iwapo usahili wake kimatumizi ni wa kiwango cha juu (Martin, 2003). Kigezo cha uchangamano wa mradi wa Swahilihub kilielekeza utafiti huu kutathmini Swahilihub na kubaini mchango wake katika ukuzaji wa Kiswahili kwa msingi wa urahisi wake kimatumizi na uamilifu wa kimatini miongoni mwa watumiaji wake. Nadharia hii pia iliongoza uwasilishaji wa data kwa kuweka wazi idadi ya watumiaji wa tovuti ya Swahilihub na kasi ya matumizi ya Kiswahili na ukuzaji wake miongoni mwa watumiaji wake.

Majaribio ni kigezo kingine muhimu sana katika kushawishi wabwiaji wa uvumbuzi kuukubali na kuutumia uvumbuzi. Majaribio ni ule uwezo wa uvumbuzi kuchunguzwa kimatumizi kabla ya kukubaliwa hatimaye (Rodgers, 2003). Kadri uvumbuzi unavyojaribiwa ndivyo ukubalifu na matumizi yake yanavyoimarishwa miongoni mwa wanajamii. Hali hii hutoa nafasi nzuri kwa watumiaji kuuelewa uvumbuzi husika na hata kuuboresha. Hali hii huchangia pakubwa kuwashawishi wabwiaji wengi wanaositasita kuukubali uvumbuzi. Hata hivyo, kigezo cha majaribio hakikutumika katika utafiti huu kwa sababu haukukusudia swala hili la majaribio katika kutathmini utendakazi wa mradi wa Swahilihub.

Aidha, uchunzaji ni kigezo cha uwezo wa uvumbuzi kuonekana kuwa na matokeo na kutoa mchango halisi unaotambuliwa miongoni mwa watumiaji wake. Kuigwa kwa wavumbuzi wanaotangulia kuukubali uvumbuzi hupigwa jeki na kuwepo kwa manufaa yanayodhihirika na kuonekena miongoni mwa wanajamii wanaotarajiwa kuukubali na kuutumia uvumbuzi husika (Parisot, 1997). Ili kufanikisha ukubalifu wa uvumbuzi

miongoni mwa wanajamii, ni muhimu kuhakikisha kwamba uvumbuzi huo una manufaa kwa watumiaji wake, uwiano, usahili wa kimatumizi na uwezo wa kubaini ubora wake miongoni mwa watumiaji wake katika jamii. Utafiti wa awali umeonyesha kwamba vigezo hivi ni muhimu sana katika kuwawezesha walimu, wahadhiri na wadau wote katika elimu kukubali kubwia na kutumia TEHAMA kufundishia na kuimarisha utendakazi wao (Parisot, 1997; Anderson, 1998; Slyke, 1998; Surendra, 2001; Bennett & Bennett, 2003 na Owino, 2011).

Hivyo basi mradi unaweza kuwa uliasisiwa kitambo lakini ukawa uvumbuzi ilmradi ungali unachukuliwa kuwa mpya miongoni mwa wanajamii katika mfumo fulani wa kijamii. Tashwishi miongoni mwa watumiaji ndicho kizingiti kikubwa zaidi kwa msambao wa uvumbuzi. Athari za uvumbuzi wowote miongoni mwa wanajamii huweza kuwafanya kuususia au kuukubali uvumbuzi husika katika jamii. Athari ni mabadiliko yanayotokea katika maisha ya mwanajamii katika mfumo wa jamii fulani. Athari hujumuisha manufaa na madhara ya uvumbuzi husika (Rodgers, 2003).

Hivyo basi, kwa mujibu wa mhimili huu wa nadharia ya msambao wa uvumbuzi (Rodgers, 2003), watumiaji wa tovuti ya Swahilihub, ambayo ni uvumbuzi mpya wa kiteknolojia miongoni mwa watumiaji wa Kiswahili, wanastahili kuelezwa ubora na udhaifu wa tovuti hii ya Swahilihub ili kuimarisha ukubalifu wake miongoni mwa wanajamii ambao ndio watumiaji wa lugha ya Kiswahili mitandaoni. Utafiti huu katika uteuzi wake wa mada uliangazia Swahilihub kama uvumbuzi ulioasisiwa katika mwaka wa 2012, na ambao bado unachukuliwa kama mradi mpya na wataalam wengi wa Kiswahili (Wamalwa, 2016). Aidha, mhimili huu wa uvumbuzi ulichangia kubainisha mchango wa wavumbuzi na wavumbuzi wa awali katika kuwashawishi watumiaji wengine kuhusu ubora na ustahilifu wa tovuti ya Swahilihub. Sifa hizi tano za uvumbuzi zilikuwa msingi muhimu katika kuchunguza mchango wa mfumo wa

Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili. Mfumo wa Swahilihub ulichunguzwa kubaini iwapo ulikuwa wa manufaa kwa watumiaji wake, iwapo uliwiana na kutimiza mahitaji ya watumiaji wake pamoja na kiwango cha urahisi au uchangamano wake. Sifa hizi zilichangia katika kuchunguza namna Swahilihub ilivyochangia katika ujenzi wa Kiswahili kimsamiati na istilahi, usambaaji wake na udumishaji wa hadhi na dhima yake miongoni mwa watumiaji wake.

**b) Vyombo vya Mawasiliano na Mitagusano ya Kijamii**

Kwa mujibu wa Rodgers, (2003) mhimili wa pili wa nadharia ya Msambao wa Uvumbuzi ni vyombo vya mawasiliano na mitagusano ya jamii. Mawasiliano ni mchakato unaowawezesha wanajamii kubuni, kushiriki na kusambaza habari miongoni mwao ili kuyafikia malengo fulani mahususi. Msambao ni aina fulani mahususi ya mawasiliano yanayohusisha uvumbuzi, wahusika na vyombo vya mawasiliano. Kwa mujibu wa mhimili huu kuna mambo matatu ya kimsingi ambayo ni:

i) Mitagusano ya kibinafsi ya kihomofilia na kiheterofilia miongoni mwa wanajamii
ii) Upeo wa msambao wa uvumbuzi unaochangiwa pakubwa na ushawishi wa viongozi
iii) Nafasi ya vyombo vya habari katika msambao wa uvumbuzi.

Vyombo vya habari na mitagusano ya kibinafsi ni zana muhimu za mawasiliano katika nadharia hii. Kwa upande mwingine, msambao ni mchakato wa kijamii unaohusisha kwa kiasi kikubwa, mitagusano ya kibinafsi miongoni mwa wanajamii husika.

Mitagusano ya kibinafsi inaweza kuwa na sifa za homofilia au heterofilia (Rodgers, 2003). Mitagusano ya kihomofilia hutokea miongoni mwa wanajamii walio na imani, itikadi, elimu, hali ya kiuchumi na sifa zinazofanana.

Kwa upande mwingine, mahusiano ya kiheterofilia hutokea miongoni mwa wanajamii walio na imani, itikadi, elimu, hali ya kiuchumi na sifa zinazotofautiana. Hivyo basi

mitagusano ya kibinafsi ina nafasi kubwa sana ya kujenga au kubadilisha mielekeo na misimamo mikali miongoni mwa wanajamii. Mhimili huu wa vyombo vya habari na mawasiliano ulielekeza utafiti huu katika uteuzi wa sampuli kwa msingi wa kimahusiano na kimtagusano. Mitagusano ya kijamii hutokea kwa njia kuu mbili: kiheterofilia. Mitagusano inayotokea miongoni mwa wanajamii walio na imani, itikadi, elimu, hali ya kiuchumi na sifa zinazotofautiana. Kwa upande mwingine ile ya kihomofilia ni mitagusano inayotokea miongoni mwa wanajamii walio na imani, itikadi, elimu, hali ya kiuchumi na sifa zinazofanana. Kwa msingi huu ilikuwa rahisi kuwateua watumiaji mbalimbali wa mradi wa Swahilihub na kuwashirikisha katika utafiti huu. Wale waliokuwa na mitagusano ya kihomofilia kama vile wanafunzi wa taaluma ya Kiswahili pamoja na viongozi wao wanaoheshimiwa miongoni mwao waliteuliwa kama watafitiwa na walishiriki katika mchakato wa ukusanyaji data.

Rodgers (2003) anadahili kwamba kuna wakati katika mchakato wa msambao wa uvumbuzi unaoitwa upeo, na unaofafanuliwa kama wakati ambapo mwelekeo fulani hushika kani na kuanza kuenea kwa kasi. Ndio upeo wa ukubalifu wa uvumbuzi na hujengwa kwa msaada wa viongozi mashuhuri wanaoheshimika katika jamii. Kwa sababu ya heshima zao, viongozi hawa huwashawishi wanajamii kuukubali au kuususia uvumbuzi husika (Greg, 2003). Hivyo basi, kwa kutumia vyombo vya habari na mitagusano mitandaoni, ni rahisi kuimarisha matumizi ya tovuti ya Swahilihub miongoni mwa watumiaji wake kwa kuwashawishi viongozi hao mashuhuri miongoni mwa watumiaji wa lugha ya Kiswahili ambao ndio wanaoendeleza na kusambaza uvumbuzi miongoni mwa washika dau wengine katika taaluma ya Kiswahili. Katika mchakato wa msambao wa uvumbuzi, vyombo vya habari huchangia pakubwa katika hatua ya uhamasisho kwa kuwa vina hadhira pana na hivyo basi huweza kuathiri mielekeo ya wanajamii kwa kiasi fulani.

Ukuzaji wa Kiswahili kwa mujibu wa Clement (2010) ni hatua zote za upanuzi na ueneaji wa matumizi ya Kiswahili. Ukuzaji wa Kiswahili, kwa msingi huu wa vyombo vya mawasiliano na mitagusano, ulikadiriwa pale ambapo mitaguasno miongoni mwa watumiaji wa Swahilhub kwa msaada wa vyombo vya mawasiliano inapowawezesha watumiaji wengi kutagusana kwenye tovuti ya Swahilihub ili kuimarisha ujenzi wa Kiswahili, usambaaji wake na hadhi na dhima yake kupaa juu. Isitoshe mitagusano hii inapopelekea watumiaji wengi kuitumia Swahilihub huyafikia malengo ya ukuzaji kwa kupanua mawanda ya matumizi yake kimisamiati, kieneo na kiwakati. Hatua hii ni muhimu sana katika ukuzaji wa Kiswahili mitandaoni.

Kwa upande mwingine, Rodgers (2003) anadai kwamba mitagusano ya kibinafsi huchangia pakubwa kuathiri misimamo na mielekeo mikali miongoni mwa wanajamii. Mitagusano hii huelekezwa na viongozi mashuhuri katika jamii. Kwa mujibu wa Greg (2003) uhusishwaji wa viongozi mashuhuri huchangia pakubwa katika kuathiri maamuzi ya wanajamii wanaotegemea sana ushauri wa viongozi hawa. Katika mahusiano ya kiheterofilia, msambao wa uvumbuzi ni rahisi kwani viongozi hawa huwaelekeza wanajamii ambao kwa sababu ya kuwa na sifa na imani tofauti, huchangamkia uvumbuzi kwa urahisi. Hata hivyo, katika mazingira ya mitagusano ya kihomofilia, ni vigumu sana kueneza uvumbuzi kwa sababu ya ile hali yao ya kujibana kwenye mawanda finyu katika jamii yao.

Upeo wa msambao wa Swahilihub ni wakati ambapo ukubalifu wake miongoni mwa watumiaji wake hufikia kilele chake. Upeo huu wa msambao wa uvumbuzi hufikiwa kwa kuwahusisha watumiaji wake walio na ushawishi mkubwa kuwaelekeza wengine katika kuikubali na kuitumia tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili mtandaoni. Hivyo basi, kutokana na upeo huu, utafiti huu ulibaini wadau na asasi muhimu katika utendakazi wa tovuti ya Swahilihub miongoni mwa watumiaji wake

walio na ushawishi mkubwa wa kuimarisha matumizi na ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kwenye mradi wa Swahilihub. Hii ilitokana na uwezo wa mitagusano ya kiheterofilia miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub kuimarisha msambao wa mradi wa Swahilihub miongoni mwa wataalamu wote wa Kiswahili.

Aidha, vyombo vya habari katika msambao wa uvumbuzi vilichangia pakubwa katika kutoa mapendekezo na kusambaza matokeo kutokana na uwezo wake mkubwa wa kuwashawishi wadau wengi wa Kiswahili. Vyombo vya habari kama vile kampuni ya *Nation Media*, magazeti ya *Taifa Leo* nchini Kenya na *Mwananchi* nchini Tanzania, vina nafasi kubwa ya kuchangia kuhamasisha wapenzi wa lugha ya Kiswahili kuhusu ustahilifu na ubora wa tovuti ya Swahilihub kama uvumbuzi unaoweza kuijenga taaluma ya Kiswahili. Uhamasisho ni kigezo muhimu katika usambaaji na udumishaji wa hadhi na dhima ya lugha ya Kiswahili miongoni mwa watumiaji wa Swahilihub. Kwa njia hii nadharia ya Msambao wa Uvumbuzi ilikuwa dira ya kukadiria namna ukuzaji wa Kiswahili ulivyojitokeza katika matumizi ya Swahilihub katika michakato ya ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kwenye vitengo mbailmbali vya Swahilihub.


**c) Muda wa Msambao wa Uvumbuzi**

Mhimili wa tatu ni muda wa msambao wa uvumbuzi katika mfumo mahsusi wa kijamii. Mchakato mzima wa ubwiaji wa uvumbuzi kuanzia uhamasisho, ushawishi, uamuzi, utekelezaji na hatimaye udhibiti huchukua muda fulani na hutokea katika mfumo mahususi wa kijamii. Mfumo wa kijamii hujumuisha hali na mambo mbalimbali yanayotagusana miongoni mwa wanajamii ili kuyafikia malengo fulani mahususi. Ni jumla ya yale yanayotokea katika mazingira maalum na ambayo huathiri kasi na uwezo wa wanajamii kuukubali uvumbuzi katika jamii. Ili kuuwekea utafiti huu mipaka ya kiwakati kwa kuzingatia kigezo cha muda, tathmini ya Swahilihub ilijikita katika kipindi cha miaka mitano ya matumizi na ukuzaji wa Kiswahili kwenye mradi wa

Swahilihub nchini Kenya kuanzia mwaka wa 2014 hadi 2019. Kigezo hiki cha muda wa msambao kilielekeza utafiti huu kuangazia hatua mbalimbali za ukuzaji wa Kiswahili katika kipindi cha miaka mitano tu. Haya yalitokana na machukulio kwamba kipindi hiki kilisheheni ubwiaji mwingi wa Swahilihub na kutoa mchango mkubwa katika ukuzaji Kiswahili.

**d) Msambao wa Uvumbuzi katika Mfumo mahsusi wa Kijamii**

Mchakato wa msambao wa uvumbuzi hutokea katika hatua nne kuu: uhamasisho, ushawishi, uamuzi na udhibiti (Rodgers, 2003). Hatua hizi hufuatana katika hali inayotokea muda fulani.




*Mchoro SURA YA KWANZA .1: Mchakato wa Msambao wa uvumbuzi*

Hatua ya kwanza katika mchakato wa msambao wa uvumbuzi ni ile ya uhamasisho. Katika hatua ya uhamasisho, mwanajamii hutambua uvumbuzi kwa kugundua uwepo wake na kujaribu kubaini ni uvumbuzi wa aina gani, kwa nini uvumbuzi huo upo na hufanya kazi kwa njia gani. Katika hatua hii, mwanajamii hutambua uwepo wa uvumbuzi, hujifunza jinsi ya kuutumia uvumbuzi ule na hatimaye hujifunza kanuni zinazoongoza katika utendakazi wa uvumbuzi husika. Ili kubuni dhana mpya, teknolojia mpya yastahili kuandamana na maelezo ya njia ya kuitumia na ufahamu wa namna inavyofanya kazi. Katika kusambazwa, lugha za walengwa hutiliwa maanani ili teknolojia hiyo ikubalike na wanajamii wa lugha hiyo. Katika mchakato wa msambao wa uvumbuzi, vyombo vya habari huchangia pakubwa katika hatua ya uhamasisho kwa kuwa hufikia hadhira pana na hivyo basi huweza kuathiri mielekeo ya wanajamii kwa kiasi fulani.

Hatua ya pili inahusu ushawishi unaotokea wakati ambapo mwanajamii ana mielekeo chanya au hasi kuhusu uvumbuzi. Ingawa kuna mielekeo mbalimbali katika hatua hii, mielekeo hiyo haimwelekezi moja kwa moja kuukataa au kuukubali uvumbuzi husika. Ushawishi ni hatua muhimu inayofuata uhamasisho kwenye mchakato wa msambao wa uvumbuzi. Ushawishi wa wanajamii na viongozi mashuhuri huchangia pakubwa katika hatua hii (Sherry, 1997).

Uamuzi ni hatua ya tatu. Hapa ndipo mwanajamii anapoamua kuukubali au kuukataa uvumbuzi. Iwapo uvumbuzi una nafasi ya kujaribiwa kabla ya kukubaliwa basi husambaa haraka sana kwani watu wengi hupenda kuufanyia uvumbuzi majaribio ndipo waukubali. Hata hivyo kuna uwezekano wa uvumbuzi kukataliwa katika hatua yoyote (Rodgers, 2003). Kuna aina mbili za kukataa uvumbuzi. Kwanza ni kuutema kabisa ambao hutokea baada ya mwanajamii kuukubali na kuujaribu uvumbuzi kisha baadaye kuamua kuutema.

Pili ni kudinda ambapo mwanajamii huukataa uvumbuzi kabisa bila hata kuujaribu kidogo mwanzoni (Rodgers, 2003).

Utekelezaji ni hatua ya nne ambapo mwanajamii huutumia uvumbuzi ingawa kuna haja ya kuendelea kujifunza na kuelekezwa kuhusu matumizi ya uvumbuzi husika. Katika hatua hii, uvumbuzi unaweza kuhuishwa upya na kupata mabadiliko yanayouboresha zaidi.

Hatimaye kuna hatua ya udhibiti ambapo maamuzi ya matumizi na utekelezaji yametokea lakini msisitizo hapa ni kwamba kuna haja ya wanajamii wengine kutiana moyo kuhusu maamuzi ya kuukubali uvumbuzi husika. Katika hatua hii mwanajamii anaweza kuukataa uvumbuzi kwa sababu ya kubadilisha na kutumia uvumbuzi mwingine bora kwa kukosa kupata manufaa aliyoyatazamia. Dhana ya utokeaji wa msambao wa uvumbuzi katika hatua mahususi ilielekeza utafiti huu katika ukusanyaji wa data, uchanganuzi wake na uwasilishaji wa matokeo ya tathmini ya utendakazi wa tovuti ya Swahilihub. Aidha mchakato wa msambao wa uvumbuzi ulisaidia pakubwa katika kubaini mchango wa vyombo vya habari na pia kutoa mapendekezo kuhusu nafasi ya vyombo hivyo katika kuimarisha matumizi na makuzi ya Kiswahili miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub nchini Kenya.

### 1.8.2 Nadharia katika Utafiti na Ukuzaji wa Kiswahili

Ukuzaji wa Kiswahili ni mchakato ambao hautokei kwenye ombwe tupu bali huchukuana na kuendana na maendeleo ya kitaifa. Kadri msambao wa uvumbuzi ulivyo mchakato unaotokea katika hatua mahususi, ndivyo ukuzaji wa Kiswahili ulivyo mchakato wala sio tukio. Ukuzaji wa Kiswahili umetokea kwa hatua mbalimbali na viwango mbalimbali katika nyakati na vipindi mbalimbali mahususi. Kumekuwepo ukuzaji wa Kiswahili wa

kipindi cha kabla ya ujio wa mitandao uliosheheni maandishi mengi kwenye vitabu, majarida na makala mbalimbali. Ukuzaji huo ulifanikiwa zaidi kwa kuwekwa katika hati za maandishi ambayo yaliipa lugha ya Kiswahili umbo la kudumu la kukaa hata karne nyingi. Mabadiliko ya kiteknolojia yamelazimu hatua kama hizo za awali kuchukuliwa ili lugha ya Kiswahili iwe na taswira hiyo au bora zaidi mtandaoni.

Nadharia ya Msambao wa Uvumbuzi ilielekeza utafiti huu kwa kuangazia ukuzaji wa Kiswahili kama mchakato unaotokea katika kipindi maalum na huathiriwa na mabadiliko mbalimbali katika jamii yakiwemo yale ya kiteknolojia yanayoelekea kuwepo kwa uvumbuzi katika kila sekta ya maisha. Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili ni uvumbuzi ulio na sifa za uvumbuzi zilizobainishwa na Rodgers (2003) kama vile: manufaa kwa watumiaji wake, uwiano na mahitaji ya watumiaji wake, ugumu au uarahisi wake kimatumizi na uwezekano wake wa kukuza faida za ukuzaji wa Kiswahili kwa muda mahususi.

Ukuzaji kwa mujibu wa Clement, (2010) ni jumla ya hatua zinazochangia ueneaji na ukuaji wa Kiswahili na kuelekea kupatikana kwa usambaaji wa Kiswahili, ujenzi wake na udumishaji wa hadhi na dhima yake kutokana na mitagusano inayotokea kwenye vyombo mbalimbali vya mawasiliano. Vigezo hivi vya ukuzaji wa Kiswahili vinajitokeza katika mihimili ya nadharia ya Msambao wa Uvumbuzi ya Rodgers (2003). Kwa kuangazia mhimili huu wa vyombo vya mawasiliano na mitagusano, nadharia ya msambao wa uvumbuzi inabainisha vigezo vya ukuzaji wa Kiswahili kama vile usambaaji wake na udumishaji wa dhima yake. Dhima ya Kiswahili inahusisha majukumu yake katika jamii kama vile kuwa lugha ya taifa, lugha ya mawasilaiano mapana pamoja na lugha ya madola. Kwa mujibu wa Mbatiah na wegine (2013) ukuzaji wa Kiswahili hubainika kutokana na udumishaji wa hadhi na dhima yake kwa msingi wa kuwajibikia dola kwa

kubuni sera zifaazo kukiwezesha kutumika kama lugha ya taifa na lugha rasmi. Kigezo hiki kinabainika wazi katika mhimili wa vyombo vya mawasiliano na mitagusano katika nadharia ya Msambao wa Uvumbuzi wa Rodgers (2003). Nadharia ya Msambao wa Uvumbuzi inaegemeza ukuzaji wa Kiswahili kwenye vigezo vyake muhimu vya ujenzi wake, usambaaji wake na udumishaji wa hadhi na dhima yake katika jamii. Dhima ya lugha ni suala la kisera linalotegemea mikakati, kauli na mipango ya serikali mbalimbali kuhusu nafasi ya Kiswahili katika shughuli mbalimbali za kisiasa, kielimu, kiuchumi na kiutamaduni.

Ingawa watafiti kadhaa wameitumia nadharia ya Msambao wa Uvumbuzi ya Rodgers (2003), si wengi miongoni mwao ambao wameitumia kuchunguza mitandao na tovuti katika shughuli za ufundishaji (Ismail, 2006). Kwanza, nadharia ya awali ya msambao wa uvumbuzi ya Rodgers (1995), ilielekeza utafiti wa Anderson na wengine (1998) uliohusu mielekeo, stadi na mienendo ya wahadhiri kuhusu matumizi yao ya TEHAMA katika Chuo Kikuu cha Canada. Anderson na wengine (1998) kwa kutumia vigezo vya Rodgers (1995) vya uainishaji wa wabwiaji wa uvumbuzi, waliwagawa wahadhiri katika makundi makuu mawili: wabwiaji awali wa uvumbuzi na wavumbuzi wengine.

Katika ugunduzi wao Anderson na wengine (1998) walieleza mikakati muhimu ya kupunguza tofauti katika viwango vya matumizi ya TEHAMA kati ya wabwiaji awali wa uvumbuzi na wavumbuzi wengine. Waligundua kwamba ingawa kundi la wavumbuzi wengine lilitumia TEHAMA katika shughuli zao za mawasiliano na katika michakato yao ya kitaaluma, hawakuseta matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji wao. Walipendekeza kwamba ili kuimarisha ukubalifu wa TEHAMA katika ufundishaji, ni muhimu kuimarisha motisha na mafundisho kwa kutumia TEHAMA. Ingawa utafiti wa Anderson na wengine (1998) uliegemezwa kwenye mihimili ya nadharia ya awali ya msambao wa uvumbuzi ya

Rodgers (1995), nguzo zake muhimu, zinazoibua na kujenga nadharia ya Rodgers (2003), zilichangia kuweka msingi wa kimaandishi ambayo yalikuwa kama dira kwa utafiti huu katika kutathmini mradi wa Swahilihub katika matumizi na ukuzaji wa Kiswahili miongoni mwa watumiaji wake nchini Kenya.

Blankenship (1998), akitumia nadharia ya awali ya Msambao wa Uvumbuzi ya Rodgers (1995) aliangazia mambo yaliyohusiana na matumizi ya tarakilishi katika ufundishaji katika Chuo Kikuu cha Virginia, Marekani. Katika utafiti wake alichunguza mielekeo kuhusu tarakilishi, upatikanaji wa tarakilishi, mafundisho kuhusu matumizi ya tarakilishi, umri, tajriba, jinsia, viwango vya elimu na mitaala. Vibadala hivi vyote vilihusishwa katika kuchangia matumizi ya tarakilishi katika ufundishaji. Hatimaye Blankesnship alitoa mapendekezo ya mikakati ifuatayo ya kuboresha ufundishaji kwa matumizi ya tarakilishi: mafundisho kuhusu matumizi ya tarakilishi katika ufundishaji kwa kuzingatia mitaala na viwango vya wanafunzi, uimarishaji wa stadi na maarifa ya wahadhiri katika matumizi ya tarakilishi na ujenzi wa maabara ya tarakilishi ili kupanua miundo-mbinu husika.

Matokeo ya utafiti huu yalichangia kubainisha maswala muhimu katika maendeleo ya kiteknolojia yaliyoweka msingi wa tathmini ya mradi wa Swahilihub katika matumizi na ukuzaji wa Kiswahili miongoni mwa watumiaji wake mtandaoni. Miongoni mwa maswala hayo yalikuwa changamoto zinazokabili teknolojia na mustakabali wake.

Surendra, (2001) aliangazia vigezo vya msambao wa uvumbuzi vya Rodgers (1995) na maoni ya wanazuoni wengine ili kubainisha ukubalifu wa matumizi ya teknolojia ya mitandao miongoni mwa maprofesa wa Chuo Kikuu cha Toronto, Ontario. Aligundua kwamba mafundisho ya matumizi ya mitandao, upatikanaji na aina mbalimbali za TEHAMA ndizo nguzo za msambao wa uvumbuzi zilizo muhimu katika usetaji wa

mitandao miongoni mwa maprofesa na wanazuoni wengine. Matokeo ya utafiti huu yalichangia kubainisha nguzo za nadharia ya msambao wa uvumbuzi kwa kuweka wazi namna nguzo hizo zilivyoimarisha matumizi ya teknolojia kama uvumbuzi mpya miongoni mwa wadau wa elimu. Matokeo ya utafiti huu yalikuwa marejeleo muhimu katika utafiti huu kwa kuchangia nyongeza kubwa ya maandishi yaliyokuwa dira muhimu katika kutathmini utendakazi wa mradi wa Swahilihub.

Aidha, Njihia (2005), alitumia nadharia ya msambao wa uvumbuzi ya Rodgers (2003) kuelekeza utafiti kuhusu matumizi ya Kiswahili katika tarakilishi. Alishughulikia miradi kama vile mradi wa Microsoft East Africa, mradi wa kugeuza matini za Kiswahili hadi usemi na mradi wa injini pekuzi ya Kiswahili katika mtandao. Utafiti huu ulijadili kwa kina juhudi mbalimbali za awali za matumizi ya teknolojia katika maendeleo ya taaluma ya Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yalitahadharisha mwelekeo wa utafiti huu wa mradi wa Swahilihub kwa kubainisha ufaafu, nguzo na udhaifu wa nadharia ya Rodgers (2003).

Nadharia ya Msambao wa Uvumbuzi ya Rodgers (2003) ilichangia pakubwa katika kuelekeza utafiti wa Moraa (2012) uliolenga kuweka wazi mbinu zilizotumika katika kuzalisha msamiati kwenye Mradi wa Microsoft. Shughuli muhimu aliyozingatia ilikuwa ni ile ya leksikolojia na leksikografia katika kutekeleza mahitaji ya lugha yo yote ile. Hata hivyo, hakuweza kuonyesha namna ambavyo matokeo ya mradi wa Microsoft East Africa yanavyoweza kutumiwa kwenye tovuti za Kiswahili ili kuendeleza taaluma ya Kiswahili. Utafiti huu uliifaa tathmini ya mradi wa Swahilihub kwa kuweka wazi matumizi ya istilahi mwafaka za kiteknolojia katika lugha ya

Kiswahili ambazo zilitumika katika utafiti huu uliobainisha matumizi na ukuzaji wa Kiswahili miongoni mwa watumiaji wa Swahilihub nchini Kenya.

## 1.9 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulitathmini Swahilihub katika ukuzaji Kiswahili uliotokana na ujio wa mitandao na mabadiliko ya kidijitali nchini Kenya.Ukuzaji huu uliegemezwa kwenye teknolojia kama mkakati wa ukuzaji kwa kuhifadhi na kuikuza lugha ya Kiswahili kiisimu na kifasihi. Ingawa kumekuwa na juhudi za awali za ukuzaji wa Kiswahili katika kipindi cha kabla ya ujio wa tovuti, utafiti huu ulilenga juhudi mahususi za ukuzaji wa Kiswahili mtandaoni. Hivyo basi, utafiti huu ulikusudia kuangazia ukuzaji wa lugha ya Kiswahili katika kipindi cha ujio wa mitandao ya kijamii na hususan kwenye tovuti ya Swahilihub. Isitoshe, utafiti huu ulitathmini utendakazi wa Swahilihub kwa misingi ya mfumo wake, urahisi wake kimatumizi na uamilifu wake kimatini. Sababu ilikuwa kwamba ni vipengele hivyo ambavyo huchangia pakubwa kuathiri mitagusano ya watumiaji wa tovuti ya Swahilihub na kuchangia pakubwa kuimarisha ukuzaji Kiswahili.

Aidha kuna aina nyingi za programu za kiteknolojia zinazotumika katika kutathmini na kuchangnua ufanisi wa tovuti mbalimbali. Miongoni mwa programu hizi ni kama vile Alexa, ARhefs, Similar web, Progressive web application miongoni mwa zingine. Utafiti huu uliteua na kutumia ARhefs na Similar web katika kutathmini utendakazi wa tovuti ya Swahilihub kwa sababu aina hizi ziliangazia kwa ukamilifu vigezo muhimu vya tathmini ya Swahilihub.

Ingawa Swahilihub hutumiwa katika mataifa mengi kote ulimwenguni, utafiti huu haungeangazia matumizi na ukuzaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa watumiaji wake katika mataifa hayo yote. Hivyo basi utafiti huu ulijikita katika kutathmini matumizi na ukuzaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa watumiaji wa Swahilihub nchini Kenya pekee. Utafiti huu uliwahusisha wahadhiri na wanafunzi wa baadhi ya vyuo vikuu nchini

Kenya pamoja na wafanyakazi na wahudumu wa *Nation Media* jijini Nairobi ili kuhakikisha kuwa hali halisi katika elimu ya juu ya matumizi na ukuzaji wa Swahilihub inabainishwa miongoni mwa watumiaji wa Swahilihub. Aidha utafiti huu ulijikita katika kipindi cha miaka mitano ya utendakazi wa tovuti ya Swahilihub ambapo michakato ya utafiti ilikuwa ikiendelea. Michakato ya utafiti huu iliangazia juhudu za Swahilihub zilizotokea tangu mwaka wa 2014 hadi 2019.

## 1.10 Hitimisho

Sura hii imeyabaini na kuyafafanua masuala ya kimsingi katika utafiti huu na ambayo yaliongoza utafiti kutoka mwanzo hadi mwisho. Mambo haya ni pamoja na usuli wa utafiti, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, misingi ya uteuzi wa mada, nadharia ya utafiti na upeo na mipaka ya utafiti.

# SURA YA PILI

# UHAKIKI WA MAANDISHI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii imeshughulika na maelezo kuhusu masuala mbalimbali yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti. Tulihakiki maandishi tuliyochukulia kama nguzo muhimu ya utafiti huu. Masuala haya muhimu yalibainisha tovuti ya Swahilihub katika upekee wake kitaaluma. Tumehakiki maandishi na kutoa maelezo kuhusu ukuzaji wa lugha, TEHAMA katika ukuzaji wa lugha, ukuzaji wa Kiswahili nchini Kenya na Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Haya yalifanywa ili kuliweka suala la utafiti wazi zaidi kwa kubainisha pengo la utafiti huu.

## 2.2 Malengo ya Tovuti ya Swahilihub

Swahilihub ni tovuti inayolenga kuikuza lugha ya Kiswahili mtandaoni. Kwa mujibu wa Choudhury (2014), tovuti ni mfumo wa matini zilizounganishwa kwenye jukwaa mahsusi ili kufikiwa na watumiaji wa jukwaa hilo kwa msaada wa mtandao wa intaneti. Tovuti huwawezesha watumiaji wake kusoma matini ambayo yamehusisha maandishi, picha, video miongoni mwa matini mengine (Choudhury, 2014). Tovuti ni chombo muhimu cha kijamii kinachohifadhi habari muhimu mtandaoni. Dhana ya tovuti kuwa chombo cha kijamii imetolewa ufafanuzi na wataalamu mbalimbali kwa kueleza maana ya vyombo vya habari vya kijamii.

Katika mwaka wa 2012, Kampuni ya *Nation Media*, kwa kuzingatia umuhimu wa taaluma ya Kiswahili, ilibuni tovuti ya Swahilihub kwa tafsiri ya Kitovu cha Kiswahili. Swahilihub ni Kitovu cha Kiswahili inayoendesha magazeti yake makuu ya Kiswahili *Taifa Leo* la

Kenya na *Mwananchi* la Tanzania. Ni kitovu kikubwa sana cha Kiswahili kote ulimwenguni. Mtandao huu unawaunganisha wasemaji, wasomi, wapenzi wa Kiswahili, wakereketwa wa Kiswahili, walimu na wanafunzi na hata taasisi za Kiswahili katika tovuti ambayo ni Kitovu cha Kiswahili. Kwa hivyo, Swahilihub huwezesha watumiaji wa Kiswahili kusakura na kusoma ili kuikuza lugha ya Kiswahili kwa ujumla. Lugha ya Kiswahili imetamba katika nyanja za teknolojia ya habari na mawasiliano na hivyo basi kudumisha hadhi na dhima yake kote ulimwenguni.

Kuanzia mwaka wa 2013 hadi mwaka wa 2014, tovuti ya Swahilihub iliendeleza shughuli zake katika ukurugenzi wa kampuni ya *Nation Media* Nairobi nchini Kenya. Mwishoni mwa mwaka wa 2015, ukurugenzi wa Swahilihub ulihamishwa hadi Dar-essalaam katika ofisi ya kampuni ya Mwananchi Communications Limited kwenye gazeti la *Mwananchi*, nchini Tanzania (Maina, 2016). Nchini Kenya, katika kampuni ya Nation Media Group kulikuwa na kitengo cha Swahilihub ambacho kilitumia gazeti la *Taifa Leo* kukuza taaluma ya Kiswahili (Maina, 2016). Tovuti ya Swahilihub ina vitengo vikuu vifuatavyo: Mwanzo, Habari, Jifunze Kiswahili, Blogu Na Ukumbi, Maktabani Jisomee, picha, video na Makala (Wamalwa, 2016). Malengo ya Swahilihub ni kukusanya kuhifadhi na kuwezesha kupatikana kwa matini ya Kiswahili katika mtandao kwa lengo la ukuzaji wa Kiswahili. Tovuti ya Swahilihub ni hazina kubwa iliyo na manufaa kwa taaluma ya Kiswahili. Swahilihub ina fani mbalimbali za lugha ya Kiswahili kama vile hadithi, mashairi, tenzi, sarufi, vitendawili, methali, semi, ripoti za utafiti mbalimbali na tasnifu za Kiswahili zilizowahi kuchapishwa (Maina, 2016).

Tovuti ya Swahilihub ambayo ni jukwaa la kimtandao ina nafasi kubwa ya ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili na kuboresha mbinu mbalimbali zinazotumiwa katika michakato ya

elimu ya Kiswahili (Maina, 2016). Swahilihub imekuwa ni kama 'mtu wa kati' kwani ni kiungo kati ya mwandishi wa makala, tasnifu au uchunguzi fulani na mtumiaji wake kwa maana ya taasisi kama vyuo, kampuni ya matangazo ya redio au runinga (Wamalwa, 2016; Maina, 2016). Swahilihub ina nafasi muhimu katika ukuzaji wa taaluma za Kiswahili. Lengo kuu la Swahilihub kama mtandao ni kuweka matini faafu kwa ajili ya watumiaji wake. Madhumuni yake ni kuwapa mtandaoni watumiaji wake habari wanazohitaji kwa muda unaofaa na kwa urahisi.

Kwa mujibu wa Clement, (2010) ukuzaji wa lugha ni hatua zinazochukuliwa ili lugha hiyo iweze kutumiwa na watu wengi zaidi na watu hao waweze kuihusisha lugha hiyo katika shughuli mbalimbali za kila siku. Ukuzaji wa lugha ni jumla ya ukuaji na ueneaji wake (Mutiso, 2014). Ukuaji humaanisha ongezeko la msamiati katika lugha mahususi huku ueneaji ni uongezekaji wa matumizi yake kieneo na kiwakati. Lugha isiyotumika au kutumiwa huvia na hatimaye hutoweka na hufa. Lugha inayotumiwa hukua na kustawi kulingana na mahitaji ya mawasiliano yaliyomo katika jamii husika. Mawasiliano ya lugha huwa nyenzo kuu katika kufanikisha shughuli za binadamu – iwe ni za kiuchumi au kisiasa, kijamii, kiutamaduni, kifasihi, kiroho, kiteknolojia, kisayansi, kielimu na kadhalika. Katika mchakato wa kukidhi mahitaji ya mawasiliano hayo, msamiati na istilahi zake hupanuka, aina mbalimbali za uzungumzaji na matumizi yake huchipuka, huchochea ubunifu katika tasnia anuwai kama vile katika sanaa za lugha na maonyesho, uvumbuzi na ugunduzi wa kisayansi na kiteknolojia, utawala na siasa, usalama na ulinzi, uzalishaji, afya bora, elimu bora na kadhalika. Vilevile, ustawi wa jamii huweza kuakisi na kusawiri ukuaji wa lugha husika.

Katika utafiti huu dhana ya ukuzaji wa lugha imesheheni jitihada mbalimbali za ukuaji na ueneaji wake miongoni mwa watumiaji wake. Ukuzaji wa lugha umejengwa kwa nguzo

kuu tatu: ujenzi wa lugha kwa misingi ya maandishi yake mapana, uundaji wa istilahi zake, ufafanuzi wa sarufi yake na uundaji wa kamusi; usambaaji wa lugha kulingana na mahitaji ya walengwa mtandaoni pamoja na udumishaji wa hadhi yake katika jamii (Cooper, 1990).

Katika sehernu nyingi duniani ukuzaji wa lugha hutokea kupitia michakato ya ufundishaji wake. Aidha, mitandao ya kijamii inatumiwa kama vifaa vya ukuzaji wa lugha kwa kufundishia masomo mbalimbali. Matumizi ya mitandao ya kijamii yanaoana na suala la uwiano wa uvumbuzi kama msingi muhimu katika nadharia ya Msambao wa Uvumbuzi (Rodgers, 2003). Hii ni kwa sababu walimu na wanafunzi wa lugha hutumia mitandao hii katika shughuli zao za kiakademia. Hata hivyo, mitandao ya kijamii kama uvumbuzi wowote ina manufaa na madhara, na kwa hivyo kuna haja ya kulifikiria suala hili kuhusu kinachoshirikishwa na madhara yake kwa watu wengine kabla ya kuanza kuunda na kupakia maudhui mtandaoni. Unachokichapisha na maudhui unayopakia yatakuwakilisha mtandaoni. Hii pia inajulikana kama sifa ya tarakilishi.

Kulingana na mtandao wa Alexa.com, nchini Kenya mtandao ambao huwavutia mamilioni ya watu ulitumika kwa mara ya kwanza katika mwaka wa 1993. Kuna mitandao mbalimbali kama vile: Facebook, Twitter, LinkedIn, Olx, Blogu na Google. Mitandao ya Facebook, Olx na Twitter ndio maarufu sana na hutumiwa na watu
mbalimbali kwa shughuli tofauti tofauti kama vile: biashara, utangazaji, elimu na siasa. Katika mwaka wa 2008, mtandao wa Facebook ulikuwa na washiriki milioni mia sita. Kufikia Machi 2013, waliotumia mtandao kote duniani kila siku walikuwa bilioni moja. Kwa upande wa Twita washiriki ni milioni mia tano (Gazeti la Daily Nation 2, 17 Juni 2014).

## 2.3 TEHAMA katika Ukuzaji Lugha

Ujenzi wa lugha ni nguzo ya kwanza ya ukuzaji wake. Mutiso, (2014) anarejelea ujenzi wa lugha kama ukuaji wake kumaanisha ongezeko la msamiati katika lugha. Lengo la ujenzi wa lugha hujumuisha mambo mbalimbali kama vile, uingizaji wake katika maandishi pale ambapo haipo kwenye maandishi, uundaji wa istilahi, ufafanuzi wa sarufi yake na uundaji wa kamusi. Mchipuko wa mitandao mbalimbali umebadili namna asasi mbalimbali zinavyoendeleza mawasiliano yao na mitagusano katika kuyafikia malengo yao. TEHAMA ni njia moja ya kufikia hadhira kubwa kupitia majukwaa ya kimtandao kama vile barua pepe, injini pekuzi ya Google, mitandao ya kijamii na tovuti anuwai (Owoche, 2019). Tovuti ni wenzo wa kipekee wa mawasiliano mtandaoni ulio na uwezo wa kuwafikia watumiaji wengi ili kukamilisha madhumuni mahususi.

Matumizi ya mitandao ya kijamii yameenea kote ulimwenguni na asilimia 67 wanatumia mitandao katika shughuli zao za kila siku (Nielson, 2009). Taaluma ya Kiswahili ina hadhira kubwa kote ulimwenguni inayohitaji kufikiwa kupitia majukwaa ya kimtandao katika juhudi za ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kote ulimwenguni. Mitandao ya kijamii ni aina ya teknolojia ya kielektroniki inayorahisisha mawasiliano na mahusiano ya watu kwenye mtandao na huweza kutokea kupitia kwa matumizi ya tarakilishi au teknolojia ya simu. Mtandao ni mfumo wa kushirikiana kwa kompyuta mbalimbali kote duniani unaowezesha kompyuta hizo kuwasiliana kati yazo. Kupitia mtandao huu watu wanaweza kutembelea tovuti mbalimbali kwa ajili ya shughuli za kila siku kama vile: biashara, masomo, siasa, dini na uchumi (William na wengine 2009).

Tangu kuasisiwa kwake na Tim Burner-Lee katika mwaka wa 1989, tovuti imepitia mabadiliko mengi katika hatua kuu tatu. Hatua ya kwanza ilihusisha kupatikana kwa

matini kwenye tovuti ambayo ingesomeka tu bila kutumiwa kwa njia yo yote ile. Hatua hii ya kwanza ilishamiri kwa kuanzia mwaka wa 1989 hadi mwaka wa 2005 (Choudhury, 2014). Katika hatua hii lengo kuu la tovuti hizi lilikuwa ni kuweka matini kwa ajili ya watumiaji ili kupatikana mtandaoni na kudhihirisha uwepo wa matini ya kimsingi kuhusu asasi fulani mtandaoni (Silva na wengine, 2008). Tovuti hii iliyorejelewa kama tovuti 1.0. ilidhihiri mawasiliano ya upande mmoja kutoka kwa matini mtandaoni ambayo hayakuwezeshwa kiteknolojia kupokea mrejesho kutoka kwa watumiaji wa tovuti husika mtandaoni. Ni kutokana na udhaifu huu ambapo maendeleo mapya yalichangia kubuni tovuti mpya ya 2.0 iliyobeba matini iliyosomeka na kushirikisha maandishi yaliyoimarisha matini yake. Tovuti katika hatua hii ziliundwa na kuratibiwa kuimarisha mawasiliano na kushirikisha matini kwa urahisi miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya 2.0 (Harris na Rea, 2009).

Hatimaye kukawa na hatua ya tatu ambapo kwa sasa pana uwezekano wa kusoma, kuandika na kutekeleza majukumu mahususi kwenye mtandao kutegemea mahitaji ya watumiaji mbalimbali wa tovuti husika. Hatua hii inarejelewa kama tovuti 3.0 ambayo pia hurejelewa kama tovuti ya kisemantiki. Tovuti ya kisemantiki inahusisha sifa za tovuti za 1.0 na 2.0 na kuzuka na jukwaa la kisemantiki linaloruhusu tarakilishi kutangamana na matini kwa ajili ya kuyakidhi mahitaji mahususi ya watumiaji tofauti wa mtandao husika. Tovuti ya kisemantiki kimsingi ina uwezo wa kubuni, kusambaza na kuchanganua matini kwenye mtandao kwa njia inayozingatia lengo na mahitaji mahususi ya watumiaji wa tovuti hiyo (Hogan, 2014). Tovuti ya kisemantiki huruhusu watumiaji wake kusikiliza, kujifunza na kuingiliana ipasavyo na matini kwa njia inayowawezesha kuyakidhi mahitaji yao mtandaoni.

Tovuti za kisemantiki zina uwezo wa kutambua na kufasiri matini kwenye mtandao kiasi kwamba inakuwa rahisi kwa injini pekuzi kama vile, Google, Yahoo, Microsoft au Yandex, kutafuta na kuzipata habari hizo na kuwaelekeza kwa urahisi watumiaji wanaohitaji habari hizo muhimu. Ili kuboresha utafutaji wa habari mahususi kwenye tovuti, muungano wa injini pekuzi kama Google, Yahoo, Microsoft, Bing na Yandex ulibuni 'Schema.org' kwa lengo la kuziwezesha kutambua na kufasiri habari kwenye matini za tovuti husika (Schema.org, 2018). Schema.org imechangia pakubwa kuimarisha upatikanaji wa matini kamili inayohitajika kuyakidhi mahitaji mahususi ya watumiaji wa tovuti husika (Campbell, 2014).

IIi kujiunga na mitandao yoyote ile katika michakato ya ukuzaji wa lugha, lazima utumie programu huria iliyo na msimbo chanzo ambao lugha huandikwa kwayo. Vivinjari vya mtandao kama vile Chrome na Firefox ni mfano wa programu huria ambazo unaweza kugeuza kutoka lugha moja hadi nyingine. Kwa mfano, kutoka Kiingereza hadi Kiswahili kama vile: • Wikipedia- kamusi huru • Google- injini pekuzi ya Google • Blog – blogu. Kupitia juhudi hizi za kimtandao imedhihirika kuwa lugha ya Kiswahili haijaachwa nyuma sana katika matumizi yake. Wataalamu mbalimbali wanafanya juhudi ili kuimarisha ukuzaji wa Kiswahili katika mitandao ya Facebook, Twita na Wikipedia.

Kwa mfano, kwa mujibu wa Kaplan & Heinlein (2010) vyombo vya habari vya kijamii hurejelea kikundi cha nyenzo za habari ambazo msingi wake umekitwa katika matumizi ya mtandao na kujengwa kwenye misingi ya tafkira na tovuti zinazotokana na teknolojia zinazoruhusu uumbaji na ubadilishanaji wa habari zilizozalishwa na mtumiaji. Nyenzo hizi hutoa mchango mkubwa kuimarisha juhudi za ukuzaji lugha. Weinberg (2009) naye anaeleza kuwa vyombo vya habari vya kijamii ni kifaa chochote ambacho mtumiaji anataka kiwe hususan kinachoweza kufikiwa kwa matumizi ya simu, tovuti na kinaweza

kuundwa upya na kutumika kila mara. Kwa mujibu wa utafiti huu, vyombo vya habari vya kijamii vinavyorejelewa ni tovuti miongoni mwavyo tovuti ya Swahilihub.

Asili ya mtandao ina mizizi katika mwongo wa 1960 wakati Marekani ilihusika katika vita vya maneno au propaganda. Mitandao ilianzishwa wakati wanajeshi walikuwa wanatafuta rnbinu za kusambaza habari nchini kote. Mtandao ni mfumo wa ulimwengu wa mitandao ya kompyuta na hutumia itifaki inayokubalika ya 'internet Suite; (TCP / IP) na inayotumikia mabilioni ya watumiaji duniani kote. TCP / IP ni mtandao wa mitandao ambayo ina mamilioni ya mitandao ya kibinafsi, ya umma, ya kielimu, ya biashara, na ya serikali yenye upana wa kimitaa na kiulimwengu. Kiswahili kimeweza kutumika kama lugha ya mawasiliano na kupiga hatua katika teknolojia hii ya mitandao. Ni bayana kuwa, lugha ya Kiswahili imekuwa lugha ya kimataifa ambayo inasornwa kwenye mitandao. Lugha ya Kiswahili pia ni chombo mwafaka cha kusambaza ujuzi wa kiteknolojia hasa katika maeneo yanayotumia lugha hii barani Afrika (Mohochi 2002).

Juhudi za TEHAMA katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili mtandaoni ni zao la hatua mbalimbali za wataalamu zinazolenga kuimarisha maumbo na miundo ya tovuti ili kuyafikia mahitaji ya watumiaji wake. Crystal (2004:10), katika kitabu chake *“Language and Internet”* amezungumzia kwa ujumla nafasi ya Iugha kwenye mtandao na athari za mtandao katika lugha. Amejadili matumizi ya vifupisho vya kimtandao katika Iugha ya Kiingereza. Kuna utafiti uliofanywa kama vile: Njihia (2005) aliyeshughulikia matumizi ya Kiswahili katika tarakilishi na kuzungumzia mradi wa Microsoft East Afrika kama mradi wa kugeuza matini za Kiswahili hadi usemi na kwa ufupi injini pekuzi ya Google. Mapendekezo ya utafiti huu yalichangia pakubwa katika kuboresha thamani ya matini inayoweza kuchangia michakato mbalimbali ya ujenzi, usambazaji na udumishaji wa

hadhi na dhima ya Kiswahili kwenye tovuti ya Swahilihub na hivyo basi kuchangia pakubwa katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili.

Naye Moraa (2012), akashughulikia matumizi ya Kiswahili katika mradi wa Microsoft East Afrika hasa mbinu za kuzalisha istilahi za Kiswahili katika mradi huo. Istilahi hizi ni wenzo muhimu katika kuimarisha thamani ya matini kwenye tovuti ya Swahilihub. Aidha, istilahi hizi zinatoa mchango mkubwa katika ukuzaji wa Kiswahili kwa kuimarisha ujenzi wake na kuzindua misamiati anuai. Vilevile Maina (2013), katika makala ya CHAKITA alizungurnzia makundi ya lugha na fasihi katika Facebook. Kwa kuwa facebook ni miongoni mwa majukwaa ya mrejesho kwenye tovuti ya Swahilihub, makala haya yanachangia pakubwa kwa kujenga kanzi ya istilahi muhimu katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kwa kuisambaza na kupanua wigo wa matumizi yake.

Ukuzaji wa lugha ya Kiswahili mtandaoni unategemea pakubwa athari za matumizi ya lugha mtandao unaorejelewa kama netspeak. Lugha mtandao hutoa mchango mkubwa wa kuimarisha taaluma ya Kiswahili mtandaoni. Batul (2009) katika utafiti wake anaeleza kuwa lugha mtandao “Netspeak” ina athari zake katika lugha mbalirnbali hasa katika enzi hizi ambazo asilimia kubwa ya vijana wanaturnia mitandao ya kijamii. “Netspeak” imeathiri sana maturnizi ya lugha ya Kiingereza. Athari hizi kwa lugha ya Kiingereza ni kigezo muhimu katika kubainisha mchango wa tovuti ya Swahilhub katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili mtandaoni. Anaendelea kusema kuwa utafiti mwingi haujashughulikia athari za lugha mtandao katika lugha mbalirnbali. Utafiti wake ulitufaa kwa vile umebainisha athari mbalimbali za lugha mtandao kwa lugha mbalimbali, jambo ambalo ni msingi mwafaka katika kuchunguza nafasi ya tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili. Pia utafiti huu umeweka msingi kuhusu athari za

“Netspeak” zinazoweza kuchangia kuimarisha taaluma ya Kiswahili. Lugha hii huitwa lugha mtandao “Netspeak' na watumiaji wanaitwa “Neticen” (Jelimo, 2015). Lugha mtandao “Netspeak” ilizuka ulimwenguni kote kutokana na majilio na athari za mapinduzi ya kielektroniki kufuatia matumizi ya teknolojia ya mawasiliano kwa kutumia kompyuta katika jamii zetu. Katika lugha ya Kiswahili “Netspeak” ni lugha mtandao. Ni lugha ambayo ni nyepesi kubadilika na yenye muundo unaowezesha mawasiliano kufanyika kwa haraka. Ilizuka kutokana na matumizi ya ujurnbe mfupi katika simu (Werry, 1996).

Lugha mtandao ni mbinu mpya ya kielektroniki ya mawasiliano ambayo imeibuka na hutumiwa kimataifa (Baron, 2004). Lugha hii imeenea zaidi hata kuliko teknolojia kumaanisha kuwa lugha mtandao ndio maarufu sana katika matumizi yake na kila uchao inabainika kuwa maneno mapya ya kimtandao yanazidi kuzuka na kuenea kote kote. Lugha mtandao imekuwa lingua franka ya kimtandao na hutumika sana katika mawasiliano. Imeweza kuathiri nyanja zote za maisha kama vile biashara, elimu, utangazaji wa habari na mawasiliano yasiyo rasmi. Pia ni mbinu mpya ya kielektroniki ya mawasiliano ambayo imeibuka na hutumiwa kimataifa (Crystal, 2006). Ni msamiati wa kimtandao na hujumuisha idadi kubwa ya matumizi ya maneno na virai. Lugha hii imezuka na hutumika sana katika lugha ya Kiswahili na lugha zingine. Kulingana na Hudson (2000), chanzo cha mabadiliko ya lugha mtandao ni kuonyesha maana mpya., Wanajamii wanapobadilika hata maneno katika lugha hubadilika. Anaendelea kusema kuwa sifa za uwazi ndizo huwezesha watu kuunda maneno mapya katika lugha ili kuonyesha mambo mapya, matukio na mawazo mbalimbali.

Kulingana na Kinsella (2010), hadi sasa wataalamu mbalimbali wameshindwa kupata dhana mwafaka ya kufafanua lugha mtandao. Wengine hueleza lugha mtandao kuwa ni

vishazi ambavyo vimefupishwa au ni maneno ambayo yamebadilishwa kifonetiki, kiishara au matumizi ya akronimu ili kutoa maana zaidi kwa watumiaji. Kwa hivyo lazima pawe na uelewa kati ya watumiaji wa lugha hii. Sababu hii ndiyo inayopelekea mtumiaji yeyote wa lugha mtandao kuwa na ufahamu wa ujumbe huo, maana yake na jinsi inavyotumiwa. Lazima awe na tajriba pana kuhusu lugha hii ili kukamilisha mawasiliano na ujumbe uliokusudiwa uweze kueleweka bila utata wowote. Lugha mtandao vilevile siyo maneno ambayo yamefupishwa pekee bali pia vishazi vilivyoongezewa maneno. Hivi sasa lugha hii imelinganishwa na lahaja kwa sababu watu wanaoelewana kilahaja huiturnia katika mawasiliano ya kawaida. Lahaja hii hutumiwa zaidi na vijana.

Pia lugha mtandao au 'Netspeak' ni aina ya lugha ambayo hukua katika mazingira ya kielektroniki na huainishwa kama lugha isiyo rasmi. Kwa mujibu wa Crystal (2006) lugha mtandao ni aina ya lugha ya kielektroniki ambayo hutumika katika maongezi, kwa mfano maneno bayana, www, blogu na ujumbe mfupi katika simu. Anasema kuwa wale watumiaji wa lugha hii huitwa “Netizen” kutoka kwa neno la Kiingereza 'Net' na 'Citizen', Anaendelea kueleza kuwa lugha mtandao ni sifa ngeru ambayo hujumuisha lugha ya rnazungurnzo, lugha andishi na sifa za kielektroniki. Kulingana na Nekesa (2010) lugha mtandao huwa na sifa za usemi na uandishi na huathiri na hutegemea aina nne za lugha moja: lugha ya maandishi, kusorna, mazungumzo na kusikiza. Hii ni kwa sababu lugha hii iliundwa mwanzo kwenye umbo andishi la lugha na imeathiri lugha kimazungumzo na kimaandishi katika maisha halisi. Kwa hivyo tofauti iliyopo baina ya lugha mtandao au “Netspeak” na lugha mazungumzo katika maisha halisi ilizuka kabla lugha ya mtandao na imefanywa kama lugha mazungumzo. Mwingiliano huu huhusu mpangilio wa maneno katika sentensi, matumizi ya ufupishaji wa kitenzi au kuongeza viambishi tamati vya vitenzi kwa maneno asilia ya Kiswahili.

*Urban Dictionary* inaeleza kuwa lugha mtandao ni namna ya kufupisha maneno na hali ya kubadilisha herufi moja ya neno na herufi nyingine au ishara kwa lengo la kuokoa muda, upigaji chapa kwa urahisi, kupunguza idadi ya maneno na kupunguza gharama ya kutuma ujurnbe. Upigaji chapa kwa haraka husababisha makosa ya kimaandishi au kitahajia na makosa hayo hukubalika katika rnawasiliano ya kimtandao. Makosa ya tahajia yamekuwa jambo la kawaida katika mawasiliano ya kimtandao na jambo hili limekuwa maarufu sana hadi kukaibuka lugha mpya iitwayo taipografia. Lugha hii huwawezesha watumiaji kutumiana matini fupifupi zenye mchanganyiko wa maneno na nambari hivyo kuibuka na lugha tofauti na inayozoeleka miongoni mwao.

Naye Crystal (2001) anasema kuwa kuna utata na ni vigumu kueleza kwa ufasaha na kikamilifu maana ya lugha mtandao. Hata hivyo anasema kuwa itaendelea kukua na kuimarika na hivi karibuni itahusishwa na sifa zake zitafanywa kuwa kanuni na sheria za kimtandao na hata kufanywa kuwa miongoni mwa lugha ambazo zinatumiwa katika jamii zetu na hata kuundiwa kamusi. Crystal (2008a & 2008b) katika makala yake, aliyoyaita "Texting" au ujumbe mfupi, anasema kuwa umatinishaji ni jambo jipya kabisa ambalo sasa linaelekea kupata lugha yake. Anaelezea kuwa katika umatinishaji, lugha mpya aliyoiita "textspeak" inakuwa kwa haraka hasa miongoni mwa vijana.

Kwa mujibu wa Jelimo (2015), lugha mtandao au 'Netspeak' ni aina ya lugha ya mkato ambayo imezuka na kukua katika mazingira ya kielektroniki na hutambulika kwa sifa zake za kimtandao kama vile matumizi ya akronimu, vifupisho, udondoshaji, uunganishaji na matumizi ya herufi na nambari. Ni lugha ambayo hutambuliwa na hutumiwa na kundi fulani la watu katika jamii na watumiaji hutumia sana ili kuficha siri au kwa matumizi ya tasfida. Tofauti iliyopo kati ya lugha mtandao na sheng ni kuwa, lugha mtandao ni lugha

andishi ambayo imezuka katika mazingira ya kielektroniki na hutumika ili kurahisisha mawasiliano. Sheng huwa ni lugha inayotumiwa na kikundi fulani cha watu kujitambulisha na hususan huwa ni lugha ya mazungumzo. Lugha mtandao ni suala ibuka ambalo kwa sasa limechangamkiwa na watumiaji wengi wa mitandao na hivyo basi kwa msingi wa nadharia ya Msambao wa Uvumbuzi, uteuzi na matumizi ya tovuti unawiana na mahitaji ya watumiaji wa mitandao anuai.

Kaplan na Haelein (2010), wanafafanua kuwa mitandao ya kijamii inawezesha uundaji na ubadilishanaji wa habari kutoka mtu mmoja hadi mwingine. Wanaendelea kusema kuwa mitandao ya kijamii inaweza kuwekwa katika kategoria mbalimbali kama vile: a) Miradi ya shirika kama vile Wikipedia. b) Blogu kama vile Twita c) Maudhui jumuiya kama vile Kamera za mitandao na Google d) Mitandao kama vile Facebook. Uwezo huu wa kuwaunganisha wataalamu mbalimbali mtandaoni ni jeki kubwa kwa juhudi za ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili mtandaoni.

Mchango wa TEHAMA katika ukuzaji wa Kiswahili umebainika kutokana na matokeo ya utafiti wa Mutembei (2011) kuhusu *kukitandawazisha Kiswahili kupitia simu za kiganjani hususan tafakari kuhusu isimujamii*. Utafiti wake uliangazia baadhi ya mikakati ya kuboresha matumizi ya simu mtandaoni na kupiga jeki juhudi mbalimbali za ukuzaji wa lugha ya Kiswahili mtandaoni. Utafiti wa Jagero, Mohochi na Indede (2013) umejadili kuhusu matumizi ya Kiswahili katika matini ya Blogu na athari zake katika ukuaji wa lugha ya Kiswahili. Kwa kutumia nadharia ya Uchambuzi Usemi Jadilifu, walibaini kuwa washiriki wa Blogu wanatumia vifupisho, maneno yasiyo sanifu, sarufi isiyo sahihi, kuchanganya misimbo, kubadilisha misimbo na matumizi ya tahajia yasiyo sahihi. Hivyo basi kuwa na athari chanya na hasi katika ukuaji wa lugha ya Kiswahili. Wameshughulikia

matini ya kisiasa. Matokeo haya yanachangia pakubwa katika ujenzi wa Kiswahili na kuimarisha sarufi ya Kiswahili, jambo ambalo ni hatua kubwa katika mchakato wa ukuzaji wa Kiswahili.

Naye Gikambi (2014) katika makala ya SwaKO ameshughulikia *"Mgeni Njoo Mwenyeji Atambe"*-athari za Facebook, Twitter na Kamera ya mtandao katika vyombo vya habari vitumiavyo Kiswahili. Vilevile ameangalia kama Kiswahili kimekuzwa na kuendelezwa au kudidimizwa katika majukwaa haya. Makala yake yaliangazia kipengele cha kipekee cha simu za mkononi na jinsi zinavyochangia katika matumizi ya Kiswahili kwenye vyombo vya habari hasa majukwaa ya *Facebook na Twitter*. Matumizi ya Kiswahili kwenye majukwaa haya ni kipengele kikubwa sana katika usambaaji na udumishaji wa hadhi na dhima ya Kiswahili. Utafiti wetu umeangazia ukuzaji wa Kiswahili kwa maana ya ujenzi wake, usambaaji wake pamoja na udumishaji wa hadhi na dhima yake miongoni mwa watumiaji wake kieneo na kiwakati. Khayesi (2002) anaeleza kwa jumla jinsi lugha ya Kiswahili inavyoweza kuingizwa na kutumiwa katika mfumo wa TEHAMA, kama ilivyofanywa katika lugha nyingine kuu duniani. Anaendelea kujadili kuhusu kuingizwa kwa lugha hii katika mfumo wa kompyuta ambao unamruhusu mtumiaji wa lugha hii kuona na kufanya mambo yote ya kompyuta katika Kiswahili. Pia kuandaa programu au kuwezesha zile zilizopo kuchanganua data za lugha hii ili ziweze kuwa na matokeo yanayoweza kutumika katika kazi mbalimbali.

Kwa mujibu wa King (2010) utafiti uliofanywa kuhusu data za vyombo vya habari vya kijamii na kuhusu mielekeo unaonyesha kuwa kuna tofauti kwa namna ambavyo vyombo hivyo hutumika, habari huzalishwa na namna watu hutumia hekima ya kimakundi kufahamishana habari ulimwenguni kote. Singh, Lehnert na Bostick (2010) walifanya

utafiti kuhusu vyombo vya habari vya kijamii ulimwenguni na matumizi ya lugha. Utafiti wao ulionyesha kuwa watu hupenda kuwasiliana kupitia vyombo vya habari vya kijamii kwa lugha zinazotumika katika maeneo yao. Hii ndiyo hali iliyodhihirika hasa kwenye maeneo ambapo Kiswahili kinatumika sana katika vyombo vya habari vya kijamii.

Matumizi ya tovuti na mitandao ya kijamii yamekuwepo na huchangia pakubwa katika nyanja mbalimbali. Matumizi ya lugha katika vyombo vya habari vya kijamii yamechangia maendeleo makubwa katika matumizi ya lugha mbalimbali hususan kwenye mawasiliano ya mtandaoni. Wataalamu mbalimbali (Crystal, 2001, Macfedries, 2004, Madden, 2016) hurejelea matumizi ya lugha hiyo kama ‘maongezi ya mtandao’.

Kwa mujibu wa Crystal (2001) sajili ya mtandaoni inayorejelewa kama ‘maongezi ya mtandao’ imezalishwa kutoka kwa vyombo vya kielektroniki na mawasiliano yanayofanikishwa kupitia kompyuta. Pamoja na hilo, anasema kuwa ‘maongezi ya mtandao’ yana aina za maandishi na usemaji wa kipekee anaourejelea kama upatanisho unaomilikiwa kielektroniki. Macfedries (2004) anaeleza kuwa ‘maongezi ya mtandao’ (pia lugha ya mtaani inayotumika katika mtandao) inaweza kuelezwa kama ‘maneno, nahau na maumbo ya kipekee kama vile akronimu LOL (laughing out loud) na OMG (Oh my God/Gosh), zinapatikana katika *Oxford English Dictionary* (2011). Matumizi ya lugha mtandao “Netspeak” yalianza mwaka wa 1978 kutokana na mawasiliano kupitia mitandao ya kompyuta na ujumbe katika simu (Jagero na Wengine, 2013). Matumizi ya 'Netspeak' yanaendelea kukua na hubadilika kila uchao kwa vile ni mbinu rahisi katika kutuma ujumbe. Pia kila siku dhana mpya na mtindo mpya huibuka na utaendelea kuimarika na kusambaa.

Ingawa watafiti wengi wameitumia nadharia ya Msambao wa Uvumbuzi wa Rodgers kuongoza kazi zao, si wengi miongoni mwao walioitumia kuchunguza tovuti ya Swahilihub katika makuzi ya taaluma ya Kiswahili (Wamalwa, 2016). Umuhimu wa kuzingatia vigezo vya Msambao wa Uvumbuzi wa Rodgers (2003) katika tathmini ya tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili nchini Kenya ulidhihirika kutokana na misingi ya nadharia hii.

## 2.4 Ukuzaji wa Kiswahili kwenye Tovuti Swahilihub

Ukuzaji wa Kiswahili ni jumla ya hatua zinazochukuliwa ili kupanua wigo wa matumizi yake katika shughuli mbalimbali za jamii na hivyo basi kuingizwa katika harakati mbalimbali kama vile katika siasa, uchumi, elimu na pia nyumbani mwa watumiaji wake. Ingawa Cooper (1990) anaangazia ukuzaji lugha kwa vigezo vitatu; ueneaji kimsamiati na sarufi, usambaaji kieneo na udumishaji hadhi, utafiti huu ulibaini kwamba ukuzaji ni swala pana linaloakisi vigezo vya ndani na nje vikiwa ni pamoja na ukuzaji kikongoo, kihadhi na kieneo. Simala (2019) na Agume (2022) wanabainisha kuwa ukuzaji lugha kihadhi ni juhudi za kimaksudi za kuathiri na kuleta mabadiliko katika majukumu ambayo lugha inatwikwa. Ukuzaji lugha kikongoo ni kusanyiko la data za semi zilizoandikwa au kunukuliwa ambazo hutumiwa kama kianzio cha ufafanuzi wa kiisimu. Ukuzaji lugha kikongoo unahusika na muundo wa ndani wa lugha. Mambo yanayozingatiwa hapa ni pamoja na kuunda othografia kwa lugha ambazo bado hazijaandikiwa, kuanzisha mabadiliko katika tahajia, kubuni maneno mapya na kuchapisha vitabu vya sarufi na makamusi. Ukuzaji wa aina hii unahusu kuendeleza mbinu za kujifunza lugha iliyoteuliwa kupitia mifumo ya elimu. Ukuzaji kikongoo pia unahusu kupanua ufunzaji na ujifunzaji wa lugha kimaksudi.

Simala (2019) anabainisha kuwa ufanisi wa ukuzaji lugha hutokana na mchakato unaofaa wa utekelezaji wake. Michakato kama hiyo huakisi ukuzaji wa lugha zote hasa lugha zinazofaa kuwa na hadhi sawa. Katika muktadha wa Kenya, Kiswahili kilipewa hadhi kama lugha rasmi sawa na Kiingereza. Kwa hivyo, juhudi za utekelezaji wa sera ya lugha ya elimu zinafaa zishughulikiwe katika mchakato mzima wa sera ya lugha na ukuzaji lugha. Ili ukuzaji wa Kiswahili utimie kikamilifu, ni lazima kuweko na uungaji mkono wa wanasiasa, yaani ukubalifu wa serikali katika shughuli nzima ya uundaji na utekelezaji wa sera ya lugha kwa ajili ya kufanikisha mchakato mzima wa ukuzaji wa Kiswahili (Legere, 2002) na Kandagor (2012; 2013a).

Aidha, kwa mujibu wa Agume (2022), ukuzaji wa lugha unaangazia ngazi mbili ambazo ndizo huzalisha uteuzi wa lugha moja au zaidi ambayo hutambuliwa katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali nchini au katika jamii husika (Hornberger, 2006; Sung, 2020). Ngazi hizi ni: Ukuzaji lugha kihadhi. Hii ni ngazi ambayo inahusu ukuzaji wa matumizi ya lugha kwa kuzingatia dhima au nafasi ya lugha yoyote iwayo katika jamii na mara nyingi ni ngazi inayoamuliwa na nguvu za kisiasa. Ilihali ukuzaji lugha kikongoo, ni ngazi inayohusu maumbo na muundo wa lugha yenyewe. Ngazi hii hulenga kukuza msamiati na matawi yote ya sarufi ya lugha ambayo ni fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Kwa hivyo, ni jitihada za kimakusudi katika kuboresha ngazi mbalimbali za sarufi ya lugha (Jernudd na Gupta, 1971; Abdulaziz, 1993; Jjingo, 2011). Hivyo basi, ufidianaji wa suala la ukuzaji lugha kihadhi, usambaaji wake kimaeneo na kiwakati pamoja na ukuzaji lugha kikongoo ni muhimu sana na uliupa utafiti huu mwanya wa kuchunguzia suala zima kutokana na misingi ya nadharia inayotumika. Ukuzaji lugha ni muhimu hasa katika jamii zenye wingilugha pale panapohitajika kujenga utaifa miongoni mwa watu wenye tamaduni tofauti tofauti (Haugen, 1987; Carreras 2018). Madai haya yanaafikiana na

muktadha wa Kenya ambako kuna lugha tofauti zaidi ya sitini na nane kutoka makabila mbalimbali. Kwa hivyo, tovuti ya Swahilihub ina nafasi muhimu katika kuendeleza Kiswahili nchini Kenya hasa kupitia elimu kwa ajili ya kutatua matatizo ya mawasiliano na kujenga utaifa miongoni mwa Wakenya.

Utandawazi ulianza kuingia polepole katika lugha ya Kiswahili tangu enzi za utawala wa kikoloni. Hii ni kwa sababu utawala wa kikoloni uliambatana na kuanzishwa kwa vyombo vya habari kama vile magazeti, redio, runinga, tovuti na simu ambao uliimarisha utandawazi na Kiswahili kupata matumizi makubwa. Hali hii ilisababisha mabadiliko kadha wa kadha hususan katika lugha ya Kiswahili. Mabadiliko hayo yanaweza kujidhihirisha katika nyanja mbalimbali kama vile utamaduni, dini, elimu, biashara na utawala. Vyote hivi kwa pamoja vilisaidia kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili ndani na nje ya Afrika (Bakita, 2004). Udumishaji wa Kiswahili hukusudia kukipa nafasi ya kutumika katika mawasiliano yaliyokusudiwa hususan katika mitandao na kwenye sera mbalimbali za matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shughuli za kiutawala na harakati za kisiasa.

Kwa hakika, mjadala kuhusu ukuzaji wa Kiswahili umetendewa haki stahiki na wanazuoni katika taaluma za isimu, isimujamii, na fasihi ya Kiswahili. Matokeo ya utafiti anuai kuhusu historia na maendeleo ya Kiswahili yamechapishwa katika majarida na vitabu mbalimbali. Taarifa na mijadala katika machapisho haya yanathibitisha jambo moja muhimu kwamba lugha ya Kiswahili na matumizi yake yamekuwa yakipanuka tena kwa kasi kubwa. Utafiti huu pia una mchango mwafaka katika kupanua wigo wa matumizi ya lugha ya Kiswahili mitandaoni kufikia viwango vya lugha zingine za kimataifa kama vile Kiingereza na Kifaransa. Ukuzaji wa Kiswahili huakisiwa na vigezo mbalimbali kama vile

upanuzi wa matumizi yake, uimarishwaji wa misamiati na istilahi zake, ongezeko la idadi ya watumiaji wake, hadhi na dhima yake kupaa juu, kuchipuka kwa aina mbalimbali za matumizi yake, uvumbuzi na ugunduzi wa kisayansi na utambuzi wake katika utawala na siasa.

Kiswahili ni miongoni mwa lugha zinazopokea maneno kutokana na matumizi yake kwenye mitandao husasan katika maendeleo ya sayansi na teknolojia, siasa, kijamii na uchumi. Kwa mfano, kuna matumizi ya istilahi nyingi za kimtandao za sayansi na teknolojia ambayo hutumiwa katika shughuli mbalimbali za kijamii. Hapo awali lugha ya Kiswahili haikupewa nafasi katika mitandao ya kijamii kwani ilionekana kama lugha isiyo ya kimtandao. Kwa hivyo, lugha kama vile Kiingereza zilipewa hadhi ya juu na hata kutumiwa katika shughuli mbalimbali za kimtandao. Matumizi ya Kiswahili katika mitandao ya kijamii yalianza kuimarika mwaka wa 2007. Kiswahili hutumika katika mitandao ya Facebook na Twitter kama wenzo wa mawasiliano. Kupitia mifumo mbalimbali mtandaoni kama vile mitandao ya kijamii, watumiaji wana uwezo wa kujenga maudhui, kuchapisha maelezo, kuwasiliana na kununua au kuuza bidhaa na kushiriki huduma mbalimbali.

Ili kuendeleza na kuimarisha juhudi za ukuzaji wa lugha ya Kiswahili mtandaoni, mradi wa maandishi ya Kiswahili wa Helsinki (Helsinki Corpus of Swahili) umechangia katika ukusanyaji wa matini mbalimbali za Kiswahili na kuzihifadhi kwenye mtandao. Mradi huu, ambao bado unaendelea, umetayarishwa na taasisi ya masomo ya Kiasia na Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Helsinki-Finland kwa ushirikiano na wataalam wengine wa Kiswahili kutoka TATAKI Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam. Mradi huu una matini mbalimbali za habari kutoka kwa magazeti tofauti ya Kiswahili, mkusanyiko wa vitabu

mbalimbali vya Kiswahili, mkusanyiko wa hotuba na mahojiano mbalimbali, bibilia na kamusi ya Kiswahili (Sewangi, 2000).

Kufikia mwaka wa 2005, makisio yalikuwa kwamba mradi huu ulikuwa na takribani idadi ya maneno milioni kumi na mbili unusu, idadi ambayo inazidi kuongezeka kila uchao (Njihia, 2005). Idadi hii kubwa ya maneno ni hazina muhimu katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili mtandaoni kupitia majukwaa ya kidijitali kama vile tovuti ya Swahilihub. Juhudi hizi za mradi wa Helsinki zimechangia pakubwa kuboresha na kuhifadhi matini mwafaka inayotumiwa kuiendeleza taaluma ya Kiswahili kwenye tovuti ya Swahilihub. Mradi huu umechangia pakubwa katika ujenzi wa lugha ya Kiswahili na hivyo basi kuisambaza na kudumisha hadhi na dhima yake kote ulimwenguni. Isitoshe, vifaa vya kisasa vya viunga mbali vinavyotumia mitambo ya satalaiti ni bora katika mchakato wa ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kupitia kwa vipindi vya ufundishaji wa lugha ya Kiswahili unaowafikia watumiaji wengi mitandaoni (Owino, 2011). Ni muhimu kutambua na kuangazia juhudi za awali kama hizi zinazoimarisha matumizi ya tovuti ya Swahilihub katika uendelezwaji wa taaluma ya Kiswahili kwani kutokana na matumizi yake walimu wanaweza kurahisisha na kuboresha zaidi ufundishaji wao.

Kiswahili, kama zilivyo lugha zote duniani, iliinukia, ikakua, na inaendelea kukua. Mintaarafu ya ukweli huu, tunaweza kudai kuwa kukua kwa Kiswahili ni ushahidi kuntu wa kukua na kustawi kwa tovuti ya Swahilihub miongoni mwa wazungumzaji wa Kiswahili hususan katika ukanda wa Afrika ya Mashariki na Kati. Lugha isiyotumika au kutumiwa huvia na hatimaye hutoweka ama hufa. Lugha inayotumiwa hukua na kustawi kulingana na mahitaji ya mawasiliano yaliyomo katika jamii husika. Mawasiliano ya lugha huwa nyenzo kuu katika kufanikisha shughuli za binadamu – iwe ni za kiuchumi au

kisiasa, kijamii, kiutamaduni, kifasihi, kiroho, kiteknolojia na kisayansi, kielimu, nk. Katika mchakato wa kukidhi mahitaji ya mawasiliano hayo, msamiati na istilahi zake hupanuka, aina mbalimbali za uzungumzaji na matumizi yake huchipuka, huchochea ubunifu katika tasnia anuwai kama vile katika sanaa za lugha na maonyesho, uvumbuzi na ugunduzi wa kisayansi na kiteknolojia, utawala na siasa, usalama na ulinzi, uzalishaji, afya bora, elimu bora, na kadhalika. Hivyo basi, ustawi wa jamii huweza kuakisi na kusawiri ukuaji wa lugha husika.

Kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili kunategemea mambo mbalimbali kama vile kutumika katika maeneo na mifumo rasmi kwenye jamii husika. Historia ya lugha ya Kiswahili inaonekana kukua tangu wakati wa biashara ya watumwa, Waarabu, kipindi cha ukoloni wa Wajerumani na kipindi cha ukoloni wa Waingereza. Harakati za kusanifisha lugha ya Kiswahili kwa hatua mbalimbali za usanifishaji wake (1928- 1930) zilichapuza kukua na kusambaa kwa lugha ya Kiswahili. Baada ya uhuru wa Tanzania, Tanganyika wakati huo, lugha ya Kiswahili ilizidi kukua hasa baada ya serikali katika mwaka 1962 kuifanya kuwa lugha ya taifa na lugha rasmi ya mawasiliano katika shughuli mbalimbali za kiserikali na zisizo za kiserikali.

Usambaaji wa Kiswahili ni nguzo ya pili ya ukuzaji inayobainika katika ueneaji wake. Usambaaji wa Kiswahili ni uongezekaji wa matumizi yake kieneo na kiwakati. Katika utafiti huu dhana ya usambaaji wa Kiswahili ilibainika kulingana na mahitaji ya walengwa mtandaoni. Mtandao wa kijamii ni tovuti au programu inayokuruhusu kuungana na marafiki na familia, na kushiriki taarifa, picha na video. Kuna zaidi ya watu bilioni moja kwenye *Facebook*, Wikipedia ina zaidi ya watumiaji bilioni nne na Twitter ina zaidi ya watumiaji milioni 500. Mitandao ya kijarnii mingi inakuruhusu kurekebisha mipangilio

yako au kudhibiti maelezo yapi unayoshiriki, jinsi unavyoyashiriki, na unayeshiriki naye. Utandawazi huweza kusaidia kuongeza msamiati wa lugha.

Vyombo mbalimbali vya kukuza Kiswahili viliundwa kama vile Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) kutokana na kamati iliyokuwa ya usanifishaji wa lugha ya Kiswahili ya Afrika Mashariki na Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam, kuvitaja kwa uchache. Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ilikuwa na jukumu la kufundisha somo la Kiswahili na wataalamu wake kuandika masuala mbalimbali ya lugha ya Kiswahili. Mazoea yamekuwa kuviangalia vyombo hivi na serikali kwa ujumla kama ndio vyombo pekee vyenye wajibu wa kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili. Tukiacha mbali vyombo hivi tulivyovitaja, yapo maeneo mengine yanayoweza kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili ambayo ama hayajaangaliwa kwa kiasi cha kutosha au yamesahaulika. Mojawapo ya maeneo ambayo matumizi ya lugha ya Kiswahili yanaweza kuchangia kukua na kuenea kwake ni mtandaoni. Lengo la utafiti huu ni kubainisha namna Swahilihub inavyosaidia kukua na kuenea kwa Kiswahili.

Lugha ya Kiswahili imepitia mabadiliko makuu katika matumizi yake kwenye mitandao ya kijamii, Sababu kuu ikiwa asimilia kubwa ya watumiaji ni vijana ambao wanataka kupitisha ujumbe baina yao kwa haraka iwezekanavyo. Kulingana na Fagan na Desai (2003), asimila 40% ya wanaotumia mtandao wa kijamii ni vijana wa kati ya miaka 1618, wakifuatwa na asimilia 35% ambao ni wanafunzi wa vyuo, asimila ya 15 % ni wale ambao hawajapata elimu na mwisho, asimilia 10% ni watu wazima kutoka miaka 66 na zaidi. Watumiaji hawa wamebuni mtindo mpya kwa kufupisha maneno na kuufanya kuwa maarufu sana miongoni mwao. Pamoja na juhudi hizi, kuna haja ya kuikuza lugha ya

Kiswahili kwenye tovuti mbalimbali kwani mitandao hii ndiyo uti wa mgongo wa usambazaji wa habari katika enzi hii ya utandawazi. Juhudi za kuiweka lugha ya Kiswahili mtandaoni zimeshika kasi. Mazrui na Mazrui (1995) wamejadili matumizi ya Kiswahili katika TEHAMA kupitia vyombo vya habari, katika nchi za Afrika Mashariki na kwingineko ulimwenguni. Ndipo sasa utafiti huu ulijikita katika kutathmini nafasi ya Swahilihub katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili mtandaoni. Upekee wa tovuti ya Swahilihub kama jukwaa la kimtandao linalokuza taaluma ya Kiswahili ndio msukumo mkubwa wa kuutathmini mradi huu. Kwa mujibu wa Khayesi (2002) aliyechunguza matumizi ya Kiswahili katika tarakilishi, TEKNOHAMA ni kiungo muhimu sana cha utandawazi. Hivyo basi lugha ya Kiswahili ndiyo lugha ya Kiafrika ambayo kwa kweli ina nafasi bora zaidi ya kuwa lugha ya utandawazi barani Afrika.

Matokeo ya utafiti wa Lacey (2004) yalibaini uwezekano wa kutumia lugha moja ya Kiafrika katika kuzihifadhi lugha zingine na kuziondolea uwezekano wa kutoweka katika matumizi ya tarakilishi. Kwa kuzitumia lugha za Kiafrika katika tarakilishi, lugha hizi zitahifadhiwa mbali na kuwa teknolojia hii itawafikia Waafrika wengi iwezekanavyo. Utafiti huu ulionyesha namna ambavyo lugha ya Kiswahili inavyoweza kukuzwa kwenye mitandao na kuwafikia watumiaji wengi wa mitandao. Uwezekano huu ni hatua kubwa ya usambaaji na udumishaji wa hadhi na dhima ya Kiswahili kote ulimwenguni. Iraki (2004) ameligusia suala la Microsoft East Africa kukifanya Kiswahili kuwa mojawapo ya lugha katika programu zake. Anaeleza kuwa kampuni hii imetambua kuwa kuna soko kubwa la huduma zake katika maeneo yanayozungumzwa Kiswahili.

Utafiti zaidi ulichangia pakubwa katika kukuza lugha ya Kiswahili mitandaoni. Njihia (2005) ametafiti kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili katika tarakilishi. Ameshughulikia miradi kama vile mradi wa Microsoft East Africa, mradi wa kugeuza

matini za Kiswahili hadi usemi na mradi wa injini pekuzi ya Kiswahili katika mtandao. Utafiti huu ulijadili kwa kina juhudi mbalimbali za awali katika maendeleo ya taaluma ya Kiswahili. Kahigi (2007) ameelezea kuhusu ujanibishaji wa Office (2003) na Windows XP. Ameelezea misingi ya uundaji wa istilahi ambayo waundaji walikubali kutumia na istilahi zilizoundwa. Uundaji wa isitilahi ni kigezo muhimu cha ukuzaji wa

Kiswahili kupitia kwa ujenzi wake. King'ei (2008) amejadili masuala ya kinadharia katika ukuzaji wa istilahi za Kiswahili akitoa mifano kutokana na mradi wa kamusi ya Microsoft. Anaendelea kusema kuwa ingawa Kiswahili Sanifu ni lugha ya watu wachache wa tabaka la wasomi pekee, lazima tukubali kuwa istilahi zinazoundwa kwa matumizi katika nyanja nyingi zinastahiki kueleweka na hata wale wasiokuwa wataalamu. Matokeo ya utafiti huu na maoni haya yalichangia katika kuweka wazi msingi wa ukuzaji wa Kiswahili kwa ujenzi wa istilahi zake na usambaaji wake kwa watumiaji wa mitandao anuai.

Owino (2011), aliangazia matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji wa riwaya ya Kiswahili katika shule za upili nchini Kenya. Matokeo ya utafiti wake yalibainisha upekee wa majukwaa ya kidijitali katika usambaaji wa Kiswahili na udumishaji wa hadhi na dhima yake kupitia kwa michakato ya ufundishaji wa lugha ya Kiswahili na hivyo basi kuwafikia watumiaji wengi wa mitandao. Utafiti wa Moraa, (2013) ulilenga kuweka wazi mbinu zilizotumika katika kuzalisha msamiati kwenye Mradi wa Microsoft. Shughuli muhimu aliyozingatia ilikuwa ni ile ya leksikolojia na leksikografia katika kutekeleza mahitaji ya lugha yoyote ile. Juhudi hizi za kileksikolojia na kilesikografia zilichangia pakubwa katika ukuzaji wa Kiswahili kupitia ujenzi wa istilahi na misamiati yake. Naye Wamalwa, (2016), alifafanua kuwa tovuti ya Swahilihub ina nafasi kubwa katika kukuza taaluma ya Kiswahili katika vyombo vya habari nchini Kenya. Vyombo vya habari nchini Kenya vina nafasi nzuri ya kudumisha hadhi na dhima ya Kiswahili miongoni mwa

watumiaji wengi wa Swahilihub mtandaoni. Hata hivyo, hakuweza kuonyesha nafasi ya tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili zaidi ya matumizi yake kwenye vyombo vya habari.

## 2.5 Maendeleo ya Tovuti ya Swahilihub katika Ukuzaji Kiswahili

Katiba ya Kenya ibara ya 7 imetambua Kiswahili kama lugha ya taifa na lugha rasmi huku ibara ya 44 ikilinda utamaduni wa jamii mbalimbali, utamaduni wa watumiaji wa Kiswahili ukiwepo. Kati ya lugha 2000 za Kiafrika, Kiswahili ndiyo lugha ya kipekee ambayo ni rasmi ya umoja wa Afrika (AU) na ya jumuiya ya Afrika Mashariki. Kiswahili kina hadhi ya nafasi ya sita kimataifa, kikitanguliwa na Kiingereza, Kifaransa, Kihispania, Kiarabu na Kireno. Kiswahili huzungumzwa na watu takribani milioni 160, kama lugha ya kwanza, ya pili na ya tatu. Hivyo basi juhudi hizi za udumishaji wa hadhi na dhima ya Kiswahili ni nguzo muhimu sana katika tathmini ya mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili.

Hali hii ya udumishaji wa hadhi ya Kiswahili inadhihirisha mwamko mkubwa wa matumizi ya mitandao ya kijamii miongoni mwa Wakenya. Tangu mwaka wa 2004, ulimwengu umeshuhudia kuongezeka kwa shughuli za kijamii mtandaoni (Simmsons, 2005). Kuibuka kwa vyombo vya habari vya kijamii na mitandao ya kijamii kumechangia kutokea kwa mikakati mipya ya kiteknolojia. Taaluma ya Kiswahili imeanza kukabiliwa na athari kubwa ya mitagusano hii ya kidijitali katika mawasiliano yanayowapa watumiaji wa Swahilihub uwezo wa kutangamana na kuchangiana kote ulimwenguni. Kenya ndiyo nchi ya tatu barani Afrika iliyo na idadi kubwa ya blogu (Chimerah, 2000). Mradi wa Swahilihub una nafasi nzuri ya kufaidika kutokana na mwamko huu kwa kuwalenga watumiaji hawa wa blogu kwenye kitengo chake maalum cha blogu na ukumbi.

Juhudi za utafiti wa wataalam mbalimbali zimechangia pakubwa katika ukuzaji wa Kiswahili nchini Kenya. Watalamu mbalimbali (Njihia, 2005, Hurskainen, 2004, Khayesi, 2002, Sewangi, 2002) wameangazia miradi mbalimbali inayohusisha TEHAMA katika juhudi za ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kwa njia mbalimbali. Juhudi hizi za kitafiti zilichangia kuzaliwa kwa miradi kama vile SALAMA (Swahili Language Manager) kutokana na mchango wa Kimmo Koskemiemi katika kubuni programu ya kiteknolojia ya kuchanganua mofolojia ya Kiswahili katika mwaka wa 1985 (Njihia, 2005). Baadaye Hurskainen akaendeleza juhudi za kuimarisha mradi wa SALAMA ukiwa na majukumu yafuatayo: kusahihisha makosa ya tahajia katika matini za Kiswahili, kuakifisha matini yoyote ile ya Kiswahili inapochapishwa kwa kutumia tarakilishi, uchanganuzi wa kimofolojia wa matini za Kiswahili pamoja na kufasiri matini za Kiswahili hadi lugha zingine au matini za lugha zingine hadi Kiswahili. SALAMA hudhamiria kudhibiti matini za Kiswahili kwa njia isiyo na ubishi na itakayorejelewa kwa haraka.

Juhudi hizi za mradi wa SALAMA za kuimarisha matini za Kiswahili mtandaoni ni hatua muhimu katika tathmini ya mchakato wa ukuzaji wa Kiswahili mitandaoni kwa msingi wa ujenzi wa Kiswahili, istilahi zake, sarufi yake na miktadha mbalimbali ya matumizi yake. Juhudi hizi za SALAMA zimechangia kupiga jeki mchakato wa ukuzaji wa Kiswahili nchini Kenya kutokana na ujenzi wake, usambaaji wake mpana na udumishaji wa hadhi na dhima yake miongoni mwa watumiaji wa Kiswahili.

Mradi wa SALAMA (Swahili Language Manager) ni programu ya tarakilishi iliyotayarishwa katika Chuo Kikuu cha Helsinki-Finland naye (Hurskainen, 2004) Arvi Hurskainen kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam. Mradi huu hushirikiana na TATAKI na ushirika huu hujulikana kama DAHE (Dar-Helsinki Archives of Swahili).

Programu ya SALAMA ni mazingira ya kompyuta ya kufanya shughuli za kiisimu za aina nyingi kwa lugha ya Kiswahili. Programu hizi ni kama vile programu ya kuchanganua mofolojia ya Kiswahili. Ujenzi wa sarufi ya Kiswahili na isimu yake ni hatua kubwa katika mchakato wa ukuzaji wa lugha nchini Kenya. Mradi wa SALAMA na ushirikiano wa DAHE ni miongoni mwa juhudi zilizochangia pakubwa ukuzaji wa Kiswahili nchini Kenya kupitia mchakato wa ufundishaji wa Kiswahili shuleni na vyuoni. Swahilihub kama jukwaa la kimtandao limejengwa kwa matini za Kiswahili ambayo imepigwa jeki kubwa kutokana na mchango wa juhudi za mradi wa SALAMA. Matini hizi ni muhimu katika ujenzi, usambaaji na udumishaji wa hadhi na dhima ya Kiswahili nchini Kenya na hivyo basi kuyakidhi mahitaji ya watumiaji wake mtandaoni.

Lengo la kubuniwa kwa Swahilihub ni ukuzaji wa Kiswahili kupitia kwa ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa kitengo cha jifunze Kiswahili na maktaba jisomee. Vitengo hivi vya tovuti ya Swahilihub vimechangiwa pakubwa na juhudi za awali za mradi wa KIKO yaani mradi wa Kiswahili Kwa Kompyuta ambayo huwa ni mazingira ya kompyuta ya kujifunza lugha ya Kiswahili. Mradi huo hutoa nafasi ya kujifunza Kiswahili kupitia tarakilishi. Mafunzo ya KIKO huwa na lengo kuu la kufundisha lugha ya Kiswahili hatua kwa hatua kwa watu binafsi au wale walio shuleni. Hatua hizi zimechangia pakubwa kufanikisha shughuli za ukuzaji wa Kiswahili nchini Kenya kupitia michakato mbalimbali ya ufundishaji wa Kiswahili.

Umuhimu wa mradi huu ni kwamba huanza kwa kuwafundisha wanafunzi kuhusu asili na umuhimu wa kujifunza Kiswahili. Pamoja na haya, wanaelezea kuwa lugha ya Kiswahili huzungumzwa katika sehemu zingine za ulimwengu na hutumiwa kwenye vituo muhimu vya redio ulimwenguni (Njihia, 2005). Matumizi haya yamekuwa na faida kubwa katika juhudi za ujenzi wa Kiswahili pamoja na usambaaji wake miongoni mwa watumiaji wake

kote nchini Kenya. Mradi huu pia hufundisha kuhusu matamshi bora ya Kiswahili kwani wao wameziorodhesha irabu na konsonanti zote za Kiswahili na kutoa mifano ya sauti zinazotokana nazo. Sarufi ya Kiswahili hufunzwa kwa kufuata mpangilio wa zamani wa kuainisha ngeli za Kiswahili na kupata jumla ya ngeli nane. Mradi huu hueleza kuwa Kiswahili huwa na majina katika hali ya wastani, udogo na ukubwa na kwamba lugha hii imekopa majina kadhaa kutoka kwa lugha zingine kama vile Kiarabu, Kireno, Kijerumani na Kiingereza (Njihia, 2005). Mafundisho haya ya lugha ya Kiswahili mtandaoni yanachangia pakubwa katika kufanikisha lengo kuu la ukuzaji wa lugha ya Kiswahili mtandaoni miongoni mwa watumiaji wake nchini Kenya na kote ulimwenguni.

Mradi wa KIKO hivyo basi ni msingi mwafaka wa kuangaziwa katika mchakato wa ukuzaji wa lugha ya Kiswahili mitandaoni kupitia majukwaa ya kijamii kama vile tovuti ya Swahilihub. Tovuti ya Swahilihub ina nafasi ya kuwafikia watumiaji wengi wa mtandao na hivyo basi kuchangia pakubwa katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kupitia vipindi na makala mbalimbali ya mafundisho ya lugha ya Kiswahili mtandaoni.

Juhudi za mradi wa KIKO ni hatua muhimu iliyochangia kuimarisha nafasi ya tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Kutokana na mchango wa mradi wa KIKO katika ujenzi wa Kiswahili nchini Kenya, usambaaji wake umeweza kupanua mawanda ya mada zinazopakuliwa kwa watumiaji wake kwa kuangazia vipengele kama vile hadithi, mashairi, tamthilia, ngonjera, tenzi, nahau, methali, uhakiki wa vitabu vya kiada na ziada kwa shule za msingi, sekondari na vyuo.

Khayesi (2002) pia anajadili suala la matumizi ya TEHAMA katika utafiti wa Kiswahili. Anafafanua kuhusu mabadiliko yaliyotokea ulimwenguni kutokana na uvumbuzi wa TEHAMA. Anaendelea kusema kuwa utafiti wa Kiswahili unaweza kufaidi kwa kiasi

kikubwa kutokana na mtandao kwa kuhifadhi matokeo ya utafiti uliofanywa, ili matokeo haya yawafikie wale ambao hawafahamu lugha ya Kiingereza. Matokeo ya utafiti huu yalichangia pakubwa katika uimarishaji wa matini na uhariri wake na hivyo basi kuboresha huduma zinazopatikana kwenye majukwaa ya kidijitali kama vile tovuti ya Swahilihub. Michango inayotokana na juhudi hizi imejenga taaluma ya Kiswahili na kuiendeleza pakubwa nchini Kenya. Utafiti huu ulijikita katika misingi ya kukifanya Kiswahili lugha ya matumizi mtandaoni kwa kuendeleza matumizi yake kwenye tovuti ya Swahilihub na kubainisha vitengo vinavyotumika kwenye tovuti ya Swahilihub ili kuyafikia malengo yake ya kukusanya, kuhifadhi na kuwawezesha watumiaji wake kuzifikia matini zinazokuza lugha ya Kiswahili.  TEHAMA katika tovuti ya Swahilihub ni hatua kubwa ya ukuzaji wa Kiswahili nchini Kenya.

Khayesi (2002) anasema kuna uwezekano wa kutumia Kiswahili kwenye mitambo ya tarakilishi katika maktaba ya vyuo vikuu nchini Kenya. Matumizi haya ya tarakilishi kwenye maktaba ya vyuo vikuu nchini Kenya ni mchango mkubwa sana katika ukuzaji wa Kiswahili. Tovuti ya Swahilihub ni suluhisho mwafaka katika mchakato wa ukuzaji wa Kiswahili nchini Kenya kwa kuwa tayari makala na matini muhimu huhifadhiwa katika vitengo vyake mbalimbali kama vile maktaba jisomee, makala, blogu na ukumbi na hata majarida.

Sewangi (2002), ametoa maoni yake kuhusu faida ya tarakilishi, lengo lake la kimsingi likiwa kutumia tarakilishi kuhifadhi data na kurahisisha kuichambua. Anafafanua kuwa kongoo matini (text corpus) ni hifadhi ya lugha katika tarakilishi ili iweze kuchanganuliwa kwa malengo mbalimbali ya kiutafiti. Kongoo matini kwenye tovuti mbalimbali ilikuwa hazina kubwa iliyochangia katika ukuzaji wa Kiswahili nchini Kenya. Katika Kiswahili

kuna programu ya kukagua usahihi wa maandishi (spell checker) na kongoo matini ya Kiswahili yenye takriban maneno milioni kumi. Uwezekano huu wa kuitumia lugha ya Kiswahili kwenye tarakilishi na kubuni programu za kongoo matini zinazohifadhi lugha katika tarakilishi ndio msingi mkuu wa ukuzaji wa Kiswahili nchini Kenya. Utafiti huu ulijikita katika kubainisha mchango, changamoto na mustakabali wa tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili.

Ni muhimu kutambua na kuangazia juhudi za awali kama hizi zinazoimarisha ukuzaji wa Kiswahili katika tovuti ya Swahilihub katika uendelezwaji wa taaluma ya Kiswahili kwani kutokana na matumizi yake walimu wanaweza kurahisisha na kuboresha zaidi ufundishaji wao. Miradi hii imetoa michango yake katika ukuzaji Kiswahili nchini Kenya kwa sababu tayari Kiswahili ni lugha ya kiteknolojia. Aidha, kuna miradi anuwai inayokuza Kiswahili kwa kukihusisha na kukiingiza katika mitandao mbalimbali.

### 2.6 Umuhimu wa Swahilihub na Mafanikio yake katika Ukuzaji Kiswahili

Mitandao ya tovuti kote ulimwenguni ilibuniwa na Tim Burners-Lee katika mwaka wa 1989 (Aghaei, Nematbakhsh, na Farsani, 2012) na imebadilika kwa muda sasa kuanzia tovuti 1.0, tovuti 2.0 hadi tovuti 3.0 inayotumika sasa (Lai,Fan,Xin na Liang, 2013). Tovuti 1.0 ndiyo iliyotangulia na kimsingi ilisheheni matini iliyowekwa mtandaoni na wataalamu mbalimbali na kutumiwa kwa kiasi kidogo tu na watu walioisakura mitandao hiyo. Asasi anuwai, makampuni na waajiri mbalimbali waliitumia kwa asilimia 90 tovuti hii ili kuwawezesha kuwafikia wateja wao kwa kuweka habari muhimu mtandaoni (Nanehkaran, 2013). Tovuti 2.0 inayojulikana pia kama wavutijamii, iliibuka katika mwaka wa 2000 na iliwezesha mitagusano ya kijamii mitandaoni miongoni mwa watumiaji wengi walio na mahitaji sawa. Ujio wa majukwaa mapya ya kidijitali

mtandaoni uliibua matumizi ya tovuti 3.0 katika mwaka wa 2006. Kimsingi tovuti 3.0 iliboresha mitagusano mitandaoni kwa kuimarisha na kuhusisha data iliyopatikana mitandaoni kwa kuifanya rahisi kupatikana na kuoanishwa na mahitaji ya watumiaji wake.

Ili kukadiria mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili, vigezo mahususi vya tathmini yake huangaziwa. Miongoni mwa vigezo hivi ni vifuatavyo: Kwanza ushindani Mtandaoni. Ushindani mtandaoni kimsingi hudhihirishwa kwa matokeo ya ubora wa tovuti fulani miongoni mwa tovuti zote zilizosajiliwa kote ulimwenguni. Kwa mujibu wa Internet Live Stats (2018), idadi ya tovuti inakadiriwa kuwa takriban tovuti bilioni 1.9 kote ulimwenguni. Hili ni ongezeko kubwa kwa idadi hiyo ambayo ilikuwa milioni 2.4 miaka kumi ya awali mnano mwaka wa 1998 (Internet Live Stats, 2018). Ushindani mtandaoni ni kigezo kinachotumiwa kutathmini ufaafu wa tovuti kwa watumiaji wake. Tovuti ya Swahilihub ina tovuti nyingine zinazoshindana nayo. Hali hii inadhihirisha ushindani mkubwa miongoni mwa tovuti zinazopatikana mtandaoni kwani tovuti zote mtandaoni zinalenga watumiaji wale wale kote ulimwenguni ambao watateua tovuti bora kwa kuzingatia vigezo mbalimbali vya utendakazi wake. Kuna takriban usakuraji kwa kiwango cha bilioni 7.6 kila siku kote ulimwenguni (Net Market Share, 2018). Watumiaji wa tovuti ya Swahilihub wametapakaa kote ulimwenguni na hivyo basi ni muhimu ufaafu wake kwa watumiaji wake uwe msingi wa kuzingatiwa kwa umakini.

Pili, ni uhariri wa Matini Mtandaoni. Matini yanayowekwa kwenye tovuti ya Swahilihub huchangia pakubwa kuwahusisha watumiaji wengi na idadi hiyo ikiimarika itaboresha nafasi ya tovuti ya Swahilihub miongoni mwa tovuti wenza ulimwenguni. Idadi hii ni kigezo muhimu katika usambaaji na udumishaji wa hadhi ya Swahilihub mtandaoni. Tovuti ya Swahilihub ni aina ya tovuti ambayo ina uwezo wa kuhamisha mazingira

yaliyo mbali pamoja na watu na kuwaleta darasani ili kuendeleza taaluma ya Kiswahili kupitia michakato anuwai ya kieleimu. Tovuti ya Swahilihub huwa na habari iliyo ya kisasa. Aidha tovuti ya Swahilihub ina uwezo wa kuhifadhi habari nyingi na kuwawezesha wanafunzi kuchangiana mawazo kwa njia ya barua pepe.

Ingawa matumizi ya tovuti ya Swahilihub hayazingatiwi kikamilifu na watumiaji, umuhimu wake na nafasi yake katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili ni mkubwa mno (Maina, 2016).

Ili kuboresha matumizi ya tovuti ya Swahilihub, ni muhimu wahudumu wake wahakikishe kwamba matini kwenye vitengo vyote ni za thamani ya juu ili kuepuka matatizo yanayotokana na udhaifu wa thamani hususan ya matini husika. Ni muhimu wahudumu wa Swahilihub wahakikishe kwamba habari zote zinazoonyeshwa kwenye tovuti ya Swahilihub zinawiana na lengo kuu la ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Ni muhimu wahudumu wa tovuti ya Swahilihub wawatahadharishe watumiaji wake kutegemea kitengo kimoja pekee. Ili kuimarisha taaluma ya Kiswahili, ni muhimu watumiaji wa tovuti ya Swahilihub wazingatie takriban vitengo vyote ili kufaidika kutokana na michango muhimu katika kila kitengo. Mambo haya yote ni muhimu katika makadirio ya utendakazi wa tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili.

Tatu, ni ukubalifu wa Swahilihub miongoni mwa tovuti nyingine. Kwa kutegemea thamani ya matini ya Swahilihub tovuti nyingine huwapendekezea watumiaji wake kutumia tovuti ya Swahilihub ili kuyafikia mahitaji yao mtandaoni. Kwa msingi huu, kuna mitagusano miongoni mwa tovuti mitandaoni inayosababisha tovuti mbalimbali kuwaelekeza watumiaji wake kutumia tovuti fulani ili kupata habari inayohitajika (Moz, 2018). Mahusiano haya huchangia pakubwa kwa tovuti kuwaelekeza watumiaji wake kwa matini ya tovuti nyingine iliyo na matini ya thamani bora na ya kutegemewa. Mahusiano

bora miongoni mwa tovuti hutokea wakati tovuti moja inaporejelea tovuti nyingine kwa kutumia istilahi za kimsingi za tovuti hiyo na pia kupatikana kwenye tovuti nyingine iliyo na istilahi sawa au maudhui yanayowiana na matini ya tovuti awali (Beal, 2018). Mahusiano bora miongoni mwa tovuti huchangia kujenga mitagusano baina ya tovuti yenye hadhi katika taaluma fulani na hivyo basi kufaidika na mahusiano hayo ( Moogan, 2014).

Nne, ni usambaaji wa Swahilihub. Usambaaji wa Swahilihub huchangia usambaaji wa Kiswahili miongoni mwa watumiaji wake. Kigezo cha usambaaji kilitumiwa katika kutathmini mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili miongoni mwa watumiaji wake. Aidha, matokeo ya Internet Live Stats kuhusu idadi ya watumiaji wa mtandao kote ulimwenguni mnamo Julai mosi mwaka wa 2018 usiku wa manane yalionyesha idadi hiyo kuwa watumiaji billioni 3.96. Idadi ya watumiaji wa mtandao ikiwa kubwa kiasi hiki inaashiria umuhimu wa tovuti ya Swahilihub na haja ya kuimarisha mchango wake kwa watumiaji wake ambao tayari wanapatikana mtandaoni. Tovuti ya Swahilihub hivyo basi ina nafasi nzuri ya kuwafikia watumiaji hao wanaopatikana tayari mtandaoni kote ulimwenguni.

Tano, ni kurasa zilizorejelewa na watumiaji wa Swahilihub. Kigezo cha idadi ya kurasa zilizorejelewa kilitumiwa kukadiria mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Kigezo hiki kimetumika kupata matokeo kuhusu tovuti ya Swahilihub kwa kipindi cha kati ya mwaka wa 2016 hadi 2018. Data ya uchunguzi wa kigezo hiki hutumiwa kubainisha idadi ya matini yaliyowekwa kwenye tovuti ya Swahilihub na ambayo ilirejelewa na watumiaji wake. Makadirio ya ruwaza za habari mpya zinazowekwa kwenye tovuti ya Swahilihub kila mara yalitumika kuonyesha idadi ya kurasa za habari zinazotolewa baada ya kurejelewa kwa muda fulani. Kwa tovuti mwafaka

idadi ya matini mpya na ile inayotolewa inastahili kuwa sawa. Kwa kawaida idadi ya matini inayotolewa huzidi idadi ya zile zinazowekwa kila mara (Adormedia na wengine, 2015).

Tovuti ya Swahilihub ni mojawapo ya maendeleo yaliyoibuka mwanzoni mwa mwaka wa elfu mbili na kumi na mbili kutokana na vyombo vya habari vya kijamii. Huu ni mradi mahususi wa kukuza, kuendeleza na kuimarisha Kiswahili kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa kongoo matini katika lugha ya Kiswahili. Aidha, mradi wa Swahilihub hurahisisha utendaji kazi wa wadau wake pamoja na kuimarisha uendelezaji wa matumizi bora ya Kiswahili, uwazi na kuongeza ufanisi wa kitaaluma. Kifungu cha pili, sehemu ya saba ya katiba ya Kenya iliyorasimishwa mnamo mwaka wa 2010 kinasema kuwa Kiswahili ni lugha rasmi na vilevile ya kitaifa nchini Kenya. Lugha ya Kiswahili imekabiliana na changamoto si haba katika kujitwalia hadhi hii ya kuwa lugha ya taifa na vilevile lugha rasmi. Lugha mbalimbali kote ulimwenguni zimepitia mabadiliko makuu na sababu kuu ni matumizi yake kwenye mitandao ya kijamii. Lugha ya Kiswahili haijapiga hatua katika matumizi yake kwenye mitandao ya kijamii kama ilivyo lugha ya Kiingereza. Tangu kubuniwa kwa Tume ya Mackay 1981 iliyohusu sera za elirnu, Kiswahili kilikuwa tu lugha ya taifa mbali na kutumiwa katika kufundisha na kutahini rnitihani ya kitaifa (Moraa, 2012)

Majilio ya teknolojia mpya kila uchao yamechangia kuandikwa habari na kutolewa maoni katika tovuti. Teknolojia mpya imebadilisha mitagusano ya wanajamii hususan namna wanavyokutana na kushiriki katika mazungumzo na majadiliano (Jagero, 2015). Mwamko huu wa kiteknolojia umechangia kuimarisha mikondo ya mitagusano ya kijamii kwa kuwaangazia pakubwa watumiaji wa tovuti mbalimbali kidijitali. Hali hii imechangia

ongezeko kubwa katika idadi ya watu wanaozuru tovuti na kuchangia kuhusu masuala ya kijamii yanayowaathiri. Idadi ya watumiaji wa mitandao kote ulimwenguni mwanzoni mwa mwaka wa 2018 ilikuwa watu bilioni tatu nukta tisa (Internet Live Stats, 2018). Hali hii inadhihirisha kuwa kuna watu wengi wanaotumia tovuti mbalimbali kote ulimwenguni. Maendeleo haya ya kiteknolojia mitandaoni yanazidi kubadilisha namna masuala mbalimbali ya kijamii yanavyowasilishwa. Kutokana na idadi hii kubwa ya watumiaji wa mitandao kote ulimwenguni, tovuti ya Swahilihub ina nafasi muhimu ya kuimarisha ukuzaji wa Kiswahili kwa msingi wa usambaaji wake na udumishaji wa hadhi na dhima yake kote ulimwenguni.

Kufikia mwaka wa 2018, kulikuwa na takriban tovuti bilioni moja nukta tisa kote ulimwenguni (Internet Live Stats, 2018). Idadi hii inajumuisha tovuti ya Swahilihub iliyoimarisha shughuli zake za kuikuza taaluma ya Kiswahili tangu kuasisiwa kwake katika mwaka wa elfu mbili na kumi na mbili. Kuwepo kwa idadi kubwa ya tovuti na wasomaji wengi kumefanya mradi wa Swahilihub kuwa na nafasi ya kudumisha hadhi na dhima ya lugha ya Kiswahili na kwa ujumla kutoa mwelekeo kuhusu mikakati mwafaka ya kuimarisha matumizi ya lugha ya Kiswahili mtandaoni.

Kwa muda mrefu sasa, lugha ya Kiingereza imeendelea kutumika zaidi na kutawala shughuli na mitagusano mitandaoni. Hata hivyo, mnamo mwaka wa 2010 zaidi ya asilimia sitini ya idadi ya watu walitumia lugha nyinginezo zisizo Kiingereza (King, 2010). Kuna mabadiliko katika mkondo wa takwimu za wanaotumia lugha mbalimbali mtandaoni (King 2010). Hali hii inaendelea kubadilika kwani lugha nyingine zimeanza kutumika zaidi mtandaoni kutokana na ongezeko kubwa la idadi ya tovuti pamoja na watumiaji wa tovuti hizi kote ulimwenguni. Hali hiyo ya wingi lugha na tofauti za kitamaduni katika

mtandao imesababisha kuwepo kwa vyombo vya habari vya kijamii vyenye wingi lugha, vikiwa na matumizi ya kipekee ulimwenguni (King, 2010).

Lugha ya Kichina ilikuwa ya pili iliyopendwa na kutumika katika mtandao baada ya Kiingereza (internetworldstates.com). Kwa sasa, mbali na lugha ya Kiingereza na Kichina, lugha ya Kiswahili inatumika katika mitandao mbalimbali kuandika habari na kutoa maoni kuhusu maswala ya kijamii. Isitoshe lugha ya Kiswahili ina nafasi muhimu ya kubuni na kusambaza dhana anuai mtandaoni, hali ambayo imezua changamoto kubwa ya kubuni sera na mikakati maalum ya matumizi ya tovuti ya Swahilihub.

Hivyo basi, ukuzaji wa lugha ya Kiswahili katika tovuti ya Swahilihub hauwezi kupuuzwa. Kuvumbuliwa kwa vyombo vya habari vya kielektroniki kumeleta mapinduzi kuhusu jinsi habari zinavyokusanywa na kusambazwa kote ulimwenguni (Simmsons, 2005). Kutokana na mabadiliko haya ya kiteknolojia na mwamko mkubwa wa matumizi ya tovuti mitandaoni, kuna haja kubwa ya kutathmini tovuti ya Swahilihub ili kubaini mchango wake katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili.

Madden, (2016) anadahili kwamba uhusishaji wa watumiaji wa mitandao ya kijamii ni kigezo kinachodhihirisha mahusiano faafu baina ya wasimamizi na watumiaji wa tovuti mbalimbali. Ndiposa wataalam wa Kiswahili waliona haja ya kuhusisha tovuti katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili na kubuni tovuti ya Swahilihub. Kiswahili ni lugha ya kimatiafa inayosomwa kupitia kwa mtandao na ambayo ina nafasi katika kumudu teknolojia mpya zinazojiri kila uchao. Tovuti ya Swahilihub kwa upande mwingine ni teknolojia mpya inayohitaji lugha ya Kiswahili kuimarisha usambazaji na ukubalifu wake miongoni mwa mamilioni ya watumiaji wa lugha hii. Lugha ya Kiswahili inakadiriwa kuzungumzwa na watu wapatao milioni sitini hapa Afrika Mashariki na kati (Guy De Pauw1, Gilles-Maurice de Schryver, and Peter W. Wagacha, 2006). Lugha hii pia

inatumika katika sehemu zingine ulimwenguni kama vile Marekani, Uarabuni, Ulaya na bara Asia. Hivyo basi lugha hii imefikia kiwango cha matumizi mapana ulimwenguni na kwa hivyo ni lugha mwafaka ikitumika kama chombo cha kusambaza uvumbuzi mpya (Msanjila, 2002).

## 2.7 Hitimisho

Sura hii ilihakiki maandishi yanayohusu ukuzaji wa lugha, TEHAMA katika ukuzaji wa lugha, ukuzaji wa Kiswahili, ukuzaji wa Kiswahili nchini Kenya pamoja na Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili nchini Kenya. Sehemu hii pia imetoa maelezo kuhusu vyombo vya habari vya kijamii na mabadiliko katika lugha, malengo na mafanikio ya Swahiulihub ili kudhihirisha pengo. Utafiti huu uliziba pengo hilo kwa kutathmini Swahilihub katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili.

Kijumla, katika sehemu hii tumehakiki maandishi mbalimbali kwa kutambua mitazamo na maoni ya wataalamu mbalimbali kuhusu ukuzaji wa lugha kwa jumla na nafasi ya tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Kwa kushughulikia dhana na umuhimu wa ukuzaji wa lugha kwenye tovuti ya Swahilihub tumeonyesha kuwa tovuti ya Swahilihub ni muhimu kwa kubaini nafasi yake kwa ujenzi wa lugha ya Kiswahili, usambaaji wake na udumishaji wa hadhi na dhima yake miongoni mwa watumiaji wake mitandaoni. Isitoshe, uhakiki wa maandishi kuhusu mijadala ibuka juu ya nafasi ya Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili nchini Kenya umeonyesha kuwa tovuti ya Swahilihub hutumika katika ujenzi wa Kiswahili, usambaaji wake na udumishaji wa hadhi na dhima yake kwa kujadili maswala ya kijamii na kitaaluma katika lugha ya Kiswahili mtandaoni. Kutokana na uhakiki wa maandishi hayo, imebainika kuwa kulikuwa na pengo lililofaa kuzibwa ambalo kwanza lilikuwa ni kubainisha viwango vya ukuzaji wa

Kiswahili miongoni mwa watumiaji wa Swahilihub. Kisha kutathmini tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili. Kadhalika, uhakiki wa maandishi umebaini historia ya tovuti ya Swahilihub, maendeleo, malengo, umuhimu na mustakabali wake na changamoto zinazokumba ukuzaji wa Kiswahili miongoni mwa watumiaji wake.

Hivyo basi, pengo lililobainika na ambalo lilifaa kuzibwa lilikuwa ni kudadavua mambo yanayochangia ukuzaji wa Kiswahili kwenye tovuti ya Swahilihub na namna ambavyo lugha ya Kiswahili inavyoweza kuchukuana na mabadiliko na maendeleo ya kiteknolojia mtandaoni. Kudadavuliwa kwa mambo hayo kulisaidia kuonyesha namna mambo hayo yanavyoweza kuathiri ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kiteknolojia mtandaoni. Aidha, juhudi mbalimbali za ukuzaji wa Kiswahili katika enzi za kiteknolojia zimeelezwa kwa kutaka kuonyesha umuhimu wa hatua hizo. Mwisho, uhakiki wa maandishi kuhusu tovuti ya Swahilihub na mabadiliko katika lugha umetoa maelezo kuonyesha namna lugha inavyotumika katika TEHAMA. Kwa kufanya hivyo, tumeonyesha pengo lililofaa kuzibwa ambalo ni kutathmini tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili nchini Kenya.

# SURA YA TATU

# MUUNDO WA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inahusu muundo wa utafiti na imepambanuliwa kupitia maelezo kuhusu vipengele vufuatavyo: mwelekeo mseto wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli ya utafiti, njia za utafiti, mbinu za utafiti, vifaa vya utafiti, utaratibu wa uchunguzi na uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo pamoja na maadili yaliyoongoza na kukamilisha utafiti.

## 3.2 Mwelekeo Mseto wa Utafiti

Utafiti huu ulitumia mwelekeo mseto wa utafiti ili kuyaafiki madhumuni. Mwelekeo mseto wa utafiti ni mtindo wa kukusanya na kuchanganua data unaochanganya mbinu za kimaelezo pamoja na mbinu za kijarabati. Kulingana na Green (1989), mwelekeo mseto wa utafiti huhusisha mbinu moja ya kijarabati (inayolenga kukusanya data ya kitakwimu) na mbinu moja ya kimaelezo (inayolenga kukusanya data ya kimaelezo) ambapo mbinu zote mbili zinatumika kwa pamoja katika utafiti mmoja. Mwelekeo mseto wa utafiti ulianza kupendekezwa kutumika mwishoni mwa miaka ya themanini wakati watafiti kutoka nyanja mbalimbali za kiakademia kama vile soshioljia na lugha walipoanza kujadili uwezekano wa mbinu ya tatu ya utafiti. Mwelekeo mseto umeanza kupata umaarufu kama njia ya tatu ya kufanya utafiti miongoni mwa watafiti wengi hata ingawa mbinu za utafiti ambazo zimekuwa zikitumika kwa wingi hapo awali ni zile za kimaelezo na kijarabati (Johnson na Omweugbuzie 2004, Cresswell na Clark 2011).

Watafiti hawa walikuwa kama vile Fielding na Fielding (1986) kutoka Uingereza, Brewer na Hunter (1989), Green (1989) kutoka Marekani, Morse (1991), Rallis (1994) na

Cresswell (2003). Watafiti hawa walianza kufanya utafiti wakitumia mwelekeo mseto wa utafiti na kuandika vitabu kuhusu mwelekeo mseto wa utafiti kama njia ya tatu ya kufanya utafiti.

Kulingana na Johnson (2007), uchanganyaji wa mbinu hizi mbili katika utafiti mmoja unaweza kutokea katika hatua zote za utafiti. Katika utafiti huu, matumizi ya mwelekeo mseto wa utafiti yalifanikisha ukusanyaji wa data na uchanganuzi wake kwa kutumia mbinu za kijarabati na kimaelezo kwa pamoja kwa namna ambayo zilichangiana kwa njia sawa. Aidha mwelekeo mseto wa utafiti katika utafiti huu ulihakikisha kuwa mbinu za kijarabati na kimaelezo za utafiti zimechanganywa katika muundo mahususi ili kuelekeza mpangilio wa kufanya utafiti mzima. Mwelekeo huu ulikuwa bora kwa utafiti huu kwa sababu ulichangia pakubwa kupata data ya kina zaidi kuhusu matumizi ya mradi wa Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili.

Kutokana na mapendekezo ya Johnson na Onweugbuzie (2004) mwelekeo mseto wa utafiti ulitumika katika utafiti huu kwa njia inayohusisha matumizi ya mbinu za kimaelezo na kijarabati kwa pamoja. Naye Gray (2009) anaelezea mwelekeo mseto wa utafiti kama ukusanyaji au uchanganuzi wa data uliotokana na mchanganyiko wa mbinu za kimaelezo na kijarabati katika utafiti mmoja ambapo data za aina hizi mbili zimekusanywa. Mwelekeo huu mseto ulitumika kwa kuhusisha mbinu mbili katika utafiti huu kwa njia ya kufaana na kukamilishana. Mbinu ya kimaelezo pamoja na kijarabati zilitumika pamoja ili kutathmini utendakazi wa mradi wa Swahilihub. Pale ambapo mbinu ya kijarabati ilikuwa na udhaifu mbinu ya kimaelezo ilifidia udhaifu huu na hivyo basi utafiti huu uliimarika. Mwelekeo mseto wa utafiti ulichangia kuongeza uthabiti wa matokeo ya utafiti huu kwa kupuuzilia mbali udhaifu wa mbinu za kijarabati na kimaelezo za kukusanya na

kuchanganua data. Kwa upande mmoja mbinu ya kijarabati hutegemea tu takwimu zinazojitokeza na kupuuza maelezo kutoka kwa wahojiwa. Kwa upande ule mwingine, mbinu ya kimaelezo hutegemea zaidi maoni ya wahojiwa kuhusu suala fulani. Udhaifu wa mbinu hizi uliepukwa kwa kutumia mbinu zote mbili katika utafiti huu kwa pamoja kama mbinu mseto. Vile vile, mwelekeo mseto wa utafiti ulichangia kuibua data ya kina zaidi ikilinganishwa na aidha mbinu ya kijarabati ama kimaelezo. Hii ni kwa sababu vifaa mbalimbali vya kukusanya data vilihusishwa katika utafiti huu mmoja.


Hata hivyo, katika kutumia mweleleko huu wa utafiti, udhaifu wake ulibainika kwa kuwa haukuweza kuzua data pale ambapo watumiaji wa tovuti ya Swahilihub hawakufurahia kutoa habari zinazolenga uwajibikaji wao katika matumzi ya tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili. Ili kukabiliana na udhaifu wa mwelekeo huu utafiti huu ulizua data kupitia matumizi ya ARhefs, Similarweb na uchunzaji. Matumizi ya kifaa cha ARhefs na Smilarweb yalichangia pakubwa kuzua data muhimu kuhusu utendakazi wa tovuti ya Swahilihub. Isitoshe watafitiwa wengi walikuwa wataalamu ambao angalau walikuwa na tajriba na hivyo basi kuelewa nafasi ya tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili.

Aidha katika kuutumia mwelekeo mseto wa utafiti ujuzi wa kutosha wa kutumia mbinu za kijarabati na kimaelezo ulihitajika ili kuimarisha uchanganuzi wa data ya kijarabati ambayo wakati mwingine huwatatiza watafiti. Vile vile mtafiti alihitaji ufahamu wa jinsi ya kutayarisha na kutumia vifaa mbalimbali vya utafiti vilivyotumiwa katika mbinu ya kijarabati kama vile ARhefs na mbinu ya kimaelezo kama vile maswali ya mahojiano.

Matayarisho haya yalichangia pakubwa kwa utafiti huu kutumia wakati mwingi katika hatua ya ukusanyaji na uchanganuzi wa data kwa vile mwelekeo huu hutumia vifaa vingi

vya kukusanya data na data inayopatikana ni nyingi vile vile. Aidha matumizi ya mwelekeo mseto wa utafiti katika utafiti huu yalichangia gharama ya juu katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data kutokana na ugumu wa kimatumizi wa vifaa vya Arhefs na Similarweb katika utafiti huu. Hali hii ilipelekea maingiliano makubwa kati ya mtafiti, watafitiwa na wataalamu wa kidijitali.

Kwa mujibu wa Cresswell (2011), mwelekeo mseto wa utafiti unaweza kuchukua miundo ama sura mbalimbali unapotumiwa katika utafiti. Miundo hii hutegemea jinsi mtafiti anavyopanga kutumia mbinu za kijarabati na kimaelezo katika utafiti wake. Kwa mfano, mtafiti anaweza akaanza kwa kutumia mbinu ya kijarabati na baadaye akatumia mbinu ya kimaelezo yaani kwa mfululizo. Aidha, mtafiti anaweza akatumia mbinu hizi mbili kwa njia sambamba. Utafiti huu ulitumia mpangilio sambamba wa mbinu changamano ya utafiti. Katika mpangilio huu, mtafiti alitumia mbinu ya utafiti ya kijarabati na kimaelezo kwa karibu kiwango sawa kila moja ya mbinu hizi mbili ikitumika kwa njia huru kutokana na ile nyingine katika hatua ya kukusanya data. Hatimaye, data hii ililetwa pamoja na kufasiriwa kwa pamoja kabla ya matokeo ya mwisho kupatikana. Katika mchoro ufuatao, mpangilio huu wa mwelekeo mseto wa utafiti uliofuatwa katika utafiti huu unadhihirika.




***Mchoro SURA YA TATU .2: Mpangilio Sambamba wa Mwelekeo Mseto wa Utafiti***

Mwelekeo mseto wa utafiti ulichangia pakubwa katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data kwa kuchanganya mbinu za kijarabati na kimaelezo katika utafiti huu ili kuelewa tovuti ya Swahilihub vyema zaidi. Kwa kutumia mbinu hii, utafiti huu ulihusisha mbinu ya kijarabati iliyotufaa kukusanya data ya kitakwimu kuhusu viwango vya utendakazi na ustahilifu wa tovuti ya Swahilihub kwa kutumia ARhefs na Similarweb pamoja na mbinu ya kimaelezo iliyolenga kukusanya data ya kimaelezo kutoka kwa watumiaji mbalimbali wa tovuti ya Swahilihub kuhusu changamoto na mustakabali wake. Ili kufanikisha utafiti huu, mwelekeo changamano wa utafiti ulikuwa msingi wa ukusanyaji na uchanganuzi wa data iliyotokana na mchanganyiko wa mbinu za kimaelezo na kijarabati. Katika utafiti huu

data za aina mbili za kijarabati na kimaelezo zilikusanywa. Aidha, mwelekeo mseto wa utafiti ulituwezesha kukusanya, kuchanganua data, kutayarisha matokeo ya utafiti na kufikia maamuzi yaliyotufaa katika kutoa mapendekezo mwafaka (Taz 5.2 na 5.3). Katika utafiti huu, mtindo wa mwelekeo mseto wa utafiti ulitumiwa katika hatua ya ukusanyaji na uchanganuzi wa data kutoka kwa mbinu zote mbili za kimaelezo na kijarabati. Mbinu za kijarabati na kimaelezo za utafiti zilichanganywa katika muundo mahsusi ili kuelekeza mpangilio wa kufanya utafiti mzima. Mbinu zote mbili zilitumika kwa pamoja katika utafiti huu.

Ili kutoa tathmini mwafaka kuhusu utendakazi wa mradi wa Swahilihub, mbinu za kijarabati katika mwelekeo mseto wa utafiti zilitumiwa kupanua upeo wa utafiti huu kwa kutumia vifaa mbalimbali vya utafiti vikiwemo ARhefs pamoja na Similarweb. Utendakazi wa Swahilihub ulibainishwa kwa kuangazia data zilizorejelea kupatikana kwa matini inayohitajika pamoja na urahisi wa kufikiwa kwa Swahilihub kupitia juhudi za kuondoa vizingiti vinavyowazuia watumiaji wake kuchagua na kusakura habari wanazohitaji kutoka kwa tovuti ya Swahilihub. Utendakazi wa tovuti ya Swahilihub ni kigezo muhimu katika utathmini wake kwa kuwa lengo kuu la mradi wa Swahilihub ni kuhifadhi na kufikisha habari kama inavyohitajika na watumiaji wake. Utafiti huu ulijikita katika kutathmni kijarabati ubora wa matini ya Swahilihub na sifa zake zinazowafanya watumiaji wake kuirejelea katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili.

Utafiti huu ulitumia mbinu za kijarabati na kitakwimu zilizohusisha tathmini ya vigezo vya utendakazi wa tovuti ya Swahilihub kwenye ARhefs ambacho ni kifaa na programu mahususi ya kiteknolojia ya tarakilishi iliyobainisha vigezo vyote mahususi vya ubora na utendakazi wa tovuti ya Swahilihub. Mbinu hii ya kijarabati ilikuwa bora kwa sababu ya

uwezo wake wa kukabiliana na idadi kubwa ya data inayopatikana kwenye tovuti ya Swahilihub kutokana na idadi kubwa ya watumiaji wake. Kwa kutumia mbinu za kijarabati utafiti huu ulibainisha vigezo maalum vya kukadiria kiwango cha ubora wa utendakazi wa tovuti ya Swahilihub. Vigezo hivi vilikuwa misingi ya kukadiria kiwango cha ufanisi wa tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa watumiaji wake nchini Kenya. Vigezo hivi vilikadiria kiwango cha matumizi ya matini kwenye tovuti ya Swahilihub pamoja na kiasi cha uhusika wa watumiaji wake mtandaoni. Utafiti huu ulikusanya data ya kitakwimu kwa kutumia Arhefs na

Similarweb huku data ya kimaelezo ikipatikana kwa kutumia mbinu anuai za kimaelezo. Data ya kitakwimu ilihusisha hoja muhimu kuhusu utendakazi wa Swahilihub huku data ya kimaelezo ikitokana na maelezo ya watumiaji mbalimbali wa Swahilihub. Ili kufanikiwa katika kutathmini utendakazi wa mradi wa Swahilihub kijarabati, utafiti huu uliangazia sifa za tovuti ya Swahilihub za kimsingi zinazoifanya kuwaridhisha watumiaji wengi iwezekanavyo mtandaoni. Miongoni mwa sifa hizi muhimu zilizoangaziwa kijarabati ni pamoja na ufaafu wake kimatumizi na ufaafu wake kiuamilifu.

Mrejesho wa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub kuhusu utendakazi wake ni kigezo muhimu cha ubora wake unaotokana na jinsi matarajio yao yanavyofikiwa kila wanapoutumia mradi wa Swahilihub. Mrejesho huu uliangazia urahisi wa tovuti ya

Swahilihub kufikiwa na watumiaji wake na kubainisha vipengele vya tovuti ya Swahilihub vinavyoifanya kuwa rahisi kutumika na hivyo basi kupata watumiaji wengi mtandaoni. Cresswell anatoa mfano kuwa iwapo mtafiti anatumia mtindo wa utafiti wa kisoroveya ambapo inamlazimu kutumia mbinu ya kijarabati ya utafiti, huenda akahitaji data zaidi iliyotokana na mbinu ya kimaelezo ya utafiti. Utafiti huu ulitumia mtindo wa usoroveya. Mtindo wa kisoroveya ulitumiwa katika utafiti huu ili kupata data kutoka kwa watumiaji

wa tovuti ya Swahilihub kwa lengo la kubainisha hali ya sasa ya ukuzaji wa Kiswahili miongoni mwa watumiaji wake (Taz. Mugenda, 2008).

Kutokana na mtindo wa utafiti wa kisoroveya, utaratibu wa kukusanya data kwa kutumia hojaji na mahojiano kutoka kwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub ulitumiwa. Hali hii ilichangia kupatikana kwa matokeo yaliyoelezea maoni, mielekeo na sifa za watumiaji wa tovuti ya Swahilihub. Utafiti huu ulitumia mtindo wa usoroveya-elezi ili kufanikisha uchunguzi wa kimaelezo miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub. Kupitia mbinu za kimaelezo za ukusanyaji data kama vile hojaji, mijadala na mahojiano, watumiaji wa tovuti ya Swahilihub walipata fursa ya kubainisha vipengee vya urahisi wa kimatumizi wa mradi wa Swahilihub kutokana na muundo wake ulivyoratibiwa wakati wa ujenzi wake.

Mbinu za kimaelezo zilitumika kufidia data zilizopatikana kijarabati ili kuufikia mrejesho huu wa watumiaji wa mradi wa Swahilihub. Mbinu za kimaelezo katika utafiti huu zilitumika kwa sababu data zilizopatikana katika utafiti kwa kutumia mbinu ya utafiti ya kijarabati zilihitaji kufafanuliwa kimaelezo ili kupata matokeo ya kutegemeka zaidi. Aidha mbinu za kimaelezo zilitumika katika utafiti huu kwa kuwa data zilizokusanywa kwa mbinu za kijarabati hazikujitosheleza kikamilifu na kulazimu zifafanuliwe zaidi kwa data nyingine zilizokusanywa kwa mbinu za kimaelezo. Hivyo basi katika utafiti huu, data za kimaelezo zilizokusanywa kwa kutumia mahojiano na mijadala ya kimakundi zilitumika kufafanua zaidi data zilizopatikana kijarabati kupitia mchakato wa kiuchanganuzi wa Arhefs pamoja na Similarweb.

Ili kuweza kuyajibu maswali ya utafiti huu, mwelekeo mseto wa utafiti ulitumiwa kama mbinu mwafaka zaidi ya utafiti. Hii ni kwa sababu utafiti huu ulihusisha data ya kijarabati

na kimaelezo. Katika utafiti huu, data iliyokusanywa kwa ama mbinu ya kijarabati au kimaelezo haikujitosheleza kikamilifu ndiposa ilibidi ifafanuliwe zaidi kwa data nyingine iliyokusanywa kwa mbinu ya kimaelezo. Data ya kijarabati ilitokana na uchunguzi wa Arhefs na Similarweb kuhusu utendakazi na ustahilifu wa tovuti ya Swahilihub na hojaji za matumizi na ukuzaji wa Kiswahili miongoni mwa watumiaji wa mradi wa Swahilihub ilhali data ya kimaelezo ilitokana na majibu ya mijadala ya kimakundi kuhusu changamoto na mustakabali wa tovuti ya Swahilihub nchini Kenya. Aidha, sio ama data ya kijarabati au ya kimaelezo ambayo ingeweza kuyajibu maswali ya utafiti huu kikamilifu. Basi mbinu hizi za kijarabati na kimaelezo zilitumika kwa pamoja katika utafiti huu ili kuchangiana katika kukusanya na kuchanganua data na hivyo basi kuyajibu maswali ya utafiti kwa njia iliyo wazi iwezekanavyo.

Katika utafiti huu, mwelekeo mseto unaohusisha mbinu za kijarabati na kimaelezo ulitumiwa katika hatua ya ukusanyaji na uchanganuzi wa data kutoka kwa mbinu zote mbili za kimaelezo na kijarabati. Mwelekeo huu mseto ulitumika kupima vipengele vya utafiti katika tathmini ya utendakazi wa mradi wa Swahilihub. Vipengele vya utendakazi wa Swahilihub vinaingiliana hali ambayo ilihitaji mwelekeo huu changamano wa utafiti ili kubaini viwango mbalimbali vya utendakazi na ustahilifu wa vitengo anuai vya Swahilihub kijarabati na kisha kuitolea data maelezo mwafaka kwa kutumia mbinu mbalimbali za kimaelezo.  Hii ni kumaanisha kuwa utafiti huu ulitumia mbinu za kimaelezo pamoja na mbinu za kijarabati kwa pamoja wala sio moja baada ya nyingine. Mwelekeo mseto wa utafiti ulitumika kutoa mwanga zaidi katika vipengele mbalimbali vya utendakazi na ustahilifu wa mradi wa Swahilihub miongoni mwa watumiaji wake.

Udhaifu wa mbinu hizi ulikwepwa kwa kuzitumia mbinu zote mbili katika utafiti huu kama mbinu mseto. Mtafiti alizingatia ujuzi wa kutosha wa kutumia mbinu za kijarabati na kimaelezo ili kukabiliana na tatizo la kuchanganua data ya kijarabati iliyotokana na ARhefs na Similarweb. Vile vile mtafiti alitayarisha na kutumia vifaa mbalimbali vya utafiti vilivyotumiwa katika mbinu ya kijarabati kama vile Arhefs, hojaji na mbinu ya kimaelezo kama vile mijadala na maswali ya mahojiano. Mtafiti aliitengea muda wa kutosha kazi hii kwa kuwa mwelekeo mseto ulihitaji wakati mwingi katika hatua ya ukusanyaji na uchanganuzi wa data kwa vile mbinu hii hutumia vifaa vingi vya kukusanya data na data iliyopatikana ni nyingi vile vile. Isitoshe kiasi cha fedha zilizohitajika zilitumiwa ili kukidhi mahitaji ya gharama ya juu inayotokana na mbinu mseto kwa vile ilitumia vifaa vingi vya utafiti na vilivyombidi mtafiti kuingiliana na wahojiwa kwa wingi.

Kutokana na matumizi ya mwelekeo mseto katika utafiti huu, tulifaulu kupata matokeo ya kina zaidi kuhusu utendakazi, ustahilifu, changamoto na mustakabali wa tovuti ya Swahilihub kwa kuwa mbinu za kijarabati na kimaelezo zilifaana na kukamilishana. Hali hii ilichangia kupanua upeo wa utafiti huu kwa kutafitia vifaa mbalimbali vya utafiti. Isitoshe, mwelekeo mseto wa utafiti uliongeza uthabiti wa matokeo ya utafiti kuhusu tovuti ya Swahilihub kwa kupuuzilia mbali udhaifu wa mbinu za kijarabati na kimaelezo za kukusanya na kuchanganua data. Kwa upande mmoja mbinu ya kijarabati katika utafiti huu haikutegemea tu takwimu zilizojitokeza kwa ARhefs na Similarweb na kupuuza maelezo kutoka kwa wahojiwa. Kwa upande ule mwingine, katika utafiti huu mbinu ya kimaelezo ilitegemea zaidi maoni ya wahojiwa kuhusu tovuti ya Swahilihub. Hali hii ilichangia kukwepa udhaifu unaotokana na mwelekeo huu wa utafiti.

### 3.3 Eneo la utafiti

Utafiti huu ulifanyika kwenye Swahilihub ambayo ni tovuti ya kitaaluma inayomilikiwa na Nation Media Group. Ujio wa mitandao umebadili mikondo ya utangamano na kwa sasa majukwaa ya kidijitali ndiyo maeneo makuu ya maenezi na ukuzaji wa lugha. Aidha data ya utafiti huu ilikusanywa kutoka vyuo vikuu kumi nchini Kenya. Utafiti huu uliendeshwa maktabani na mtandaoni. Maktabani, usomaji na upekuzi mpana wa vitabu, majarida, magazeti hasa gazeti la *Taifa Leo* na tasnifu zinazohusiana na mada hii umefanywa. Vilevile tumesakura mtandao ili kusoma yale yaliyoandikwa kuhusu mada.
Zoezi hili la usomaji maktabani na usakuraji mtandaoni lililofanyika kati ya mwaka wa 2014 hadi mwaka wa 2019 lilituwezesha kung'amua dhana za kimsingi, kuelewa kwa kina mihimili ya nadharia iliyotegemewa katika uchanganuzi wa data. Aidha usomaji huu umempevusha mtafiti kuhusu uhakiki wa maandishi kuhusu mada na kumsaidia kupata data muhimu iliyohitajika katika utafiti huu.

### 3.4 Sampuli ya Utafiti

Uteuzi wa sampuli katika utafiti huu ulielekezwa na aina mbalimbali za sampuli ili kuyakidhi madhumuni mahususi ya utafiti huu. Ingawa kuna aina mbalimbali za sampuli utafiti huu ulijikita tu kwenye aina tatu za sampuli zikiwa pamoja na sampuli kusudio, sampuli nasibu na sampuli elekezi. Uchunguzi wa kimaelezo ulijumuisha hali ilivyo kuhusu nafasi ya tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili nchini Kenya kwa kuhusisha michakato ya uchanganuzi, uainishaji na upimaji. (Taz. Ipara,2003). Mtindo wa usoroveya-elezi ulikuwa bora kwa utafiti huu kwa sababu uliwezesha uchunguzi wa kina kufanyika na kubainisha changamoto na mustakabali wa tovuti ya Swahilihub. Hii ni kwa sababu vifaa kadhaa vya ukusanyaji wa data vilitumiwa na pia

mtindo huu ulitoa nafasi kubwa ya kufanya utazamaji nyanjani. Usoroveya pia katika utafiti huu uliwezesha ukusanyaji data haraka na kupata majumui kuhusu watumiaji wa tovuti ya Swahilihub kutoka kwa sampuli ndogo iliyoteuliwa na kutumiwa. Hivyo basi, mtindo wa kisoroveya ulifanikisha upatikanaji wa habari katika hali halisi wakati wa utafiti kutoka kwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub. Utafiti huu ulitumia mtindo wa kisoroveya wa sampuli ndogo kwa vile ulilenga sampuli ndogo ya watumiaji wa mradi wa Swahilihub vyuoni nchini Kenya. (Taz. Schilling (2013: 106), Cresswell na Clark, 2011).

Uteuzi wa sampuli ulifanywa kwa njia ya kimakusudi. Sampuli kimakusudi ilihusu uteuzi wa moja kwa moja wa tovuti ya Swahilihub miongoni mwa mitandao mingine ya kijamii kwa sababu ya sifa zake maluum zilizolengwa kwenye utafiti huu. Mtafiti aliteua kimakusudi tovuti ya Swahilihub miongoni mwa mitandao ya kijamii kwa kuwa ni tovuti inayotumia Kiswahili kutoka kwa sampuli kubwa ya mitandao yote ya kijamii. Hii ni kwa sababu mitandao ni mingi lakini si yote imeandikwa kwa Kiswahili au ina matumizi ya Kiswahili. Kwa mujibu wa Kothari (2004), sampuli makusudi hutokana na uteuzi wa kimakusudi ambapo mtafiti huchagua vipengele ambavyo hutumiwa kama sampuli kuwakilisha kikundi cha watu. Mugenda na Mugenda (1999) wanasema kuwa mbinu hii inamruhusu mtafiti kutumia watu, vitu, hali au tabia ambazo zina taarifa inayohitajika kwa kuzingatia malengo ya mtafiti.

Uteuzi wa sampuli kimakusudi ni mbinu muhimu ya uteuzi wa sampuli isiyokuwa ya kubahatisha iliyompa mtafiti uhuru wa kuteuwa tovuti ya Swahilihub kwa kutegemea upekee wake katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Tovuti ya Swahilihub iliteuliwa kimaksudi kwa kuzingatia upekee wake wa kutoa data muhimu na ya kutosha katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kikamilifu. Isitoshe sampuli hii ilikuwa mwafaka katika

utafiti huu kwa sababu tovuti ya Swahilihub iliakisiwa kuwa ndiyo tovuti iliyokuwa na data mwafaka kuhusu ukuzaji wa lugha ya Kiswahili mtandaoni. Hali hii ilichangia pakubwa katika kuteua sampuli iliyokuwa na habari mahususi kuhusu matumizi na ukuzaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub.

Aidha, Mugenda na Mugenda (2013) wanazidi kueleza kuwa rnbinu hii ya uteuzi wa sampuli kimakusudi inaweza kuambatana na matumizi ya mbinu nyingine ili kupata sampuli halisi. Hivyo basi sampuli ya kinasibu pia ilitumika katika kuchagua watumiaji wa Swahilihub kutoka vyuo mbalimbali vilivyoshirikishwa katika utafiti huu. Sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kinasibu kwa kuhakikisha kuwa kila mhusika miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub aliwakilishwa katika sampuli kwa njia sawa na kwa kuepukana na mapendeleo. (Taz Best na Khan 2010:35).

Mchakato huu wa uteuzi wa sampuli ulihakikisha kwamba sampuli ya utafiti huu haikuteuliwa kiholela yaani bila kufuata utaratibu wo wote ule bali utaratibu maalum wa uteuzi wa sampuli ulizingatiwa. Isitoshe, sampuli elekezi pia ilitumiwa katika kubaini jumuiya finyu na hatimaye sampuli halisi ya utafiti. Sampuli elekezi ni mbinu ya kuteuwa sampuli ambapo mhusika mmoja katika jumuiya hutumiwa na mtafiti katika kuwafikia wahusika wengine ambao wana sifa ambazo zitafaa utafiti wake (Best na Khan 2010). Sampuli elekezi ilitumiwa katika utafiti huu kwa kuwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub huwa wametapakaa au kuchanganyika katika mitandao kote ulimwenguni. Hivyo basi, baada ya kuwapata watafitiwa wachache walioitumia tovuti ya Swahilihub, walitumiwa kuwafikia wengine walioitumia tovuti ya Swahilihub katika shughuli za ukuzaji wa lugha ya Kiswahili.

Jumuiya ya utafiti wetu ilikuwa na watumiaji wa mitandao anuwai kutoka vyuo vikuu tofauti na hivyo basi ili kuwafikia watumiaji wa tovuti ya Swahilihub pekee, mbinu ya sampuli elekezi ilitufaidi. Mbinu elekezi ilitumika hasa pale mwanafunzi mmoja wa kila mwaka katika kila chuo kikuu alitumiwa kuwaelekeza watafiti kwa wanafunzi wengine waliokuwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub. Kusudi la kutumia sampuli elekezi lilikuwa kuweza kupata sampuli ya utafti huu kwa haraka na kwa uhakika zaidi.

Baada ya kuhakikisha kuwa watumiaji wote waliopatikana kwa kutumia mbinu elekezi walikuwa wanafunzi wa vyuo vikuu na watumiaji wa tovuti ya Swahilihub, mbinu ya sampuli nasibu ilitumiwa ili kuchagua sampuli ya wanafunzi waliohusika katika utafiti huu. Mbinu ya sampuli nasibu ilihakikisha kwamba nafasi sawa imetolewa kwa kila mhusika katika jumuiya finyu iliyoshirikishwa katika utafiti huu.

Uteuzi wa watafitiwa katika utafiti huu uliegemezwa kwenye misingi ya nadharia ya Msambao wa Uvumbuzi wa Rodgers (2003). Kutokana na msingi wa mitagusano ya kihomofilia na kiheterofilia ilikuwa rahisi kuwateua watumiaji mbalimbali wa mradi wa Swahilihub na kuwashirikisha katika utafiti huu. Wale waliokuwa na mitagusano ya kihomofilia kama vile wanafunzi wa taaluma ya Kiswahili pamoja na viongozi wao wanaoheshimiwa miongoni mwao.

Kwa kutumia aina hizi tatu za sampuli, utafiti huu uliteua idadi ndogo ya wanafunzi 320 kutoka vyuo kumi nchini Kenya, wahadhiri 15 na wahudumu wa 5 wa Nation Media Group ili kuwakilisha watumiaji wa tovuti ya Swahilihub (Schilling, 2007:168, Best na Khan, 2010, Milroy 1987:54, Patrick, 2009). Utafiti wetu ulifuata mchakato maalum wa kisayansijamii uliopendekezwa na Patrick, (2009) ili kupata sampuli mwafaka ambayo iliweza kutoa uwakilishi kamili wa jumuiya ya utafiti. Patrick (2009) anasema kuwa

uteuzi wa idadi mwafaka ya sampuli ya utafiti huanza kwa kubainisha idadi ya jumuiya pana ya utafiti katika eneo la utafiti. Jumuiya pana ya utafiti huu ilikuwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub miongoni mwa wanafunzi na wahadhiri wa vyuo vikuu vyote nchini Kenya. Vyuo hivi vilikuwa na takriban wanfunzi 300,000. Jumuiya finyu ya utafiti huu ilikuwa wanafunzi na wahadhiri wa taaluma ya Kiswahili katika vyuo vikuu 10 ncihini Kenya ambao idadi yao kwa jumla ilikuwa takriban 8,000 ikichukuliwa kuwa kila chuo kilikuwa na wanafunzi takriban 800 wa taaluma ya Kiswahili kuanzia mwaka wa kwanza hadi wa nne. Ni kutokana na jumuiya hii finyu ambapo idadi ya sampuli ya utafiti iliteuliwa.

Kwa kuwa idadi ya watafitiwa kutoka vyuo vyote ilikuwa 8,000 ambayo ilikuwa chini ya watafitiwa 10,000 kama anavyopendekeza Patrick (2009), basi fomula yake iliteuliwa kuelekeza uteuzi wa sampuli katika utafiti huu. Idadi ya sampuli ya utafiti huu ilihesabiwa kwa kutumia fomula ya kupata idadi ya sampuli ikiwa idadi ya jumuiya finyu haizidi 10,000 na idadi ya jumuiya pana ni zaidi ya 10,000.

Fomula yake Patrick (2009) ni ifuatayo:-

$nf = \frac{N}{n}$

/(e2)+z

Ambapo:

nf= idadi ya sampuli.  N=

Jumuiya pana  n = Jumuiya finyu

e=1.96 (utegemevu ukiwa 95%)

z=( kiwango kubalifu cha

makosa).

Basi katika kuhesabu idadi ya sampuli ya utafiti huu kwa mujibu wa fomula hii tulipata,

$$nf = \frac{300{,}000}{8000}$$

/((1.962)+5.0)

nf=339.0600 (Takriban watu 340).

Hatimaye, sampuli nzima ya utafiti huu ilikuwa 340 kutoka kwa vyuo vyote 10. Idadi ya wanafunzi walioshirikishwa katika sampuli hii kutoka kila chuo ilikuwa 32 na kwa hivyo ikizingatiwa kuwa jumuiya pana ya utafiti huu ilikuwa 300,000 na jumuiya finyu ilikuwa wanafunzi 8,000, basi sampuli ya wanafunzi 320 pamoja na idadi ya wahadhiri 15 na wahudumu 5 wa Nation Media Group katika kitengo cha tovuti ya Swahilihub ikawa 20 na kufanya jumla ya jumuiya finyu kuwa 340 (320+15+5). Idadi hii ilipatikana kuwa mwafaka kwa utafiti huu na ambayo ingehakikisha kuwa data iliyopatikana ilikuwa ya kutegemeka.

Kwa jumla kuna takriban wanafunzi 300,000 katika vyuo vikuu vyote nchini Kenya. Ni kutokana na vyuo hivi vikuu ambapo jumuiya finyu iliteuliwa na mtafiti kupitia sampuli kusudio. Jumuiya finyu ya utafiti huu ilihusisha vyuo 10 nchini Kenya. Kutokana na vyuo hivi 10, jumuiya finyu ya wanafunzi 800 wa taaluma ya Kiswahili kutoka mwaka wa kwanza hadi wa nne, yaani wanafunzi 200 kila mwaka wa taaluma ya Kiswahili, iliteuliwa kutoka kila chuo na kwa hivyo jumla ya wanafunzi 8,000 ilipatikana. Ni kutokana na jumuiya finyu hii ya jumla ya vyuo 10 ambapo sampuli ya utafiti huu iliteuliwa. Jumuiya hii finyu inaonyeshwa katika jedwali lifuatalo.

*Jedwali SURA YA TATU .1: Jumuiya finyu ya utafiti*

| **Watafitiwa** | **Idadi ya wanafunzi** | **Idadi ya wahadhiri** | **Jumla** |
|---|---|---|---|
| Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro | 32 | 1 | 33 |
| Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Maseno | 32 | 1 | 33 |
| Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kibabii | 32 | 2 | 34 |
| Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Nairobi | 32 | 2 | 34 |
| Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi | 32 | 2 | 34 |
| Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kisii | 32 | 1 | 33 |
| Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mlima Kenya | 32 | 2 | 34 |
| Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Machakos | 32 | 1 | 33 |
| Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Jaramogi Oginga Odinga | 32 | 2 | 34 |
| Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha USIU | 32 | 1 | 33 |
| Wahudumu wa Nation Media Group | 5 | | 5 |
| **Jumla** | | | **340** |

Jedwali 3.1 inaonyesha idadi ya vyuo vilivyoteuliwa pamoja na idadi ya wanafunzi, wahadhiri na wahudumu wa Nation Media Group walioteuliwa kupata idadi halisi ya watafitiwa 340 waliohusika katika utafiti huu.

### 3.5 Njia za Utafiti.

Ili kuweza kutathmini mchango wa tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili, utafiti huu ulitumia njia mbalimbali za ukusanyaji data kama zifuatazo: mahojiano, hojaji, uchunzaji na mijadala ya kimakundi.

#### 3.5.1 Mahojiano

Ili kupata data kuhusu mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili, mahojiano yalifanyika kwa wahudumu wa Nation Media Group pamoja na wasimamizi wa mradi wa Swahilihub kwa lengo la kubaini mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Meneja wa Nation Media Group pamoja na mkuu wa kitengo cha Swahilihub walihojiwa kwa sababu ya nafasi yao muhimu katika usimamizi wa mradi wa Swahilihub pamoja na michango yao kuhusu ruwaza na uratibu wa mfumo wa Swahilihub. Vile vile, wahadhiri wa Kiswahili katika vyuo kumi nchini Kenya walihojiwa kutokana na nafasi yao katika shughuli za elimu ya Kiswahili. Shughuli hizi za elimu ya Kiswahili ni nguzo muhimu katika mchakato wa ukuzaji wa Kiswahili katika ujenzi wake, usambaaji na udumishaji wa hadhi na dhima ya Kiswahili kwenye tovuti ya Swahilihub. Mahojiano hayo yalisaidia kubaini maoni na mitazamo yao kuhusu mchango wa tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili. Mahojiano yalitumika katika utafiti huu ili kupata mrejesho wa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub kuhusu mchango wake na kubaini vigezo muhimu vya utendakazi wake.

Mahojiano pia yalichangia kukadiria jinsi matarajio ya watumiaji wa Swahilihub yalivyofikiwa kila walipoutumia mradi wa Swahilihub. Mrejesho huu kutoka kwa waliohojiwa nyanjani uliangazia mchango wa tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili miongoni mwa watumiaji wake na kubainisha vipengele vya tovuti ya Swahilihub vinavyoifanya kuwa rahisi kutumika na hivyo basi kupata watumiaji wengi mtandaoni. Mpango wa kukutana na wasailiwa ulifanywa wiki moja kabla ya kukutana nao. Kila msailiwa alipewa muda wa kutosha kushiriki kikamilifu. Usaili ulifanywa kwa njia ya kirafiki hali ambayo ilifanya wasailiwa kuwa huru kuyajibu maswali kwa njia iliyo shwari.

### 3.5.2 Hojaji

Hojaji zilisambazwa miongoni mwa wanafunzi katika vyuo vikuu kumi vilivyoteuliwa nchini Kenya ili kupata mrejesho kuhusu mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili. Wanafunzi walioshirikishwa katika sampuli ya utafiti huu walipewa hojaji za ukuzaji wa lugha ya Kiswahili katika tovuti ya Swahilihub walizotarajiwa kuzijibu. Wanafunzi hawa walitakiwa kuyajibu maswali yaliyohusiana na ukuzaji wa lugha ya Kiswahili katika tovuti ya Swahilihub. Maswali haya yalikuwa yakilenga kubaini viwango vyao vya ukuzaji wa lugha ya Kiswahili katika tovuti ya Swahilihub na hivyo basi kubaini mchango wa tovuti ya Swahilihub. (taz. Viambatisho II,III,na IV)

Wanafunzi waliosambaziwa hojaji walizijaza na majibu yao yalichanganuliwa kwa lengo la kubaini mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Wanafunzi wa Kiswahili walitafitiwa kwa sababu ya nafasi yao muhimu katika mchakato wa elimu ya Kiswahili na umuhimu wa mradi wa Swahilihub katika elimu ya Kiswahili pamoja na michango yao kuhusu changamoto zinazowakabili katika matumizi ya Swahilihub pamoja

na mustakabali wake katika ukuzaji wa Kiswahili. Michango hii ya elimu ya Kiswahili ni msingi muhimu katika mchakato wa ukuzaji wa Kiswahili katika ujenzi wake, usambaaji na udumishaji wa hadhi na dhima ya Kiswahili kwenye tovuti ya Swahilihub. Majibu yao kwenye hojaji yalisaidia kubaini maoni na mitazamo yao kuhusu mchango wa tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili.

Hojaji ilisaidia kupata maelezo ya kimsingi ya historia na habari kuhusu tovuti ya Swahilihub kutoka kwa watumiaji wake. Hojaji ilikuwa muhimu katika utafiti huu kwa sababu ni mbinu mwafaka sana katika kukusanya data ili kuyafikia madhumuni ya utafiti huu kuhusu mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili.
Aidha mtafiti alitumia hojaji ili kupata data iliyohusiana na utendakazi wa tovuti ya Swahilihub na hivyo basi kumwezesha kutoa maelezo kamili kwa matokeo ya data hizo. Majibu kutokana na hojaji yaliweka msingi kwa mada ya utafiti. Hatimaye katika utafiti huu, ili kuendana na maoni ya Baker (1992) hojaji za mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili zilibuniwa ili kubaini kutoka kwa watafitiwa iwapo Swahilihub ilichangia katika ujenzi wa lugha ya Kiswahili, usambaaji wake na udumishaji wa hadhi na dhima yake mtandaoni. Nafasi ya mfumo wa Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili ulipimwa kwa kuzingatia vipengele mbalimbali vya utendakazi wake kutokana na maswali yaliyoandaliwa kwenye hojaji za utafiti huu. Kufanya hivyo kulimpa mtafiti msingi bora wa kueleza na kupendekeza njia mwafaka za kukuza taaluma ya Kiswahili kwenye tovuti ya Swahilihub.

### 3.5.3 Uchunzaji Mtandaoni

Ili kuchunguza masuala muhimu kuhusu mfumo wa Swahilihub, utafiti huu ulishirikisha michakato ya uchunzaji kwa kutazama vipengee mbalimbali vya matumizi yake

mtandaoni. Mtafiti alipata fursa ya kusakura tovuti ya Swahilihub ili kupata maelezo ya kimsingi kuhusu mfumo wa tovuti ya Swahilihub. Data zilikusanywa kutoka kwa tovuti ya Swahilihub kwa kurejelea habari na maoni yaliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili yaliyohusu masuala ya ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili kiteknolojia kutoka mwaka wa 2014 hadi 2019. Mchakato wa uchunzaji hapa ulihusisha matumizi ya ARhefs katika uchunguzi wa vipengele mbalimbali vya Swahilihub ili kupata data kuhusu mchango wake katika ukuzaji wa Kiswahili. Uchunguzi huu ulifanywa kwa lengo la kubaini mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Matokeo ya uchunguzi huu yalichangia kutoa tathmini kuhusu mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili mtandaoni. Tathmini hii ya Swahilihub ilikuwa msingi muhimu katika mchakato wa ukuzaji wa Kiswahili katika ujenzi wake, usambaaji na udumishaji wa hadhi na dhima ya Kiswahili kwenye tovuti ya Swahilihub.

Ili kufanikisha uchunzaji wa tovuti ya Swahilihub mtandaoni, utafiti ulihusisha Arhefs ili kukusanya data kiuchanganuzi mtandaoni kuhusu utendakazi wa Swahilihub. Utafiti huu ulijikita katika uchunguzi wa habari kwenye tovuti ya Swahilihub ili kupata data kuhusu mfumo wake. Kothari (2003) anaeleza kuwa kwa kutumia mbinu ya uchunzaji, mtafiti hutafuta data kwa kushuhudia mambo yeye mwenyewe na hata wakati mwingine bila kuuliza watafitiwa jambo lo lote. Lengo kuu lilikuwa ni kubaini vipengee mbalimbali vya mfumo wa Swahilihub vinavyochangia utendakazi wake mtandaoni kwa kufanya uchanganuzi wa dhati kwenye ARhefs na Similarweb.

### 3.5.4 Mijadala ya Makundi

Watafitiwa walishirikishwa katika mijadala ya kimakundi iliyoendeshwa miongoni mwa wanafunzi katika vyuo vikuu kumi vilivyoteuliwa nchini Kenya ili kupata mrejesho

kuhusu mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili. Wanafunzi waliowekwa kwenye makundi walielekezwa kwenye mijadala iliyozua majibu yaliyochanganuliwa kwa lengo la kubaini mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Wanafunzi wa Kiswahili na wadau wengine walishirikishwa kwa sababu ya nafasi yao muhimu katika mchakato wa elimu ya Kiswahili na umuhimu wa mradi wa Swahilihub katika elimu ya Kiswahili. Majibu ya mijadala hii yalibaini changamoto zinazowakabili watumiaji wa Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili pamoja na mustakabali wake katika mchakato wa ukuzaji wa Kiswahili katika ujenzi wake, usambaaji na udumishaji wa hadhi na dhima yake. Michango yao kwenye mijadala ya kimakundi ilisaidia kubaini maoni na mitazamo yao kuhusu mchango wa tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili. Mijadala ya makundi katika utafiti huu pia ilitumiwa ili kupata data muhimu kuhusu mradi wa Swahilihub miongoni mwa watumiaji wake.

Mijadala kwenye makundi iliendeshwa miongoni mwa watumiaji wa mradi wa Swahilihub katika vyuo vikuu kumi nchini Kenya ili kupata data muhimu kimaelezo kuhusu mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili.

## 3.6 Mbinu za Utafiti

Ukusanyaji wa data ulifanywa kwa kutumia mbinu zifuatazo: usaili, hojaji, uchunzaji na mijadala ya kimakundi.

### 3.6.1 Usaili

Usaili ulitumiwa kama mbinu maalumu ya ukusanyaji wa habari kuhusu mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Usaili ulikuwa mbinu ya kupima ukweli wa majibu ya wasailiwa kwa kuongezea pale ambapo palikuwa na upungufu na kudondosha pale palipokuwa nyongeza isiyofaa. Usaili ulitumiwa kukusanyia data

kuhusu ukuzaji wa Kiswahili kwenye tovuti ya Swahilihub ili kuchunguza kwa namna gani mfumo wa Swahilihub unavyochangia katika ukuzaji wa Kiswahili nchini Kenya. Majibu ya wahojiwa yalichangia pakubwa kubaini namna mfumo wa Swahilihub unavyochangia katika ukuzaji wa Kiswahili mtandaoni. Mfumo wa Swahilihub ulibainika kutokana na mwonekano wake, umbo lake na muundo wake. Kwenye hojaji na katika usaili yaliwiana na hali ilivyo kwenye tovuti ya Swahilihub. Usaili ulihusisha maswali yaliyobaini viwango vya ukuzaji wa Kiswahili kwenye tovuti ya Swahilihub na kubaini changamoto za matumizi ya Swahilihub pamoja na mikakati mahususi ya ukuzaji wa Kiswahili.

### 3.6.2 Hojaji

Wahadhiri na wanafunzi wa Kiswahili kutoka vyuo vikuu waliteuliwa kujaza hojaji kuhusu matumizi ya tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kwa kutumia mwongozo wa maswali ya hojaji. Vipengele kadhaa kuhusu tovuti ya Swahilihub vilibainishwa kupitia mbinu hii. Mwongozo wa hojaji ulitumiwa kwa sababu ni kifaa chepesi kisicho na gharama kubwa kutafuta data kutoka kwa watafitiwa kwa muda mfupi na hivyo kuokoa muda. Isitoshe kutokana na utafiti awali, mtafiti alibaini kwamba watafitiwa wake wangeweza kujaza hojaji kwa sababu walikuwa wasomi walioelewa umuhimu wa mchakato mzima wa utafiti.

Kuhusu kwa namna gani mfumo wa Swahilihub unavyochangia katika ukuzaji wa Kiswahili nchini Kenya, maswali ya hojaji yaliyotungwa yaliwapa watafitiwa nafasi ya kutoa majibu yaliyobainisha nafasi ya umbo na muundo wa Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili. Maswali yaliyotungwa yalilenga kubaini urahisi wa Swahilihub kimatumizi. Katika utafiti huu watumiaji wa Swahilihub walipata fursa ya kuonyesha ni kwa viwango

gani ukuzaji wa Kiswahili unatokea kwenye tovuti ya Swahilihub. Aidha kutokana na maswali ya hojaji ya utafiti huu watumiaji wa tovuti ya Swahilihub walipata nafasi ya kubaini changamoto za matumizi yake pamoja na kupendekeza mikakati ya ukuzaji wa Kiswahili inayoweza kuimarishwa kwenye tovuti ya Swahilihub.

### 3.6.3 Uchunzaji Shiriki

Mtafiti alitafuta data kwa kushuhudia ukuzwaji wa taaluma ya Kiswahili kwenye tovuti ya Swahilihub kwa kuisakura tovuti ya Swahilihub ili kubaini kwa namna gani mfumo wa Swahilihub unavyochangia katika ukuzaji wa Kiswahili nchini Kenya. Mwongozo wa uchunzaji shiriki ulitumiwa kukusanyia data katika tovuti ya Swahilihub ili kuchunguza iwapo umbo na muundo wa tovuti ya Swahilihub lilichangia katika ukuzaji wa Kiswahili. Katika kutafuta data kwa kushuhudia ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili kwenye tovuti ya Swahilihub mtafiti aliandaa orodha ya vipengee muhimu vilivyomwelekeza kupata habari kuhusu mchango wa tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Orodha hii ilikuwa muhimu kwa mtafiti katika kuisakura tovuti ya Swahilihub ili kubaini shughuli zilizoendeshwa na zilizochangia ukuzaji wa lugha ya Kiswahili.

Isitoshe, matumizi ya mbinu ya uchunzaji yaliwezesha kunukuliwa kwa matukio yo yote mtandaoni yanayohusiana na umbo na muundo wa tovuti ya Swahilihub. Kwa kutumia mbinu hii, maelezo yalipatikana kutokana na uchunguzi wa mtafiti mwenyewe pasipo kumuuliza mtafitiwa maswali yo yote kama anavyodahili (Kothari, 2003). Huu ndio msingi uliozingatiwa katika kuchagua mbinu ya uchunzaji. Uchunzaji ulifanyika mtandaoni ili kubaini vipengele vya tathmini ya Swahilihub kwa msingi wa matini yake, ushindani mtandaoni, ushirikiano na tovuti nyingine pamoja na urejeleaji wa matini ya

Swahilihub. Kwa kutumia mbinu hii ya uchunzaji shiriki mtafiti aliweza kushuhudia na kukadiria mchango wa tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili mtandaoni.

Tovuti ya Swahilihub imechunguzwa kwa kutumia Arhefs ili kubainisha nafasi yake kimatumizi miongoni mwa tovuti nyingine kote ulimwenguni. Uchunguzi huu ulibainisha istilahi zinazoelekeza watumiaji wengi wa tovuti ya Swahilihub, idadi na mtiririko wa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub na tovuti nyingine zinazowaelekeza watumiaji wake kurejelea mtandao wa Swahilihub.

### 3.6.4 Mijadala ya Kimakundi

Mijadala ya kimakundi ililenga kubaini mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa watumiaji wake. Ili kuwiana na maoni ya Mugenda (2008), mijadala isiyo rasmi ya kimakundi ilitumiwa kwa kuwa ilikuwa mwafaka kwa utafiti huu. Mtafiti aliwashirikisha wanafunzi kumi na watano katika kila chuo katika mijadala ya kimakundi iliyoongozwa na maswali yaliyokuwa yametayarishwa awali.
(taz. Kiambatisho I). Mijadala hii iliangazia mada mbalimbali kuhusu mfumo wa Swahilihub, changamoto za matumizi yake pamoja na mikakati mbalimbali ya ukuzaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub nchini Kenya.
Mijadala hii ililenga kubaini mchango wa Swahilihub katika ukuzaji Kiswahili miongoni mwa watumiaji wake na kupata mrejesho kutoka kwao. Kwa mujibu wa Mugenda (2008), mijadala isiyo rasmi ya kimakundi huwa mwafaka kwa utafiti kwani sampuli huwa imetulia katika mazingira yasiyo rasmi jambo linalowafanya wajieleze kikawaida na bila uoga. Mbinu ya uchunzaji shiriki ilitumiwa na watafiti ili kupata data inayotakikana kutoka kwa sampuli kupitia kusikiliza mijadala hii kwa umakini.

### 3.7 Vifaa vya Utafiti

Data yote katika utafiti huu ilikusanywa kwa kutumia vifaa mbalimbali vya utafiti kwa mujibu wa mbinu mbalimbali za utafiti. Vifaa hivi ni vifuatavyo:-

#### 3.7.1 Dodoso

Dodoso ilitumiwa kama kifaa maalumu cha ukusanyaji wa habari kuhusu utendakazi wa mradi wa Swahilihub katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili. Maswali yaliyoongoza usaili nyanjani yaliandaliwa kwa lengo la kupata habari kuhusu mchango wa tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili miongoni mwa watumiaji wake. Maswali kwenye dodoso yalikuwa kama dira ya kuongoza na kupima ukweli wa majibu ya wasailiwa kwa kuongezea pale ambapo palikuwa na upungufu na kudondosha pale palipokuwa nyongeza isiyofaa. Dodoso ilikuwa mwafaka kwa kuwa iliufaa mchakato mzima wa usaili uliofanywa kwa njia ya kirafiki hali ambayo ilifanya wasailiwa kuwa huru kuyajibu maswali bila wasiwasi. Dodoso ilihusisha maswali yasiyofuata utaratibu maalumu ili kuondoa urasmi ambao aghalabu hutinga mawasiliano ili kupata data kutoka kwa wasailiwa.

#### 3.7.2 Hojaji za Ukuzaji wa Kiswahili kwenye Tovuti ya Swahilihub

Hojaji za ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kwenye tovuti ya Swahilihub ziliandaliwa na kutumiwa katika mchakato wa ukusanyaji data nyanjani. Hojaji hizi zilikuwa na orodha ya maswali yaliyotayarishwa awali ili kukusanya data iliyoibuliwa na majibu kuhusu mfumo wa Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili, vipengele mbalimbali vya tathmini ya tovuti ya Swahilihub pamoja na changamoto na mikakati ya ukuzaji wa Swahilihub. Hojaji hizi zilitumika kukusanya data kubwa kwa kipindi kifupi cha wakati. Hivyo basi maswali ya

hojaji yalitungwa kwa njia ambayo yaliibua data yote inayotakikana kwa usahihi kwa lengo la kubaini mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya

Kiswahili. Borg na Gall (2003:127) wanaeleza kuwa “hojaji za matumizi na ukuzaji wa lugha zafaa kutayarishwa kwa njia ya kuzifanya ziweze kugusia aina kuu tatu za mielekeo kutoka kwa watafitiwa. Aina hizi tatu za mielekeo ni pamoja na: mielekeo inayohusu kupenda au kutopenda, mielekeo inayohusu ufahamu wa mtu kuhusu jambo au hali fulani na hatimaye mielekeo inayohusu moyo wa mtu wa kurekebisha jambo ama hali fulani.

Isitoshe, mielekeo ya watumiaji wa tovuti ya Swahilihub inayohusu ufahamu wa watafitiwa kuhusu mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili ilibainika kutokana na majibu waliyotolea hojaji za utafiti huu. Vile vile, hojaji za utafiti huu zilitumiwa kubainisha viwango vya ukuzaji wa Kiswahili kwenye tovuti ya Swahilihub miongoni mwa watumiaji wake. Kwa njia hii watafitiwa walibainisha mchango wa tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa watumiaji wake nchini Kenya. Viwango vya ukuzaji wa Kiswahili miongoni mwa watumiaji wa Swahilihub vilibainika kutokana na ufahamu waliokuwa nao watumiaji wa tovuti ya Swahilihub kutokana na majibu yao kwa maswali ya hojaji katika utafiti huu.

Hali kadhalika, mielekeo inayohusu watafitiwa kuwa na nia ya kuboresha mikakati ya ukuzaji wa Kiswahili kwenye tovuti ya Swahilihub ilibainika kutokana na majibu yaliyotokana na maswali ya hojaji za utafiti huu. Katika kubaini changamoto zilizowakabili watumiaji wa tovuti ya Swahilihub, watafitiwa walionyesha nia ya kukabiliana na changamoto husika na kutoa mapendekezo kuhusu mustakabli wa tovuti ya Swahilihub ili kuimarisha mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya

Kiswahili.

### 3.7.3 Mwongozo wa Uchunzaji kwa Msaada wa ARhefs

Katika utafiti huu, kifaa cha ARhesfs kiliteuliwa miongoni mwa vifaa vingine ili kutoa matokeo mwafaka ya tathmini ya utendakazi wa mradi wa Swahilihub katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili. Kwa kutumia kifaa hiki, mtafiti alichunguza na kupata data za kimsingi kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili miongoni mwa watumiaji mbalimbali wa tovuti ya Swahilihub, historia ya matumizi ya tovuti ya Swahilihub, nafasi ya tovuti ya Swahilihub miongoni mwa tovuti zingine kote ulimwenguni pamoja na muundo, taswira na mkao wa kurasa mbalimbali za tovuti ya Swahilihub.

Mwongozo wa uchunzaji ulitumiwa kukusanyia data katika tovuti ya Swahilihub ili kuchunguza iwapo majibu ya watafitiwa kwenye hojaji na katika usaili yaliwiana na hali ilivyo kwenye tovuti ya Swahilihub. Katika utafiti huu mtafiti alifanikiwa kwa kutumia mwongozo wa uchunzaji, uliomwezesha kutafuta data kwa kushuhudia mambo yeye mwenyewe bila kuuliza watafitiwa jambo lo lote. Uchunzaji ulifanywa kwa msaada wa programu ya uchanganuzi mtandaoni ya ARhefs ili kubaini vipengee mbalimbali vya umbo na muundo wa tovuti ya Swahilihub. Michakato ya uchunzaji ilijumuisha upimaji, ukusanyaji, uchanganuzi na uwasilishaji wa ripoti ya data ya intaneti kwa kusudi la kuelewa na kutumia kwa ukamilifu tovuti ya Swahilihub. ARhefs ni programu ya kiteknolojia kwenye tarakilishi iliyotumiwa katika tathmini ya utendakazi wa tovuti ya Swahilihub kwa kukusanya na kuchanganua data kwenye tovuti ya Swahilihub na kutambua changamoto zinazokabili utendakazi wake miongoni mwa watumiaji wake. Arhefs ilitumiwa kwa uchanganuzi wa vipengele vyote vya tovuti ya Swahilihub vinavyohusu umbo na muundo wake mtandaoni. Mtafiti alikuwa na orodha ya vipengee vya tovuti ya Swahilihub ambavyo alitumia kuthibitisha matumizi yavyo.

Vipengele hivi vilikuwa pamoja na viwango vya matumizi yake, umbo lake, muundo wake na matini yake. Mifano ya vifaa vya kiteknolojia vya tathmini ya tovuti ni SimilarWeb, Google Analytica, Alexa na Arhefs miongoni mwa vifaa vingine. Ubora wa vifaa hivi hutokana na uwezo wao wa kukagua data katika muktadha wa muda mahususi (Paukkeri, 2017). Watafiti wanaweza kuchunguza data za tovuti husika kwa muda mfupi tu, kila wiki, kila siku, kila mwezi au hata kila mwaka (O'Brien na Toms, 2013).

### 3.7.4 Picha na Video

Ili kuyaafiki madhumuni ya utafiti huu, picha mbalimbali zilichukuliwa na video kurekodiwa kwa ajili ya uchanganuzi na uwasilishaji wa data. Shughuli katika baadhi ya mahojiano na wahudumu na wasimamizi wa mradi wa Swahilihub zilirekodiwa na picha za matukio anuwai kwenye tovuti ya Swahilihub zikachukuliwa. Picha hizi zilikuwa muhimu katika upangaji, uchanganuzi na uwasilishaji wa data kuhusu utendakazi wa mradi wa Swahilihub katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili miongoni mwa watumiaji wake nchini Kenya. Picha hizi zilibainisha kipengee cha muundo wa tovuti ya Swahilihub na kuonyesha misingi ya ustahilifu na ukubalifu wa kila kitengo cha mradi wa Swahilihub. Aidha picha hizi zilichangia pakubwa kuratibu na kupanga vyema data na matokeo ya utafiti huu katika sura ya nne. Utafiti huu ulikusanya data nyanjani kama njia kuu ya ukusanyaji data miongoni mwa watumiaji wa mradi wa Swahilihub ambao ndio watafitiwa.

### 3.7.5 Mwongozo wa Mijadala ya Makundi

Ili kuwashirikisha wanafunzi kumi na watano katika kila chuo katika mijadala ya kimakundi, miongozo ya mijadala kwa makundi iliandaliwa. Mijadala ya makundi iliongozwa na maswali yaliyokuwa yametayarishwa awali kwenye miongozo ya mijadala

kwa makundi. (taz. Kiambatisho I). Mijadala hii iliangazia mada mbalimbali kuhusu utendakazi wa mradi wa Swahilihub katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili miongoni mwa watumiaji wake nchini Kenya.

Watafitiwa walioteuliwa kwa mijadala ya kimakundi ni wanafunzi wa taaluma ya Kiswahili pamoja na watumiaji wengine wa tovuti ya Swahilihub ambao waliandaliwa mazingira matulivu na yasiyo rasmi jambo lililowafanya wajieleze kikawaida na bila uoga wo wote. Maswali katika miongozo ya mijadala ya makundi yalikuwa shirikishi na hivyo basi yalitumiwa na watafiti ili kupata data iliyotakikana kutoka kwa sampuli kupitia kusikiliza mijadala hii kwa umakini.

## 3.8 Utegemezi na Uaminifu wa Vifaa vya Utafiti

Kwa kuzingatia maoni ya Creswell (2003) kuhusu utegemezi katika data ya utafiti huu, mtafiti alihakikisha kuwa kiwango cha uchunguzi kuhusu mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kiliakisi ubora kiasi kwamba utafiti kama huu unaweza kufanywa tena na matokeo yakawa sawa na yale ya awali ya utafiti huu. Utegemezi katika data ya utafiti huu ulitokana na matumizi ya mbinu mwafaka za kijarabati na kimaelezo katika mchakato wote wa utafiti kiasi kwamba utafiti wo wote wa baadaye utakaotumia mwelekeo mseto utapata matokeo sawa na yale ya awali. Ili data za utafiti unaoshirikisha tathmini ya mchango wa tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kuwa tegemezi, mtafiti alizingatia maoni ya Van Dijk (2001) aliyependekeza kufikiwa kwa data za utafiti kwa urahisi na kuwa matokeo ya utafiti yanafaa kufikiwa kwa urahisi na kusomwa na watafitiwa. Data za utafiti huu ni tegemezi kwa vile zinaweza kufikiwa kwa urahisi kutokana na ripoti ya utafiti huu inayoakisi michakato yote iliyozingatiwa katika utafiti tangu mwanzo hadi mwisho, yaani ukusanyaji, uainishaji, uchanganuzi na ufasiri

wa data na pia kuifikia nakala ya tasnifu iliyotokana na utafiti huu mtandaoni na hasa katika tovuti ya Swahilihub.

Uaminifu wa data ya utafiti ulikuwa wa hali ya juu kwa kuwa vipimo vya kisayansi na utazamaji vilivyotumika vilikuwa ni vya kweli na halisi kwa mujibu wa maoni ya Creswell (2003). Vipimo hivi vya kisayansi vilikuwa ni pamoja na mbinu za kijarabati na kimaelezo zilizoshirikishwa katika hatua zote za utafiti zikiwemo hatua za ukusanyaji, uainishaji, uchanganuzi na ufasiri wa data. Isitoshe kwa kufanya majaribio ya vifaa mtafiti alihakikisha kuwa vifaa vyote vya utafiti huu vilikuwa na uwezo wa kupima kikamilifu kilichotarajiwa kupimwa ili kupata data zinazoyafikia madhumuni ya utafiti huu. Hali hii ilifikiwa kwa kuhakikisha kwamba vipengele vya kimsingi kuhusu mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili vilidokezwa katika vifaa hivyo.

Mwelekeo mseto wa utafiti ulichangia pakubwa katika kuweka pamoja uchanganuzi wa umbo na muundo wa tovuti ya Swahilihub, stakabadhi muhimu za mradi wa Swahilihub na kutafuta ruwaza na mahusiano kuhusu utendakazi wa mradi wa Swahilihub miongoni mwa watumiaji wake. Hatua hii iliwiana na maoni ya Creswell (2003) kuhusu uaminifu wa utafiti husika. Maelezo ambayo yalikuwa ni ya kuaminika yalihifadhiwa na yale ambayo hayakuwa ya kuaminika yalitupiliwa mbali. Vilevile kwa kutumia mwelekeo mseto wa utafiti kama anavyodahili Creswell (2003) ukweli wa data ya kimaelezo ulihakikishwa kwa kuendesha mijadala ya kimantiki miongoni mwa watumiaji wa mradi wa Swahilihub nchini Kenya. Mfumo wa kipembuzi ulizingatiwa katika uchanganuzi kwa kuibua mjadala wa kimantiki hususan kwa kurejelea mitazamo ya wataalamu mbalimbali. Aidha katika utafiti huu, uaminifu katika data ulizingatiwa kwa kutumia misingi ya nadharia ya Msambao wa Uvumbuzi wa Rodgers, (2003) katika kukusanya na kuainisha

data ya utafiti. Isitoshe, uaminifu wa vifaa ulizingatiwa kwa kushirikisha vipengele vya kimsingi katika matumizi ya tovuti ya Swahilihub kukuza lugha ya Kiswahili. Vipengele hivyo vilikuwa tathmini ya mchango wa tovuti ya Swahilihub, ushindani wake mtandaoni na ukubalifu wa matini kwenye vitengo mbalimbali vya tovuti ya Swahilihub na matumizi yake pamoja na changamoto zinazokumba tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili. Hatimaye mustakabali wa mradi wa Swahilihub ni kigezo kikuu kilichojitokeza katika utafiti huu na hivyo basi kuimraisha uaminifu wa matokeo yake.

Uthabiti wa data ya utafiti huu ulijitokeza katika ukamilifu wa vifaa vilivyotumika katika mchakato wa ukusanyaji data. Uthabiti wa vifaa katika utafiti huu ulitokana na ukamilifu wa vifaa mintarafu vipengele vilivyoainishwa kwenye vifaa hivyo. Vipengele hivyo vilikuwa pamoja na muundo wa Swahilihub, matini iliyopatikana kwenye tovuti ya Swahilihub, nafasi ya mradi wa Swahilihub miongoni mwa tovuti zingine mtandaoni pamoja na ustahilifu wa vitengo anuai kwenye tovuti ya Swahilihub. Vile vile, katika utafiti huu, uthabiti wa vifaa ulizingatiwa kwa kurejelea uelekezi wa baadhi ya wataalam wa lugha ya Kiswahili. Uelekezi huu wa wataalamu mbalimbali uliwiana na maoni ya Orodho (2004) kwamba vifaa vya utafiti vinaweza kudhibitishwa na wataalamu mbalimbali.

Uthabiti wa vifaa vya utafiti huu aidha ulihakikishwa baada ya vifaa hivyo kutathminiwa na kufanyiwa marekebisho na baadhi ya wahadhiri katika Idara ya Lugha na Fasihi, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro wakiwemo wasimamizi wa kazi hii. Vile vile, uthabiti wa vifaa hivyo uliamuliwa baada ya vifaa hivyo kufanyiwa majaribio katika chuo kikuu kimoja katika eneo tofauti na lile la utafiti lakini lenye sifa sawa na eneo la utafiti.

Kabla ya kuenda nyanjani kukusanya data, mtafiti alivifanyia majaribio vifaa vya utafiti. Majaribio haya yalifanywa kwa kuteua tovuti ya Chrome kwa ajili ya kufanyiwa majaribio kwa kutumia programu anuwai changanuzi za kiteknolojia zikiwa pamoja na Arhefs, Avera na Similarweb. Hii ndiyo hatua ya mwisho ya kuhakikisha kuwa vifaa vya utafiti ni vya uhakika katika ukusanyaji wa data (Mugenda, 2003). Hii ni kwa sababu majaribio haya yalimpa mtafiti fursa halisi ya kufanyia vifaa vya utafiti kazi nyanjani akitumia idadi ndogo ya watafitiwa. Lengo kuu lilikuwa ni kubaini iwapo kulikuwa na shida yo yote katika uamilifu wa Arhefs, Similarweb na pia katika maswali ya hojaji na mahojiano kama vile maswali tata na yasiyoeleweka vyema na watafitiwa.

Isitoshe, ili kukadiria uthabiti, uaminifu na utegemevu wa vifaa vya kimaelezo katika utafiti huu, mtafiti alitumia Chuo kikuu cha Chuka katika kuvifanyia vifaa hivyo majaribio katika utafiti awali. Aidha, mtafiti alipata fursa ya kupima iwapo vifaa vyake vya utafiti vinaibua data ya kutosha au la, pia iwapo data inayopatikana kutoka kwa watafitiwa ni mwafaka katika kuyajibu maswali ya utafiti na hatimaye kuyafikia madhumuni ya utafiti huu kupitia njia nne teule. Miongoni mwa njia hizo ni pamoja na: mahojiano, hojaji, uchunzaji mtandaoni na mijadala ya kimakundi. Majaribio haya yalimwezesha mtafiti kutathmini upya vifaa vya ukusanyaji wa data na madhumuni ya utafiti kwa minajili ya kuyapiga msasa zaidi.

### 3.9 Utaratibu wa Uchunguzi, Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Utaratibu mahususi ulitumiwa katika uchunguzi, uchanganuzi na uwasilishaji wa data zilizokusanywa kwa msaada wa vifaa mbalimbali vya utafiti. Utaratibu huu ulizingatia data za kijarabati pamoja na data za kimaelezo kwa mujibu wa mwelekeo mseto wa utafiti. Data zilizokusanywa kupitia mahojiano, uchunzaji na hojaji zilipangwa katika kategoria tofauti.

Kategoria ya kwanza ilichanganua data kutokana na maelezo ya kiutangulizi kuhusu watafitiwa. Kategoria ya pili iliwasilisha data kuhusu mchango wa tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili nchini Kenya. Pia changamoto zinazokumba tovuti ya Swahilihub zilishughulikiwa katika kategoria hii. Kila sehemu ilifanyiwa uchanganuzi kwa msaada wa programu ya tarakilishi ya kitakwimu kwa sayansi jamii (SPSS 23) na idadi kujumuishwa kwa mfumo wa kiasilimia kwa kutumia chati na majedwali ili kurahisisha uchambuzi na uchanganuzi.

Matokeo na mapendekezo yalitolewa kwa misingi ya data ambazo zilikuwa zimechanganuliwa. Data ya utafiti iliainishwa kulingana na malengo ya utafiti na jinsi Kiswahili kinavyokuzwa na kuendelezwa katika tovuti ya Swahilihub kufikia sasa. Data ya utafiti imechanganuliwa kwa kuzingatia maswali, malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia ya msambao wa uvumbuzi wa Rodgers (2003). Uchanganuzi wa data umezingatia hatua tatu kutegemea malengo ya utafiti. Hatua ya kwanza imehusu mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Hatua ya pili imebaini changamoto za matumizi ya Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili.

Hatua ya tatu imehusu mustakabali wa Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili Uchanganuzi wa data katika utafiti ulikuwa hatua muhimu sana ya kupanga na kuipa maana data iliyokusanywa. Uhakiki wa data ulifanywa kwa lengo la kuhakikisha kuwa ni sahihi na kubalifu. Uchanganuzi wa kithamani ulitumiwa. Mugenda na Mugenda (1999) wanaeleza kuwa katika utafiti wa kithamani, uchanganuzi wa data wakati mwingine huwa tata na huchukuwa muda mwingi lakini uchanganuzi huo hulenga kueleza kwa undani na kikamilifu namna mada za utafiti zinavyohusiana. Mtafiti alichanganua data kwa

kuongozwa na nadharia ya msambao wa uvumbuzi (Rodgers, 2003). Viwango vitatu vilishirikishwa katika uchanganuzi huo; misingi, mchakato, ubwiaji na sifa.

Hatimaye uwasilishaji wa data ulifanywa kwa kuzingatia vigezo vikuu viwili. Kigezo cha mwelekeo mseto wa utafiti pamoja na kigezo cha nadharia na madhumini ya utafiti huu. Kutokana na mwelekeo mseto wa utafiti, mbinu za kijarabati na kimaelezo zilitumiwa kwa njia sambamba. Data iliyopatikana kijarabati ndiyo iliyohusu mfumo wa Swahilihub na kubainisha viwango vyake vya ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Data hii ilipatikana kutokana na tathmini ya tovuti ya Swahilihub kupitia programu ya Arhefs.
Hivyo basi katika uwasilishaji wake ni data za kijarabati kuhusu mchango wa Swahilihub zilizotangualia. Kisha kukafuata data za kimaelezo zilizokusanywa kupitia mbinu za kimaelezo kama vile mahojiano, hojaji na mijadala ya kimakundi.

Data hizi za kimaelezo ziliwasilishwa baada ya zile za kijarabati. Aidha kigezo cha nadharia na madhumuni ya utafiti kilizingatiwa katika uwasilishaji wa data. Data zilizotokana na madhumuni ya kwanza kuhusu mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili ambazo zilikusanywa kwa kutumia mbinu za kijarabati ziliwasilishwa kwanza. Kisha data zilizohusu changamoto za ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kwenye tovuti ya Swahilihub pamoja na mustakabali wa Swahilihub ziliwasilishwa mtawalia kufuatia mtiririko wa madhumuni kuanzia ya kwanza hadi ya mwisho. Data hizi zilikusanywa kwa kutumia mbinu za kimaelezo.

## 3.10 Maadili katika Utafiti

Utafiti huu ulifanywa kwa kuzingatia misingi ya kimaadili. Kwanza, maswala ya kimaadili yaliyozingatiwa katika utafiti huu yalikuwa ni pamoja na pendekezo la utafiti kupitishwa na jopo linaloshughulikia shahada za kiwango cha juu katika Chuo Kikuu cha

Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro. Pili, utafiti huu uliendeshwa kwa kuzingatia mbinu za utafiti zinazokubalika na sio zinazofikiriwa tu na mtafiti. Tatu, utaratibu wa kupata idhini ya kufanya utafiti kutoka kwa kitengo kinachohusika na utafiti chuoni na katika wizara ya elimu ilifuatwa. Kutokana na utaratibu huu idhini ya kufanya utafiti ilitolewa na utaratibu mwafaka wa kufanya utafiti halali ukazingatiwa.

Nne, data zilizokusanywa kutoka kwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub zilitumika kwa minajili ya utafiti huu pekee na si kwa shughuli nyinginezo ambazo zingeweza kuhujumu haki za watafitiwa. Tano, mtafiti alijiepusha na maoni na hisia za kibinafsi katika uchanganuzi na ufasiri wa data. Aidha, mtafiti pia alitoa maelezo kamilifu kuhusu data alizopata katika tovuti ya Swahilihub pamoja na maelezo kuhusu data hizo kwa kuzingatia mbinu za utafiti zinazokubalika. Aidha, majina ya watafitiwa hayakutajwa na badala yake misimbo ilitumika ili kuhifadhi utambulisho wao.

### 3.11 Hitimisho

Katika sura hii vipengele vilivyoshughulikiwa ni: mwelekeo mseto wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli ya utafiti, aina ya sampuli , mchakato wa uteuzi wa sampuli, njia za utafiti, mbinu za utafiti, vifaa vya utafiti, uaminifu na utegemezi wa vifaa vya utafiti na uthabiti wa vifaa. Kila njia na mbinu imeelezwa kwa undani jinsi ilivyotumiwa kufanikisha utafiti huu. Aidha utaratibu wa uchunguzi, uchanganuzi na uwasilishaji wa data pia umeshughulikiwa. Data ilipangwa na kuainishwa kwa mada ndogo za utafiti ili kuchanganuliwa. Misingi iliyoibua mijadala, maumbo na mitindo ya lugha iliainishwa na kupangwa kwa minajili ya uchanganuzi. Sura hii imewasilisha pia maswala mbalimbali ya kimaadili yaliyoshughulikiwa katika utafiti huu. Uchanganuzi wa kithamani ulitumiwa

ambapo nguzo muhimu ya nadharia iliyoongoza ukusanyaji, uchanganuzi, ufasiri na uwasilishaji data imeelezwa.

## SURA YA NNE


## MCHANGO WA SWAHILIHUB KATIKA UKUZAJI WA KISWAHILI

### 4.1 Utangulizi

Sura hii iliwasilisha data iliyokusanywa nyanjani kuhusu mchango wa tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili nchini Kenya kwa kutumia vifaa anuwai vya ukusanyaji data. Uwasilishaji wa data za utafiti huu uliongozwa na madhumuni na nadharia ya utafiti. Utafiti huu ulitokana na haja ya kubainisha na kutathmini mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili miongoni mwa watumiaji wake. Ili kuyafikia madhumuni haya, vigezo muhimu vya tathmini ya tovuti ya Swahilihub viliangaziwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka wa 2014 hadi 2019 kupitia michakato ya utafiti. Aidha, mwelekeo mseto wa utafiti ulichangia katika kuelewa vyema zaidi mchango wa Swahilihub kutokana na mtindo wa kuchanganya mbinu za kijarabati na kimaelezo katika utafiti huu. Data iliyokusanywa iliwasilishwa kimaelezo na vile vile kitakwimu kwa kuwa ilihusu uwasilishaji kwa kutumia tarakimu za asilimia, chati na majedwali. Utafiti huu ulitumia mwelekeo mseto wa utafiti katika kuwasilisha na kisha baadaye kuchanganua data iliyokusanywa. Aidha, mwelekeo mseto wa utafiti ulielekeza utafiti huu katika utayarishaji na uwasilishaji wa data ili kuyafikia majumui, mapendekezo na mahitimisho. Ili kuwasilisha matokeo ya utafiti huu data za kimaelezo pamoja na zile za kitakwimu ziliangaziwa kwa pamoja moja baada ya nyingine.

Sampuli nzima ya utafiti huu ilikuwa katika kategoria kuu mbili. Kulikuwa na kategoria ya wanafunzi na ile ya wahadhiri pamoja na wasimamizi wa mradi wa Swahilihub. Idadi ya wanafunzi walioshiriki katika utafiti huu ilikuwa asilimia 94.11(320) ya watafitiwa 340

huku idadi ya wahadhiri, wasimamizi na wahudumu wa mradi wa Swahilihub ikiwa asilimia 5.88%(20)  (Taz. Chati 4.1).




*Chati SURA YA NNE .1: Kategoria za Watafitiwa*

## 4.2 Mfumo wa Swahilihub na Ukuzaji wa Kiswahili Nchini Kenya

Mfumo wa Swahilihub ulibainika kwa kutathmini muundo wake na umbo lake pamoja na urahisi wake kimatumizi ili kuweka wazi namna Swahilihub ilivyofumbwa pamoja na mwonekano wake kwa watumiaji wake. Kigezo cha urahisi wa kimatumizi husheheni ubora wa mfumo wa tovuti na namna habari zilivyopangwa kwenye tovuti husika kwa namna inayochangia kufanikisha matumizi yake (Diffly, 2006). Utendakazi wa tovuti hujumuisha upatikanaji wa habari muhimu kuhusu huduma fulani mahususi kwenye mtandao. Ufikiaji wa tovuti hurejelea upakiaji wa data na habari kwa njia inayowezesha watumiaji wa tovuti kuzifikia kwa urahisi habari muhimu wanazozitafuta (Leung, Law na Lee, 2016).

Data ya uchunguzi huu kuhusu mfumo wa mradi wa Swahilihub ilitokana na uchanganuzi wa tovuti ya Swahilihub kwa kutumia Arhefs. Ni kutokana na data hii ambapo vipengele mbalimbali vya utendakazi wa Swahilihub kiumbo na kimuundo vilibainishwa. Matokeo ya utafiti huu yalibainisha manufaa ya tovuti ya Swahilihub na uwezo wake wa kuchangia katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili. Hali hii ndiyo iliyorejelewa na Rodgers, (2003) kama uchunzaji ambao ni uwezo wa uvumbuzi kuonekana kuwa wa manufaa na kutoa mchango halisi unaotambuliwa miongoni mwa watumiaji wake. Kuigwa kwa wavumbuzi waliotangulia kuukubali mradi wa Swahilihub kulipigwa jeki na ithibati ya kuwepo kwa manufaa yaliyodhihirika na kuonekana miongoni mwa watumiaji waliotarajiwa kuukubali na kuutumia mradi huu wa Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Vitengo vya tovuti ya Swahilihub vilitumika kukuza taaluma ya Kiswahili kwa viwango mbalimbali.

**Jedwali SURA YA NNE .2 Matumizi ya Vitengo mbalimbali vya tovuti ya Swahilihub**

| Vitengo vya Swahilihub | Naitumia sana | | Naitumia | | Siitumii | | Sijui | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi | Asilimia % | Idadi | Asilimia % | Idadi | Asilimia % | Idadi | Asilimia % |
| "Mwanzo" | 27 | 10.7% | 81 | 32.1% | 66 | 26.2% | 78 | 31.0% |
| "Habari" | 65 | 24.7% | 109 | 41.4% | 42 | 16.0% | 47 | 17.9% |
| "Jifunze Kiswahili" | 68 | 26.6% | 93 | 36.3% | 41 | 16.0% | 54 | 21.1% |
| "Blogu na ukumbi" | 26 | 10.8% | 49 | 20.4% | 77 | 3 2.1% | 88 | 36.7% |
| "Maktabani jisomee" | 60 | 22.8% | 92 | 35.0% | 51 | 19.4% | 60 | 22.8% |
| "Picha" | 39 | 14.7% | 81 | 30.6% | 83 | 31.3% | 62 | 23.4% |
| "Video" | 30 | 11.7% | 68 | 26.5% | 93 | 36.2% | 66 | 25.7% |

Mchango wa vitengo mbalimbali vya Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili ulibainika kupitia kwa vitengo vyake vyote. Matumizi ya vitengo mbalimbali yalitokea kwa asilimia 48 (156) ya watumiaji wake mtandaoni. Asilimia hii ilitokana na mchango wa vitengo vyote vinane (Mwanzo, Maktabani Jisomee, Blogu na Ukumbi, Picha, Habari, Makala, Video na Jifunze Kiswahili). Vitengo hivi havikutumiwa kwa kiwango cha asilimia 52 (176) ya watumiaji wa tovuti ya Swahilihub (Taz.Chati 4.44).

Kuhusu matumizi ya Mwanzo, matokeo ya utafiti huu yalionyesha kwamba asilimia 10.7 (36) ya watumiaji wa tovuti ya Swahilihub walikiri kukitumia sana kitengo hiki kwenye tovuti ya Swahilihub huku asilimia 32.7 (126) wakiitumia na hivyo basi kubainisha kuwa asilimia 43.4 (147) ya watafitiwa walikitumia kitengo hiki kwenye tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili. Takriban asilimia 56.6 (192) ya watafitiwa hawakukitumia kitengo cha Mwanzo katika mitagusano miongoni mwao licha ya kitengo hiki kuwa na umuhimu kwenye tovuti ya Swahilihub (Taz. Chati .4.2). Hii ni licha ya umuhimu wake wa kuimarisha mitagusano ya kibinafsi ambayo huchangia kuathiri misimamo na mielekeo mikali miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub. Mitagusano hii huelekezwa na wadau mashuhuri katika jamii.




**Chati SURA YA NNE .2: Matokeo ya Matumizi ya Mwanzo**

Watumiaji wa tovuti ya Swahilihub waliokiri kutotumia kitengo cha mwanzo walitaja uchangamano wake kama sababu kuu. Machukulio yao kuhusu ugumu wa kuelewa matumizi ya kitengo cha Mwanzo yalichangia matokeo ya matumizi yake kwa kiwango

cha chini. Uvumbuzi wowote unapochukuliwa kuwa changamano na mgumu kutumia inakuwa vigumu kukubaliwa na kutumiwa na wanajamii Rodgers, (2003). Matokeo ya utafiti huu yalibaini kuwa kiwango cha uwiano wa kitengo cha Mwanzo kilikuwa chini miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub kutokana na namna kitengo hiki kilivyochukuliwa kutoingiliana na hali, maadili na mazoea yao katika shughuli zao za awali na michakato yao mitandaoni. Ili kufanikisha msambao wa uvumbuzi, uwiano huchangia pakubwa.

Habari ni miongoni mwa vitengo vya tovuti ya Swahilihub vilivyotumiwa katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Mrejesho wa watafitiwa ulibaini kuwa kitengo hiki kina umuhimu sana katika ujenzi wa mwonekano bora katika muundo wa tovuti ya Swahilihub na hivyo basi kinachangia kuipa tovuti hii taswira na nafasi bora ya kuteuliwa kwa matumizi miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub mtandaoni

(Taz. Picha 4.40).




:


**Picha SURA YA NNE .1: Kitengo cha Habari**

Aidha, matokeo ya utafiti huu yalionyesha kwamba asilimia 24.7 (83) ya watumiaji wa tovuti ya Swahilihub walikiri kukitumia sana kitengo cha Habari huku asilimia 41.4 (140) wakikitumia na hivyo basi kwa jumla kudhihirisha kuwa asilimia 66.1 (224) ya watafitiwa walikitumia kitengo hiki kwenye tovuti ya Swahilihub. Takriban asilimia 33.9 (115) ya watafitiwa hawakukitumia kitengo cha Habari kuikuza lugha ya Kiswahili licha ya kitengo hiki kuwa muhimu kwenye Swahilihub (Taz. Chati 4.3).




**Chati SURA YA NNE .3: Matokeo ya Matumizi ya Habari**

Kitengo cha Jifunze Kiswahili kilitumika sana miongoni mwa asilimia 26.6 ya watumiaji wa Swahilihub walioshiriki kwenye utafiti huu huku asilimia 36.3 wakikitumia kwa wastani. Ingawa asilimia 62.9 (235) ya watafitiwa walikitumia kitengo hiki, matumizi yake hayakudhihirika miongoni mwa asilimia 37.1 ya watumiaji wa tovuti ya Swahilihub. (Taz. Chati 4.4).




**Chati SURA YA NNE .4: Matokeo ya matumizi ya Jifunze Kiswahili**

Picha ni kitengo kimojawapo cha vitengo vinane vya tovuti ya Swahilihub vinavyotumiwa katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Kuhusu matumizi ya picha, matokeo ya utafiti huu yalionyesha kwamba ni asilimia 14.7 (watu 49) ya watumiaji waliokiri kukitumia sana kitengo hiki katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili na asilimia 30.6 (104) walioitumia na hivyo basi kudhihirisha kuwa asilimia 45.3 (154) ya watafitiwa ndio walioitumia picha kuikuza lugha ya Kiswahili. Takriban 54.7 (185) ya watafitiwa hawakukitumia kitengo cha picha katika shughuli zao kuikuza lugha ya Kiswahili licha ya picha kuwa kitengo muhimu kwenye tovuti ya Swahilihub.




**Chati SURA YA NNE .5: Matokeo ya matumizi ya picha**

Kuhusu matumizi ya Blogu na Ukumbi, asilimia 10.8 ya watumiaji wa tovuti ya Swahilihub walikiri kukitumia sana kitengo hiki huku asilimia 20.4 wakikitumia hivyo basi kwa jumla asilimia 31.2 (106) ya watafitiwa ndio walioitumia Blogu na Ukumbi katika shughuli zao mtandaoni (Taz. Chati 4.6 na Picha 4.36).





*Picha SURA YA NNE .2: Kitengo cha Blogu na Ukumbi*

Matokeo ya uchunguzi uliofanywa na ARhefs pamoja na mrejesho wa mahojiano, mijadala na hojaji yalibainisha kuwa takriban asilimia 68.8 (233) ya watafitiwa hawakukitumia kitengo cha blogu na ukumbi kuikuza taaluma ya Kiswahili licha ya kuwa kitengo muhimu. Matokeo haya ni duni yakilinganishwa na yale ya utafiti wa awali kuhusu ukubalifu wa tovuti za hoteli. Matokeo haya yalibainisha ukubalifu kwa asilimia 48% kwa mujibu wa utafiti wa Owoche, (2019).

Matokeo haya yalichangiwa na ukosefu wa uwiano wa kitengo cha Blogu na Ukumbi miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub ambao walikichukulia kama kitengo kisichoingiliana na hali, maadili na mazoea yao ya awali. Ili kufanikisha msambao wa uvumbuzi, uwiano huchangia pakubwa. Kitengo hiki kilichukuliwa kama kitengo kisichoweza kuchangia kwa vyovyote michakato ya ufundishaji na hivyo basi watumiaji wengi wa tovuti ya Swahilihub walikikwepa. Iwapo matumizi ya Blogu na Ukumbi yatawiana na imani, maadili na mahitaji ya watumiaji wa tovuti ya Swahilihub basi matumizi yake yataongezeka haraka na kwa urahisi.

Matokeo ya utafiti huu yalibaini kuwa uchangamano ni sababu nyingine ya matumizi duni ya Blogu na Ukumbi. Blogu na Ukumbi ilichukuliwa kuwa na ugumu wa kuelewa na kuitumia miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub. Uvumbuzi wo wote unapochukuliwa kuwa changamano na mgumu kutumia inakuwa vigumu kukubaliwa na kutumiwa na wanajamii Rodgers, (2003). Ni rahisi kwa uvumbuzi kukubaliwa na kutumiwa na wabwiaji wengi iwapo matumizi ya mashine yanayohusika ni sahili na rahisi kuelewa (Martin, 2003).




**Chati SURA YA NNE .6: Matokeo ya Matumizi ya Blogu na Ukumbi**

Katika mchakato wa ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili, tovuti ya Swahilihub ilitumia kitengo cha Maktabani Jisomee. Maktabani Jisomee ni kitengo cha tovuti ya Swahilihub ambacho hutumiwa kunasa watumiaji wake kupitia kwa mawasilisho ya hoja mahususi na dhana mbalimbali zinazojenga hifadhi ya masuala muhimu katika michakato ya ukuzaji wa lugha ya Kiswahili (Taz. Picha 4.5).




*Picha SURA YA NNE .3: Kitengo cha Maktabani Jisomee*

Kuhusu matumizi ya Maktabani Jisomee, matokeo ya utafiti huu yalibaini kwamba ni asilimia 22.8 (77) ya watumiaji waliokiri kukitumia sana kitengo hiki katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili na asilimia 35.0 (119) waliitumia na hivyo basi kudhihirisha kuwa kwa jumla asilimia 57.8 (196) ya watafitiwa ndio waliokitumia kitengo cha Maktabani Jisomee kuikuza taaluma ya Kiswahili.




**Picha SURA YA NNE .4: Kitengo cha Video**

Tovuti ya Swahilihub inapakia video mtandaoni na katika kurasa zake za YouTube, Facebook na Twitter kwa Kiswahili Sanifu na kwa njia hii kitengo hiki kinakuza lugha ya Kiswahili kwa kuangazia masuala yanayokuza teknohama na usasa katika uboreshaji wa Kiswahili. Kiswahili hutumika katika mitandao ya Facebook na Twita kama nyenzo za mawasiliano. Matokeo ya utafiti huu yalibaini kwamba ni asilimia 11.7 (39) pekee ya watumiaji wa tovuti ya Swahilihub waliokiri kukitumia sana kitengo cha video katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili na asilimia 26.5 (90) waliitumia na hivyo basi kudhihirisha kuwa asilimia 38.2 (129) ya watafitiwa ndio walioitumia video katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili. Uchunguzi uliofanywa kwa msaada wa ARhefs ulibainisha pia kuwa takriban asilimia 61.8 (210) ya watafitiwa hawakukitumia kitengo cha video kuiendeleza taaluma ya Kiswahili licha ya kuwa kitengo muhimu kwenye tovuti ya Swahilihub.

Hali hii ilichangiwa na ukosefu wa uwazi kuhusu manufaa ya tovuti ya Swahilihub na kiwango ambacho tovuti hii ilivyochukuliwa kuwa ya manufaa kwa wabwiaji wake. Ukosefu wa motisha miongoni mwa watumiaji wa Swahilihub ulichangiwa na kutokuwa na uwazi kuhusu manufaa ya lugha ya Kiswahili katika mawanda yake mapana. Kiwango cha uwiano wa video miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub kilikuwa chini kutokana na kufanikisha machukulio yao kwamba video haikuingiliana na hali, maadili na mazoea yao ya awali. Iwapo matumizi ya uvumbuzi yanawiana na imani, maadili na mahitaji ya wabwiaji basi uvumbuzi huo hukubalika haraka na kwa urahisi. Uvumbuzi wowote unapochukuliwa kuwa changamano na ngumu kutumia inakuwa vigumu kukubaliwa na kutumiwa na wanajamii Rodgers, (2003). Ni rahisi kwa uvumbuzi kukubaliwa na kutumiwa na wabwiaji wengi iwapo matumizi ya mashine yanayohusika ni sahili na rahisi kuelewaka (Martin, 2003).




*Chati SURA YA NNE .7: Matokeo ya matumizi ya video*




*Picha SURA YA NNE .5: Mikakati mbalimbali ya matumizi ya Video.*

Ukuzaji wa Kiswahili umebainika katika kitengo hiki kwa misingi mikuu ifuatayo:

Makala ni kitengo kimojawapo cha vitengo vya tovuti ya Swahilihub vinavyotumiwa katika ukuzaji na maendeleo ya taaluma ya Kiswahili. Ni kitengo cha mwisho katika orodha ya vitengo vyote kwenye jukwaa la Swahilihub. Kitengo hiki hukusudia kuimarisha na kuhifadhi matini inayohitajika katika ukuzaji wa tovuti ya Swahilihub miongoni mwa watumiaji wake (Taz. Picha 4.41).




*Picha SURA YA NNE .6: Kitengo cha Makala*

Kitengo cha habari ndicho kilichotumiwa kwa wingi kwa asilimia 66 (224) kikifuatwa kwa karibu na jifunze Kiswahili kwa asilimia 63 (225) maktabani jisomee kwa asilimia 58 (197) na makala kwa asilimia 56 huku blogu na ukumbi kikitumiwa kwa kiwango cha chini zaidi kwa asilimia 31 kikifuatwa na video kwa asilimia 32 ya matumizi. Matokeo haya yalibainisha kwamba vitengo vya Habari, Jifunze Kiswahili, Maktabani Jisomee na Makala viliwafikia watuamiaji wengi zaidi kuliko vitengo vingine vyote. Hii ilitokana na mchango wa moja kwa moja wa vitengo hivi katika usambaaji na udumishaji wa Kiswahili kupitia ufundishaji wake. Ni thibitisho kwamba matini iliyopatikana kwenye vitengo hivi ilikuwa stahilifu na faafu zaidi na hivyo basi kuwapendeza watumiaji wengi wa tovuti ya Swahilihub. Vitengo vya Video na Blogu na Ukumbi havikuwapendeza watumiaji wengi, na hivyo basi kuepukwa na watumiaji wengi kwa asilimia 69 na 68 mtawalia. Ingawa matokeo ya matumizi yao ni ya chini, vitengo vya Video na Blogu na Ukumbi, huwa ni rahisi kutumia na vilichangia pakubwa katika usambaaji wa Kiswahili miongoni mwa watumiaji wengi mtandaoni.


Kutokana na matokeo ya utafiti huu, tulibaini kuwa tovuti ya Swahilihub imeumbwa kama jukwaa la TEHAMA ambalo lina nafasi kubwa ya kukuza taaluma ya Kiswahili kwa kuboresha mbinu mbalimbali zinazotumiwa kuijenga, kuisambaza na kuimarisha hadhi na dhima yake kupitia michakato ya elimu ya Kiswahili. TEHAMA hutokea kwa namna mbalimbali kwenye tovuti ya Swahilihub kupitia vitengo vyake mbalimbali vinavyotumika katika ueneaji na ukuaji wa lugha ya Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kwamba vitengo hivyo vilitumiwa kwa kiasi tofauti tofauti na watumiaji wa Swahilihub huku wengine wakivitumia sana, wengine wakivitumia, wengine wakisema hawajui na wengine hawavitumii kabisa.

Hata hivyo kwa jumla zaidi ya asilimia 52 (176) ya watafitiwa walikiri kutotumia vitengo vyovyote vya tovuti ya Swahilihub kama jukwaa la ujenzi, usambaaji na udumishaji wa hadhi na dhima ya Kiswahili mtandaoni. Matokeo haya yanaashiria mwamko wa kiwango cha chini

cha matumizi ya tovuti ya Swahilihub. Kwa mujibu wa nadharia ya Msambao wa Uvumbuzi wa (Rodgers, 2003) msambao wa uvumbuzi hutokea katika hatua mbalimbali (Taz. 1.8.4). Watafitiwa wengi asilimia 52 (176) walikiri kutotumia tovuti ya Swahilihub kwa kukosa kujua iwapo tovuti hiyo ipo na hata inavyofanya kazi. Kutokana na data ya hojaji iliyopatikana nyanjani, utafiti huu ulitambua kuwa watumiaji wa Swahilihub hupata maarifa kuhusu masuala ya Kiswahili miongoni mwa mambo mengine mengi ya kimsingi katika maisha na jamii kwa upana wake. Tovuti ya Swahilihub inategemewa katika kusambaza habari na maarifa kwa lugha ya Kiswahili kwa haraka na kwa watu wengi duniani. Kwa msingi huu Swahilihub inatoa mchango mkubwa katika ukuzaji wa Kiswahili kwa kuijengea kanzi ya istilahi na hivyo basi kuwezesha usambaaji wake miongoni mwa watu wengi. Utafiti huu umebaini kuwa tovuti ya Swahilihub ilibuniwa katika mfumo ambao unamwezesha mtu yeyote kupakua data yoyote akiwa mahali popote ulimwenguni almuradi ameunganishwa kwenye masafa ya mtandao. Uzinduzi pekee wa tovuti ya Swahilihub hautoshi, bali ni muhimu tovuti hii ifikie hadhira lengwa na kwa wakati unaofaa. Miongoni mwa mambo yanayochangia ukuzaji wa Kiswahili ni idadi ya watu walioubwia uvumbuzi wa mradi wa Swahilihub katika kipindi cha takriban mwongo mmoja tangu kuasisiwa kwake.

Matokeo haya ya chini huenda yalitokana na mapuuza miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub na pia kuchangiwa na ukosefu wa maelekezo faafu kwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub kuhusu ni wapi hasa wanapoweza kupata habari mahususi wanazohitaji. Isitoshe, matokeo haya ya chini huenda yalichangiwa na gharama kubwa ya fedha inayohitajika kwa uhariri wa matini kwenye vitengo hivi. Matini kwenye kitengo cha Blogu na Ukumbi yanahitaji sio tu uhariri wa kila mara bali pia yanastahili mchango wa utafiti wa dhati kwa gharama kubwa. Ili kuimarisha matumizi ya vitengo hivi, utafiti mbalimbali wa kuboresha matini na muundo wa tovuti ya Swahilihub unastahili kufanyika kila mara.

Licha ya umuhimu wa vitengo hivi, matokeo haya yalibainisha idadi ya juu ya wale waliokwepa kuvitumia. Hali hii ilichangiwa na kiwango cha chini cha uwiano wa vitengo hivyo miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub. Vitengo hivi vilichukuliwa kuingiliana kwa kiwango cha chini na hali, maadili na mazoea ya awali ya watumiaji wa Swahilihub (Taz.1.8.3.). Ili kufanikisha msambao na ukubalifu wa tovuti ya Swahilihub, uwiano wake miongoni mwa watumiaji wake huchangia pakubwa kuathiri mielekeo, imani, maadili, na maoni yao. Iwapo matumizi ya tovuti ya Swahilihub yanawiana na imani, maadili na mahitaji ya watumiaji wake basi ukubalifu wake unaweza kuimarika haraka na kwa urahisi.




**Picha SURA YA NNE .7: Vitengo mbali mbali vya Tovuti ya Swahilihub.**

Utafiti huu uligundua kwamba watumiaji wachache wa tovuti ya Swahilihub, asilimia 48 (163) huvitumia vitengo mbalimbali vya tovuti ya Swahilihub kama ilivyoonyeshwa katika jedwali 4.1. Hii ni idadi ya watumiaji wa tovuti ya Swahilihub waliofikia hatua ya tatu ya Rodgers, (2003) ya uamuzi wa kuitumia tovuti ya Swahilihub (Taz. Mchoro 1.1.). Hii ndiyo asilimia 48 (163) ya watafitiwa walioamua kuukubali na kuutumia mradi wa Swahilihub katika shughuli mbalimbali za ukuzaji wa Kiswahili kwa jumla.

### 4.2.1. Misingi ya Ukuzaji Kiswahili katika tovuti ya Swahilihub

Kwa mujibu wa maandishi yaliyohakikiwa, ukuzaji wa Kiswahili ni jumla ya hatua zinazochukuliwa ili kupanua wigo wa matumizi yake katika shughuli mbalimbali za jamii na hivyo basi kuingizwa katika harakati mbalimbali kama vile katika siasa, uchumi, elimu na pia majumbani mwa watumiaji wake. Ukuzaji wa Kiswahili huakisiwa kwa vigezo mbalimbali kama vile upanuzi wa matumizi yake, uimarishwaji wa misamiati na istilahi zake, ongezeko la idadi ya watumiaji wake, hadhi na dhima yake kupaa juu, kuchipuka kwa aina mbalimbali za matumizi yake, uvumbuzi na ugunduzi wa kisayansi na utambuzi wake katika utawala na siasa. Usambaaji wa Kiswahili ni nguzo muhimu ya ukuzaji wake inayojumuisha ueneaji wake. Usambaaji wa Kiswahili ni uongezekaji wa matumizi yake kieneo na kiwakati. Tovuti ya Swahilihub ilibaini dhana ya usambaaji wa Kiswahili kupitia mikakati yake ya kuyafikia mahitaji ya watumiaji wake mtandaoni na kuwaruhusu kuungana na marafiki na familia, na kushiriki taarifa, picha na video. Ingawa Cooper (1990) aliangazia ukuzaji lugha kwa vigezo vitatu; ueneaji kimsamiati na sarufi, usambaaji kieneo na udumishaji hadhi, utafiti huu ulibaini kwamba ukuzaji ni swala pana linaloakisi vigezo vya ndani na nje vikiwa ni pamoja na ukuzaji kikongoo, kihadhi na kieneo. Ukuzaji lugha kikongoo ni kusanyiko la data za semi zilizoandikwa au kunukuliwa ambazo hutumiwa kama kianzio cha ufafanuzi wa kiisimu. Ukuzaji lugha kikongoo unahusika na muundo wa ndani wa lugha. Mambo yanayozingatiwa hapa ni pamoja na kuunda othografia kwa lugha ambazo bado hazijaandikiwa, kuanzisha mabadiliko katika tahajia, kubuni maneno mapya na kuchapisha vitabu vya sarufi na makamusi.

Ukuzaji wa aina hii unahusu kuendeleza mbinu za kujifunza lugha iliyoteuliwa kupitia mifumo ya elimu. Ukuzaji kikongoo pia unahusu kupanua ufunzaji na ujifunzaji wa lugha kimaksudi.

Simala (2019) na Agume (2022) wanabainisha kuwa ukuzaji lugha kihadhi ni juhudi za kimaksudi za kuathiri na kuleta mabadiliko katika majukumu ambayo lugha inatwikwa. Aidha, wataalam hawa wanabainisha kuwa ufanisi wa ukuzaji lugha hutokana na mchakato unaofaa wa utekelezaji wake. Michakato kama hiyo huakisi ukuzaji wa lugha zote hasa lugha zinazofaa kuwa na hadhi sawa. Tathmini ya Swahilihub ilitokana na uchunguzi wa kiteknolojia wa Arhefs pamoja na matokeo yaliyopatikana kwenye majibu ya hojaji na usaili nyanjani. Tathmini hii iliegemezwa kwenye vigezo vitatu vya ukuzaji wa Kiswahili: ukuzaji kikongoo, usambaaji na ukuzaji wake kihadhi na dhima. Watafitiwa walioshiriki katika utafiti huu walikiri kwamba waliweza kuitumia tovuti ya Swahilihub kwa njia anuai ili kuikuza lugha ya Kiswahili. Miongoni mwa njia hizo za ukuzaji ni pamoja na ujenzi wake kiisimu, usambaaji wa fasihi yake na udumishaji wa hadhi yake kupitia utafiti mbalimbali wa kitaaluma. Njia hizi mbalimbali zimebainishwa katika jedwali 4.1.


Katika muktadha wa Kenya, Kiswahili kilipewa hadhi kama lugha rasmi sawa na Kiingereza. Kwa hivyo, juhudi za utekelezaji wa sera ya lugha ya elimu zinafaa zishughulikiwe katika mchakato mzima wa sera ya lugha na ukuzaji lugha. Ili ukuzaji wa Kiswahili utimie kikamilifu, ni lazima kuweko na uungaji mkono wa wanasiasa, yaani ukubalifu wa serikali katika shughuli nzima ya uundaji na utekelezaji wa sera ya lugha kwa ajili ya kufanikisha mchakato mzima wa ukuzaji wa Kiswahili (Legere, 2002) na Kandagor (2012; 2013a). Utafiti huu ulibaini mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili kwa misingi mitatu ya ukuzaji wa lugha: ukuzaji kikongoo, yaani ujenzi wa msamiati na maarifa katika mawanda ya Kiswahili kama vile riwaya, tamthilia na ushairi wa Kiswahili; usambaaji wa Kiswahili pamoja na udumishaji wa hadhi na dhima ya Kiswahili (Cooper, 1990; Simala, 2019 na Agume, 2022).

#### 4.2.1.1. Ukuzaji Kiswahili kikongoo katika Swahilihub

Katika sehemu hii, matokeo ya utafiti yamebaini kwamba Swahilihub imechangia ukuzaji Kiswahili kikongoo. Ukuzaji wa lugha ya Kiswahili ulidhihirika katika hatua ya nne ya utekelezaji wa msambao kupitia vitengo mbalimbali vya tovuti ya Swahilihub kama ifuatavyo.

##### 4.2.1.1.1 Jifunze Kiswahili

Matini ya Kiswahili ni nguzo muhimu katika ukuzaji wake mtandaoni. Matini katika kitengo cha Jifunze Kiswahili ilitumiwa kama raslimali muhimu katika ujenzi wa msamiati, istilahi na sarufi ya lugha ya Kiswahili. Matini kwenye kitengo cha Jifunze Kiswahili yalichangia katika ujenzi wa sarufi na msamiati wa Kiswahili kwa kuhifadhi matini yaliyohaririwa ili kuyakidhi mahitaji ya watumiaji wake kwenye tovuti ya Swahilihub. Ufundishaji wa Kiswahili ulitegemea pakubwa thamani ya matini ya Kiswahili katika kitengo hiki.


NYUMBANI MAKTABA UTAFITI/IKISIRI HADITHI MASHAIRI/TENZI MAKALA VIDEO

TAIFALEO HABARI

Taifaleo

HIFADHI YA KISWAHILI

METHALI
MISEMO
NAHAU
VITENDAWILI

MAGAZETI YA KISWAHILI

Mwananchi – Tanzania
Mwanaspoti – Tanzania
Taifa Leo – Kenya
Mtanzania – Tanzania
Habari Leo – Tanzania
Majira – Tanzania
Nipashe – Tanzania
Tanzania Daima – Tanzania

VYANZO VYA KISWAHILI

Redio
Runinga
Magazeti
Vitabu

Wahenga ni wazee wenye akili waliotutangulia. Walifikiria na kutunga misemo kwa lengo la kuadabisha, kuonya, kukumbusha wajibu wa kila kundi katika jamii. Ipo misemo ambayo inawagusa vijana, wazee, watu wazima, wanawake, wanaume.

Mathalani vifo vya wajawazito vilipokithiri enzi hizo, wahenga walibaini chanzo ni ulaji wa mayai kipindi chote cha mimba na kusababisha mtoto kunenepa sana huko tumboni na kushindwa kupita kwenye njia ya uzazi. Hivyo, wakaanzisha msemo kama, 'Mama mjamzito akila mayai, mtoto atazaliwa bila nywele' ili kuzuia ulaji wa kupindukia wa mayai kwa wajawazito.

Tupitie misemo hii ya wahenga;

1. Huwezi kusukuma gari bovu ukiwa umekaa ndani yake

Hii inamaanisha lazima uteremke chini. Maana hiyo inakwenda mbali zaidi kwamba unapohitaji kutatua tatizo ni lazima uwashirikishe wengine waliokuzidi maarifa.

2. Samaki anayefumba mdomo wake, hashikwi na ndoano ya mvuvi

Ni ushauri kwamba ujiepusha kuzungumza kila jambo kwani kuna watu wengi huenda wana hamu ya kukunasa kupitia kukosea kwako. Kumbuka hakuna binadamu mkamilifu chini ya jua.

3. Maskini hana hoja, ana haja

Inatukumbusha kwamba tufanye kila njia kuukimbia umaskini.

4. Hujafa hujauumbika

Kila mtu anathamani, uhai ni suala la muda tu.

MAONI MAPYA

Amani Njoka on Uundaji wa maneno ya Kiswahili
PETER M.ELIAS on Uundaji wa maneno ya Kiswahili
Amani Njoka on Wahitimu 35 watunukiwa shahada ya Kiswahili UDSM, mwanafunzi wa Kiswahili aongoza
Robert Ayubu on Wahitimu 35 watunukiwa shahada ya Kiswahili UDSM, mwanafunzi wa Kiswahili aongoza
Gadi Solomon on Muuaji asakwe

**Picha SURA YA NNE .8: Mifano ya misemo katika ujenzi wa msamiati kwenye kitengo cha Jifunze Kiswahili**

Ujenzi wa Kiswahili ulitokea kwenye kitengo hiki kutokana na makala yaliyoimarisha sarufi ya Kiswahili na kuuboresha usanifu wake miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub. Kwa mfano misemo katika picha 4.24 ilichangia katika ujenzi wa misamiati na istilahi na usambaaji wa misemo ya Kiswahili kote ulimwenguni. Gazeti la *Taifa Leo*, ambalo mpaka sasa ni gazeti pekee la Kiswahili nchini Kenya, linaandaa mitihani yenye majibu katika Kiswahili na masomo mengine na kuichapisha gazetini ili itumike shuleni bila malipo. Gazeti la *Taifa Leo* pia linachapisha makala ya lugha na fasihi kutoka kwa wataalamu wa Kiswahili yanayolenga wanafunzi na walimu wa shule za upili nchini Kenya.

Isitoshe, tovuti ya Swahilihub, inayoendeshwa na gazeti hili pamoja na lile la *Mwananchi* nchini Tanzania, imechapisha miongozo ya fasihi iliyozamia kwa kina maudhui, fani, wahusika, mtiririko na maswali ya udurusu wa fasihi katika vitabu teule vya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine na Mstahiki Meya*. Miongozo kama hii inatoa nafasi kwa wanafunzi kuelewa dhana anuwai za fasihi na kuikuza Kiswahili kwa hadhira pana ya watumiaji wa tovuti ya Swahilihub. Habari, maoni na makala kemkem katika *Taifa Leo* yanaangazia masuala ibuka kote duniani kama vile siasa, michezo, uchumi, dini, jamii, elimu na kadhalika na ni chombo mufti cha kufundishia isimu jamii, ufahamu, ufupisho, sarufi na hata mashairi ya Jumamosi na Jumapili.

Mwananchi

TAIFALEO HABARI

Taifaleo

HIFADHI YA KISWAHILI

METHALI
MISEMO
NAHAU
VITENDAWILI

MAGAZETI YA KISWAHILI

Mwananchi – Tanzania
Mwanaspoti – Tanzania
Taifa Leo – Kenya
Mtanzania – Tanzania
Habari Leo – Tanzania
Majira – Tanzania
Nipashe – Tanzania
Tanzania Daima – Tanzania

VYANZO VYA KISWAHILI

Redio
Runinga
Magazeti
Vitabu
Majarida
Vipeperushi
Vyama
Asasi
Taasisi
Vikundi

iliundwa na nchi za Kenya, Tanganyika, Uganda na Zanzibar. Jumuiya ya sasa iliundwa mwaka 1967 na kuvunjika mwaka 1977.

Lugha ya Kiswahili ilionekana kuwa ni nyenzo madhubuti ya kuimarisha ushirikiano baina ya nchi hizi hasa kwenye masuala ya elimu, uchumi, ustawi wa jamii, sayansi, teknolojia, utamaduni na lugha Jumuiya mpya imeleta mabadiliko katika utendaji na mipango ya kazi.

Kwa mujibu wa Mtendaji Mkuu wa Kamisheni ya Kiswahili, Prof Kenneth Inyani Simala, Jumuiya mpya inaashiria utangamano wa kikanda unaoendana na mwelekeo wa sasa wa dunia ambapo lugha inachukuliwa kama taasisi muhimu inayostahili kuzingatiwa kwa makini.

Hivyo lugha ya Kiswahili inaagaliwa kama nyenzo muhimu katika kuimarisha ushirikiano na utangamano wa kikanda kwa maendeleo endelevu.

**Na Antoney Owino Oloo**

Chuo Kikuu cha Kababtii Lugha ya Kiswahili ambayo ndiyo inayoongoza kwa ukubwa na umaarufu miongoni mwa lugha kuu za asili za Afrika imezidi kushuhudia mwamko mpya. Kadiri inavyozidi kubadilika na kuashiria dalili za kutumiwa na watu wengi duniani kote, ndivyo inavyozidi kukumbatia na kutumika kwenye majukwaa mbalimbali ya utandawazi.

Miongoni mwa majukwaa hayo ni Swahili Hub ambao ni mradi mahususi wa kukikuza, kukiendeleza na kukiimarisha Kiswahili. Tafsiri ya Swahili Hub ni kitovu cha Kiswahili. Kitovu hiki kina tovuti yake inayohifadhi, kukuza na kuendeleza taaluma ya Kiswahili mtandaoni.

Ni mojawapo ya majukwaa yanayohimiza matumizi ya lugha ya Kiswahili mtandaoni. Kiswahili pia inatumika vilivyo katika tovuti ya kupeana, kupeleka na kutafuta taarifa.

Tovuti za Kiswahili zimezagaa duniani na nyingi ziko Marekani na Ulaya na hata Afrika zimeanza tovuti zenye kufundisha Kiswahili, kusoma na kusikia kupita kompyuta.


Zipo kamusi za Kiswahili, makala na maelazo ya kitaaluma kuhusu Kiswahili. Ziko injini za (search engines) zenye kutumia Kiswahili (mfano Google). Juhudi mmbalimbali zimekuwa zikifanywa katika kukienzi Kiswahili katika naja za sayansi na teknolojia. Miongoni mwa juhudi hizo ni kutekeleza Mradi wa Swahili Language Manager (SALAMA) kwa ushirikiano na TATAKI na Kikuu cha Helniski unaokusanya maneno na matini za lugha ya Kiswahili, kuwa na kusanyo la data za Kiswahili na kisha kuchanganua kiisimu, kupatia tafsiri za Kiingereza na kuhifadhi kwa ajili ya watumiaji.

MAONI MAPYA

Amani Njoka on Uundaji wa maneno ya Kiswahili
PETER M.ELIAS on Uundaji wa maneno ya Kiswahili
Amani Njoka on Wahitimu 35 watunukiwa shahada ya Kiswahili UDSM, mwanafunzi wa Kiswahili aongoza
Robert Ayubu on Wahitimu 35 watunukiwa shahada ya Kiswahili UDSM, mwanafunzi wa Kiswahili aongoza
Gadi Solomon on Muuaji asakwe

**Picha SURA YA NNE .9: Makala za tafiti mbalimbali kwenye kitengo cha Jifunze Kiswahili**

Kitengo hiki kililenga kuikuza lugha ya Kiswahili kupitia kwa michakato na mikakati anuai. Kwa mfano makala ya Owino katika picha 4.4 ilichangia katika usambaaji wa Kiswahili kupitia kwa majukwaa ya kidijitali. Kwenye kitengo hiki kuliwekwa makala zilizowaelekeza wanafunzi wa viwango mbalimbali. Vile vile kitengo hiki kilikuwa na nakala mbalimbali za insha bora zilizotuzwa na kuchangia katika juhudi za ukuzaji wa Kiswahili miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub. Vipindi mbalimbali vya ufundishaji wa Kiswahili viliendeshwa kwenye kitengo hiki kwa ushirikiano na redio Q-fm. Vipindi hivi vilitoa mchango mkubwa katika ujenzi wa sarufi, istilahi na misamiati ya Kiswahili miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub. Mashairi ya Kiswahili yaliyohifadhiwa katika kitengo hiki yalitoa mchango mkubwa katika ujenzi wa Kiswahili na udumishaji wake kikongoo miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub. Nyimbo za taarab na muziki wa kitamaduni zilitoa mchango mkubwa katika mchakato wa ufundishaji wa fasihi ya Kiswahili mtandaoni. Methali, misemo na nahau zilichangia kupiga jeki mikakati ya ufundishaji wa Kiswahili mtandaoni.




**Picha SURA YA NNE .10: Ujenzi wa lugha kupitia  nahau kwenye kitengo cha Jifunze Kiswahili**

Katika kuijenga lugha ya Kiswahili kisarufi, istilahi na misamiati, wasimamizi wa Swahilihub walihusisha mradi wa kamusi za mtandao wa Chuo Kikuu cha Yale unaojulikana kama 'The Internet Living Swahili Dictionary' ili kuboresha kiwango cha istilahi na misamiati yake mtandaoni. Mradi huu ulitokana pia na juhudi za wataalamu wengi wa Kiswahili kutoka kote ulimwenguni. Mradi huu hupokea michango kutoka kwa wataalamu anuwai na kuihariri ili kupata nakala kamilifu ya kamusi mtandaoni. Pamoja na *Kamusi Kuu* na miongozo katika picha 4.5, kamusi hizi zilichangia katika ujenzi wa Kiswahili kupitia upanuzi wa misamiti na istilahi zake mtandaoni. Kufikia sasa mradi huu wa kamusi za kimtandao una makamusi ya Kiswahili-Kiingereza, Kiingreza-Kiswahili, mwongozo wa matamshi bora ya lugha ya Kiswahili, mafunzo ya sarufi ya Kiswahili na tafsiri kupitia mtandao. Mradi huu una kamusi zifuatazo: English- Swahili Dictionary (1995); Swahili- English Dictionary (1995) na Kamusi ya Russian- Swahili- Russian. Kamusi hizi zinapatikana mtandaoni na zimetumiwa haswa kwa kufuata maagizo ipasavyo katika tovuti ya Swahilihub.




**Picha SURA YA NNE .11: Umuhimu wa Kitengo cha Jifunze Kiswahili**


Kutokana na matokeo ya mijadala ya makundi, mahojiano na mrejesho wa hojaji, kigezo kilichochangia katika ubwiaji na matumizi ya kitengo cha Jifunze Kiswahili kilikuwa ni uwazi kuhusu manufaa yake na jinsi kitengo hiki kilivyochukuliwa kuwa cha manufaa kwa wanafunzi wa Kiswahili. Isitoshe uwiano wa kitengo hiki na machukulio ya watumiaji wake kwa namna kilivyochukuliwa kuingiliana na hali, maadili na mazoea yao katika michakato ya ufundishaji na ujifunzaji lugha ya Kiswahili yalikuwa na manufaa kwa ubwiaji wa tovuti ya Swahilihub. Ili kufanikisha msambao wa uvumbuzi, uwiano huchangia pakubwa.

#### 4.2.1.1.2 Blogu na Ukumbi

Matumizi ya kitengo cha Blogu na Ukumbi yalichangia katika ukuzaji wa Kiswahili kikongoo. Shughuli za kiuchumi, kisiasa, kijamii, kitamaduni, kisayansi, kielimu, kiroho na kiteknolojia hutokea kwa kiwango kikubwa kwenye kitengo cha blogu na ukumbi. Shughuli hizi huchangia matumizi ya istilahi na misamiati mwafaka ili kuyakidhi mahitaji ya watumiaji wa Swahilihub. Tovuti hii inawapa wanajamii nafasi ya kuyasoma mambo haya kwa nia ya kujiboresha zaidi na kuikuza lugha ya Kiswahili. Taarifa hizi zinawafikia pindi zinapopakiwa. Awali, kabla ya kuzinduliwa kwa tovuti ya Swahilihub, ujuzi huu ulipatikana kwa ugumu sana kwani watumiaji walihitajika kutafuta machapisho haya moja kwa moja. Vilevile, tovuti ya Swahilihub inawapa watumiaji wake uhuru wa kutoa maoni kuhusu taarifa zinazopakiwa kwenye Swahilihub papo hapo pindi habari hizo zinapopakiwa. Watumiaji wa tovuti ya Swahilihub ni watu wa kutoka sehemu mbalimbali za ulimwengu. Mtagusano wa watu hawa wenye tajriba, mielekeo na uelewa tofauti wa mambo unawasaidia wanajamii kukuzana hasa wanapotoa maoni yao mbalimbali kuhusu masuala haya ibuka. Mitagusano hii huchangia pakubwa katika usambaaji wa Kiswahili na udumishaji wa hadhi na dhima yake katika maeneo mbalimbali kote ulimwenguni.

Kiswahili ni miongoni mwa lugha zinazopokea maneno kutokana na matumizi yake kwenye mitandao hususan katika maendeleo ya sayansi na teknolojia, siasa, kijamii na uchumi. Kwa

mfano, kuna istilahi nyingi za kimtandao za sayansi na teknolojia ambazo hutumiwa katika shughuli mbalimbali za kijamii kwenye vitengo vyote vinane vya Swahilihub. Kitengo hiki kiliimarisha uvumbuzi na ubunifu wa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub. Kitengo cha Blogu na Ukumbi ni jukwaa muhimu katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kupitia kwa mawasiliano na mitagusano miongoni mwa wataalam wa Kiswahili. Kwa mujibu wa Rodgers (2003) mawasiliano ni mchakato unaowawezesha wanajamii husika kubuni, kushiriki na kusambaza habari miongoni mwao ili kuyafikia malengo fulani mahususi. Vyombo vya habari kama vile runinga na redio mbalimbali na mitagusano ya kibinafsi ni zana muhimu za mawasiliano miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub.




**Picha SURA YA NNE .12: Mitagusano kwenye Blogu na ukumbi katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili**

Blogu na Ukumbi ni kitengo kilicho na nafasi kubwa ya kufikisha tovuti ya Swahilihub kwenye upeo wa matumizi yake katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Rodgers (2003) anadahili kwamba upeo ni tukio katika mchakato wa msambao wa uvumbuzi ambapo uvumbuzi huo hushika kani na kuanza kuenea kwa kasi. Upeo ni kigezo cha ukubalifu wa tovuti ya Swahilihub na hujengwa kwa msaada wa ushirikiano na utangamano wa wataalamu na washikadau mashuhuri wanaoheshimika katika taaluma ya Kiswahili. Swahilihub hutegemea kitengo hiki cha Blogu na Ukumbi ili kufanikisha lengo lake la kushirikiana na waandishi, wahariri wa makala na wenye blogu za Kiswahili katika kuongeza wigo wa mawasiliano yao Afrika Mashariki na duniani kote.

#### 4.2.1.1.3 Maktabani Jisomee

Matumizi ya kitengo cha Maktabani Jisomee yalichangia pakubwa katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili kwa ujenzi wa istilahi, sarufi na matini mwafaka. Matumizi ya kitengo hiki yaliimarisha usikilizaji na ubunifu wa wanafunzi mtandaoni. Vitabu mbalimbali kwa mfano makamusi ya Kiswahili Sanifu, mwongozo wa waandishi wa Kiswahili sanifu, vilichangia katika kujenga misamiati na istilahi ya lugha ya Kiswahili. Tazama picha 4.6 na picha 4.8.





**Picha SURA YA NNE .13: Mifano ya vitabu katika kitengo cha Maktabani Jisomee**

Mchango wa Swahilihub kwa mchakato wa ukuzaji wa Kiswahili umebainika katika juhudi za wanazuoni katika taaluma za isimu, isimujamii, fasihi na utafiti wa nyanja anuai za Kiswahili. Kwa mfano kitabu cha mwongozo kwa waandishi wa Kiswahili Sanifu kilichangia katika maenezi ya Kiswahili Sanifu kieneo na kiwakati. Tazama picha 4.8. Vitabu kama vile kamusi kuu na mwongozo kwa waandishi wa Kiswahili Sanifu katika kitengo hiki pia vilidhihirisha uwezo wa Swahilihub kuimarisha ujenzi wa misamiati ya Kiswahili na kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili.





**Picha SURA YA NNE .14: Michakato ya ukuzaji wa lugha ya Kiswahili**

Picha 4.9 inatoa maelezo yanayoafiki mchango wa kitengo cha Maktabani Jisomee katika ukuzaji Kiswahili kwa kubaini Makala anuai zinazopatikana katika kitengo hiki kwa mfano Makala kuhusu miaka 50 ya uhuru wa Tanzania, mawaidha ya dini ya kiislamu, darubini ya kaunti za kenya, dondoo za hapa na pale, pamoja na tahariri na maoni. Makala hizi zimetoa mchango mkubwa katika kuijenga michakato mbalimbali ya ukuzaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa watumiaji wa Swahilihub mtandaoni. Aidha kitengo cha Maktabani Jisomee kilichangia katika ujenzi wa lugha ya Kiswahili kupitia sehemu ya neno la siku na kuimarisha hazina ya istilahi na misamiati miongoni mwa watumiaji wa Swahilihub. Kwa mfano neno la siku katika picha 4.9 ni kikopesa na muktadha wa matumizi yake uliotolewa ulichangia katika ukuzaji wa Kiswahili miongoni mwa watumiaji wa Swahilihub wanaojifunza kuitumia lugha ya Kiswahili kwa ufasaha.




**Picha SURA YA NNE .15: Magazeti mbalimbali katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili**

Kitengo cha Maktabani Jisomee kilichangia katika kuwapa walimu na wanafunzi wa shule za msingi na upili nafasi ya kufaidika na hazina ya Kiswahili iliyohifadhiwa kwenye magazeti ya *Taifa Leo*, mwanaspoti na *Mwananchi* yaliyopatikana kwenye tovuti ya Swahilihub (Tazama picha 4.10). Kutokana na hazina hii walimu wa Kiswahili walijipatia nakala za kutosha za magazeti na makala zilizohifadhiwa katika maktaba ili wazitumie katika vipindi vyao na hata kuwaelekeza wanafunzi wao kuzisoma. Walimu waliweza kushiriki katika hafla na vikao vya Kiswahili vinavyofadhiliwa na Taifa Leo na kutoa mchango wao kuhusu jinsi ya kuikuza lugha hii rasmi na ya taifa ambayo imekuwa somo lenye changamoto kwa wanafunzi. Kitengo cha Maktabani Jisomee kiliwapa walimu nafasi ya kujipatia nakala za miongozo ya fasihi ya Kiswahili ili wajiandae kikamilifu kufunza fasihi darasani. Kwa mfano mashairi ya Sefu Sharifu Hamad yalichangia kuikuza lugha ya Kiswahili kwa kuijengea misamiati na istilahi za kishairi.  Tazama picha 4.11.




**Picha SURA YA NNE .16: Ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kupitia ushari na tenzi**

Kwa mfano kitengo cha Maktabani Jisomee kilitumiwa kuhifadhi matini ya ushairi na tenzi (Taz. Picha 4.11), yaliyochangia kupanua kanzi ya maandishi yaliyofikiwa na watumiaji wengi wa tovuti ya Swahilihub. Uhifadhi huu wa matini ulipanua wigo wa matumizi ya matini yaliyowafikia watumiaji wengi mtandaoni na hivyo basi kuikuza lugha ya Kiswahili mtandaoni.

Hata hivyo, uchunguzi uliofanywa ulibainisha kuwa licha ya umuhimu wake kwenye tovuti ya Swahilihub, takriban 42.2 (143) ya watafitiwa hawakukitumia kitengo cha Maktabani Jisomee katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili. Hili ni jambo linalovunja moyo kwani watumiaji wote wa tovuti ya Swahilihub wanastahili kutumia Maktabani Jisomee kwani kutokana na maoni ya watafitiwa na matokeo ya usakuraji wa tovuti ya Swahilihub, kuna makala ya kitaaluma yanayoandaliwa na wadau mbalimbali kuhusu vipengele mbalimbali vya taaluma ya Kiswahili. Hata hivyo, matokeo kutokana na mijadala na mahojiano yalionyesha kwamba pana haja ya wataalamu wa Kiswahili kujiandaa mapema ili maandalizi ya makala yao kwenye kitengo hiki yaweze kuwahimiza watumiaji wa kitengo hiki wakifaidikie.

#### 4.2.1.1.4 Picha


Picha ni kitengo cha tovuti ya Swahilihub ambacho hutumia kanda zilizonaswa kuwasilisha hoja mahususi (Taz. Picha 4.12).




**Picha SURA YA NNE .17: Kitengo cha Picha**

Ukuzaji wa Kiswahili umebainika katika kitengo hiki kwa misingi mikuu ifuatayo:

Tovuti ya Swahilihub, inapakia picha mtandaoni na katika kurasa zake za YouTube, Facebook na Twitter kwa Kiswahili sanifu. Kitengo cha picha kilitumika katika ufundishaji wa Kiswahili kwa kuhusishwa mtandaoni ambapo wanafunzi wote wa mtandaoni walikiri kukitumia na kuweza kuona kisha kupata maelezo kuhusu dhana anuai (Tazama picha 4.13).



NYUMBANI | MAKTABA | UTAFITI/IKISIRI | HADITHI | MASHAIRI/TENZI | MAKALA | VIDEO

TAIFALEO HABARI

Taifaleo

HIFADHI YA KISWAHILI

METHALI
MISEMO
NAHAU
VITENDAWILI

MAGAZETI YA KISWAHILI

Mwananchi – Tanzania
Mwanaspoti – Tanzania
Taifa Leo – Kenya
Mtanzania – Tanzania
Habari Leo – Tanzania
Majira – Tanzania
Nipashe – Tanzania
Tanzania Daima – Tanzania

VYANZO VYA KISWAHILI

Redio
Runinga
Magazeti
Vitabu
Majarida
Vipeperushi
Vyama
Asasi
Taasisi
Vikundi

Amani Njoka, Swahili Hub

Hunioni lakini nakupikia-**Gesi**

Ingawa sina mbawa naruka kama ndege-**Tiara**

Jiwe la mviringo, maji umeyatoa wapi?-**Jicho**

Kaa hapa, nikae hapa tumfinye mchawi-**Kula ugali**

Namkata mwanangu huku nalia-**Kitunguu**

Ana mabaka kama chui-**Chapati**

Imamu wangu hana msikiti-**Jogoo**

Nilienda naye, narudi peke yangu-**Kujisaidia msalani**

Popoo mbili zavuka mto-**Macho**

Nimekaa mbali na wenzangu wala sina mwenzi-**Dole gumba**

Rafiki yangu anatembelea tumbo-**Nyoka**

Natembea na nyumba yangu-**Kobe**

Sichoki kuubeba mzigo wangu-**Konokono**

Sahani letu dogo linatusaidia-**Mwezi**

Mbwa wangu hung'ata kwa nyuma-**Nyigu**

Natoka juu nateremka chini-**Majani ya miti**

Liwali amekonda lakini hana mganga-**Sindano**

Mama hana miguu lakini mtoto anayo-**Yai na kifaranga**

Nyoka wa chuma-**Garimoshi**

Nyumba yangu haina mlango-**Yai**

Orodha yangu ni ya milele-**Anga na nyota**

MAONI MAPYA

Amani Njoka on Uundaji wa maneno ya Kiswahili
PETER M.ELIAS on Uundaji wa maneno ya Kiswahili
Amani Njoka on Wahitimu 35 watunukiwa shahada ya Kiswahili UDSM, mwanafunzi wa Kiswahili aongoza
Robert Ayubu on Wahitimu 35 watunukiwa shahada ya Kiswahili UDSM, mwanafunzi wa Kiswahili aongoza
Gadi Solomon on Muuaji asakwe

**Picha SURA YA NNE .18: Vitendawili katika Kitengo cha Picha**

Kwa mfano katika picha 4.13, matumizi ya vitendawili yalichangia katika ujenzi wa misamiati ya Kiswahili miongoni mwa watumiaji wa Swahilihub. Tazama mifano mbalimbali ya vitendawili vilivyobainika katika picha 4.13 hapo juu. Hali hii inakuza misamiati, istilahi na usanifu wa lugha ya Kiswahili ili kuendana na masuala ibuka ya ki-teknohama na usasa katika ukuzaji wa Kiswahili. Mchakato huu ulichangia kusambaza dhana, istilahi na misamiati mipya katika juhudi za kuijenga lugha ya Kiswahili miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub. Kubuniwa kwa misamiati na dhana zilizochangia katika kuboresha ufundishaji wa Kiswahili kuliimarisha ujenzi wa Kiswahili na kwa njia hii kukuza Kiswahili miongoni mwa wanafunzi waliohusika katika mafundisho haya mtandaoni.


Matokeo ya mijadala ya makundi katika utafiti huu yalibaini kuwa picha ziliwatia wanafunzi motisha, zilichangia uelewaji wao, zilitoa tajriba tofauti, ziliongeza msisitizo kwa mafunzo, zilihimiza uhusikaji, na kubadilisha mitazamo na mbinu za mwalimu pamoja na mwanafunzi. Kwa njia hii mawasiliano yaliyotokea yaliimarisha ujenzi wa Kiswahili na kuyakidhi mahitaji ya wanafunzi mtandaoni. Walimu walitaja kuwa na uwezo wa kuboresha ufundishaji wao kwa kuhifadhi makala wanazotumia kufundishia kwenye mradi wa Swahilihub na kuwahimiza wanafunzi kuzifikia kwenye tovuti hii. Ufundishaji wa Kiswahili mtandaoni ni mchango mkubwa katika ujenzi wa sarufi yake, misamiati yake na upanuzi wa istilahi zake kwa watumiaji wa Swahilihub kote ulimwenguni.




**Picha SURA YA NNE .19: Picha katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili**

#### 4.2.1.1.5. Video

Kupitia kitengo cha video, watumiaji walipata nafasi ya kujenga maudhui, kuchapisha maelezo, kuwasiliana na kununua au kuuza bidhaa na kushiriki huduma mbalimbali. Baadhi ya taarifa zilizopakiwa katika video kwenye tovuti ya Swahilihub ni zile zinazohusu masuala ibuka. Masuala haya ni kama vile mapenzi, afya, ndoa, muziki, mitindo ya kisasa, teknolojia, lugha miongoni mwa masuala mengine muhimu. (Taz picha 4.15).




**Picha SURA YA NNE .20: Mifano ya Video iliyochangia ujenzi wa msamiati wa Kiswahili.**

Swahilihub ilipakia video mtandaoni na katika kurasa zake za YouTube, Facebook na Twitter kwa Kiswahili Sanifu na kwa njia hii kuikuza lugha ya Kiswahili. Vile vile, kitengo hiki cha Swahilihub kilikuwa na nakala mbalimbali za video za vipindi mbalimbali vya runinga ya NTV pamoja na sauti za wataalamu na walimu wa Kiswahili ambazo zilichangia katika juhudi za ukuzaji wa Kiswahili miongoni mwa watumiaji wake. Vipindi vya redio na runinga ya NTV vilipeperushwa kwa Kiswahili na kuwafikia watumiaji wengi kote ulimwenguni. Hali hii ilichangia ukuzaji wa Kiswahili kwa kuimarisha usambaaji wake kwa eneo kubwa zaidi. Vipindi mbalimbali vya ufundishaji wa Kiswahili viliendeshwa kwenye kitengo hiki kwa ushirikiano na redio Q-fm. Vipindi hivi vilitoa mchango mkubwa katika ujenzi wa sarufi, istilahi na misamiati ya Kiswahili miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub.

Vipindi hivi pia vilichangia kuwahamasisha watumiaji wa Swahilihub kuhusu nafasi ya Kiswahili katika kuimarisha maendeleo katika jamii. Mashairi ya Kiswahili yaliyohifadhiwa katika kitengo hiki yalitoa mchango mkubwa katika ujenzi wa Kiswahili kikongoo na udumishaji wa hadhi na dhima ya Kiswahili miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub. Nyimbo za taarab na muziki wa kitamaduni zilitoa mchango mkubwa katika mchakato wa ufundishaji wa fasihi ya Kiswahili mtandaoni. Methali, misemo na Nahau zilichangia kupiga jeki mikakati ya ufundishaji wa Kiswahili mtandaoni.

#### 4.2.1.2 Ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kutokana na usambaaji wake

Katika sehemu hii, matokeo ya utafiti yamebaini kwamba Swahilihub imechangia ukuzaji Kiswahili kutokana na usmbaaji wake kimaeneo na kiwakati. Usambaaji wa Kiswahili ni

uongezekaji wa matumizi yake kieneo na kiwakati. Tovuti ya Swahilihub ilifanikisha usambaaji wa Kiswahili kupitia mikakati yake ya kuyafikia mahitaji ya watumiaji wake mtandaoni. Tovuti ya Swahilihub iliwapa nafasi watumiaji wake kuungana na marafiki na familia, na kushiriki taarifa, picha na video. Mitagusano hii ilichangia pakubwa katika maenezi ya lugha ya Kiswahili miongoni mwa watumiaji wa Swahilihub. Ueneaji huu ulitokana na ushirikiano uliokuwepo baina ya mitandao mingi ya kijamii na Swahilihub. Ushirikiano huu ulihusisha Facebook, Wikipedia, Google+, Twita na Linkedln. Tovuti hizi ni baadhi ya mitandao mikubwa kabisa kwenye intaneti. Kuna zaidi ya watu bilioni moja kwenye Facebook, Wikipedia ina zaidi ya watumiaji bilioni nne na Twita ina zaidi ya watumiaji milioni 500. Ushirikiano wa Swahilihub na majukwaa haya ya kijamii ulichangia katika kuieneza lugha ya Kiswahili kwa hadhira pana kote ulimwenguni na hivyo basi kuikuza zaidi.


#### 4.2.1.2.1 Mwanzo

Watafitiwa walitoa mrejesho kwamba kitengo cha Mwanzo ni kigezo muhimu sana katika ujenzi wa muundo wa tovuti ya Swahilihub kwa kuwa kigezo hiki kinachangia kuipa tovuti hii taswira inayowakaribisha na kupendeza watumiaji wa tovuti ya Swahilihub mtandaoni (Taz. Picha 4.2).




**Picha SURA YA NNE .21: Vitendawili katika ujenzi wa misamiati kwenye Kitengo cha Mwanzo**

Matumizi ya Mwanzo kama kitengo cha tovuti ya Swahilihub yaliweza kuchangia ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kwa kuelekeza watumiaji wa tovuti ya Swahilihub kwenye vitengo vyote ambavyo vilikidhi mahitaji yao mtandaoni. Matumizi yake yana nafasi inayofaa katika kuimarisha uamilifu wa tovuti ya Swahilihub mtandaoni. Hivyo basi kitengo cha Mwanzo kina uwezo wa kubainisha ubora na manufaa ya tovuti ya Swahilihub kwa watumiaji wake mtandaoni.




**Picha SURA YA NNE .22: Mchango wa vitendawili katika ukuzaji wa kiswahili**

Hali hii ni tofauti na ilivyokuwa kabla ya kubuniwa kwa tovuti ya Swahilihub katika mwaka wa 2012 ambapo msomaji angehitajika kutafuta kitabu au jarida lenyewe ili aweze kusoma. Changamoto za kutafuta vitabu hivyo maktabani sasa zimepunguzwa. Isitoshe, watumiaji wake wana uwezo wa kupokea habari pindi zinapotokea na hata kuweza kupashana wenyewe kwa wenyewe. Watumiaji walieleza kwamba wanaweza badilishana ujumbe kwa njia ya maandishi, picha au video kwa kutumiana tu kiungo cha taarifa husika. Mtumiaji mmoja hahitaji kuinukuu taarifa yote ili aweze kushiriki na wenzake. Badala yake, anahitajika tu kusambaza kiungo cha (URL) habari zenyewe. Baadaye mhusika wa pili anaweza kuifikia kokote aliko kwa kubonyeza kwenye linki hiyo ambayo itamwezesha kuifikia taarifa husika katika tovuti ya Swahilihub.

#### 4.2.1.2.2 Habari


Habari huangazia masuala yanayochangia teknohama na usasa katika ukuzaji wa Kiswahili. Runinga ya QTV na NTV zinakuza Kiswahili hewani na katika kurasa zake za YouTube, Msasa wa Lugha, Facebook na Twitter. Kitengo hiki huonyesha video na picha zilizopigwa na kutolewa maelezo kwa Kiswahili. Vipindi hivi vya Habari vilichangia katika kujenga sarufi, istilahi na misamiati ya lugha ya Kiswahili na kueneza misamiati yake miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub. Matokeo ya utafiti huu yalibaini kuwa kitengo cha Habari ndicho kilichotumiwa kwa kiasi kikubwa miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub. Matokeo haya yalitokana na uwiano wa kitengo hiki kwa kuwa kitengo hiki kilichukuliwa kuingiliana na hali, maadili na mazoea yao ya awali kuhusu Habari na mambo muhimu waliyohitaji kutoka mtandaoni. Uwiano huu ulichangia pakubwa ufanisi wa matumizi ya kitengo cha Habari miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub. Vile vile, kigezo kingine kilichochangia katika matumizi ya kitengo cha Habari kilikuwa ni uwazi kuhusu manufaa yake na kwa kuwa kilichukuliwa kuwa wa

manufaa kwa watumiaji wake. Aidha katika mchakato wa msambao wa tovuti ya Swahilihub, vyombo vya habari huchangia pakubwa katika hatua ya uhamasisho kwa kuwa vina hadhira pana na hivyo basi huweza kuathiri mielekeo ya wanajamii kwa kiasi fulani. Tovuti ya Swahilihub ni mtandao unaoendelezwa na kampuni ya Nation Media na magazeti ya *Taifa Leo* nchini Kenya na *Mwananchi* nchini Tanzania.




*Picha SURA YA NNE .23: Nafasi ya Kitengo cha Habari*

Kwa upande mwingine, msambao ni mchakato wa kijamii unaohusisha kwa kiasi kikubwa, mitagusano ya kibinafsi miongoni mwa wanajamii husika.





**Picha SURA YA NNE .24: Nafasi ya vyombo vya Habari katika Kitengo cha Habari**

Picha 4.18 inabainisha nafasi ya kitengo cha Habari katika usambaaji wa Kiswahili kupitia vyombo vya habari. Hivyo basi mitagusano ya kibinafsi ina nafasi kubwa sana ya kujenga au kubadilisha mielekeo na misimamo mikali miongoni mwa wanajamii. Mitagusano hii kwenye vyombo vya habari ilichangia kuimarisha matumizi ya kitengo cha habari miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub. Ndiposa kitengo cha Habari kikawa na watumiaji wengi zaidi kwa asilimia takriban 66 (224) kikilinganishwa na idadi ya watumiaji wa vitengo vingine vya tovuti ya Swahilihub.

#### 4.2.1.2.3 Jifunze Kiswahili

Matini ya Kiswahili yalichangia katika usambaaji na ueneaji wake mtandaoni miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub. Mchango wa matini katika kitengo cha Jifunze Kiswahili ulibainika kutokana na uhifadhi wa matini yaliyohaririwa ili kuyakidhi mahitaji ya watumiaji wake kwenye tovuti ya Swahilihub. Asilimia 63 (214) ya wahojiwa walikiri kukitumia kitengo cha Jifunze Kiswahili katika shughuli na mitagusano yao mitandaoni. Kwa maelezo zaidi (Taz. Chati 4.8). Hii ni idadi kubwa ya watumiaji wa tovuti ya Swahilihub ikichukuliwa kwamba wengi wa waliotumia kitengo hiki walilenga kujifunza au kufundisha lugha ya Kiswahili na hivyo basi kuikuza taaluma ya Kiswahili kwa msambao wake mpana mtandaoni. Idadi hii ni ishara kwamba matini iliyoko kwenye kitengo hiki cha Jifunze Kiswahili na michakato ya ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili ni faafu na hivyo basi kuwapendeza watumiaji wengi wa tovuti ya Swahilihub. Msambao na ueneaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub ni hatua kubwa sana katika ukuzaji Kiswahili. Matokeo haya yaliwiana na yale ya Wamalwa, (2016) na kuangazia maoni ya Hoerup, (2001) kwamba kila uvumbuzi huathiri mielekeo, imani, maadili, na maoni ya walimu kuhusu ufundishaji na utendakazi wao. Kwa kuwa

matumizi ya kitengo cha Jifunze Kiswahili yaliwiana na imani, maadili na mahitaji ya watumiaji wake, tovuti ya Swahilihub ilikubalika haraka na kwa urahisi katika michakato ya ufundishaji na ujifunzaji lugha.



NYUMBANI | MAKTABA | UTAFITI/IKISIRI | HADITHI | MASHAIRI/TENZI | MAKALA | VIDEO

Taifaleo

**HIFADHI YA KISWAHILI**

METHALI
MISEMO
NAHAU
VITENDAWILI

**MAGAZETI YA KISWAHILI**

Mwananchi – Tanzania
Mwanaspoti – Tanzania
Taifa Leo – Kenya
Mtanzania – Tanzania
Habari Leo – Tanzania
Majira – Tanzania
Nipashe – Tanzania
Tanzania Daima – Tanzania

**VYANZO VYA KISWAHILI**

Redio
Runinga
Magazeti
Vitabu
Majarida
Vipeperushi

Amani Njoka, Swahili Hub

**Nyama ya ulimi**: maneno mazuri, habari nzuri. Unaweza kumpa mtu maneno mazuri ya kufurahisha au kumfariji, huko ni kumpa nyama ya ulimi.

**Kumbatia chui**: kama vile chui alivyomkali ndivyo ambavyo kuna watu wanaweza kuwazoea watu wakali, hawaaminiki, wanafiki, wambea na baadaye wakakuletea madhara. Vilevile unaweza kufanya utani na zaha katika mambo ya hatari kama umeme, moto au maji ya kina kirefu yakakudhuru.

**Huna kichwa wala miguu**:huna umuhimu wowote, faida, mpango, utaratibu. Huna mwelekeo wowote katika maisha au jambo unalolifanya.

**Mstari wa mbele**:kuwa wa kwanza, fanya jambo wa kwanza na ukamilifu. Hamasisha, onesha mfano.

**Kuwa na moyo**: kuwa na bidii, kutokuchoka, kuwa na huruma, toa msaada, fanya jambo bila kukataa tamaa.

**Kuwa popo**:kutokuwa na msimamo, hueleweki upo upande gani.

**Mapana kwa marefu**:maelezo ya kina, ufafanuzi usio na shaka. Fanya jambo kwa kuangalia madhara yake kwa kina. Jiridhishe kabla juu ya faida na hasara kabla hujafanya jambo lolote. Fanya kwa usahihi na ukamili.

**Tia chumvi**: ongeza maneno yasiyokuwepo, chongea kwa maneno yasiyo ya kweli, uongo.

**Maji ya shingo**: zidiwa, elemewa na jambo. Fika mwisho, kukosa namna yoyote ya kufanya unapozidiwa nguvu na kitu/mtu.

**MAONI MAPYA**

Amani Njoka on Uundaji wa maneno ya Kiswahili
PETER M.ELIAS on Uundaji wa maneno ya Kiswahili
Amani Njoka on Wahitimu 35 watunukiwa shahada ya Kiswahili UDSM, mwanafunzi wa Kiswahili aongoza
Robert Ayubu on Wahitimu 35 watunukiwa shahada ya Kiswahili UDSM, mwanafunzi wa Kiswahili aongoza
Gadi Solomon on Muuaji asakwe

**Picha SURA YA NNE .25: Nahau katika ukuzaji wa Kiswahili kwenye Kitengo cha Jifunze Kiswahili.**


Urejeleaji kwa kiwango kikubwa cha matini ya Swahilihub ulichangia ongezeko katika idadi ya watumiaji wa Kiswahili na kuikuza lugha ya Kiswahili mtandaoni. Kwa kuzingatia vigezo hivi, makadirio ya ustahilifu wa Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili yalifanyika. Matini yaliyotiwa kwenye tovuti ya Swahilihub yalichangia kuwahusisha watumiaji wengi na idadi hiyo iliimarika na kuboresha nafasi ya tovuti ya Swahilihub miongoni mwa tovuti mbalimbali ulimwenguni (Taz. Picha 4.18 na 4.19)

Ufundishaji wa Kiswahili ulitegemea thamani ya matini ya Kiswahili katika kitengo hiki. Usambaaji wa Kiswahili ulitokea kwenye kitengo hiki kutokana na makala yaliyowafikia watumiaji wengi wa tovuti ya Swahilihub. Msambao huu ulitokana na mchango wa gazeti la *Taifa Leo,* ambalo lilipakiwa kwenye kitengo hiki cha Jifunze Kiswahili. Gazeti la *Taifa Leo* lina upekee wa kuwafikia wadau wengi wa Kiswahili nchini Kenya na watumiaji wengine kote ulimwenguni kupitia kwa tovuti ya Swahilihub. Mitihani iliyoandaliwa pamoja na majibu yake katika Kiswahili na kuchapishwa gazetini ili itumike shuleni bila malipo iliwafikia watumiaji wengi wa tovuti ya Swahilihub mtandaoni. Ueneaji mpana wa makala haya ni hatua kubwa katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili mtandaoni.

Gazeti la *Taifa Leo* pia linachapisha makala ya lugha na fasihi kutoka kwa wataalamu wa Kiswahili yanayolenga wanafunzi na walimu wa shule za upili nchini Kenya.  Isitoshe, tovuti ya Swahilihub, inayoendeshwa na gazeti hili pamoja na lile la *Mwananchi* nchini Tanzania, imechapisha miongozo ya fasihi iliyozamia kwa kina maudhui, fani, wahusika, mtiririko na maswali ya udurusu wa fasihi katika vitabu teule kama vile *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* na *Mstahiki Meya*. Miongozo hii inatoa nafasi kwa wanafunzi kuelewa dhana anuwai za fasihi na kuikuza Kiswahili kwa hadhira pana ya watumiaji wa tovuti ya Swahilihub. Habari, maoni na makala anuai katika *Taifa Leo* yaliangazia masuala ibuka kote duniani kama vile siasa, michezo,

uchumi, dini, jamii, elimu na kadhalika. Hatua hii ni upanuzi wa mawanda ya ueneaji wa lugha ya Kiswahili katika utajiri wa utamaduni na fasihi yake kwa hadhira pana mtandaoni.

Matokeo ya utafiti huu yalibaini kuwa kitengo hiki kina manufaa kwa wanafunzi kwani kinawapa nafasi ya kuusakura mtandao ili kumaizi maswala husika kwenye tovuti ya Swahilihub. Kitengo cha Jifunze Kiswahili kilitumiwa na wahitimu ambao kabla ya kumaliza mafunzo yao walisomeshwa ili waweze kukabiliana na masuala ya ajira. Wahitimu wa shahada ya kwanza ya masomo ya sanaa, kwa mfano, wakishahitimu waliendelea kusomea taaluma ya kufundisha lugha ya Kiswahili kwa wageni. Mafunzo kama haya yaliwawezesha wahitimu hawa kumudu kuwafundisha wageni kokote ulimwenguni kupitia kwa matini na makala yaliyopakiwa kwenye kitengo cha jifunze Kiswahili. Jifunze Kiswahili ni kitengo cha tovuti ya Swahilihub chenye ushawishi na mvuto wa hali ya juu kuliko vitengo vingine vyote (Wamalwa, 2016). Hii ni kwa sababu kitengo hiki hutoa nafasi kubwa kwa watumiaji wa jukwaa hili kujifunza maswala mbalimbali kuhusu taaluma ya Kiswahili na hivyo basi kuchangia ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili mtandaoni.(Taz. Picha 4.28).



NYUMBANI | MAKTABA | UTAFITI/IKISIRI | HADITHI | MASHAIRI/TENZI | MAKALA | VIDEO

**MWANANCHI HABARI**

Mwananchi

**TAIFALEO HABARI**

Taifaleo

**HIFADHI YA KISWAHILI**

METHALI
MISEMO
NAHAU
VITENDAWILI

**MAGAZETI YA KISWAHILI**

Mwananchi – Tanzania
Mwanaspoti – Tanzania
Taifa Leo – Kenya
Mtanzania – Tanzania
Habari Leo – Tanzania
Majira – Tanzania
Nipashe – Tanzania
Tanzania Daima – Tanzania

**VYANZO VYA KISWAHILI**

Redio
Runinga
Magazeti
Vitabu
Majarida
Vipeperushi

**Tutumie Kiswahili kufundishia**

• MAY 26, 2021

Profesa Raymond Mosha Gazeti hili mara kadhaa limekuwa na mjadala kuhusu kutumia Kiswahili au Kiingereza kufundishia shuleni na vyuoni. Wapo wanaosema kwamba tuendelee kutumia Kiingereza, kwa sababu hatuna msamiati wa kutosha wa Kiswahili katika kufundishia. Wanaongeza kwamba Kiingereza ni lugha kubwa duniani hivyo tuendelee kuitumia. Wanadai kwamba wahitimu wetu hawatamudu soko la ajira nje ikiwa wamejifunza kwa Kiswahili. Hizo ni baadhi ya sababu zinazotelewa. Wapo pia wanaotetea matumizi ya Kiswahili kufundishia wakisema kwamba wanafunzi wetu wataelewa masomo vizuri zaidi tukitumia Kiswahili. Katika toleo la tarehe 27 Aprili mwaka huu, mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Faraja Kristomus, alionyesha...

**Tutilie mkazo ujifunzaji wa Kiswahili kwa wageni kuboresha mawasiliano na kipato**

• FEBRUARY 22, 2021

Amani Njoka, Swahili Hub Bilas haka haitakuwa mara ya kwanza kwa andiko kama hili au linalofanana na hili kuonekana katika safu hii. Tanzania imeendelea kuwa na mahusiano mazuri baina ya mataifa mengi duniani katika nyanja mbalimbali. Tanzania imekuwa mwenyeji wa mikutano mingi ya kimataifa na sehemu salama katika nyanja mbalimbali za kijamii, kiuchumi na


**MATANGAZO**

**MAONI MAPYA**

Amani Njoka on Uundaji wa maneno ya Kiswahili
PETER M.ELIAS on Uundaji wa maneno ya Kiswahili
Amani Njoka on Wahitimu 35 watunukiwa shahada ya Kiswahili UDSM, mwanafunzi wa Kiswahili aongoza
Robert Ayubu on Wahitimu 35 watunukiwa shahada ya Kiswahili UDSM, mwanafunzi wa Kiswahili aongoza
Gadi Solomon on Muuaji asakwe

**Picha SURA YA NNE .26: Prof Mosha katika ujenzi wa msamiati kupitia ufundishaji kwenye kitengo cha Jifunze Kiswahili**

Jifunze Kiswahili ni kitengo kilicholenga kuikuza lugha ya Kiswahili kupitia kwa michakato na mikakati anuai ya ufundishaji. Kwa mfano kikao cha Prof. Raymond Mosha hapo juu kilichangia katika ujenzi wa istilahi za Kiswahili. Kwenye kitengo hiki kuliwekwa vinasa sauti vilivyowaelekeza wanafunzi wa viwango mbalimbali kuanzia wale wa daraja la chini, wale wa kiwango wastani pamoja na wale wa kiwango cha upeo cha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Pia kulikuwa na matini kuhusu tamaduni za Waswahili zilizoandaliwa na taasisi ya utafiti wa taaluma za Kiswahili Afrika Mashariki (RISSEA). Matini kutoka RISSEA yalichangia kuchota kutoka kwa utajiri wa tamaduni za Kiafrika na kutajirisha makala ya ufundishaji wa sarufi pamoja na misamiati na istilahi za lugha ya Kiswahili. Nakala za mitihani ya kitaifa ya shule za msingi (KCPE) na upili (KCSE) zilipakiwa kwenye kitengo hiki cha Jifunze Kiswahili na kuchangia katika ukuzaji wa Kiswahili kutokana na maandalizi mwafaka ya wanafunzi katika viwango hivyo.





*Picha SURA YA NNE .27: Mifano ya vitabu vilivyochangia usambaaji wa Kiswahili.*

Kitengo cha Jifunze Kiswahili kilichangia katika kuwapa walimu na wanafunzi wa shule za msingi na upili nafasi ya kufaidika na hazina ya Kiswahili iliyohifadhiwa kwenye vitabu, miongozo, makamusi, magazeti ya *Taifa Leo*, *Mwanaspoti* na *Mwananchi* yaliyopatikana kwenye tovuti ya Swahilihub (Tazama picha 4.29). Kwa mfano *Kamusi Kuu ya Kiswahili* iliyopatikana kwenye kitengo cha Jifunze Kiswahili ilikuwa dira kwa wanafunzi walioitumia. Kutokana na hazina hii walimu wa Kiswahili walijipatia nakala za kutosha za magazeti na makala zilizohifadhiwa katika maktaba ili wazitumie katika vipindi vyao na hata kuwaelekeza wanafunzi wao kuzisoma.




*Picha SURA YA NNE .28: Kitengo cha Jifunze Kiswahili*

Upakiaji wa matini yenye thamani ni hatua muhimu katika mchakato wa ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kwenye tovuti ya Swahilihub. Katika tovuti, matini ndio mfalme lakini mtawala ni mtumiaji wake (Owoche, 2020). Uhariri wa matini mtandaoni ulifanyika katika tovuti ya Swahilihub ili kukagua matini yake mtandaoni kwa kusudi la kutoa matini isiyofaa na kuweka ile iliyo ya kisasa zaidi kwa minajili ya kupata nafasi bora miongoni mwa tovuti zote ulimwenguni (Taz. Picha 4.27, 4.28, 4.29 na 4.30). Ustahilifu wa tovuti ya Swahilihub kiuamilifu ni kigezo muhimu katika tathmini yake kwa kuwa lengo lake kuu ni kuhifadhi na kufikisha habari kama inavyohitajika na watumiaji wake. Uhariri huu uliangazia uboreshaji wa isitilahi zinazoelekeza watumiaji mtandaoni na kuchangia ujenzi wa Kiswahili, uimarishwaji wa thamani ya matini mtandaoni na uhusishwaji wa matini kwa kuzilinganisha na kuzilinganua mtandaoni.



Mwananchi

TAIFALEO HABARI

Taifaleo

HIFADHI YA KISWAHILI

METHALI
MISEMO
NAHAU
VITENDAWILI

MAGAZETI YA KISWAHILI

Mwananchi – Tanzania
Mwanaspoti – Tanzania
Taifa Leo – Kenya
Mtanzania – Tanzania
Habari Leo – Tanzania
Majira – Tanzania
Nipashe – Tanzania
Tanzania Daima – Tanzania

VYANZO VYA KISWAHILI

Redio
Runinga
Magazeti
Vitabu
Majarida
Vipeperushi
Vyama
Asasi
Taasisi
Vikundi

baada ya Tanganyika kupata uhuru, lugha ya Kiswahili iliendelea kutumika katika sekta mbalimbali ingawa kwa viwango tofauti tofauti. Mathalan katika sekta ya elimu, Kiswahili liliendelea kutumika na sasa kinatumika kama njia ya mawasiliano katika ufundishaji wa masomo ya shule za msingi na vyuo vya ualimu ngazi ya cheti.Adha, Kiswahili ni somo la lazima kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne. Kwa upande wa elimu ya sekondari hadi vyuo vikuu, lugha ya mawasiliano ni Kiingereza na Kiswahili kinaendelea kufundishwa kama somo.

Kwa maelezo zaidi kuhusu utafiti uliofanywa kufanywa na mabingwa wa lugha asiliana na Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili (TATAKI), Chuo Kikuu cha D'Salaam au Shule ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Serikali (SUZA), Zanzibar.

*********************

**IKISIRI**

Hili ni neno jipya ambalo halijafahamika sana kwani linatumika katika masuala ya kitaaluma hususan masuala ya utafiti. Kwa kawaida watafiti wanapoandika maelezo kuhusu maudhui wa mada waliotayarisha, hupenda kutoa maelezo mafupi kwa wale wasomaji ambao hawana muda wa kusoma ripoti yote.

Hivyo huandika maelezo mafupi ya kuweka jambo bayana. Huu ni ufupisho wa ripoti husika au ikisiri.

Katika programu ya kongamano la Kimataifa lililotayarishwa na Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki, Mada Kuu ilikuwa "Kuleta mabadiliko katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kutumia Kiswahili.

Mada zifuatazo ni matokea ya ikisiri zilizotayarishwa:

1. **Kiswahili kwa uimarishaji wa Ushirikiano na Utangamano wa kanda ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.**

**Na Anna M. Kishe wa Teofilo Kisanji University,**

Dar es Salaam.

Maelezo yafuatayo yanakusudia kujadili dhima ya lugha ya Kiswahili katika kuimarisha ushirikiano na utangamano wa ukanda wa Afrika Mashariki. Utangamano wa Afrika Mashariki kupitia Kiswahili si jambo geni kabisa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki Kiswahili kilikuwapo na kilikuwa

MAONI MAPYA

Amani Njoka on Uundaji wa maneno ya Kiswahili
PETER M.ELIAS on Uundaji wa maneno ya Kiswahili
Amani Njoka on Wahitimu 35 watunukiwa shahada ya Kiswahili UDSM, mwanafunzi wa Kiswahili aongoza
Robert Ayubu on Wahitimu 35 watunukiwa shahada ya Kiswahili UDSM, mwanafunzi wa Kiswahili aongoza
Gadi Solomon on Muuaji asakwe

*Picha SURA YA NNE .29: Mifano ya Makala katika Kitengo cha Jifunze Kiswahili*

Makala za watalaam kama vile Anna Kishe kutoka Chuo Kikuu cha Kisanji kuhusu Kiswahili kwa uimarishaji wa utangamano na ushirikiano wa kanda ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ilichangia katika ukuzaji wa Kiswahili (Taz. Picha 4.31). Swahilihub ina hazina ya maarifa mengi ya kazi za kifasihi na kiisimu zilizofanyiwa utafiti na mabingwa wa Kiswahili katika taaluma ya mashairi, tenzi, hadithi, nahau, na kadhalika. Isimu ya Kiswahili imebainika kama muundo, maumbo, maana na matamshi fasaha ya Kiswahili. Juhudi hizi zilichangia katika kuimarisha hadhi na dhima ya Kiswahili na kupanua mipaka ya matumizi yake kimaeneo na kiwakati. Kigezo kingine muhimu kilichochangia ukuzaji wa Kiswahili katika tovuti ya Swahilihub kilikuwa idadi ya matini iliyowekwa kwenye tovuti hii pamoja na umaarufu wa tovuti zilizorejelea na kuwaelekeza watumiaji wake kwa matini ya Swahilihub.

#### 4.2.1.2.4 Blogu na Ukumbi

Blogu na Ukumbi ni kitengo kilicho na nafasi kubwa ya kushawishi watumiaji wengi kutangamana kwa misingi ya mitagusano ya kijamii na kuchangia ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili mtandaoni kwa usambaaji wake. (Taz. Picha 4.20). Matokeo ya utafiti huu sawa na yale ya Jagero (2013), yalibaini kuwa Blogu zina nafasi ya kuimarisha mawasiliano bora miongoni mwa watumiaji wa Swahilihub kwa kuendeleza mijadala kuhusu masuala mahsusi. Mijadala kama hii huchangia kuzua mrejesho kutoka kwa watumiaji wa Swahilihub kuhusu ustahilifu wake kwa mahitaji yao. Kutokana na maoni ya watafitiwa ni rahisi kusambaza mradi wa Swahilihub miongoni mwa wataalam kwa kuwashawishi wanafunzi, wanazuoni na wasomi wengine. Matokeo ya utafiti yalidhihirisha kuwa kitengo cha Blogu na Ukumbi kina makala ya kitaaluma yanayoandaliwa na wadau mbalimbali kuhusu vipengele mbalimbali vya taaluma ya Kiswahili. Kitengo hiki pia kina uwezo wa kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji kupitia kwa wingi wa matini na makala kwenye magazeti yanayoendeleza taaluma ya Kiswahili (Taz. Picha 4.10).





**Picha SURA YA NNE .30: Nafasi ya Blogu na ukumbi katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili**

Kwa kutumia tovuti ya Swahilihub kama jukwaa muhimu mtandaoni, walimu na wanafunzi wanaweza kujadiliana, kuwasiliana na kuchangiana hoja na mawazo muhimu yanayolenga kuimarisha taaluma ya Kiswahili. Ili kuimarisha idadi ya watumiaji wa kitengo cha Blogu na Ukumbi na kuboresha matumizi ya Blogu na Ukumbi katika tovuti ya Swahilihub kwa jumla, wanafunzi wanaweza kuhimizwa kufanya uchambuzi wa kazi mbalimbali za taaluma ya Kiswahili kwa kutumia Blogu na Ukumbi kama jukwaa la majadiliano miongoni mwao. Tovuti ya Swahilihub inapotumiwa hivi huwapa watumiaji motisha na ari ya kushughulikia kwa dhati taaluma ya Kiswahili. Kwa njia hii ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili unaweza kuboreshwa na wadau wote. Matumizi ya Blogu na Ukumbi pia yanaweza kujitokeza katika majadiliano yanayowahusisha walimu na wanafunzi kutoka shule zilizo mbali.

#### 4.2.1.2.5 Picha

Michakato mbalimbali ya elimu iliyojitokeza kwenye kitengo cha picha ilichangia katika ongezeko la idadi ya watumiaji wa Kiswahili katika maeneo anuwai. Tovuti ya Swahilihub kwa kutumia kitengo cha picha ilitekeleza majukumu mengi ya kielimu na kuchangia upanuzi wa mawanda ya matumizi ya lugha ya Kiswahili kote ulimwenguni. Picha mbalimbali zilizotumika katika tovuti ya Swahilihub zilichochea ari kubwa miongoni mwa wanafunzi na kuwavutia na hivyo kufanya ufundishaji kuwa wa maana. Ufundishaji wa Kiswahili uliotokea kwenye kitengo cha picha ulichangia katika ueneaji wa matumizi ya Kiswahili kieneo na kiwakati. Katika picha 4.14, matokeo ya mtihani wa kitaifa wa kidato cha nne yalitolewa na kusambazwa miongoni mwa watumiaji wa Swahilihub kote nchini kwa lugha ya Kiswahili. Isitoshe kulikuwa na hadithi fupi mbalimbali zilizochangia katika upanuzi wa msamiati na pia kusambaza Kiswahili kote ulimwenguni (Taz. Picha 4.21).



NYUMBANI | MAKTABA | UTAFITI/IKISIRI | HADITHI | MASHAIRI/TENZI | MAKALA | VIDEO

**MWANANCHI HABARI**

**Mwananchi**

**TAIFALEO HABARI**

Taifaleo

**HIFADHI YA KISWAHILI**

METHALI
MISEMO
NAHAU
VITENDAWILI

**MAGAZETI YA KISWAHILI**

Mwananchi – Tanzania
Mwanaspoti – Tanzania
Taifa Leo – Kenya
Mtanzania – Tanzania
Habari Leo – Tanzania
Majira – Tanzania
Nipashe – Tanzania
Tanzania Daima – Tanzania

**VYANZO VYA KISWAHILI**

Redio
Runinga

HADITHI

MARCH 9, 2021

JINA LA MTUNZI: Shung Thong Xhi

Mawasiliano: 0623410370, 0693548469

INSTAGRAM: @Shungthong

***UTANGULIZI: Wiki iliyopita tulianza sehemu ya kwanza ya hadithi tamu ya Mfalme Izana, sasa endelea…….***

"Nimekuja kuonana na kiongozi mkuu wa mila…!?"

Wale vijana walio kuwa nje pale waliinamisha nyuso zao wakati Mizana anaongea kuonyesha heshima!.

**MATANGAZO**

**MAONI MAPYA**

Amani Njoka on Uundaji wa maneno ya Kiswahili
PETER M.ELIAS on Uundaji wa maneno ya Kiswahili
Amani Njoka on Wahitimu 35 watunukiwa shahada ya Kiswahili UDSM, mwanafunzi wa Kiswahili aongoza
Robert Ayubu on Wahitimu 35 watunukiwa shahada ya Kiswahili UDSM, mwanafunzi wa Kiswahili aongoza
Gadi Solomon on Muuaji asakwe

**Picha SURA YA NNE .31: Ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kupitia Hadithi**


Kwa mfano hadithi fupi zilizotungwa na Shang Thong Xhi katika picha ya 4.21. zilichangia katika kueneza Kiswahili kote ulimwenguni. Hali hii ilichangia ukuzaji wa Kiswahili kwa kuimarisha msambao wa istilahi kwa njia ya habari iliyowafikia wengi. Kwa wengi wa watumiaji wa Swahilihub hususan wageni waliosoma hadithi fupi katika picha hii ya 4.4 kwa mfano, walifaidika kwa kujenga kanzi ya istilahi za Kiswahili kwa kumaizi kauli ya kutia fora kwa mtihani kwa maana ya kupita mtihani huo. Kauli kama hizi zilichangia kuikuza lugha ya Kiswahili katika usanifu wake kimatumizi miongoni mwa watumiaji wa Swahilihub. Michakato hii ilieneza matumizi ya Kiswahili miongoni mwa watumiaji wa Kiswahili mtandaoni.

Ingawa palitokea ukuzaji wa Kiswahili kwenye kitengo hiki cha picha, michakato hii haikuwa ya viwango vya kukikidhi mahitaji ya wataalamu mbalimbali wa lugha hususan wanazuoni ambao wangetegemea kupata matini ya thamani ya kitaaluma kwenye kitengo hiki cha picha. Hata hivyo, mijadala ya kitaaluma na matokeo ya utafiti mbalimbali yaliyohifadhiwa kwenye tovuti ya Swahilihub yaliimarisha usambaaji wa Kiswahili kwa hadhira pana.

#### 4.2.1.2.6. Video

Kitengo cha video kiliwawezesha watumiaji wa tovuti ya Swahilihub kuutumia mradi wa Swahilihub kwa njia mbalimbali. Katika hatua hii, tovuti ya Swahilihub iliweza kuhuishwa upya na kupata mabadiliko yaliyoiboresha zaidi. Tovuti ya Swahilihub ilidhihirisha ushirikiano mkubwa na tovuti nyingine kama vile mtanzania.co.tz na mwananchi.com. Ushirikiano huu ulichangia kupanua wigo wa matini na kuthibitisha thamani ya juu ya matini kwenye tovuti ya Swahilihub. Ushirikiano huu ulichangia katika usambaaji wa Kiswahili kwa maeneo mbalimbali na kuchangia ueneaji wa lugha

ya Kiswahili kieneo na kiwakati kote ulimwenguni. Kwa njia hii watumiaji wa tovuti ya Swahilihub walitiwa hamu ya kumakinikia michakato ya kitaaluma kwenye jukwaa la Swahilihub na kuikuza lugha ya Kiswahili mtandaoni. Katika mchakato wa msambao wa uvumbuzi, vyombo vya habari huchangia katika hatua ya uhamasisho kwa kuwa hufikia hadhira pana na hivyo basi huweza kuathiri mielekeo ya wanajamii kwa kiasi fulani (Rodgers, 2003).





**Picha SURA YA NNE .32: Mifano ya Video iliyochangia usambaaji wa Kiswahili**

Picha 4.22 inaonyesha mifano ya video na magazeti yaliyotumika kusambaza lugha ya Kiswahili yakiwa ni pamoja na *Taifa Leo* nchini Kenya, *Mtanzania, Habari Leo, Nipashe*, Tanzania *Daima na Mwananchi* yakitoleshwa nchini Tanzania na kuchangia pakubwa katika maenezi ya lugha ya Kiswahili miongoni mwa watumiaji wa Swahilihub kote ulimwenguni. Aidha, vipindi mbalimbali vya ufundishaji wa Kiswahili viliendeshwa kwenye kitengo hiki kwa ushirikiano na redio Q-fm.

#### 4.2.1.2.7. Maktabani Jisomee

Matokeo ya utafti huu yalionyesha kuwa kuna wanafunzi wengi duniani wanaojiendeleza katika lugha ya Kiswahili kwa kutumia matini za Kiswahili katika kitengo cha Maktabani Jisomee. Matini kwenye kitengo cha Maktabani Jisomee zinahifadhiwa kwa muhtasari kama machapisho katika tovuti ya Swahilihub. Aidha magazeti ya *Taifa Leo*, *Mwananchi*, *Mwanaspoti*, *Mtanzania* yalitoa mchango mkubwa katika kusambaza misemo, vitendawili nahau na methali katika lugha ya Kiswahili kote ulimwenguni. (Tazama picha 4.8)



NYUMBANI | MAKTABA | UTAFITI/IKISIRI | HADITHI | MASHAIRI/TENZI | MAKALA | VIDEO

MWANANCHI HABARI

Mwananchi

TAIFALEO HABARI

Taifaleo

HIFADHI YA KISWAHILI

METHALI
MISEMO
NAHAU
VITENDAWILI

MAGAZETI YA KISWAHILI

Mwananchi – Tanzania
Mwanaspoti – Tanzania
Taifa Leo – Kenya
Mtanzania – Tanzania
Habari Leo – Tanzania

MISEMO YA KISWAHILI NA MAANA YAKE

• JUNE 12, 2019

Wahenga ni wazee wenye akili waliotutangulia. Walifikiria na kutunga misemo kwa lengo la kuadabisha, kuonya, kukumbusha wajibu wa kila kundi katika jamii. Ipo misemo ambayo inawagusa vijana, wazee, watu wazima, wanawake, wanaume. Mathalani vifo vya wajawazito vilipokithiri enzi hizo, wahenga walibaini chanzo ni ulaji wa mayai kipindi chote cha mimba na kusababisha mtoto kunenepa sana huko tumboni na kushindwa kupita kwenye njia ya uzazi. Hivyo, wakaanzisha msemo kama, 'Mama mjamzito akila mayai, mtoto atazaliwa bila nywele' ili kuzuia ulaji wa kupindukia wa mayai kwa wajawazito. Tupitie misemo hii ya wahenga; 1. Huwezi kusukuma gari bovu ukiwa umekaa ndani yake Hii...


MATANGAZO

MAONI MAPYA

Amani Njoka on Uundaji wa maneno ya Kiswahili
PETER M.ELIAS on Uundaji wa maneno ya Kiswahili
Amani Njoka on Wahitimu 35 watunukiwa shahada ya Kiswahili UDSM, mwanafunzi wa Kiswahili aongoza
Robert Ayubu on Wahitimu 35 watunukiwa shahada ya Kiswahili UDSM, mwanafunzi wa Kiswahili aongoza
Gadi Solomon on Muuaji asakwe

**Picha SURA YA NNE .33: Mifano ya misemo ya lugha ya Kiswahili**

Picha 4.23 inatoa mifano ya misemo ya lugha ya Kiswahili iliyochangia katika ukuzaji wake mtandaoni. Walimu na wadau wote waliokusudia kuzitumia makala hizi walifanya mikataba na usimamizi wa tovuti ya Swahilihub na hatimaye kuwa na makubaliano ya malipo na kwa njia hii kuwapatia vijana ajira na pia kupata fedha za kigeni. Jitihada hizi huchangia katika kuwafikia watu wengi na kwa njia hii kuipa lugha ya Kiswahili matumizi mapana miongoni mwa washika dau wa Kiswahili. Matokeo haya yanadhihirisha kwamba matumizi ya tovuti ya Swahilihub kwa njia hii yalipanua wigo wa matumizi ya lugha ya Kiswahili kieneo na kiwakati.




*Picha SURA YA NNE .34: Ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kupitia Mashairi*

Mashairi mbalimbali yaliyopatikana katika kitengo cha Maktabani Jisomee yalifanikisha maelezo ya walimu kuhusu masuala mbalimbali kama vile masuala ya uana ambayo yalishughulikiwa ipasavyo kwa kuhusisha tovuti ya Swahilihub katika ufundishaji (Taz. Picha 4.24). Pamoja na mashairi haya palikuwa na vitabu na makamusi yaliyochangia katika usambaaji wa lugha ya Kiswahili. Kwa mfano katika tovuti ya Swahilihub, kwenye kitengo cha Maktabani Jisomee, kulikuwa na hazina ya vipindi vya Kamusi ya Changamka vilivyopakiwa mtandaoni. Vipindi hivi viliendelea kupiga hatua kila uchao katika kukitumia Kiswahili katika programu zake na kwa kufanya hivyo Kiswahili kama lugha kiliendelea kujitajirisha na msamiati na kusambaza istilahi na kuisanifu lugha ya Kiswahili. Ujisomeaji wa masuala mbalimbali kuhusu lugha ya Kiswahili katika kitengo hiki ulichangia ongezeko la idadi ya watumiaji wa lugha ya Kiswahili kote ulimwenguni. Maktabani Jisomee ni kitengo kilichochangia ongezeko la idadi ya watumiaji wa Kiswahili kutokana na matini yaliyopakiwa ili kuwafikia watumiaji wengi wa tovuti ya Swahilihub. Kwenye kitengo hiki kuliwekwa matini yaliyowaelekeza watumiaji wa tovuti ya Swahilihub wa viwango mbalimbali kuanzia wale wa daraja la chini hadi wale wa juu (Tazama picha 4.5, 4.6,4.7,4.8 na 4.9.). Ujifunzaji wa Kiswahili uliotokea katika kitengo cha Maktabani Jisomee ulichangia katika ongezeko la idadi ya watumiaji wa Kiswahili na kupanua matumizi yake kieneo miongoni mwa walimu, wanafunzi na watumiaji wote wa Swahilihub.


#### 4.2.1.3 Ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kutokana na udumishaji wa hadhi yake

Udumishaji wa hadhi na dhima ya Kiswahili hutokana na nafasi na majukumu inayopewa lugha ya Kiswahili katika maamuzi ya kisera na matumizi mapana ya lugha ya Kiswahili. Katika sehemu hii, matokeo ya utafiti yamebaini kwamba Swahilihub imechangia ukuzaji Kiswahili kihadhi na dhima. Kiswahili ni lugha iliyo na hadhi kubwa

sana barani Afrika na tovuti ya Swahilihub inatoa nafasi ya kuimakinikia ili iimarishe dhima yake kote ulimwenguni. Makala yaliyohifadhiwa kwenye vitengo vya Swahilihub ni chanzo cha sera za serikali kubuniwa ili kubaini haja na msukumo wa kukikuza Kiswahili katika karne ya 21. Msukumo huu ulitolewa kwa serikali za Afrika Mashariki kama wenyeji wa lugha ya Kiswahili ili hadhi yake iimarishwe na kuwafaidi wenyeji na wageni. Swahilihub kupitia kwa vitengo vyake ilikuza Kiswahili miongoni mwa wasemaji wa Kiafrika na wa kimataifa ambao idadi yao kwa sasa inazidi milioni mia moja kote ulimwenguni.

#### 4.2.1.3.1 Mwanzo

Mwanzo ni miongoni mwa vitengo vya tovuti ya Swahilihub vilivyotumiwa katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kihadhi. Mwanzo ndicho kitengo kinachotoa maelezo mafupi kuhusu vitengo vyote vya tovuti ya Swahilihub. Kitengo hiki ni mlango unaowakaribisha watumiaji wa Swahilihub mtandaoni kwa kuwaonyesha ni kipi kinapatikana wapi na kila kitengo kina matini gani kwa ajili ya kuyakidhi mahitaji ya watumiaji wa tovuti ya Swahilihub. Kitengo cha mwanzo ndicho kinachotoa habari za kimsingi kuhusu kila kitengo cha Swahilihub na hutoa taswira inayowakaribisha watumiaji wa tovuti ya Swahilihub katika vitengo vyake vyote. Ujenzi wa lugha ya Kiswahili ulijitokeza kwenye vitengo mbalimbali na kwa viwango mbalimbali.




**Picha SURA YA NNE .35: Matini muhimu katika kitengo cha mwanzo**

Matumizi ya Mwanzo kama kitengo cha tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili yalifaa katika kuimarisha uamilifu na ukubalifu wake kwa kutoa taswira mwafaka kuhusu mwonekano wake (Taz Picha 4.38). Hatua ya kwanza katika mchakato wa msambao wa tovuti ya Swahilihub ni uhamasisho. Katika hatua hii, mtumiaji wa tovuti ya Swahilihub hugundua uwepo wake na kujaribu kubaini ni uvumbuzi wa aina gani, ina kusudi lipi na hufanya kazi kwa njia gani. Jambo la kimsingi katika hatua hii ni mtumiaji wa tovuti ya Swahilihub kutambua uwepo wake na kujifunza jinsi ya kuitumia na hatimaye hujifunza kanuni zinazoongoza katika utendakazi wake. Ili kubuni, kueneza na kusambaza dhana na misamiati mipya kupitia kwa tovuti ya Swahilihub, maelezo ya njia ya kuitumia na ufahamu wa namna inavyofanya kazi yalichangia pakubwa. Katika kusambaza tovuti ya Swahilihub, lugha ya walengwa ambayo ni Kiswahili ilitiliwa maanani ili mradi huu ukubalike na watumiaji wa lugha ya Kiswahili.

Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kwamba taswira inayotokana na mwonekano wa kurasa za vitengo vyote vya Swahilihub ni ya kupendeza na hivyo basi watumiaji wengi wanaozuru tovuti ya Swahilihub walipendezwa na mwonekano wa vitengo hivyo. Watumiaji wa tovuti ya Swahilihub wana uwezo wa kuamua iwapo wataendelea kuitumia au la kwa muda wa sekunde chache tu wa kusakura mtandaoni.





**Picha SURA YA NNE .36: Kitengo cha Mwanzo**

Mwonekano huu ulichangia kuwapa nafasi watumiaji wengi wa Swahilihub kuitumia tovuti ya Swahilihub na hivyo basi kuchangia usambaaji lugha ya Kiswahili miongoni mwa watumiaji wake mtandaoni.

#### 4.2.1.3.2 Jifunze Kiswahili

Jifunze Kiswahili ni kitengo kingine cha tovuti ya Swahilihub chenye ushawishi na mvuto wa hali ya juu kuliko vitengo vingine vyote (Wamalwa, 2016). Hii ni kwa sababu kitengo hiki hutoa nafasi kubwa kwa watumiaji wa jukwaa hili kujifunza maswala mbalimbali kuhusu taaluma ya Kiswahili na hivyo basi kuchangia ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili mtandaoni. Serikali za Afrika Mashariki zimekuwa mbioni kama wenyeji wa lugha ya Kiswahili katika kuhakikisha kuwa hadhi ya lugha hii imeimarishwa na kuwafaidi wenyeji na wageni. Swahilihub kupitia kwa vitengo vyake ilipanua hadhi na dhima ya Kiswahili miongoni mwa wasemaji wake kote ulimwenguni.





*Picha SURA YA NNE .37: Ushawishi wa viongozi mbalimbali kote ulimwenguni katika Kitengo cha Jifunze Kiswahili.*

Barani Afrika, lugha ya Kiswahili ina hadhi miongoni mwa wadau na asasi mbalimbali. Tovuti ya Swahilihub ilichangia katika kuimarisha hadhi ya Kiswahili na kuimakinikia ili dhima yake ipanuke kote ulimwenguni. Makala yaliyohifadhiwa kwenye kitengo cha Jifunze Kiswahili yalitumika kubuni sera za serikali na asasi anuwai ili kuimarisha nafasi na dhima ya Kiswahili. Matokeo ya baadhi ya utafiti wa Kiswahili katika vyuo vikuu vya ughaibuni na hata Afrika yamepakiwa kwenye kitengo cha Jifunze Kiswahili na kuwafikia watumiaji wa Swahilihub kote ulimwenguni. Hali hii inashadidia nafasi ya kiutandawazi ya lugha ya Kiswahili kote ulimwenguni.

Tovuti ya Swahilihub ilifanikisha lengo lake la kushirikiana na waandishi, wahariri wa makala na wenye blogu za Kiswahili katika kukitangaza Kiswahili ndani ya Afrika Mashariki na duniani kote. Juhudi hizi zilichangia katika kufanikisha hatua muhimu katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili mtandaoni. Utafiti wa kitaaluma umekuwa na umuhimu mkubwa katika kudumisha hadhi na dhima ya Kiswahili ulimwenguni. Juhudi kama hizi zimeipa lugha ya Kiswahili nafasi ya pili baada ya Kiarabu katika lugha zinazotumika katika shughuli za kiuchumi, kisiasa, na kijamii barani Afrika. Miongoni mwa mafanikio ya Swahilihub kupitia mchango wa ripoti za utafiti katika kitengo cha Jifunze Kiswahili ni kwamba nchi mbalimbali za Afrika Mashariki zimeanza kuunda sera na serikali zao zimeweka mikakati ya ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Kiswahili pia ni lingua franka katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati barani Afrika. Mafanikio haya ni ithibati kwamba Swahilihub ilitoa mchango mkubwa sana katika udumishaji wa hadhi na dhima ya Kiswahili kote ulimwenguni.

#### 4.2.1.3.3 Maktabani Jisomee


Matokeo ya utafiti anuai kuhusu historia na maendeleo ya Kiswahili yamechapishwa katika kitengo cha Maktabani Jisomee (Tazama picha 4.25).




*Picha SURA YA NNE .38: Hifadhi ya utafiti wa lugha ya Kiswahili*

Taarifa na mijadala katika machapisho haya yanathibitisha jambo moja muhimu kwamba lugha ya Kiswahili na matumizi yake yamekuwa yakipanuka tena kwa kasi kubwa kwenye vitengo mbalimbali vya Swahilihub. Matokeo ya baadhi ya utafiti wa Kiswahili katika vyuo vikuu vya Uropa, Marekani, Ujapani, Uchina, na hata Afrika yamepakiwa kwenye kitengo cha Maktabani Jisomee na kuwafikia watumiaji wa Swahilihub kote ulimwenguni. Kwa mfano Kiswahili kwa wenyeji katika picha 4.25. Utafiti huu wa kitaaluma ni hatua muhimu katika kudumisha hadhi na dhima ya Kiswahili ulimwenguni. Juhudi kama hizi zimeipa lugha ya Kiswahili nafasi ya pili baada ya Kiarabu katika lugha zinazotumika katika shughuli za kiuchumi, kisiasa, na kijamii barani Afrika. Hali hii ni hatua muhimu katika ukuzaji wa Kiswahili kwa kuimarisha hadhi yake.

Miongoni mwa mafanikio ya Swahilihub kupitia mchango wa ripoti za utafiti katika kitengo cha Maktabani Jisomee ni kwamba Kiswahili kimeanza kuundiwa sera na serikali za nchi za Afrika Mashariki. Kiswahili pia ni lugha kuu ya mipaka katika ukanda wa Afrika Mashariki na kati barani Afrika. Mafanikio haya ni idhibati kwamba kupitia kwa makala mbalimbali za utafiti (Taz. Picha 4.26), Swahilihub inatoa mchango mkubwa sana katika udumishaji wa hadhi na dhima ya Kiswahili kote ulimwenguni kwa kuwa kuna soko kubwa la huduma zake katika maeneo yanayozungumzwa Kiswahili, ikikadiriwa kuwa Kiswahili hutumiwa na watu takribani milioni mia moja na ishirini kote ulimwenguni.




**Picha SURA YA NNE .39: Hifadhi ya Makala za utafiti wa lugha ya Kiswahili**

Katika picha 4.39, makala ya Zuhura kuhusu mchango wa lahaja katika kukikuza Kiswahili Sanifu yalichangia katika kuimarisha matini ya Swahilihub na katika ukuzaji wa Kiswahili. Ili kufanikisha lengo lake la kushirikiana na waandishi, wahariri wa makala na wenye blogu za Kiswahili katika kuongeza wigo wa


mawasiliano na kukitangaza Kiswahili ndani ya Afrika Mashariki na duniani kote, tovuti ya Swahilihub inapigwa jeki na michango ya hatua hizi muhimu katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili mtandaoni.

Aidha katika mchakato wa msambao wa Swahilihub, makala huchangia katika hatua ya uhamasisho na uchunzaji pamoja na majaribio ya tovuti ya Swahilihub kwa kuwa Swahilihub ina hadhira pana na hivyo basi huweza kuathiri mielekeo ya watumiaji wake kwa kiasi fulani (Taz. Picha 4.26 na 4.27). Isitoshe kutokana na utendakazi wa mradi wa Swahilihub, tovuti 165 ziliwaelekeza watumiaji wake kurejelea matini ya Swahilihub katika kitengo cha Maktabani Jisomee kama ishara tosha ya kuaminika kwa matini ya Swahilihub. Tovuti zenye hadhi na dhima kuu kama mtanzania.co.tz na mwananchi.com ziliwaelekeza watumiaji wake kurejelea matini ya Swahilihub kama msingi wa usambaaji na udumishaji wa hadhi na dhima ya Kiswahili. Ongezeko hili la idadi ya tovuti zinazorejelea matini ya Swahilihub ni thibitisho kwamba matini iliyopo kwenye tovuti ya Swahilihub ina upya unaowavutia na kuwapendeza watumiaji wa tovuti nyingine. Kupendekezwa kwa matini ya tovuti ya Swahilihub ni ishara ya kuaminika na kutegemeka kwa tovuti ya Swahilihub miongoni mwa watumiaji wa tovuti zingine kote ulimwenguni. Mchakato huu mzima ni hatua kubwa katika ukuzaji wa Kiswahili kwa msingi wa ujenzi wake, usambaaji wake na udumishaji wa hadhi na dhima yake.

#### 4.2.1.3.4 Video

Hapo awali lugha ya Kiswahili haikupewa nafasi katika mitandao ya kijamii kwani ilionekana kama lugha isiyo ya kiteknolojia. Kwa hivyo, lugha kama vile Kiingereza zilipewa hadhi ya juu na hata kutumiwa katika shughuli mbalimbali za kimtandao. Asilimia 48(163) ya watafitiwa walikiri kujua na kushawishiwa kutumia tovuti ya Swahilihub wakiwemo viongozi na asasi mashuhuri katika taaluma ya Kiswahili. Miongoni mwa asasi zilizotajwa na watafitiwa ni pamoja na vyama vya kitaaluma vya Kiswahili kama vile, CHAKITA, CHAKAMA pamoja na

taasisi kama vile TATAKI na KAKAMA. Mchango wa kituo cha televisheni cha Nation ulikuwa wa maana katika hatua hii muhimu ya uhamasisho na ushawishi. Ushawishi wa wanajamii wenza na viongozi mashuhuri huchangia katika hatua hii. Aidha hadhi ya Kiswahili imejengwa na kauli za viongozi mbalimbali waliochangia katika kuipa lugha ya Kiswahili hadhi ya juu. Kwa mfano kauli ya rais Yoweri Kaguta Museveni ya kutaka nchi zote barani Afrika kuitumia Kiswahili ni mfano bora wa mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa hadhi ya lugha ya Kiswahili (Tazama 4.33).





*Picha SURA YA NNE .40: Mifano ya ushawishi wa viongozi uliochangia usambaaji wa Kiswahili.*

Matokeo kutoka kwa watafitiwa yalibaini manufaa ya matumizi mengi ya kitengo cha video katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kwani huongeza uwazi wa ufundishaji, humfanya mwanafunzi kuwa na msisimko wa kiakili ambao humfanya kuwa na hamu zaidi katika kazi ya sanaa inayofundishwa ( Taz. Picha 4.31,4.32 na 4.33). Isitoshe, ushirikiano uliodhihirika baina ya Swahilihub na tovuti nyingine ulichangia kupanua wigo wa matini kwenye kitengo cha video na kuthibitisha thamani ya juu ya matini yake. Ushirikiano huu ulichangia katika usambaaji wa Kiswahili kwa upana kwenye ukanda wa Afrika Mashariki na Kati na hata Ughaibuni. Msambao huu wa lugha ya Kiswahili ulibainisha uwezo wa lugha hii kumudu changamoto zinazoikumba katika matumizi mapana na kudumisha hadhi na dhima ya Kiswahili kote ulimwenguni. Matokeo haya yanabainisha kuwa Swahilihub ina mchango mwafaka katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kwa kupanua wigo wa matumizi ya lugha yake mitandaoni kufikia viwango vya lugha zingine za kimataifa kama vile Kiingereza na Kifaransa. Kuimarika kwa matini ya video kutokana ushirikiano wa tovuti anuai kulichangia ushindani mkuu mtandaoni uliobainika miongoni mwa tovuti bilioni 1.9. Swahilihub ilikuwa katika nafasi ya 2,411,967 miongoni mwa takriban tovuti bilioni 1.9 kote ulimwenguni. Nafasi hii inaipa Swahilihub uwezo wa kudumisha hadhi na dhima ya Kiswahili kote ulimwenguni. Hiki ni kigezo muhimu katika ukuzaji wa Kiswahili mtandaoni kutokana na usambaaji wa Swahilihub miongoni mwa watumiaji wa mitandao anuai.

#### 4.2.1.3.5 Makala.

Kitengo cha Makala kiliangazia vipindi vya mahojiano na wataalamu mbalimbali waliobobea katika nyanja na tasnia mbalimbali. Tovuti ya Swahilihub inalenga kuwa na hazina ya data muhimu ya asasi, taasisi, tasnia, idara mbalimbali za umma, waandishi na

wachapishaji kwa njia ya makongamano, semina, warsha ili kubadilishana mawazo kwa maswala anuwai. Hazina hii ilijengwa kwa ushirikiano wa karibu na wasanii, waandishi, wataalamu mbalimbali na taasisi ambazo zina makala na data muhimu zinazoweza kuijenga hazina hiyo. Vipindi hivi vilivyowahusisha wasanii na wataalamu anuwai vilichangia upanuzi wa soko kwa huduma za Swahilihub na vikawa hatua kubwa katika kuchangia kupanua wigo wa matumizi ya tovuti ya Swahilihub miongoni mwa watumiaji wengi wa mitandao kote ulimwenguni. Na hatimaye kusaidia katika kuleta utandawazi kwa haraka kati ya mataifa yanayoendelea kupitia TEHAMA ambayo msingi wake upo katika teknolojia ya tarakilishi. Ushirikiano wa karibu na miradi kama hii ni njia moja ya kupata na kujenga ghala la matini bora katika tovuti ya Swahilihub kwa lengo la ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kote ulimwenguni.




**Picha SURA YA NNE .41: Vitendawili kwenye Kitengo cha Makala**

Miongoni mwa vigezo vya ukubalifu wa uvumbuzi anavyopendekeza Rodgers (2003) ni manufaa ya uvumbuzi husika. Hiki ndicho kigezo kikubwa sana katika ukubalifu wa uvumbuzi kwa kuwa uwazi kuhusu manufaa yake ni nguzo muhimu ya ukubalifu wake. Ili kuboresha uvumbuzi na kufanya manufaa ya uvumbuzi kudhihirika, matini inayohifadhiwa kwenye tovuti inastahili kuwa ya thamani ili kuyakidhi mahitaji ya watumiaji wake (Rodgers, 2003).

## 4.3 Swahilihub na Ukuzaji wa Kiswahili Nchini Kenya

Kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili kunategemea mambo mbalimbali kama vile kutumika katika maeneo na mifumo rasmi kwenye jamii husika. Hasa utafiti huu ulitaka

kubaini ukuzaji wa Kiswahili miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub kimatini na kimfumo. Uhariri wa matini ulichangia matumizi mapana ya istilahi 5300 miongoni mwa watumiaji 3709 wa mradi wa Swahilihub. Ongezeko hili la idadi ya msamiati wa Kiswahili ni hatua muhimu katika ujenzi wa taaluma ya Kiswahili kama msingi wa ukuzaji wake mtandaoni. Tathmini hii ilitokana na uchunguzi wa kiteknolojia wa ARhefs pamoja na matokeo yaliyopatikana kwenye majibu ya hojaji na usaili nyanjani. Tathmini hii iliegemezwa kwenye vigezo vitatu vya ukuzaji wa Kiswahili: ujenzi, usambaaji na udumishaji wa hadhi na dhima ya Kiswahili. Kwa mujibu wa Rodgers (2003) mawasiliano ni mchakato unaowawezesha wanajamii husika kubuni, kushiriki na kusambaza habari miongoni mwao ili kuyafikia malengo fulani mahususi.

Mchango wa Swahilihub kwa mchakato wa ukuzaji wa Kiswahili umebainika kwa juhudi za wanazuoni katika taaluma za isimu, isimujamii, na fasihi na utafiti wa nyanja anuai za Kiswahili. Matokeo ya utafiti anuai kuhusu historia na maendeleo ya Kiswahili yamechapishwa katika vitengo mbalimbali vya Swahilihub kama vile Maktabani Jisomee, Jifunze Kiswahili na Makala mbalimbali. Taarifa na mijadala katika machapisho haya yanathibitisha jambo moja muhimu kwamba lugha ya Kiswahili na matumizi yake yamekuwa yakipanuka tena kwa kasi kubwa kwenye vitengo mbalimbali vya Swahilihub. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu, Swahilihub ina istilahi takriban 5,300 ambazo zimerejelewa tangu kuasisiwa kwake takriban mwongo mmoja uliopita. Matumizi ya istilahi hizi miongoni mwa watumiaji wa Swahilihub ni dhihirisho la ukuzaji wa Kiswahili kwa msingi wa ujenzi wa istilahi zake. Istilahi hizi zilitumika miongoni mwa watumiaji 3709 wa Swahilihub. Hii ni idadi kubwa ya watumiaji waliofaidika na mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili kwa kupanua mawanda ya matumizi yake kwa msingi wa ukuzaji wa Kiswahili kwa usambaaji wake.

Utafiti huu pia una mchango mwafaka katika kupanua wigo wa matumizi ya lugha ya

Kiswahili mitandaoni kufikia viwango vya lugha zingine za kimataifa kama vile Kiingereza na Kifaransa. Kutokana na ugunduzi wetu ushindani mkuu mtandaoni ulibainika miongoni mwa tovuti bilioni 1.9. Swahilihub ilikuwa katika nafasi ya 2,411,967. Nafasi hii inaipa Swahilihub uwezo wa kudumisha hadhi na dhima ya Kiswahili kote ulimwenguni. Hiki ni kigezo muhimu katika ukuzaji wa Kiswahili mtandaoni kutokana na usambaaji wa Swahilihub miongoni mwa watumiaji wa mitandao anuai.

Kiswahili ni miongoni mwa lugha zinazopokea maneno kutokana na matumizi yake kwenye mitandao hususan katika maendeleo ya sayansi na teknolojia, siasa, kijamii na uchumi. Kwa mfano, kuna matumizi ya istilahi nyingi za kimtandao za sayansi na teknolojia ambayo hutumiwa katika shughuli mbalimbali za kijamii kwenye vitengo vyote vinane vya Swahilihub. Kuhusu matumizi ya Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili, ilibainika kwamba asilimia 93.7(318) ya watumiaji wa Swahilihub wamekuwa wakiitumia kwa mwaka mmoja kuikuza taaluma ya Kiswahili huku asilimia 6.3 tu wakiitumia kwa shughuli zingine za ziada zilizochangia pia katika maendeleo ya taaluma ya Kiswahili. Hata hivyo kwa watumiaji wa Swahilihub kwa muda wa miaka mitano, ilibainika kwamba asilimia 100 ya watumiaji wa Swahilihub wamekuwa wakiitumia kuendeleza taaluma ya Kiswahili (Taz. Chati 4.10).

Matumizi ya Kiswahili katika tovuti ya Swahilihub yalianza kuimarika mwaka wa 2014.

Kiswahili hutumika katika mitandao ya Facebook na Twitter kama nyenzo za mawasiliano. Kupitia mifumo mbalimbali mtandaoni kama vile tovuti ya Swahilihub, watumiaji wana uwezo wa kujenga maudhui, kuchapisha maelezo, kuwasiliana na kununua au kuuza bidhaa na kushiriki huduma mbalimbali.

Usambaaji wa Kiswahili ni nguzo muhimu ya ukuzaji wake inayojumuisha ueneaji wake. Usambaaji wa Kiswahili ni uongezekaji wa matumizi yake kieneo na kiwakati. Katika utafiti huu dhana ya usambaaji wa Kiswahili ilibainika kulingana na mahitaji ya watumiaji wa Swahilihub mtandaoni. Swahilihub ilidhihirisha ushirikiano mkubwa na tovuti nyingine kama vile mtanzania.co.tz na mwananchi.com.

Ushirikiano huu ulichangia kupanua wigo wa matini na kuthibitisha thamani ya juu ya matini kwenye tovuti ya Swahilihub na kwa njia hii kujenga usambaaji wa Kiswahili kwa maeneo mbalimbali na kudumisha hadhi na dhima ya Kiswahili kote ulimwenguni. Swahilihub ilibainisha mchango wake katika ukuzaji wa Kiswahili kwa kuwezesha ujenzi wake, usambaaji wake na udumishaji wa hadhi na dhima yake mtandaoni. Aidha, ushahidi kwamba thamani ya matini ya Swahilihub ilikuwa ya ngazi ya juu ni ushirikiano huu ambao pia uliibua ushirikiano mkubwa kati ya tovuti nyingine zilizokuwa katika nafasi nzuri kuliko Swahilihub. Isitoshe kutokana na utendakazi wa mradi wa Swahilihub, tovuti 165 ziliwaelekeza watumiaji wake kurejelea matini ya Swahilihub kama ishara tosha ya kuaminika kwa matini ya Swahilihub. Tovuti zenye hadhi na dhima kuu kama mtanzania.co.tz na mwananchi.com ziliwaelekeza watumiaji wake kurejelea matini ya Swahilihub kama msingi wa usambaaji na udumishaji wa hadhi na dhima ya Kiswahili. Ongezeko hili la tovuti zinazorejelea matini ya Swahilihub ni thibitisho kwamba matini iliyopo kwenye tovuti ya Swahilihub ina upya unaowavutia na kuwapendeza watumiaji wa tovuti nyingine. Kupendeza kwa matini ya tovuti ya Swahilihub ni ishara ya kuaminika na kutegemeka kwa tovuti hii miongoni mwa watumiaji wa tovuti zingine kote ulimwenguni. Mchakato huu mzima ni hatua kubwa katika ukuzaji wa Kiswahili kwa msingi wa ujenzi wake, usambaaji wake na udumishaji wa hadhi na dhima yake.


Mradi wa Swahilihub ulipata watumiaji wake kutoka maeneo mbalimbali yakiwemo nchi za Afrika Mashariki na ugaibuni. Tovuti ya Swahilihub hurejelewa zaidi katika nchi ya Tanzania kwa asilimia 60.4 ikifuatiwa na Kenya kwa asilimia 28.5 ikifuatwa kwa karibu na Marekani Kaskazini, Ujerumani na mataifa mengine ya Ulaya kwa asilimia 11.1 iliyosalia. Mataifa mengi ya ughaibuni yanayotumia tovuti ya Swahilihub yamekuwa na uhusiano wa kiutawala na nchi za Afrika Mashariki zinazozungumza lugha ya Kiswahili. Swahilihub hivyo basi ilichangia katika ukuzaji wa Kiswahili kwa kuimarisha usambaaji wake pamoja na hadhi na dhima yake kote ulimwenguni kwa njia mbalimbali. Watafitiwa walioshiriki katika utafiti huu walikiri kwamba waliweza kuitumia tovuti ya Swahilihub kwa njia anuai ili kuikuza lugha ya Kiswahili. Miongoni mwa njia hizo za ukuzaji ni pamoja na ujenzi wake kiisimu, usambaaji wa fasihi yake na udumishaji wa hadhi yake kupitia utafiti mbalimbali wa kitaaluma. Njia hizi zimebainishwa katika jedwali 4.2. Swahilihub hutumiwa kwa njia mbalimbali na kwa malengo anuwai. Utafiti huu uligundua kwamba asilimia 48 ya watumiaji wa Swahilihub huitumia kwa kusudi la kukuza Kiswahili kwa kuzingatia vigezo vyake anuwai. Asilimia 13.49 (46) walitaja njia mbalimbali walizotumia Swahilihub kukuza taaluma ya Kiswahili. Kuhusu njia mahususi za matumizi ya Swahilihub katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili, asilimia 7.9 (26) ya watafitiwa walikiri kuitumia Swahilihub kwa sababu ina uamilifu wa kifasihi, kiisimu, kimtandao na kiutafiti. Swahilihub iligunduliwa kuchangia katika kuimarisha taaluma ya Kiswahili kwa kujenga vipengele mbalimbali vya kifasihi, kiisimu pamoja na kuimarisha utafiti na matumizi mwafaka ya mtandao kuimarisha taaluma ya Kiswahili (Taz. Jedwali 4.2).

**Jedwali SURA YA NNE .3: Njia za Ukuzaji wa Kiswahili kwenye Swahilihub**

| **Ukuzaji wa Kiswahili kwenye Swahilihub** | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Haikuitikiwa | 280 | 92.1 |
| Ukuzaji kwa ujenzi wake kiisimu | 6 | 2.0 |
| Ukuzaji kwa usambaaji wa kifasihi | 6 | 2.0 |
| Ukuzaji kwa hadhi na dhima yake | 8 | 2.6 |
| Ukuzaji wa kiutafiti | 4 | 1.3 |
| **Total** | **304** | **100.0** |


**Jedwali SURA YA NNE .4: Njia mbalimbali za matumizi ya Swahilihub**

| | | | Njia za ukuzaji wa Kiswahili kwenye Swahilihub kando na zile zilizotajwa | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Haikuitikiwa** | **Ukuzaji kifasihi** | **Ukuzaji kiisimu** | **Ukuzaji wa Hadhi** | **Ukuzaji kiutafiti** | |
| Je, wewe na walimu wako mwanatumia swahilihub kukuza Kiswahili | Ndiyo | Idadi | 188 | 1 | 3 | 6 | 2 | 200 |
| | | % Jumla | 66.7% | 0.4% | 1.1% | 2.1% | 0.7% | 70.9% |
| | La | Idadi | 71 | 4 | 3 | 2 | 2 | 82 |
| | | Jumla | 25.2% | 1.4% | 1.1% | 0.7% | 0.7% | 29.1% |
| Jumla | | Idadi | 259 | 5 | 6 | 8 | 4 | 282 |




*Chati SURA YA NNE .8: Matumizi chini ya miaka mitano*

Kwa jumla matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa idadi kubwa ya wabwiaji wa Swahilihub, takriban asilimia 97.5(318) ya watumiaji wa Swahilihub, wamekuwa wakiitumia kuendeleza taaluma ya Kiswahili kwa muda wa chini ya miaka mitano, huku asilimia 2.5 tu wakiitumia kwa muda wa zaidi ya miaka mitano kwa shughuli za kijamii zisizowiana na maendeleo ya taaluma ya Kiswahili. Sampuli wakilishi ya watumiaji wa Swahilihub wenye tajriba ya miaka mbalimbali ya utumiaji ilihusishwa katika utafiti huu, hivyo basi kupata matokeo yanayoweza kutegemewa na kuaminika. Matokeo haya yalionyeshwa katika jedwali 3.1 na 4.1.




*Chati SURA YA NNE .9: Matumizi ya zaidi ya miaka mitano*

## 4.4 Tathmini ya Swahilihub katika Ukuzaji wa Kiswahili Nchini Kenya

Tathmini ya tovuti ni jambo muhimu na la kimsingi katika mchakato wa kuimarisha na kuboresha utendakazi wa tovuti husika. Kuna utafiti anuwai wa awali uliofanywa kutathmini ufaafu na utendakazi wa tovuti mbalimbali katika nyanja tofauti. Utafiti huu ulilenga kubaini ni kwa kiwango gani mashirika mbalimbali na asasi mbalimbali za kiserikali na za kibiashara zilivyotumia tovuti zao kuwafikia na kutagusana na watumiaji wao mitandaoni. Msingi muhimu ulioangaziwa ni kanuni za mawasiliano yaliyojengwa kwenye msingi wa mrejesho thabiti kutoka kwa watumiaji wa tovuti hizi.

Kuna mielekeo mbalimbali ya kutathmini tovuti. Mielekeo hii ni pamoja na kitakwimu inayotumia vigezo vya utendakazi wa tovuti kwenye programu ya tarakilishi, ya pili ni

kutumia mrejesho wa watumiaji wa tovuti, tatu ni kutumia fomula kuchakata matokeo ya tathmini husika huku ya nne ikiwa ni kutumia tathmini ya moja kwa moja inayotegemea tajriba, ujuzi na maarifa ya wataalamu wa utathmini wa tovuti. Rababah, Al-Shboul, na Al-Sayyed (2011) wanafafanua ubora wa tovuti kuwa kigezo cha mrejesho wa watumiaji wake kuhusu utendakazi wake unaotokana na jinsi matarajio yao yanavyofikiwa kila wanapoitumia tovuti husika. Ili kufanikiwa katika majukumu yake, tovuti bora lazima ziwe na sifa za kimsingi zinazozifanya kuwahusisha watumiaji wengi iwezekanavyo. Miongoni mwa sifa hizi muhimu ni ufaafu kimatumizi, ufaafu kimatini na urahisi wa kufikiwa na watumiaji wake (Diffly, 2006). Ufaafu wa kimatumizi huangazia vipengele vya tovuti husika vinavyoifanya kuwa rahisi kutumika. Kwa mujibu wa Nielson (1994) urahisi wa kimatumizi wa tovuti hutokana na muundo wake ulivyoratibiwa wakati wa ujenzi wake.

Ufaafu kiuamilifu unarejelea kupatikana kwa matini inayohitajika huku urahisi wa kufikiwa  ni juhudi za kuondoa vizingiti vinavyowazuia watumiaji wake kuchagua na kusakura habari wanazohitaji kwa tovuti mahsusi (Leung, Law na Lee, 2016). Ufaafu wa tovuti kiuamilifu ni kigezo muhimu katika kuitolea tathmini yake kwa kuwa lengo kuu la kila tovuti ni kuhifadhi na kufikisha habari kama inavyohitajika na watumiaji wake (Hidayat, 2011; Ip, Law na Lee, 2012). Katika tovuti matini ndio mfalme lakini mtawala ni mtumiaji wake. Utafiti huu ulijikita katika kutathmni ufaafu wa matini ya Swahilihub na sifa zake zinazowafanya watumiaji wake kuirejelea katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili.

Tathmini ya tovuti tangu jadi imefanyika kwa msaada wa mbinu anuwai zikiwemo hesabu za kitakwimu, mrejesho kutoka kwa watumiaji pamoja na mbinu mseto (Law, Qi,Buhalis, 2010). Tathmini ya mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili itachangia pakubwa kuimarisha nafasi yake miongoni mwa tovuti bilioni 1.9 zinazopatikana kote


ulimwenguni. Kwa kuangazia idadi hii kubwa ya tovuti na usakuraji unaoendelea mtandaoni kila siku, ushindani mtandaoni ni kigezo muhimu wa kukadiria ufaafu wa tovuti ya Swahilihub miongoni mwa tovuti wenza kote ulimwenguni. Utafiti huu ulitumia mwelekeo wa kwanza wa kitakwimu uliohusisha tathmini ya vigezo vya ufaafu wa tovuti ya Swahilihub kwenye programu mahususi ya kiteknolojia ya tarakilishi. Mwelekeo huu ulikuwa bora kwa sababu ya uwezo wake wa kukabiliana na idadi kubwa ya data inayopatikana kwenye tovuti ya Swahilihub kutokana na wingi wa watumiaji wake.

Katika mwelekeo huu kuna vigezo maalum vya kukadiria kiwango cha ufaafu wa tovuti. Kamusi ya Cambridge (2015) inafafanua vigezo vya tathmini ya tovuti kama misingi ya kukadiria kiwango cha ufanisi wa tovuti husika. Vigezo vya tathmini ya tovuti ni misingi ya kukadiria kiwango cha ufanisi wa tovuti husika (Kamusi ya Cambridge, 2015). Vigezo hivi, vikiwa pamoja na ushindani mtandaoni, uhariri wa matini pamoja na urahisi wa kimatumizi, vilisaidia kukadiria kiwango cha ukuzaji wa Kiswahili kwenye tovuti ya Swahilihub. Utafiti huu ulibainisha vipengele muhimu vya tovuti ya Swahilihub na kuchangia pakubwa kuweka wazi maandishi kuhusu mradi wa Swahilihub, historia yake, malengo yake na changamoto zinazoukabili mradi huu wa Swahilihub. Vigezo hivi vilikuwa vifuatavyo:

### 4.4.1 Kitambulisho Mahususi cha Tovuti ya Swahilihub

Kutokana na uchunguzi wa kijarabati wa tovuti ya Swahilihub kwa kutumia Arhefs, ilibainika kwamba tovuti ya Swahilihub inatambuliwa kwa kupewa nambari maalum ya kuirejelea kama kitambulisho chake cha kipekee. Kitambulisho hiki mahususi cha tovuti ya Swahilihub kinachotumiwa kuirejelea miongoni mwa mitandao mingine kote ulimwenguni ilibainika kuwa 82.112.114.21. Hiki ndicho kitambulisho cha kipekee cha tovuti ya Swahilihub miongoni mwa tovuti zote bilioni 1.9 kote ulimwenguni (Internet

Live Stats, 2018).




Picha SURA YA NNE .42: Kitambulisho maalum cha tovuti ya Swahilihub kwa mujibu wa AHREFS

### 4.4.2 Ushindani wa Tovuti ya Swahilihub Mtandaoni

Miongoni mwa vipengele muhimu vya mfumo katika kutathmini utendakazi wa tovuti yoyote ni uwezo wake wa kushindana ili kupata idadi kubwa ya watumiaji miongoni mwa tovuti nyingine mtandaoni. Kipengele hiki ndicho kinachobainisha viwango vya ushindani vya tovuti ya Swahilihub mtandaoni miongoni mwa tovuti mbalimbali. Kutokana na ushindani huu mtandaoni, kampuni ya google ilichangia katika kutoa nafasi za ubora wa tovuti zote kwa kuangazia misingi mbalimbali ya utendakazi wa tovuti husika kwa watumiaji wake.

Miongoni mwa maswala muhimu katika kutambua na kubaini nafasi ya mradi wa Swahilihub ni kiwango chake cha ushindani mtandaoni miongoni mwa tovuti nyingine. Kutokana na data ya uchunguzi wa Arhefs kuhusu nafasi ya tovuti ya Swahilihub miongoni mwa tovuti zingine kote ulimwenguni, utafiti huu uligundua kwamba tovuti ya Swahilihub ilichukua nafasi ya milioni mbili, laki nne na elfu kumi na moja, mia saba na sitini na saba (2,411,767) kwa takriban tovuti bilioni 1.9 zilizopatikana kwenye sajili ya tovuti inayotumika kote ulimwenguni. Haya ni kwa mujibu wa uchunguzi wa kwanza uliofanywa katika mwezi wa Januari mwaka wa 2018. Kwa mujibu wa Internet Live Stats (2018), idadi ya tovuti ilikadiriwa kuwa takriban tovuti bilioni 1.9 kote ulimwenguni (Taz. Picha 4.45, 4.46 na 4.47).

Kutokana na data hii kuhusu uwezo wa mradi wa Swahilihub kustahimili ushindani mkubwa mtandaoni, nafasi yake kwa takriban tovuti bilioni 1.9 zilizopatikana kwenye sajili ya tovuti inayotumika kote ulimwenguni, ni milioni mbili, laki nne na elfu kumi na moja, mia saba na sitini na saba (2,411,767). Nafasi hii ya tovuti ya Swahilihub inaonyesha kwamba tovuti ya Swahilihub haijawapendeza na kuwafikia watumiaji wengi mtandaoni

na hivyo basi kupata nafasi duni katika kipengee cha utendakazi cha ushindani mtandaoni. Hivyo basi kutokana na data hii utafiti huu unazua matokeo kwamba tovuti ya Swahilihub haikuwa na uwezo wa kustahimili ushindani mkubwa mtandaoni na hivyo basi ilikosa kupata watumiaji wengi mtandaoni ikilinganishwa na tovuti zingine mtandaoni.

Matokeo haya kuhusu utendakazi wa mradi wa Swahilihub yalitokana na mambo mengi ya kimuundo. Miongoni mwa mambo haya yaliyochangia matokeo haya ni kiwango cha chini cha uhusishwaji wa mitandao ya kijamii kwenye jukwaa la Swahilihub. Watumiaji wengi wa tovuti mitandaoni walibainisha kwamba wao huchangamkia tovuti zilizohusisha mitandao mbalimbali ya kijamii kama njia mojawapo ya kutoa maoni yao kuhusu huduma za tovuti husika na kupata mrejesho kutoka kwa wasimamizi wake. Kuna zaidi ya watu bilioni moja kwenye Facebook, Wikipedia ina zaidi ya watumiaji bilioni nne na Twitter ina zaidi ya watumiaji milioni 500. Mitandao ya kijarnii mingi inakuruhusu kurekebisha mipangilio yako au kudhibiti maelezo yapi unayoshiriki, jinsi unavyoyashiriki, na unayeshiriki naye (Jelimo, 2015) Kwa mujibu wa Owoche, (2019), watumiaji wengi huteua na kutumia mitandao ya kijamii badala ya tovuti mahususi. Kwa mfano “Facebook” ina takriban watumiaji bilioni mbili kila mwezi, “instagram” ikiwa na watumiaji milioni 813 huku “twitter” ikiwa na watumiaji milioni 330 (Owoche, 2019).

Hivyo basi mitandao hii ya kijamii ni wenzo kubwa wa kupata mrejesho kutoka kwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub kwa kuwa inachangia pakubwa kuimarisha idadi ya watumiaji wake mtandaoni. Nafasi ya tovuti ya Swahilihub kwa sasa ni milioni mbili laki nne, na huenda nafasi hii ilitokana na tovuti ya Swahilihub kukosa kutumia kikamilifu mitandao mingi ya kijamii ili kupata data muhimu kuhusu hisia na maoni ya watumiaji walio wengi na wanaotumia kwa wingi mitandao hii muhimu ya kijamii.

Mitandao hii huchangia kupata mrejesho kutoka kwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub. Mrejesho huu ni muhimu katika uhariri wa matini ya tovuti ya Swahilihub na upangaji na uratibu wa kurasa za tovuti ya Swahilihub kwa kuweka matini mbalimbali mahali zinapostahili kwa kutegemea sifa za mitandao hiyo ya kijamii. Miongoni mwa majukwaa haya ya mitandao, tovuti ya Swahilihub ina mitandao miwili tu ya kijamii ambayo ni "Facebook" na "Twitter" ilihali kuna takriban mitandao minane ya kijamii inayoweza kuimarisha utendakazi wake. Katika kitandazi cha Facebook kwa mfano kuna istilahi anuwai za kiteknolojia zinazotumiwa miongoni mwa watumiaji wake kama ilivyo katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali SURA YA NNE .5: Baadhi ya Istilahi za Kiswahili kwenye Jukwaa la Facebook**

| | **English** | **Kiswahili** |
|---|---|---|
| 1 | Facebook Page | Ukurasa wa Facebook |
| 2 | Add picture | Ongeza picha |
| 3 | Advert | Matangazo |
| 4 | Account settings | Mipangilio ya Akaunti |
| 5 | Activity log | Rekodi ya shughuli |
| 6 | About | Kuhusu |
| 7 | Applications | Vitumizi |

| | | |
|---|---|---|
| 8 | Application | Program |
| 9 | Blockings | Zuia |
| 10 | More friends | Marafiki Zaidi |
| 11 | Password | Neno siri |
| 12 | Pokes | Midukuo |
| 13 | Political views | Maoni ya kisiasa |
| 14 | Post a profile picture | Sambaza picha |
| 15 | Name | Jina |
| 16 | Menu | Menyu |
| 17 | Favorites | Vipendavyo |
| 18 | Family members | Wanafamilia |
| 19 | Events | Matukio |
| 20 | Email | Barua pepe |
| 21 | Edit profile picture | Hariri picha ya wasifu |
| 22 | Edit | Hariri |
| 23 | Data policy | Sera ya matumizi ya data |
| 24 | Create page | Buni ukurasa |

| | | |
|---|---|---|
| 25 | Change language | Badilisha lugha |

Katika ukurasa wa Facebook, mashirika ambayo hutumia lugha ya Kiswahili hutumia mtandao huu kuhifadhi utafiti na kazi mbalimbali za Kiswahili ili kufikia umma na wapenzi wa Kiswahili kwa muda mfupi. Kwa mfano, mradi wa Swahilihub Kitandazi cha Facebook hutumiwa na mamilioni ya watu kuwasiliana. Matokeo ya mijadala na mrejesho wa mahojiano na hojaji yalibaini kwamba hali hii ni mojawapo ya sababu kuu zilizopelekea mradi wa Swahilihub kukosa uwezo wa kushindana na tovuti nyingine mtandaoni.

Tovuti ya Swahilihub ina nafasi bora ya kuimarisha utendakazi wake kwa kutumia vitengo vyake vyote vinane na kuimarisha uhusishwaji wa mitandao ya kijamii kama mbinu ya kupata mrejesho kutoka kwa watumiaji wa mitandao hiyo. Mitandao ya kijamii ni njia mwafaka ya kuwafikia watumiaji wengi wapya wa tovuti ya Swahilihub ambao kwa sasa hupatikana kwenye mitandao ya kijamii kama vile twitter, ‘facebook’, ‘whats app’ na hata ‘instagram’. Mitandao hii ya kijamii pia huwapa watumiaji nafasi ya kuchangia kuboresha utendakazi wa tovuti ya Swahilihub kwa kuwafikia watumiaji wapya wengi na hivyo basi kuimarisha nafasi yake kutoka milioni mbili laki nne miongoni mwa tovuti nyingine ulimwenguni. Hali hii ni ishara tosha ya kudorora kwa utendakazi wa tovuti ya Swahilihub ikichukuliwa kwamba hii ni nafasi ya milioni mbili na laki nne miongoni mwa takriban tovuti bilioni 1.9 kote ulimwenguni. Kuna ushindani mkubwa miongoni mwa tovuti mbalimbali kote ulimwenguni kutokana na idadi kubwa ya tovuti zinazorejelewa mtandaoni, ambayo ni takriban bilioni 1.9, pamoja na idadi kubwa ya watumiaji wa intaneti, ambayo ni bilioni 3.96 (Live Stats, 2018).

Matarajio ya watumiaji na urahisi wa matumizi ya tovuti ni vigezo muhimu katika utendakazi wa tovuti hiyo. Kwa mujibu wa Owoche, (2019), katika mwaka wa 2006 watumiaji wa tovuti walitarajia muda wa kupatikana kwa matini mtandaoni kuwa sekunde nne au hata muda mfupi zaidi (DoubleClick, 2018). Watumiaji wa mitandao kwa sasa wanatarajia muda mfupi sana kuliko sekunde nne. Kutokana na muda huu wa sekunde nne unaotarajiwa na watumiaji wa mitandao, watumiaji hufanya maamuzi yao kuhusu utendakazi wa tovuti husika. Asilimia 53 ya watumiaji wa tovuti wataacha kuitumia tovuti hiyo baada ya kusubiri kupata data waliyotafuta kwa muda wa zaidi ya sekunde tatu. Vilevile asilimia 80 ya watumiaji wa tovuti hawataitumia tena baada kuhangaishwa kwa kungojea sana mtandaoni (DoubleClick, 2018). Asilimia 47 ya watumiaji wa tovuti hutarajia muda huu wa kufikia matini mtandaoni kuwa sekunde mbili. Mtumiaji akicheleweshwa kwa sekunde moja tu kunawezachangia kutoridhika kwa watumiaji kwa asilimia 16 na kupoteza mapato kwa asilimia 7

Watumiaji hawa ama hutafuta habari, hutoa maoni yao au pengine hujulisha wenzao kuhusu utendakazi wa tovuti mbalimbali wanazorejelea. Idadi ya watumiaji wa tovuti ya Swahilihub ilitegemea kiwango cha ubora na utendakazi wake. Kwa mujibu wa Wagner (2017) utendakazi wa tovuti ni dhana inayorejelea kasi au ule muda unaochukuliwa na tovuti kuwasilisha matini kwa mtumiaji. Huu ni muda unaoakisi ubora wa tovuti kwa kuonyesha wakati wa kuingia kwa mtumiaji kwa tovuti anapotafuta habari na wakati habari na matini muhimu anayoitafuta inapowasilishwa na kukabidhiwa mtumiaji huyu mtandaoni. Utendakazi wa tovuti ya Swahilihub ni dhana inayochangia pakubwa idadi ndogo ya watumiaji wake. Isitoshe kuna baadhi ya mambo mengi yanayochangia utendakazi wa Swahilihub yanayohusu muundo wake na jinsi tovuti ya Swahilihub kama jukwaa inavyokidhi matarajio ya watumiaji wake kimatini.

Utafiti huu ulibainisha kwamba utendakazi wa tovuti ya Swahilihub ulikuwa chini kwa sababu watumiaji wake walifikiwa habari sekunde 15 baada ya kuingia kwenye tovuti ya Swahilihub. Hivyo basi watumiaji wengi yaani asilimia 88 ya watafitiwa walichagua tovuti zingine zilizofikisha matini kwa muda unaofaa yaani sekunde tatu au hata chini ya sekunde mbili. Asilimia 52 (176) ya watumiaji wa tovuti ya Swahilihub walikiri kuhangaishwa na kasi yake kwa kuwa walicheleweshwa kupata habari muhimu walizohitaji mtandaoni. Kigezo hiki cha muda wa kupatikana kwa matini ni muhimu sana na huchangia katika kuamuliwa kwa nafasi ya tovuti ya Swahilihub miongoni mwa tovuti zingine ulimwenguni. Data ya utafiti huu ikilinganishwa na matokeo ya utafiti wa awali inadhihirisha kwamba muda wa kupatikana kwa matini mtandaoni ni swala muhimu sana linalochangia utendakazi wa tovuti husika.

Katika utafiti huu, tovuti ya Swahilihub ilichukua nafasi ya milioni mbili na laki nne kwa sababu ya muda wa kupatikana kwa matini unaostahili kuimarishwa. Kutokana na matokeo haya, ni dhahiri kwamba haitoshi tu kuwa na tovuti ya Swahilihub mtandaoni bali pia ni jambo la maana kwa tovuti ya Swahilihub kuimarisha nafasi yake miongoni mwa tovuti zingine ulimwenguni kwa kuimarisha utendakzai wake kwa kuboresha kigezo cha muda wa kuwafikishia watumiaji wake matini mtandaoni. Ingawa kuna watumiaji wengi wa mitandao kuna uwezekano wa watumiaji hawa kutojua kuhusu tovuti ya Swahilihub iwapo wasimamizi wake hawataimarisha utandakazi wake.

### 4.4.3 Nafasi ya Swahilihub katika uchunguzi wa pili miezi mitatu baadaye




Picha SURA YA NNE .43: Nafasi ya Swahilihub katika uchunguzi wa pili miezi mitatu baadaye

Nafasi ya tovuti mtandaoni kimsingi ni kigezo cha utendakazi na ubora wake kama ilivyobainishwa kwenye orodha ya ubora wa tovuti zote kote ulimwenguni (Live Stats, 2018). Data ya uchunguzi wa pili uliofanywa baada ya kipindi cha miezi mitatu katika mwaka wa 2018 ilionyesha nafasi ya tovuti ya Swahilihub miongoni mwa tovuti nyingine kote ulimwenguni (Taz. Picha 4.47). Kwa mujibu wa matokeo haya, tovuti ya Swahilihub ilichukua nafasi ya 2,407,755 miongoni mwa tovuti bilioni 1.9 zinazopatikana kwenye sajili ya tovuti zote kote ulimwenguni. Hii ni nafasi iliyokaribiana sana na 2,411,767 katika chati ya kwanza (Taz. Picha 4.1). Katika takriban tathmini zote tovuti ya Swahilihub ilichukua nafasi ya milioni mbili laki nne.

#### 4.4.3.1 Kuimarika kwa Nafasi ya Swahilihub kwa muda wa miezi mitatu




**Picha SURA YA NNE .44: Kuimarika kwa Nafasi ya Swahilihub kwa Muda wa miezi mitatu**

Uchunguzi wa kina wa nafasi ya tovuti ya Swahilihub kwa kipindi cha siku 90 ulibainisha kwamba kumekuwa na uimarikaji wa ubora na utendakazi wake miongoni mwa watumiaji wake kutokana data iliyoonyesha mabadiliko katika nafasi ya tovuti ya Swahilihub. Hali hii ilionyesha tovuti ya Swahilihub ikiwa katika nafasi ya milioni mbili laki nne na ikaimarika hadi milioni mbili laki tatu katika kipindi cha miezi mitatu. Hali hii ilitokana na uhariri wa matini ya tovuti ya Swahilihub uliofanywa na wasimamizi wake kila mara na hivyo basi kuwafikia watumiaji wengi zaidi wa tovuti ya Swahilihub (Taz picha 4.48). Kuimarika kwa nafasi ya tovuti ya Swahilihub ni ishara tosha kwamba juhudi mbalimbali zinawekwa na wasimamizi wa tovuti hii ili kuhakikisha kwamba vipengele mbalimbali vya utendakazi wa tovuti ya Swahilihub vimeimarishwa na kuwafikia watumiaji wengi mtandaoni.


#### 4.4.3.2 Ushirikiano wa Swahilihub na Tovuti Nyingine

Ushirikiano wa tovuti ya Swahilihub na tovuti nyingine mtandaoni ulibainishwa kwa kuangazia idadi na thamani ya tovuti nyingine zilizopendekeza matumizi ya matini ya tovuti ya Swahilihub kwa watumiaji wake. Mitagusano miongoni mwa tovuti mitandaoni husababisha tovuti mbalimbali kuwaelekeza watumiaji wake kutumia tovuti fulani ili kupata habari inayohitajika (Moz, 2018). Mahusiano haya yalichangia tovuti zingine kuwaelekeza watumiaji wake kwa tovuti ya Swahilihub kwa kutambua thamani ya matini ya tovuti ya Swahilihub kuwa ya kutegemewa. Mahusiano bora miongoni mwa tovuti hizi yalitokea wakati tovuti hizo zilipowaelekeza watumiaji wake kurejelea tovuti ya Swahilihub kwa kutumia istilahi za kimsingi za tovuti ya Swahilihub na pia kupatikana kwenye tovuti nyingine iliyo na istilahi sawa au maudhui yanyaowiana na matini ya tovuti ya Swahilihub.

Kuhusu ustahilifu wa tovuti ya Swahilihub, data ya utafiti huu ilionyesha kuwa kuna takriban tovuti mia moja na sitini na tano zinazowaelekeza watumiaji wake kurejelea matini kwenye tovuti ya Swahilihub kupata habari muhimu kuhusu maswala mbalimbali. Miongoni mwa tovuti hizo ni tovuti mia moja na thelathini na nne zilizorejelea Swahilihub kila mara huku tovuti thelathini na moja zikirejelea tovuti ya Swahilihub mara moja moja tu. Idadi kubwa ya tovuti hizi ni zile zilizoangazia masuala ya elimu kwa jumla (Taz. Picha 4.47). Idadi kubwa ya tovuti zinazorejelea matini ya tovuti ya Swahilihub ni dhihirisho bora la kiwango cha ukubalifu wa tovuti ya Swahilihub. Thamani ya tovuti zinazorejelea Swahilihub ilikuwa bora kama ilivyobainika katika picha kwenye (Taz. Picha 4.48). Tovuti ya mtanzania.co.tz pamoja na mwananchi.co.tz zina watumiaji wengi na hivyo kuwa katika nafasi bora kuliko tovuti ya Swahilihub. Kwa kuwa kigezo cha idadi ya watumiaji hutumiwa katika kuamua nafasi na hadhi ya tovuti mtandaoni, tovuti ya mtanzania pamoja na ile ya mwananchi zilikuwa katika nafasi bora kuliko Swahilihub. Data za uchunguzi wa utafiti huu zilibaini kwamba tovuti za mtanzania na mwanachi zilirejelea matini za Swahilihub na kuwaelekeza watumiaji wake kutumia matini ya Swahilihub. Kutokana na hadhi ya tovuti hizi, ni thibitisho kwamba tovuti ya Swahilihub ilifaidika na kurejelewa kwa matini yake kwenye tovuti hizi.

#### 4.4.3.3 Tovuti Nyingine zinazoshughulikia lugha ya Kiswahili

Kutokana na matokeo ya uchunguzi wa Arhefs, kuna tovuti nyingine thelathini na nne zinazowasilisha matini yake kwa lugha ya Kiswahili. Matokeo ya uchunguzi huu yalionyesha kwamba hamna hata tovuti moja iliyo na jina linaloshabihiana na lile la Swahilihub.com. (Taz. 4.49).




*Picha SURA YA NNE .45: Tovuti Nyingine zinazoshughulikia lugha ya Kiswahili.*

Kigezo kingine kilichoangaziwa katika mahusiano haya kilikuwa ustahilifu, hadhi na thamani ya tovuti nyingine zilizorejelea na kuwaelekeza watumiaji wake kutumia tovuti ya Swahilihub. Miongoni mwa tovuti 34 zinazoshughulikia masuala ya lugha ya Kiswahili, kuna tovuti mbili zilizoshindana na tovuti ya Swahilihub kwa kiwango kikubwa kuliko tovuti zingine zote. Hizi ni tovuti zilizo na hadhi na umaarufu mkubwa miongoni mwa wataalamu na wanazuoni wa lugha ya Kiswahili.

Picha 4.48 inaonyesha tovuti mbili shindani ambazo ni mtanzania.co.tz na mwananchi.com. Picha hii inaonyesha kwamba tovuti ya mwananchi ndiyo iliyo na watumiaji wengi zaidi kwa kiwango cha 1500 katika mwaka wa 2018 ikifuatiwa na mtanzania.co.tz ikiwa na idadi ya watumiaji 750 katika mwaka wa 2018 na Swahilihub 500 katika mwaka wa 2018. Tofauti hii inachangiwa pakubwa na tovuti ya mwananchi na tovuti ya mtanzania kuwa tovuti za kiserikali zilizo na watumiaji wengi kote nchini Tanzania ikilinganishwa na tovuti ya Swahilihub ambayo ni tovuti ya kijamii wala sio ya kiserikali. Tovuti ya Swahilihub hutegemea nia za watumiaji kibinafsi. Katika utafiti huu kutokana na mrejesho wa hojaji na mijadala ya kimakundi, ilibainika kwamba asilimia 75 ya watumiaji waliamua kukimbilia tovuti nyingine kwa sababu ya kucheleweshwa wakitafuta habari na matini bora kwenye tovuti ya Swahilihub. Hali hii ilidhihirika miongoni mwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub ambao walikiri kukumbana na ugumu wa kimatumizi uliochangia pakubwa uamuzi wao wa kutafuta habari hizo kwenye tovuti nyingine.

### 4.4.4 Uhariri wa matini ya Tovuti ya Swahilihub

Katika utafiti huu ukaguzi wa thamani ya matini kwenye tovuti ya Swahilihub mtandaoni ulifanywa ili kubaini mchakato wa uhariri kwa kusudi la kutoa matini isiyofaa na kuweka ile iliyo ya kisasa zaidi kwa minajili ya kupata nafasi bora zaidi miongoni mwa tovuti zote ulimwenguni. Uhariri huu uliangazia uboreshaji wa isitilahi zilizoelekeza watumiaji mtandaoni, uimarishwaji wa thamani ya matini mtandaoni na uhusishwaji wa matini kwa kuzilinganisha na kuzilinganua mtandaoni. Kigezo kingine muhimu hapa ni idadi ya matini iliyowekwa kwenye tovuti ya Swahilihub pamoja na umaarufu wa tovuti zilizorejelea na kuwaelekeza watumiaji wake kwa matini ya Swahilihub. Mambo haya yote yalikuwa muhimu katika makadirio ya utendakazi wa tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili.  Matini yanayowekwa kwenye tovuti ya Swahilihub huchangia pakubwa kuwahusisha watumiaji wengi na idadi hiyo ikiimarika itaboresha nafasi ya tovuti ya Swahilihub miongoni mwa tovuti nyingine ulimwenguni.


Aghalabu, nyenzo ya kutegemewa na wasomi kwa muda mrefu katika kuhifadhi matini kutokana na utafiti mwingi wa Kiswahili imekuwa vitabu na majarida. Tovuti ya Swahilihub imetokea kuwa mradi wa kutegemewa kwa kiwango kikubwa katika uhifadhi. Tovuti hii imebuniwa kwa narnna ya kuwezesha uhifadhi wa matini muhimu ya Kiswahili kwa njia ambayo hayawezi kupotea. Matini haya yanaweza kurejelewa baada ya kipindi kirefu cha wakati kwa kubonyeza tu sehemu yalikohifadhiwa. Baadhi ya matini haya ni kama vile insha bora za Kiswahili. Insha hizi zimeteuliwa kimaksudi kuwa kielelezo kwa waandishi limbukeni. Ili kubaini viwango vya uhariri wa matini kwenye tovuti ya Swahilihub, utafiti huu uliangazia vigezo vifatavyo: urejeleaji wa Swahilihub na tovuti

nyingine, ruwaza ya matini mpya na za kale kwenye tovuti pamoja na thamani ya matini kwenye tovuti ya Swahilihub.

#### 4.4.4.1 Kurasa za matini zilizorejelewa na watumiaji wa Swahilihub

Kwa mujibu wa uchunguzi wa Arhefs idadi ya dhana na istilahi zilizorejelewa na watumiaji wa tovuti ya Swahilihub katika kipindi cha miaka mitano tangu kubuniwa kwake ni takribani elfu tano na mia tatu. Idadi hii ni ndogo sana ilikichukuliwa kwamba kipindi cha urejeleaji wake ni miaka mitano. Hii ni kumaanisha kwamba ni takriban istilahi elfu moja tu zilizorejelewa kila mwaka wa utafiti huu. Hii inaashiria kuwa watumiaji wa Swahilihub ni wachache au ufikiaji wa matini kwenye tovuti ya Swahilihub unakumbwa na changamoto anuai.


Kuhusu thamani na ustahilifu wa tavuti ya Swahilihub kwa watumiaji wake, ilibainika kuwa kuna takriban tovuti mia moja na sitini na tano zilizowaelekeza watumiaji wake kurejelea matini kwenye tovuti ya Swahilihub kupata habari muhimu kuhusu maswala mbalimbali. Miongoni mwa tovuti hizo ni tovuti mia moja na thelathini na nne zilizorejelea tovuti ya Swahilihub kila mara huku tovuti thelathini na nne zikirejelea tovuti ya Swahilihub mara moja moja tu. Idadi kubwa ya tovuti hizi ni zile zilizoangazia masuala ya elimu kwa jumla (Taz. Picha 4.5). Data hii ni muhimu katika kubainisha utendakazi wa Swahilihub kwa kuangazia kiwango cha matumizi ya matini yake miongoni mwa watumiaji wa tovuti nyingine.




**Picha SURA YA NNE .46: Kurasa za matini zilizorejelewa na watumiaji wa tovuti ya Swahilihub**

Kutokana na uchunguzi wa Arhefs kwa kipindi cha kati ya mwaka wa 2016 hadi 2018 ilibainika kwamba kumekuwa na ongezeko la idadi ya kurasa za matini zilizorejelewa kwenye tovuti ya Swahilihub kuanzia mwaka wa 2016 hadi mwaka wa 2018. Katika mwaka wa 2016, matokeo yalionyesha kwamba kulikuwa na matini kwenye kurasa ishirini tu zilizorejelewa na watumiaji wa tovuti ya Swahilihub huku idadi hii ikiongezeka kila mwaka. Ongezeko hili lilifikia kilele katika mwaka wa 2018 ambapo matini kwenye takriban kurasa mia saba na ishirini yalirejelewa na watumiaji wa mradi wa Swahilihub. Matokeo haya yanadhihirisha ongezeko kubwa katika idadi ya matini yaliyowekwa kwenye tovuti ya Swahilihub na ambayo ilirejelewa na watumiaji wa mradi wa Swahilihub.com.

#### 4.4.4.2 Ruwaza ya Tovuti mpya na za kale zilizorejelea Swahilihub




**Picha SURA YA NNE .47: Ruwaza ya Tovuti mpya na za kale zilizorejelea tovuti ya  Swahilihub.**

Ingawa data ya uchunguzi wa Arhefs ilibainisha kuwa idadi ya dhana na istilahi zilizorejelewa na watumiaji wa tovuti ya Swahilihub katika kipindi cha miaka mitano tangu kubuniwa kwake ilikuwa takribani elfu tano na mia tatu, kulitokea ongezeko katika idadi hii. Picha 4.51 inaonyesha ruwaza ya tovuti mpya kila mara zilizoendelea kurejelea tovuti ya Swahilihub zinazodhihirika katika chati hii kwa rangi ya samawati  huku zile tovuti zinazorejelea tovuti ya Swahilihub kwa muda tu kisha kusitisha urejeleaji huo zinadhihirika kwa rangi ya hudhurungi. Hali hii inatokana na mtiririko wa tovuti mpya zinazorejelea tovuti ya Swahilihub na zile zinazorejelea kwa muda fulani kisha zinasitisha urejeleaji huo kwa muda mahususi.

Matokeo  ya uchunguzi huu yalibainisha kuwa katika mwezi wa Januari mwaka wa 2014, kulikuwa na idadi kubwa ya tovuti mpya zilizorejelea tovuti ya Swahilihub kuliko tovuti zile zilizositisha urejeleaji wa tovuti ya Swahilihub. Katika mwezi wa Januari mwaka wa 2015 na mwaka wa 2016 kulikuwa na idadi chache mno ya tovuti zilizorejelea matini ya tovuti ya Swahilihub na zile zilizositisha urejeleaji wa tovuti ya Swahilihub. Hali hii ilitokana na kipindi cha utasa kwa sababu ya ukarabati uliokuwa ukiendelea katika muundo wa tovuti ya Swahilihub kati ya mwaka wa 2015 na mwaka wa 2016.  Ukarabati huu ulizuia urejeleaji kwenye tovuti ya Swahilihub. Hali hii inaoana na matokeo katika chati ya pili na tatu yaliyoangaziwa hapo juu. Kipindi hiki cha utasa pia huenda kilichangiwa na viwango vya chini vya uhamasisho katika hatua ya kwanza ya usambaaji wa tovuti ya Swahilihub miongoni mwa watumiaji wake. Matokeo ya mwezi wa Januari kuanzia mwaka wa 2017 hadi 2019 yalidhihirisha ongezeko kubwa katika urejeleaji wa tovuti ya Swahilihub huku idadi ya tovuti 30 mpya zikiongezeka na tovuti tano tu zikisitisha urejeaji wa tovuti ya Swahilihub.

Hali hii pia inawiana na matokeo yaliyoonyeshwa katika chati ya pili na chati ya tatu. Matokeo haya yalionyesha kwamba kati ya mwaka wa 2017 na mwaka wa 2019

kumekuwa na ongezeko kubwa la idadi ya tovuti zilizorejelea tovuti ya Swahilihub ikilinganishwa na idadi ya tovuti zilizokoma kurejelea tovuti ya Swahilihub. Ongezeko hili lilikuwa katika kiwango cha takriban tovuti 30 na kupunguzwa kwa idadi zinazorejelea tovuti ya Swahilihub kwa takriban tovuti 10 tu.

Ustahilifu wa tovuti ya Swahilihub kiuamilifu ni kigezo muhimu katika utathmini wake kwa kuwa lengo lake kuu ni kuhifadhi na kufikisha habari kama inavyohitajika na watumiaji wake. Katika tovuti matini ndio mfalme lakini mtawala ni mtumiaji wake. Uhariri wa matini mtandaoni ulifanyika katika tovuti ya Swahilihub ili kukagua matini yake mtandaoni kwa kusudi la kutoa matini isiyofaa na kuweka ile iliyo ya kisasa zaidi kwa minajili ya kupata nafasi bora zaidi miongoni mwa tovuti zote ulimwenguni. Uhariri huu uliangazia uboreshaji wa isitilahi zinazoelekeza watumiaji mtandaoni, uimarishwaji wa thamani ya matini mtandaoni na uhusishwaji wa matini kwa kuzilinganisha na kuzilinganua mtandaoni.

Kigezo kingine muhimu hapa kilikuwa idadi ya matini iliyowekwa kwenye tovuti ya Swahilihub pamoja na umaarufu wa tovuti zilizorejelea na kuwaelekeza watumiaji wake kwa matini ya tovuti ya Swahilihub. Mambo haya yote yalichangia pakubwa katika makadirio ya ufaafu wa tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Matini yaliyowekwa kwenye tovuti ya Swahilihub yalichangia pakubwa kuwahusisha watumiaji wengi na idadi hiyo iliimarika na kuboresha nafasi ya tovuti ya Swahilihub miongoni mwa tovuti wenza ulimwenguni (Taz. Picha 4.2,4.3 na 4.4) Hata hivyo, ni muhimu kutaja kuwa matini yanayopatikana humu ni ya miaka ya nyuma mno. 246

Mazungurnzo baina ya mtafiti na meneja wa mradi wa Swahilihub yalibaini kuwa uhifadhi wa matini ya kitambo katika Swahilihub ni suala ambalo ni la kiteknolojia na vilevile linalotokana na upungufu wa nguvu kazi. Hata hivyo, hali hii inatazamiwa

kushughulikiwa wakati tovuti hii itakapokarabatiwa ili kuwezesha kupakia data ya hivi karibuni kabisa katika tovuti ya Swahilihub,

#### 4.4.4.3 Watumiaji wa Tovuti Nyingine waliorejelea Swahilihub

Kigezo cha idadi ya tovuti zilizopendekeza matumizi ya matini kwenye tovuti ya Swahilihub pamoja na umaarufu wa tovuti hizo kilichangia kuwaridhisha watumiaji wao kuhusu ustahilifu wa tovuti ya Swahilihub. Kupendekezwa kwa matini ya tovuti ya Swahilihub ni ishara ya kuaminika na kutegemeka kwa tovuti ya Swahilihub miongoni mwa watumiaji wa tovuti zingine kote ulimwenguni. Mambo haya yote ni muhimu katika makadirio ya ufaafu wa tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Kuhusu ukubalifu wa tovuti ya Swahilihub, matokeo yalionyesha kulikuwa na takriban tovuti mia moja na sitini na tisa zilizowaelekeza watumiaji wake kurejelea matini kwenye tovuti ya Swahilihub kupata habari muhimu kuhusu maswala mbalimbali. Miongoni mwa tovuti hizo kulikuwa na tovuti mia moja na thelathini na tano zilizorejelea tovuti ya Swahilihub kila mara huku tovuti thelathini na nne zikirejelea tovuti ya Swahilihub mara moja moja tu. Idadi kubwa ya tovuti hizo zilikuwa zile zilizoangazia masuala ya elimu kwa jumla (Taz.Picha 4.52)




**Picha SURA YA NNE .48: Tovuti Zilizorejelea tovuti ya Swahilihub**

Picha 4.52 inaonyesha idadi ya kurasa zilizorejelea tovuti ya Swahilihub kuanzia mwaka wa 2014 hadi 2019. Picha hii inaonyesha idadi ndogo sana za kurasa zilizorejelea tovuti ya Swahilihub kuanzia mwaka wa 2014 hadi mwaka 2017. Idadi hii iliongezeka kuanzia 0 hadi 459,766 katika mwezi wa nne mwaka wa 2019. Kwa kuangazia matokeo haya kiwango cha upeo wa msambao kwa mujibu wa Rodgers, (2003) hakijafikiwa katika ukubalifu wa tovuti ya Swahilihub miongoni mwa watumiaji wake hasa kuanzia mwaka wa 2014 hadi mwaka wa 2017. Hata hivyo matokeo ya mwaka wa 2018 hadi 2019 yalionyesha ongezeko kubwa la idadi ya kurasa zilizorejelewa kutokana na watumiaji wengi kuhamasishwa na kuamua kuitumia tovuti ya Swahilihub. Matokeo ya uchunguzi huu wa Arhefs (Taz. Picha 4.51) yanabainisha kwamba kuna uwezekano mkubwa wa tovuti ya Swahilihub kupata watumiaji wengi kutokana na juhudi za kuhariri matini yake ili kuyakidhi mahitaji ya watumiaji wake (Taz. Picha 4.50). Juhudi kama hizi zinapowekwa zinachangia pakubwa katika kuimarisha idadi ya watumiaji wa vitengo mbalimbali vya Swahilihub kutoka kwa asilimia ndogo zilizopatikana katika utafiti huu (Taz. Chati 4.8).

Mahojiano na wasimamizi wa mradi wa Swahilihub yalibaini kuwa wanafunzi wa shahada ya uzamili na uzamifu wanatarajiwa kufaidi pakubwa kutokana na tovuti ya Swahilihub hivi karibuni. Kwa mujibu wa meneja wa Swahilihub, mazungurnzo kuhusu mradi wa kupakia iksiri na tasnifu za Kiswahili kutoka kwa vyuo vinavyofunza Kiswahili ulimwenguni yanatarajiwa kuanza hivi karibuni baada ya kuifanyia tovuti hii ukarabati. Utafiti huu uligundua kutokana na mahojiano na wasimamizi wa Swahilihub, kuwa kampuni ya Nation Media Group iliweka mikakati ya kushauriana na vyuo vikuu ili waweze kushirikiana kwa kuweka mkataba. Hata hivyo, kufikia sasa hakuna

mazungurnzo yoyote yaliyofanywa baina ya kampuni ya Nation Media Group na chuo chochote kuhusu suala hili.

Shughuli hii inatarajiwa kusaidia katika kuhifadhi kazi hizi kwa manufaa ya wasomi na watafiti wa Kiswahili. Hatua hii pia inalenga kuboresha utafiti wa Kiswahili kwani watafiti wataweza kufaharnu maeneo ambayo tayari yamefanyiwa utafiti wa Kiswahili kote ulimwenguni. Ufahamu huu utawawezesha kuzingatia tafiti zingine au labda kuboresha tafiti zilizofanywa tayari. Hali hii pia itawawezesha kupata data nyingi kuhusu yaliyoandikwa katika nyanja mbalimbali za usomi wa Kiswahili. Zaidi ya yote, watafiti wa Kiswahili wataweza kuboresha viwango vya utafiti unaofanywa katika taaluma ya Kiswahili kutokana na kulinganisha mbali na kupata data muhimu za kimsingi ili kubuni mada zao za utafiti.

Ni kutokana na juhudi hizi za wasimamizi wa tovuti ya Swahilihub kuhariri matini yake ndipo asilimia kubwa waliitikia kutumia kitengo cha Jifunze Kiswahili kwa wingi kwa kiasi cha asilimia 62.9 ya watumiaji wa tovuti ya Swahilihub. Idadi hii kubwa ya watumiaji wa kitengo hiki ilitokana na kupatikana kwa matini yaliyowafaa watumiaji hawa katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili (Taz. Picha 4.51). Ufaafu wa tovuti kiuamilifu ni kigezo muhimu katika utathmini wake kwa kuwa lengo kuu la kila tovuti ni kuhifadhi na kufikisha habari kama inavyohitajika na watumiaji wake (Hidayat, 2011; Ip, Law na Lee, 2012). Uhuru wa kuchapisha habari katika mtandao unaelezwa na Evans (2008). Aidha Evans (2008) anaeleza kuwa watu wameruhusiwa kuchapisha habari katika mtandao badala ya kuwa wasomaji. Katika tovuti, vikao vya kutuma ujumbe, mtandao wa kijamii kama vile Facebook na jukwaa kama vile Twitter vinafahamika kama vyombo vya habari vinavyozalishwa na watumiaji (Swedowsky, 2009). Matumizi ya vyombo vya habari vya kijamii hayafanani ulimwenguni kote.

Kwa mujibu wa Gavalda (2018), michango ya kampeni ya Rais Obama katika mwaka wa 2011 iliongezeka kwa asilimia 14 kutokana na kuimarishwa kwa kasi ya kupatikana kwa matini kwenye tovuti yake kwa sekunde tatu. Hali hii inadhihirisha umuhimu wa kuimarishwa kwa muda wa kupatikana kwa matini mtandaoni kama kigezo cha kuridhika kwa watumiaji wa tovuti husika. Utafiti uliofanywa na AOL iliyokadiria utendakazi wa tovuti mbalimbali ulibainisha kwamba watumiaji wa takriban asilimia 10 ya tovuti bora zaidi walisakura matini nyingi kwa asilimia 50 zaidi ikilinganishwa na watumiaji wa asilimia 10 ya tovuti zilizo katika nafasi ya chini kabisa (Wagner, 2017).

Wamalwa (2016), katika utafiti wake alifafanua kuwa tovuti ya Swahilihub ina nafasi kubwa katika kukuza taaluma ya Kiswahili katika vyombo vya habari nchini Kenya.
Hata hivyo, hakuweza kuonyesha jinsi tovuti ya Swahilihub inavyoendeleza taaluma ya Kiswahili zaidi ya matumizi yake kwenye vyombo vya habari. Utafiti huu ulibainisha vipengele muhimu vya tovuti ya Swahilihub na kuchangia pakubwa kuweka wazi maandishi kuhusu mradi wa Swahilihub, historia yake, malengo yake na changamoto zinazoukabili mradi huu wa Swahilihub.

### 4.4.4 Usambaaji wa tovuti ya Swahilihub kimaeneo.

Rodgers (2003) anafafanua viwango vya ubwiaji kama kasi ya uvumbuzi unaokubaliwa na wanajamii. Kwa mfano idadi ya watu waliotumia uvumbuzi katika kipindi fulani mahususi inaweza kutumika kupima kiasi cha ukubalifu wa uvumbuzi husika (Rodgers, 2003). Kasi ya ubwiaji wa uvumbuzi ni kigezo muhimu kilichochangia katika kupima namna ambavyo matumizi ya tovuti ya Swahilihub yalivyokubaliwa katika kuendeleza taaluma ya Kiswahili. Hali hii ilidhihirika katika uzoefu wa wataalamu katika kuvitumia vitengo mbalimbali vya tovuti ya Swahilihub pamoja na matokeo ya uchanganuzi wa

Arhefs. Katika utafiti huu, usambaaji na ukubalifu wa tovuti ya Swahilihub kama uvumbuzi mpya katika maendeleo ya taaluma ya Kiswahili kwa jumla ulizingatiwa kama kigezo muhimu katika ufanikishaji wa matumizi yake.


Kwa mujibu wa matokeo ya uchunguzi wa Arhefs kulikuwa na takriban watumiaji wa tovuti ya Swahilihub 3709 katika kipindi cha miaka mitano tangu kubuniwa kwake. Idadi hii ni ndogo sana ikilinganishwa na idadi ya watumiaji wote wa intaneti kote ulimwenguni. Kwa mujibu wa Live Stats (2018), kufikia mwezi wa Julai mwaka wa 2018, idadi ya watumiaji wa intaneti kote ulimwenguni ilikuwa takriban bilioni 3.96. Hivyo basi idadi ya watu wanaotumia tovuti ya Swahilihub ikiwa 3709 kwa kipindi cha miaka mitano ilikuwa idadi ndogo sana ikilinganishwa na idadi kubwa ya watu bilioni 3.96 ya watumiaji wote wa tovuti mbalimbali kote ulimwenguni.

Kutokana na matokeo haya, msambao wa uvumbuzi wa tovuti ya Swahilihub haujafikia kiwango cha upeo katika asilimia 75 ya ubwiaji miongoni mwa watumiaji wake. Matokeo haya yanatokana na idadi ndogo ya mitandao ya kijamii inayotumiwa ili kuwafikia watumiaji wa tovuti ya Swahilihub kwa minajili ya kupata mrejesho kutoka kwa watumiaji wake. Tovuti ya Swahilihub ina mitandao ya kijamii miwili tu inayotumiwa kupata mrejesho moja kwa moja kutoka kwa watumiaji wake. Mitandao hii ni Facebook na twitter. Idadi hii ndogo ya watumiaji wa Swahilihub kote ulimwenguni kwa kipindi cha miaka mitano ilitokana na uchache wa majukwaa mtandaoni kwa mujibu wa mrejesho kutoka kwa watumiaji wa Swahilihub uliowiana na matokeo ya utafiti wa Wamalwa (2016). Aligundua kwamba kuna haja ya kuimarisha matumizi ya majukwaa anuwai ili kupata mrejesho kamilifu kutoka kwa watumiaji wa Swahilihub mtandaoni.

Kwa mujibu wa Owoche, (2019) mitandao ya kijamii hutumiwa kwa asilimia 75 miongoni mwa watumiaji wote wa tovuti. Hii inamaanisha kwamba watumiaji wengi wa tovuti huchagua mitandao ya kijamii kwa matumizi yao. Hivyo basi tovuti ya Swahilihub inastahili kuimarisha mitagusano miongoni mwa watumiaji wake kwa kujenga msingi madhubuti wa matumizi wa aina mbalimbali za mitandao ya kijamii na kuimarisha viwango vya mrejesho wa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub.

Kwa mujibu wa matokeo ya utafitii wa awali (Wamalwa, 2016), teknolojia ya kimtandao ni uvumbuzi usioweza kupingika au kuzuiliwa kusambaa ' miongoni mwa wanajamii. Usambaaji wa tovuti ya Swahilihub unategemea mikakati ya kuwahamasisha wanajamii kuhusu kuwepo kwa teknolojia hii. Suala la uhamasisho kuhusu tovuti ya Swahilihub ni muhimu katika kuimarisha usambaaji wake miongoni mwa watumiaji wake mtandaoni. Sawa na utafiti huu matokeo ya utafiti wa Wamalwa, (2016) yalibainisha kwamba pana haja ya wadau mbalimbali wa Kiswahili kufafanuliwa kuhusu umuhimu wa kuturnia tovuti za Kiswahili kama vile Swahilihub ili wafahamu na kuikubali teknolojia hii.

Isitoshe, mbali na kutumia magazeti, redio na runinga katika kunadi kuwepo kwa tovuti ya Swahilihub, wasimamizi wa mradi huu wanafaa kuzingatia makongamano na matumizi ya mitandao ya kijamii katika kufanikisha juhudi hizi. Mbinu hizi mbili, yaani, makongamano na matumizi ya mitandao ya kijamii zinaonekana kuwa na uwezo wa kuwafikia watu wengi kwa wepesi





**VITAMBULISHO MAHUSUSI VYA TOVUTI**

| | | |
|---|---|---|
| .com | 133 | 80% |
| .org | 6 | 3% |
| .tz | 5 | 3% |
| .ke | 3 | 1% |
| .net | 3 | 1% |
| .info | 2 | 1% |
| .biz | 1 | <1% |
| .club | 1 | <1% |
| .edu | 1 | <1% |
| .gr | 1 | <1% |
| .pk | 1 | <1% |
| .ru | 1 | <1% |
| .show | 1 | <1% |
| .top | 1 | <1% |
| .ua | 1 | <1% |




**Picha SURA YA NNE .49: Urejeleaji wa Matini ya tovuti ya Swahilihub Kimaeneo.**


Idadi ya watumiaji waliofaidika kwa kutumia tovuti ya Swahilihub ilikuwa takriban watu elfu tatu mia saba na tisa kuanzia kubuniwa kwake hadi wakati wa utafiti huu. Idadi hii ya watumiaji imesambaa kwa njia tofauti kote ulimwenguni. Picha ya 10 ilibainisha upatikanaji na matumizi ya matini ya tovuti ya Swahilihub kimaeneo.




*Picha SURA YA NNE .50: Urejeleaji zaidi wa Matini ya Swahilihub Kimaeneo.*

Tovuti ya Swahilihub hurejelewa zaidi katika nchi ya Tanzania kwa asilimia 60.4 ikifuatiwa na nchi ya Kenya kwa asilimia 28.5 ikifuatwa kwa karibu na Marekani Kaskazini, Ujerumani na mataifa mengine ya Ulaya kwa asilimia 11.1 (38) iliyosalia. Mataifa mengi ya ughaibuni yanayotumia tovuti ya Swahilihub yamekuwa na uhusiano wa kiutawala na nchi za Afrika Mashariki zinazozungumza lugha ya Kiswahili. Maeneo yaliyokolezwa rangi ya samawati zaidi yana watumiaji wengi wa tovuti ya Swahilihub. Kwa mujibu wa chati 2, mtiririko wa matini zilizorejelewa kwenye tovuti ya Swahilihub umebainishwa kwa kuangazia urejeleaji huo kila mwaka kuanzia mwaka wa 2016 hadi 2018. Hivyo basi, katika chati ya 2, matumizi ya tovuti ya Swahilihub yamebainishwa katika vipindi maalum katika mwezi wa

Januari, Juni na Disemba kila mwaka kwa kipindi cha kati ya mwaka wa 2016 hadi 2018 (Taz. Chati 4.1).




*Picha SURA YA NNE .51: Matumizi ya tovuti ya Swahilihub*

Matokeo katika utafiti huu yalionyesha kuwa katika mwaka wa 2016 ni takriban kurasa 250 zilizorejelewa huku idadi hiyo ikiongezeka katika mwaka wa 2017 hadi 1540. Idadi

hii iliongezeka katika mwaka uliofutia wa 2018 hadi kurasa 1650. Hakukuwa na matokeo yoyote ya uchunguzi huu kati ya mwaka wa 2012 hadi 2015. Hali hii ilitokana na uwezekano kwamba kulikuwa na kipindi cha utasa cha uratibu na ukarabati wa jukwaa hili la Swahilihub. Hatua ya kwanza katika mchakato wa msambao wa tovuti ya Swahilihub ni ile ya uhamasisho kuhusu uwepo na umuhimu wake. Katika kipindi hiki cha utasa, watumiaji wa tovuti ya Swahilihub walikuwa tu wamegundua uwepo wake na kujaribu kubaini ina manufaa gani, kwa nini ipo na hufanya kazi kwa njia gani. Katika miaka ya kwanza ya matumizi ya tovuti ya Swahilihub kulikuwa na watumiaji wachache kwa sababu huo ndio wakati watumiaji wake walikuwa wakitambua uwepo wa tovuti ya Swahilihub na kujifunza jinsi ya kuutumia uvumbuzi huu na hatimaye kujifunza kanuni zilizoongoza katika utendakazi wa tovuti ya Swahilihub. Kwa mujibu wa matokeo ya Arhefs, uwezekano wa kuchunguza kurasa zilizorejelewa kwenye mtandao wa Swahilihub ulibainika tu kuanzia mwaka wa 2016 wala sio miaka iliyotangulia.

## 4.5 Changamoto za Matumizi ya Swahilihub katika Ukuzaji wa Kiswahili

Madhumuni ya tatu ya utafiti huu yalikuwa kupambanua changamoto za matumizi ya tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili nchini Kenya. Utafiti huu ulikusudia kubaini changamoto za matumizi ya Swahilihub katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili kimatini na kimuundo miongoni mwa watumiaji wake. Matokeo ya tathmnini hii yalitokana na uchunguzi wa kiteknoljia wa Arhefs. Adiha utafiti huu pia uligundua kwamba kuna changamoto za matumizi ya Swahilihub kuendeleza taaluma ya Kiswahili sawa na matokeo ya utafiti wa Jagero, Mohochi na Indede (2013) uliojadili kuhusu matumizi ya Kiswahili katika matini ya Blogu na athari zake katika ukuaji wa lugha ya Kiswahili. Kwa kutumia nadharia ya Uchambuzi Usemi Jadilifu. walibaini kuwa washiriki

wa Blogu wanatumia vifupisho, maneno yasiyo sanifu, sarufi isio sahihi, kuchanganya misimbo, ubadilishaji misimbo na matumizi ya tahajia yasiyo sahihi.

Hivyo kuwa na athari chanya na hasi katika ukuaji wa lugha ya Kiswahili. Tovuti ya Swahilihub pia ilikumbwa na athari hasi na chanya kutokana na matumizi ya matini yake katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili.

Mwamko wa kutumia Swahilihub nchini Kenya bado hauridhishi, hivyo kutishia suala zima la ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili. Kisababishi mara nyingi huwa ni ukosefu wa fedha na kwa kiasi mapuuza. Kwa ufupi utafiti huu umefichua kwamba kuna nduni zifuatazo kuhusiana na matumizi ya Swahilihub katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili nazo ni ukosefu, upungufu na kutotumiwa ipasavyo kwa tovuti ya Swahilihub.

**Jedwali SURA YA NNE .6: Changamoto katika matumizi ya Swahilihub**

| Changamoto | Idadi | Asilimia | Asilimia Jumlifi |
|---|---|---|---|
| gharama na miundo msingi | 30 | 9.9 | 9.9 |
| Haikuitikiwa | 95 | 31.3 | 41.1 |
| istilahi na tafsiri | 37 | 12.2 | 53.3 |
| Kutokuweko kwa lugha-ishara kwenye Swahilihub | 8 | 2.6 | 55.9 |
| miundo msingi | 5 | 1.6 | 57.6 |
| tovuti wenza | 11 | 3.6 | 61.2 |
| ufaafu na ukamilifu wa matini | 51 | 16.8 | 78.0 |
| ugumu wa kimatumizi | 67 | 22.0 | 100.0 |
| Total | 304 | 100.0 | |

### 4.5.1 Gharama na miundombinu

Mojawapo ya changamoto zinazokumba matumizi ya Swahilihub katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili ni ufinyu wa bajeti za watumiaji na taasisi husika. Kuhusu gharama na ukosefu wa miundo msingi, iligunduliwa kwamba ni 9.9% ya watumiaji walikiri kwamba Swahilihub haipatikani kwa sababu ya gharama kubwa sana na ukosefu wa miundo msingi mwafaka. Ukosefu wa fedha za kutosha katika ununuzi na urekebishaji wa vyombo vya mradi wa Swahilihub ni changamoto kubwa inayokabili matumizi yake katika ukuzaji wa taaluma ya kiswahili nchini Kenya.

Moraa (2012) anatambua katika utafiti wake kuwa pamekuwa na changamoto kubwa ya kuwekeza na kufadhili miradi ya kiteknolojia ya Kiswahili. Hali hii inatokana na wawekezaji hawa pamoja na wafadhili kuwa na uoga wa ikiwa miradi hiyo itazalisha faida. Mataifa tajiri na yenye kumiliki teknolojia ulimwenguni yanaunga mkono teknolojia za lugha ya Kiingereza, Kifaransa miongoni mwa lugha zingine za Ughaibuni katika kuendeleza utandawazi. Hali hii inatokana na dhana hasi kuwa Kiswahili si lugha inayoweza kuzalisha faida .iwapo teknolojia yoyote ile inaweza kuwekezwa ndani yake. Udhaifu huu unaifanya lugha ya Kiswahili kuendelea kulemewa na upinzani wa lugha za kigeni na kuzuka kwa Sheng' hasa nchini Kenya.

Aidha katika vyuo mbalimbali nchini Kenya, maswala yanayopewa kipaumbele katika makadirio ya fedha za matumizi katika shughuli za kielimu ni ujenzi wa madarasa, ununuzi wa vifaa vingine bila kukipa kitengo cha teknolojia kiwango cha fedha cha kutosha. Pamoja na mambo mengine, katika baadhi ya vyuo nchini Kenya, vyombo vya kiteknolojia vipo katika viwango duni kitaalamu, hivyo kuwakatisha tamaa watumiaji Swahilihub. Uchakavu wa tarakilishi katika baadhi ya vyuo na vituo vya intaneti ni jambo linaloendelea kudumaza matumizi ya Swahilihub katika ukuzaji wa taaluma ya kiswahili.

Hivyo basi msukumo wa ziada unahitajika ili kuwahimiza wataalamu,wanafunzi na walimu kutilia mkazo matumizi ya Swahilihub kuendeleza taaluma ya kiswahili. Aidha changamoto nyingine ni usambaaji finyu na upatikanaji wa Swahilihub miongoni mwa watumiaji wa mitandao nchini Kenya. Isitoshe, jambo la kusikitisha ni kuwa upatikanaji wa miundo misingi ya Swahilihub unadhihiri katika sehemu za mijini huku zile sehemu za vijijini zikikosa miundo misingi hii muhimu. Ni lazima kuwe na nia ya dhati ya

kuhakikisha upatikanaji wake unawafikia wadau wote kwa muda na gharama nafuu. Swahilihub haiwezi kuwa na maana sana kama misingi yake itakuwa baadhi ya sehemu za nchi pekee. Jambo linalodhihirika ni kwamba Swahilihub haikupatikana kwa wingi katika sehemu nyingi nchini kenya. Huenda hali hii imechangiwa na ukosefu wa miundo msingi, jambo linalotatiza matumizi ya Swahilihub.

Licha ya majibu ambayo mtafiti alipata kupitia kwa usaili, alifanya uchunzaji nyanjani ambao ulifichua namna ambavyo wadau wengi hutumia vitengo mbalimbali vya Swahilihub ili kuendeleza taaluma ya Kiswahili. Swahilihub itakuwa na maana zaidi, kama ina uwezo wa kuvunja vigingi vya matatizo ya usafiri na umbali, kwa kuwaunganisha watumiaji wa vijijini na mijini na kuwafanya washirikiane katika shughuli mbalimbali, ikiwemo matumizi ya Swahilihub katika ukuzwaji wa taaluma ya Kiswahili.

### 4.5.2 Matumizi ya istilahi.

Istilahi geni na tafsiri tata ni miongoni mwa changamoto zinazokumba matumizi ya Swahilihub katika ukuzwaji wa taaluma ya Kiswahili. Iligunduliwa kwamba ni 12.2% ya watumiaji waliokiri kwamba hutatizika sana wanapotumia Swahilihub kwa sababu ya matumizi ya istilahi geni na tafsiri tata. Jambo hili ni changamoto kubwa inayokabili matumizi ya Swahilihub katika ukuzwaji wa taaluma ya kiswahili nchini Kenya. Ukosefu wa chornbo maalumu cha kushirikisha, kuongoza na kuratibu uundaji wa istilahi za kiteknolojia kwa Kiswahili ni changamoto kubwa sana. Swahilihub kikiwa chombo kinachotumia Kiswahili, kinahitaji misamiati ya kimtandao ya kukiwezesha katika uwasilishaji wa taarifa za habari za Kiswahili. Changamoto hii ni kikwazo kikubwa kwa mratibu wa taarifa katika tovuti ya Swahilihub hasa anapokuwa anapakia taarifa zenyewe ambazo zinahitaji kupakiwa kwa Kiswahili.

Ni muhimu pawepo na chombo maalum cha kushughulikia msamiati wa kiteknolojia badala ya kuwa na watu pamoja na makundi ya binafsi yanayoshughulikia uundaji wa istilahi hizi. Matokeo ya hali hii ni kuundwa kwa istilahi nyingi ambazo zinaeleza dhana moja. Jambo hili linavuruga dhamira msingi ya harakati za kukuza Kiswahili kwa kutumia tovuti ya Swahilihub mtandaoni. Baadhi ya misamiati inayotumika katika kutaja baadhi ya teknolojia zinazohusishwa na tovuti ni migumu sana. Kufikia sasa, bado hatuna jina la Kiswahili lenye kurejelea mitandao ya kijamii kama vile Twitter, Facebook, Instagram miongoni mwa misamiati mingine ya kiteknolojia. Ugumu wa misamiati hii ni hatari katika mawasiliano hasa ya kiteknolojia kwani huenda baadhi ya misamiati hiyo ikatumika bila ufahamu wa watumiaji. Kutokana na hali hii, watumiaji hawa wanaweza kukosa baadhi ya taarifa muhimu.

### 4.5.3 Uchache wa wataalamu

Kizingiti kingine ni uchache wa wataalamu wa lugha ya Kiswahili ambao pia wana ujuzi wa masuala ya kiteknolojia. Kwa sasa, wengi wa wataalamu wanaotumika huwa ni nguli wa ubapa mmoja. Wengi wao wameisomea teknolojia lakini hawafahamu narnna ya kutumia teknolojia hiyo kwa lugha ya Kiswahili. Hali hii inalemaza juhudi za kuikweza lugha ya Kiswahili katika jukwaa la utandwazi kwa ukamilifu. Mahojiano yet una wasimamizi wa mradi wa Swahilihub yalibaini kuwa upungufu wa nguvu-kazi hasa wa wahariri ni changamoto kubwa mno. Wafanyakazi waliopo sasa ' hawawezi kuhariri na kupakia taarifa kwenye tovuti hii kwa ukamilifu kutokana na uchache wao.

Swahilihub inahitaji waratibu na wahariri wengi ikilinganishwa na ilivyo sasa.kwani kwa sasa mradi huu una wafanyakazi watatu pekee yao. Hili linaifanya tovuti hii kutoweza kutimiza malengo yake katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kama ilivyokusudiwa.

Mradi huu unahitaji wanahabari wa kukusanya taarifa, wataalamu na watafiti wa Kiswahili kufanikisha masuala ya usomi katika tovuti hii, wanateknolojia wa kuikarabati tovuti hii kila mara ili iweze kukidhi mahitaji ya watumiaji mbali na kuwa na wahariri wa kusanifisha chochote kinachopakiwa humu.

### 4.5.4 Ukosefu wa Lugha-Ishara na tafsiri

Aidha, miongoni mwa changamoto za matumizi ya Swahilihub katika ukuzwaji wa taaluma ya Kiswahili ni ukosefu wa lugha-ishara katika tovuti ya Swahilihub. Wengi walioshiriki katika utafiti huu walitaja ukosefu wa lugha ishara kama changamoto inayowakabili watumiaji wa Swahilihub. Kuhusu mikakati ya kuboresha matumizi ya tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili, watafitiwa walipendekeza mikakati anuwai pamoja na kuboresha matini husika, kuimarisha utendakazi wa vitengo mbalimbali vya Swahilihub, kuweka mikakati ya kuboresha miundo msingi ya kuhusisha maswala ibuka katika tovuti ya Swahilihub, kupanua mawanda ya matumizi ya tovuti ya Swahilihub, kutumia Swahilihub kufundishia darasani na kuweka mikakati faafu ya kuhamasisha matumizi ya tovuti ya Swahilihub kwa wadau wengi wa taaluma ya Kiswahili.

### 4.5.5. Uchangamano wa Kimuundo wa Swahilihub

Ugumu wa kimatumizi wa tovuti ya Swahilihub ulidhihirika miongoni mwa 22.0 ya watafitiwa kama mojawapo ya changamoto zinazokumba matumizi ya Swahilihub katika ukuzwaji wa taaluma ya Kiswahili. Uchunzaji wa tovuti ya Swahilihub uliuwezesha utafiti huu kubaini kuwa uumbaji wa tovuti ya Swahilihihub haujakamilika kama inavyohitajika. Vitengo kama vile Huduma ya Tafsiri, Jifunze

Kiswahili, Maktabani Jisomee havijakarnilika karna. Mataokeo ya mahojiano baina ya Meneja wa mradi huu yanabaini kuwa bado tovuti ya Swahilihub haijakamilika katika uumbaji wake japo kampuni ya NMG inaweka mikakati ya kuikarabati tovuti hii ili iweze kukidhi mahitaji yote kama ilivyokuwa imeratibiwa awali. Isitoshe, motokeo ya mahojiano hayo yanaonyesha kuwa hii ilikuwa awamu ya kwanza kwanza ya uratibu wa tovuti hii na hivyo basi inahitaji kuchunguzwa upya na kuikarabati ili ikidhi mahitaji yote ya watumiaji wake. Hivyo basi, tovuti ya Swahilihub inahitaji kukarabatiwa ili iweze kukidhi mahitaji ya wapokezi kikamilifu.

Uvumbuzi wo wote unapochukuliwa kuwa changamano na ngumu kutumia inakuwa vigumu kukubaliwa na kutumiwa na wanajamii Rodgers, (2003). Martin, (2003) anasisitiza kwamba ni rahisi kwa uvumbuzi kukubaliwa na kutumiwa na wabwiaji wengi iwapo matumizi ya mashine yanayohusika ni sahili na rahisi kuelewa. Watumiaji wengi wa Swahilihub walikiri kwamba ugumu wa kimatumizi ya Swahilihub ni miongoni mwa mambo yaliyochangia wengi wao kusitasita au kukataa kuisimamia. Hali hii ni changamoto kubwa inayokabili matumizi ya Swahilihub katika uendelezwaji wa taaluma ya Kiswahili nchini Kenya. Katika vyuo mbalimbali nchini Kenya, wahojiwa wengi 22.0 (74) walitaja ugumu wa kimatumizi ya tovuti ya Swahilihub kama changamoto kubwa sana katika matumizi yake kuendeleza taaluma ya Kiswahili. Watumiaji wa tovuti ya Swahilihub waliokiri kutotumia kitengo cha mwanzo walitaja uchangamano wake kama sababu kuu. Machukulio yao kuhusu ugumu wa kuelewa matumizi ya kitengo cha Mwanzo yalichangia matokeo ya matumizi yake kwa kiwango cha chini. Uvumbuzi wowote unapochukuliwa kuwa changamano na mgumu kutumia inakuwa vigumu kukubaliwa na kutumiwa na wanajamii Rodgers, (2003). Matokeo ya utafiti huu yalibaini kuwa kiwango cha uwiano wa kitengo cha Mwanzo kilikuwa chini miongoni mwa

watumiaji wa tovuti ya Swahilihub kutokana na namna kitengo hiki kilivyochukuliwa kutoingiliana na hali, maadili na mazoea yao katika shughuli zao za awali na michakato yao mitandaoni. Ili kufanikisha msambao wa uvumbuzi, uwiano huchangia pakubwa.

IIi kuwezesha kupakua taarifa yoyote kutoka kwenye tovuti ya Swahilihub ama kwa njia ya maandishi, picha, video au mbinu mseto, sharti mtumiaji awe na mjazo katika kadi ya simu itakayomwezesha kusakura mtandao hasa yule anayetumia sirnu ya mkono. Usimamizi wa tovuti hii unahitaji nguvu kazi ya kiwango cha juu. Sharti pawe na wasimamizi mbalimbali wa miradi tofautitofauti inayoendeshwa na tovuti husika. Panahitajika wahariri wa kuzipiga msasa habari na vipindi vinavyorushwa hewani, maafisa wa mauzo pamoja na wale wanaozitafuta habari hizo na kuzipakia. Hali hii ndiyo imechangia pakubwa kwa tovuti ya Swahilihub kutoweza kufanikiwa kikamilifu katika juhudi zake.


**4.5.6. Tovuti nyingine na Lugha ya mawasiliano**

Aidha, 3.6% ya watumiaji wa Swahilihub walikiri kwamba lugha ni kikwazo kikubwa katika matumizi faafu ya Swahilihub katika ukuzwaji wa taaluma ya Kiswahili. Ingawa wadau wengi wana mwamko wa kutumia Swahilihub, bado lugha ya mawasiliano kwenye Swahilihub ni tatizo kubwa. Hii ni kwa sababu makala mengine ya Swahilihub yameandikwa kwa lugha zingine ambazo siyo Kiswahili, hivyo kuifanya Swahilihub kutokuwa na manufaa kwa wataalamu, walimu, wanafunzi pamoja na washika dau wengine nchini Kenya. Aidha uteuzi wa tovuti ya kuendeleza taaluma ya kiswahili ni changamoto inayokabili matumizi ya Swahilihub. Hali hii inatishia matumizi ya Swahilihub kama tovuti ya kuendeleza taaluma ya kiswahili. Isitoshe

tovuti wenza zinazotumia lugha ya Kiswahili kama vile mwananchi.com na mtanzania.com ni majukwaa ya kimtandao yanayotumia Kiswahili na kurejelewa na watumiaji wengi wa lugha ya Kiswahili kuliko Swahilihub.

### 4.6 Mustakabali wa Swahilihub katika Ukuzaji wa Kiswahili


Utafiti huu ulikusudia kujadili mustakabali wa tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili. Utafiti huu ulibaini kwamba mradi wa Swahilihub una mustakabali mwafaka kutokana na maendeleo na mabadiliko yanayotokea katika mitandao kote ulimwenguni. Aidha, mabadiliko haya yanayotokea kila mara kwenye matini ya mradi wa Swahilihub ni jambo ambalo linazidi kutoa mchango mkubwa katika kuimarisha na umaarufu wake mtandaoni.




**Chati SURA YA NNE .10: Mikakati ya Ukuzaji wa Kiswahili kwenye Swahilihub**

Chati 4.10, inaonyesha sababu mbalimbali walizotoa watafitiwa za kuwafanya wasiitumie tovuti ya Swahilihub kuendeleza taaluma ya Kiswahili. Sababu hizi ndizo pia zilizokuwa

hoja walizotoa kama mapendekezo ya kuboresha tovuti ya Swahilihub kuendeleza taaluma ya Kiswahili. Asilimia 61.2 (208) ya watafitiwa walitaja kwamba tovuti ya Swahilihub haifikii malengo yake kwa sababu ya thamani ya chini ya matini inayohifadhiwa kwenye tovuti ya Swahilihub. Hivyo basi wahudumu wa Swahilihub wanastahili kuboresha matini husika kwenye tovuti ya Swahilihub. Asilimia 14.3 (48) ya watafitiwa walikiri kwamba uratibu wa vitengo mbalimbali vya Swahilihub vinastahili kuboreshwa. Asilimia 2.0(7) ya watafitiwa walikiri kutotumia Swahilihub kwa kukosa baadhi ya miundo msingi ya Ki-Swahilihub ambayo huchangia kuimarisha matumizi ya tovuti ya Swahilihub. Asilimia 6.2(21) ya watafitiwa walikiri kutotumia Swahilihub kwa sababu ya mawanda finyu matini ya Ki-Swahilihub ambayo huchangia kuimarisha matumizi ya tovuti ya Swahilihub. Baadhi ya mambo yanayojitokeza katika tovuti ya Swahilihub yalikuwa ya kimatumbuizo na hivyo basi kuna haja ya kupanua mawanda ya kimatumizi ya tovuti ya Swahilihub. Asilimia 6.2 (21) ya watafitiwa walikiri kutotumia Swahilihub kwa sababu ya kutotumiwa kufundishia vipengele mbalimbali vya lugha ya Kiswahili. Hivyo basi ni vyema wanazuoni waitumie tovuti ya Swahilihub kufundishia lugha ya Kiswahili. Asilimia 4.1 (13) ya watafitiwa wanapendekeza kwamba ni muhimu kuhamasisha matumizi ya Swahilihub miongoni mwa wadau wote wa taaluma ya Kiswahili.




*Chati SURA YA NNE .11: Swahilihub katika Ukuzaji wa Kiswahili*


Ili kuwezesha ukubalifu wa Swahilihub katika jamii, ni muhimu kuhakikisha kwamba manufaa yake kwa watumiaji wake yanadhihirika, uwiano, usahili katika matumizi yake na uwezo wa idhibati ya ubora wake kubainika miongoni mwa watumiaji wake miongoni mwa wataalam wa Kiswahili. Tafiti za awali zimeonyesha kwamba vigezo hivi ni muhimu sana katika kuwawezesha walimu, wahadhiri na wadau wote katika elimu kukubali kubwia na kutumia majukwaa ya mitandao kufundishia na kuimarisha utendakazi wao

( Parisot, 1997; (Anderson, Varnhagen, & Campbell, 1998) Anderson, 1998; Slyke, 1998; Surendra, 2001; Bennett&Bennett, 2003; na Owino, 2011)

Utafiti huu ulifichua kwamba ingawa kuna changamoto nyingi zinazokabili tovuti ya Swahilihub, kuna matumaini ya kuiboresha na kuifanya kuwa faafu zaidi kwa watumiaji wake. Miongoni mwa hoja muhimu zilizotolewa kuhusu mustakabali wa Swahilihub ni kwamba tovuti hii inaweza kuboresha, kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili pamoja na

kuimarisha utafiti miongoni mwa wataalamu wa Kiswahili. Hoja hizi zimejitokeza zaidi katika chati 4.15 ifuatavyo:

## 4.7 Mustakabali wa Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili




*Chati SURA YA NNE .12: Mustakabali wa Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili*

Utafiti huu uligundua kwamba asilimia 10.86 ya watumiaji wa Swahilihub wanatazamia tovuti hii kuchangia kuboresha lugha ya Kiswahili kwa njia nyingi. Mikakati ya kuiboresha lugha ya kiswahili hususan uimarishaji na ukuzaji wa lugha ya Kiswahili.

Aidha watumiaji hawa walikiri kwamba Swahilihub inaweza kuimarisha taaluma ya Kiswahili kupitia ufundishaji na ujifunzaji darasani vyuoni na shuleni. Vitengo vya Swahilihub kama vile maktaba jisomee na jifunze Kiswahili vinaweza kutumiwa

kuboresha matumizi ya lugha ya Kiswahili miongoni mwa wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili.

Asilimia 13. 49 (46) ya walioshiriki katika utafiti huu walisema kuwa Swahilihub inaweza kutumiwa kueneza lugha ya Kiswahili miongoni mwa watu wasioijua lugha ya kiswahili. Vitego kama vile jifunze Kiswahili, maktaba jisomee, video na blogu na ukumbi vinaweza kuchangia kueneza lugha ya Kiswahili miongoni mwa watumiaji wapya wa lugha ya Kiswahili.

Asilimia 13.16 (45) ya walioshiriki katika utafiti huu walisema kuwa Swahilihub inaweza kutumiwa kukuza lugha ya Kiswahili miongoni mwa wadau wa taaluma ya kiswahili. Uhifadhi wa matini mbalimbali pamoja na picha, na video huchangia pakubwa kujenga ghala la matini ambalo huchangia kujenga na kuhifadhi taaluma ya kiswahilli. Isitoshe vitengo kama vile jifunze Kiswahili, maktaba jisomee, video na blogu na ukumbi vinaweza kuchangia kueneza lugha ya Kiswahili miongoni mwa watumiaji wa lugha ya Kiswahili kwa kuendesha tafiti anuwai kuhusu taaluma ya kiswahili. Asilimia 3.68 (12) ya walioshiriki katika utafiti huu walisema kuwa Swahilihub inaweza kutumiwa kukuza lugha ya Kiswahili miongoni mwa wadau wa taaluma ya Kiswahili kupitia kwa tafiti mbalimbali za kitaaluma.

### 4.7.1 Matumizi duni ya matini ya tovuti ya Swahilihub

Utafiti huu aidha ulifichua kwamba 16.8 (57) ya watafitiwa walikiri kwamba japo baadhi ya matini zilipatikana katika tovuti ya Swahilihub hazikuwiana na viwango faafu kitaaluma. Matini zingine hazikutumiwa katika kuendeleza taaluma ya kiswahili lakini zilitumiwa kwa kazi na shughuli zingine tu kama burudani, muziki miongoni mwa shughuli zingine. Kuna haja kubwa ya kuwaelekeza wadau kuhusiana na matumizi

mwafaka ya Swahilihub katika ukuzaji wa taaaluma ya kiswahili. Wadau wengi watumiao Swahilihub, huchukulia makala zote kuwa za kiwango cha kitaaluma huku ukweli ni kwamba baadhi ya makala kwenye tovuti ya Swahilihub hazikidhi viwango vinavyostahiki. Vile vile, wadau wengine wanaomiliki simu na teknolojia nyingine za mawasiliano, wanafanya hivyo kwa sababu vifaa hivyo huongeza hadhi ya mmiliki katika jamii na kutoa mwonekano wa kisasa kwa mtumiaji wa Swahilihub.

### 4.7.2 Mkabala wa tathmini ya tovuti za ukuzaji wa lugha

Mihimili ya nadharia ya Msambao wa Uvumbuzi, yaani uvumbuzi, vyombo vya mawasiliano na mitagusano ya kijamii,muda wa msambao, na michakato ya msambao wa uvumbuzi imefanikisha tathmni ya mradi wa Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Mihimili hii imewezesha kujadili umuhimu wa tovuti ya Swahilihub kwa watumiaji wake. Kwa mfano, kuna baadhi ya watumiaji wa Swahilihub wanaoturnia tovuti hii kupata habari huku wengine wakijinufaisha na burudani miongoni mwa faida zingine. Aidha, mihimili hii iliiwezesha sura hii vilevile kufafanua sababu ya watumiaji kuchagua na kutumia Swahilihub kutokana na narnna inavyokidhi mahitaji yao.

Hata hivyo nadharia hii ilikuwa na udhaifu wake ambao utafiti huu ulikusudia kuboresha kwa kubuni mkabala mpya. Kutokana na matokeo ya utafiti huu kuna haja ya kuangazia upya nadharia zinazohusu teknolojia kwa Kiswahili. Hali hii inahitaji nadharia za kufanikisha ufafanuzi wa masuala muhimu ya kiusomi kwa kuzingatia utendakazi wa mihimili ya nadharia hizo kama ilivyo katika nyanja zingine za Kiswahili kama vile sarufi na fasihi. Kwa kufanya hivi, tutapunguza hali ya kutafsiri nadharia hizi kutoka kwa lugha za kigeni kabla ya kuzitumikiza. Hili litawezesha uchambuzi na uhakiki wa baadhi ya teknolojia zinazovumbuliwa kwa sasa na kwa siku za baadaye kwa urahisi.

Katika kuangazia mustakabali wa tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili, utafiti huu ulikusudia kubuni mkabala bora wa tathmini ya tovuti za ukuzaji wa lugha ili kutoa mchango wake katika kukidhi haja ya kuboresha nadharia za kiteknolojia katika taaluma ya Kiswahili. Hii ilitokana na changamoto zilizojitokeza katika utafiti huu kuhusu namna ya kuchanganua na kutathmini tovuti ya Swahilihub kwa misingi ya nadharia na mikabala iliyopo.

Mkabala ni wakilisho la sehemu zote za au baadhi tu ya sehemu za mfumo mahususi unaobuniwa kusaidia katika kuelewa mfumo huo. Mkabala ni miundo mbinu ya uchanganuzi wa mfumo mahususi. Mkabala unahusisha wakilisho sahili la hali halisi katika mfumo maalumu. Mkabala mara nyingi hutumiwa na waamuzi kufanya maamuzi muhimu kwa kutegemea vigezo fulani maalumu (Bhattacherjee, 2012). Haja ya kubuni na kuboresha mkabala wa tathmini ya tovuti ilitokana na matokeo ya tathmini ya tovuti ya Swahilihub yaliyotokana na uchunguzi wa kiteknolojia wa ARhefs. Ujio wa intaneti umebadili namna asasi mbalimbali zinavyoendeleza shughuli zake na kuwasiliana na wadau anuai.

Sehemu hii iliangazia data iliyokusanywa nyanjani na iliyokuwa mwafaka katika kubuni mkabala bora wa tathmini ya tovuti mbalimbali za ukuzaji wa lugha. Lengo la sehemu hii lilikuwa kupendekeza na kubuni mkabala bora wa tathmini ya tovuti katika ukuzaji wa lugha. Mkabala huu wa tathmini ya tovuti ulibuniwa kutokana na data iliyokusanywa kwa msaada wa hojaji, usaili, majadiliano na uchunzaji. Data kutokana na hojaji ya tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili ilichangia katika kuzua majumui yaliyobuni na kuboresha mkabala wa tathmini ya tovuti za ukuzaji wa lugha.

Matokeo ya utafiti huu yalizua haja ya kuboresha nadharia ya msambao wa uvumbuzi kwa kubuni mkabala bora kutokana na data ya msambao wa
tovuti ya Swahilihub.


Hivyo basi, utafiti huu ulinuia kubuni na kuboresha mkabala wa tathmini ya tovuti katika usambaaji, ubwiaji, ukubalifu na ustahilifu wa tovuti katika ukuzaji wa lugha. Kuna njia nyingi za mawasiliano zikiwa pamoja na barua pepe, majukwaa ya kijamii na tovuti anuwai. Miongoni mwa majukwaa haya, tovuti ndilo jukwaa linalotumiwa zaidi na asasi anuwai katika mitagusano na wadau mitandaoni. Hali hii imetokana na uwezo mkubwa wa tovuti kuwafikia wadau wengi mtandaoni.

Hata hivyo anavyodahili Owoche, (2019), kuwepo na tovuti pekee sio hakikisho la ufanisi kwenye mtandao bali pia panahitajika mchakato wa tathmini yake kila mara. Tathmini kama hii ya kila mara itaendana na mabadiliko ya kiteknolojia yanayotokea kila wakati katika jamii. Haja ya kubuni na kuboresha mkabala wa tathmini ya tovuti ilitokana na matokeo ya tathmini ya tovuti ya Swahilihub yaliyotokana na uchunguzi wa kiteknolojia wa Arhefs. Program anuwai za teknolojia za tathmini ya tovuti hazizingatiwi katika mitindo mipya ya tathmini za tovuti mtandaoni. Mkabala mpya wa tathmini ya tovuti ulibuniwa kutokana na matokeo ya utafiti huu na kwa kuhusisha teknolojia mpya zinazojiri. Mkabala wa tathmini ya tovuti ni muhimu katika kubaini namna ambavyo na kwa kiasi ambacho majukwaa ya mtandaoni, matini na viwango vya matumizi ya tovuti yanavyochangia katika kueneza dhana fulani mtandaoni.


Kubuniwa kwa mkabala katika utafiti huu ilikuwa muhimu kama njia mwafaka ya utafiti huu kuchangia katika kuhusisha hali halisi katika jamii katika mchakato wa tathmini ya tovuti mtandaoni. Kwa msaada wa mkabala, utafiti unaweza kubashiri, kupima na

kutambua mifumo changamano au matukio maalum. Mikabala ni muhimu sana katika shughuli za watafiti kwa michakato ya utafiti na kuwasilisha matokeo ya tafiti hizo. Mikabala husaidia katika kupima na kuelewa masuala changamano katika mifumo ya kijamii kwa kuhusisha mchakato mzima wa utafiti na jamii.

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, tulibuni na kuboresha mkabala wa kithamani. Matokeo ya utafiti huu yalibainisha kwamba nafasi ya Swahilihub miongoni mwa tovuti nyingine ilikuwa duni kwa nafasi ya milioni mbili nukta nne kwa idadi ya bilioni moja nukta tisa. Idadi ya watumiaji wa tovuti ya Swahilihub ilitegemea kiwango cha ubora na utendakazi wake. Utendakazi huu wa tovuti ni dhana inayorejelea kasi au ule muda unaochukuliwa na tovuti kuwasilisha matini kwa mtumiaji. Huu ni muda unaokadiria ubora wa tovuti kwa kuonyesha wakati wa kuingia kwa mtumiaji kwa tovuti anapotafuta habari na wakati habari na matini muhimu anayoitafuta inapowasilishwa na kukabidhiwa mtumiaji huyu mtandaoni.




**Mchoro SURA YA NNE .3: Mkabala wa Rodgers(2003)**




**Mchoro SURA YA NNE .4: Mkabala Mpya (2024)**

Utendakazi wa tovuti ya Swahilihub ni dhana iliyochangiwa pakubwa na mambo mengi kuhusu muundo wa tovuti ya Swahilihub na jinsi tovuti ya Swahilihub kama jukwaa inavyokidhi matarajio ya watumiaji wake kimatini. Kutokana na matokeo haya tulibainisha vipengele muhimu vinavyoweza kubuni na kuboresha mkabala wa tathmini ya tovuti katika ukuzaji wa lugha kwa kuzingatia masuala muhimu katika muundo wa tovuti hii. Kwanza kabisa ni kigezo cha muundo wa uvumbuzi husika kimatumizi. Muundo ukiwa sahili utaboresha matumizi kwa msingi wa urahisi wa kimatumizi. Hivyo basi katika mkabala mpya uliobuniwa kwenye utafiti huu, kigezo cha muundo wa uvumbuzi husika kimezingatiwa tofauti na mkabala wa awali ambao haukupewa uzito unaohalisi.

Pili ni kuzingatia matarajio ya watumiaji wa uvumbuzi husika. Matarajio ya watumiaji na urahisi wa matumizi ya tovuti ni vigezo muhimu katika utendakazi wa tovuti hiyo. Kwa mfano katika mwaka wa 2006 watumiaji wa tovuti walitarajia muda wa kupatikana kwa matini mtandaoni kuwa sekunde nne au hata muda mfupi zaidi (DoubleClick, 2018). Watumiaji wa mitandao kwa sasa wanatarajia muda mfupi sana kuliko sekunde nne. Kutokana na matokeo haya yaliyoipa kipaumbele dhana ya matarajio ya watumiaji, kulibuniwa mkabala wa tathmini ya tovuti unaozingatia kigezo cha matarajio ya watumiaji kama kipengee muhimu katika msambao wa tovuti kama uvumbuzi maalum.

Katika mkabala huu, kuna vipengee mahususi kuhusu miundo ya mfumo wa kijamii pamoja na sifa za uvumbuzi unaohusika. Vipenge hivi vina nafasi mwafaka katika kuimarisha uhamisho pamoja na ushawishi katika mchakato mzima wa ubwiaji wa uvumbuzi husika. Katika mchakato wa msambao wa uvumbuzi hatua mbili ambazo ni uamuzi na udhibiti hazijaimarishwa kwa kubainisha vipengele mahususi vya

kuzifanikisha katika mchakato mzima wa msambao wa uvumbuzi. Kutokana na matokeo ya utafiti huu, kuna vipengele viwili muhimu vinavyopendekezwa kuimarisha hatua hizo mbili kwenye mchakato wa msambao wa uvumbuzi. Katika hatua ya uamuzi, utafiti huu unapendekeza kipengele cha muundo wa uvumbuzi kujengwa ili kuimarisha hatua hii muhimu ya uamuzi. Muundo wa uvumbuzi unasheheni urahisi wa kimatumizi ya uvumbuzi kwa watumiaji wake pamoja na ubora na ustahilifu wa matini kwemye tovuti husika. Jambo jingine muhimu hapa ni urejeleaji wa matini yaliyoko kwenye tovuti husika miongoni mwa watumiaji wa tovuti nyingine. Urejeleaji huu ukiimarishwa utawapa watumiaji wa tovuti husika hakikisho kwamba matini yake yamekubalika kwa matumizi mapana miongoni mwa watumiaji wa tovuti anuwai.

Isitoshe utafiti huu unapendekeza kipengee cha mahitaji ya watumiaji kwa kuzingatia matarajio ya watumiaji wa tovuti husika. Hali hii inawahimiza na kuwatia moyo watumiaji wa tovuti na kuimarisha hatua ya udhibiti katika mchakato wa msambao wa uvumbuzi. Muda wa kupatikana matini kwenye tovuti husika ni swala muhimu sana katika kuyafikia matarajio ya watumiaji wa tovuti husika. Kila mtumiaji wa tovuti huwa na matarajio ya kupata habari anayoitafuta kwa muda unaostahili na hivyo basi ni muhimu mkabala wo wote wa tathmini ya tovuti uzingatie matarajio ya watumiaji wa tovuti husika. Matarajio haya yakiangaziwa mtumiaji hupata nafasi ya kudhibiti uamuzi wake wa kubwia uvumbuzi husika.

### 4.7.3 Hitimisho

Katika sura hii tumeeleza kuhusu mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili na kujadili kwa jumla vitengo mbalimbali vya Swahilihub, Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili, tathmini ya tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili, changamoto

zinazowakabili watumiaji wa Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili na mustakabali wa tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili. Ukuzaji wa Kiswahili ulitokea kwa viwango tofauti katika vitengo vya tovuti ya Swahilihub kupitia vitendawili, mashairi na tendi, vitabu, makamusi, miongozo, magazeti pamoja na Makala ya utafiti. Tathmini ya Swahilihub ilitolewa kwa kuzingatia vigezo mbalimbali vikiwemo ushindani mtandaoni, uharriri wa matini, ushirikiano na urejeleaji wa tovuti nyingine pamoja na kitambulisho maalum cha Swahilihub. Changamoto zilizobainika katika ukuzaji wa Kiswahili kwenye tovuti ya Swahilihub ni uchangamano wa Swahilihub, matumizi ya lugha anuwai mtandaoni, miundombinu duni pamoja na matumizi ya istilahi, tafsiri na uchache wa wataalamu. Aidha tumetoa pendekezo la mkabala mpya wa mwaka wa 2021 wa tathmini ya tovuti mbalimbali katika ukuzaji wa lugha. Sura hii iliwasilisha matokeo kuhusu mchango wa tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili. Utafiti huu uligundua kwamba tovuti ya Swahilihub ina nafasi kubwa ya kuchangia mikakati mbalimbali ya ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili katika ujenzi wake, usambaaji wake pamoja na udumishaji wa hadhi na dhima yake. Hata hivyo kutokana na matokeo ya utafiti huu, mchango wa vitengo vya Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili, haujafikia lengo lake la kuwa na hazina ya data muhimu ya asasi, taasisi, idara mbalimbali za umma, waandishi na wachapishaji.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Muhtasari

Tasnifu hii inatokana na utafiti kuhusu mchango wa Swahilihub katika ukuzaji Kiswahili nchini Kenya. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kutathmini mchango wa tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili nchini Kenya. Hili lilitokana na mitagusano iliyopo miongoni mwa tovuti mbalimbali mtandaoni inayochangia tovuti hizi kuelekezana, kuchangiana na kurejeleana katika juhudi za kutimiza matilaba ya watumiaji wake kote ulimwenguni. Ni mahusiano haya ya tovuti mtandaoni yaliyozua haja ya kutathmini tovuti ya Swahilihub ili kubaini mchango wake katika juhudi za ukuzaji wa lugha ya Kiswahili mtandaoni.

Utafiti huu uliweka wazi suala la tovuti ya Swahilihub kuwa na vitengo mbalimbali na sifa za uvumbuzi zinazohitaji ufasili ili ieleweke na kukubalika kama swala ibuka miongoni mwa wataalamu wa Kiswahili. Aidha utafiti huu ulikidhi haja kubwa ya kubaini ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kupitia kwa matumizi ya Swahilihub miongoni mwa wadau wa lugha ya Kiswahili hasa wanapoeleza hisia, mitazamo na misimamo yao ambayo inaweza kuaminika au kuwa imetiwa chumvi, kupotosha au hata kuchochea.
Hili lilizua haja ya kuchunguza na kuweka wazi namna suala la ukuzaji wa lugha ya Kiswahili nchini Kenya linavyojitokeza katika tovuti ya Swahilihub.

Sura ya kwanza imeeleza masuala ya kimsingi katika utafiti huu. Tulijadili suala la ukuzaji wa Kiswahili katika enzi za mitandao ya kijamii na nafasi ya tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili. Tulionyesha kwamba mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili ni suala muhimu ambalo linahitaji

kushughulikiwa kwa dhati. Aidha tulionyesha kwamba ili kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia ni muhimu wadau wa Kiswahili wazingatie na kudumisha matumizi ya tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili. Usuli wa utafiti huu ulifafanua maswala muhimu kuhusu suala zima la TEHAMA na Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Aidha, maelezo yalitolewa kuonyesha kuwa TEHAMA ni kipengee muhimu katika maendeleo ya lugha ya Kiswahili hususan katika mitandao ya kijamii kwa vile kupitia kwa tovuti ndipo yale yanayosemwa na wataalamu yanaweza kufahamika.

Katika sura hii, usuli, misingi ya uteuzi wa mada, upeo wa utafiti pamoja na nadharia ya utafiti imeelezwa. Kisha tukaeleza umuhimu wa utafiti, maswali ya utafiti, misingi ya uteuzi wa mada ya utafiti, tahadhania za utafiti, pamoja na upeo wa utafiti. Nadharia ya msambao wa uvumbuzi ilifafanuliwa kwa kurejelea mchango wa wataalamu mbalimbali. Aidha, nguzo muhimu za nadharia zilifafanuliwa na namna zilivyotumika katika utafiti hususan kukusanya na kuchanganua data pamoja na kueleza istilahi maalum. Aidha sura ya kwanza imeorodhesha dhana kama zilivyotumika kwenye
utafiti huu.

Sura ya pili ilihakiki maandishi yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti kwa kuzingatia maoni mbalimbali kuhusu mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili. Sura hii ilihakiki maandishi mbalimbali kwa kutambua mitazamo na maoni ya wataalamu mbalimbali kuhusu Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili. Aidha, maelezo yalitolewa kuhusu dhana ya ukuzaji lugha, TEHAMA katika ukuzaji lugha, ukuzaji wa Kiswahili, Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili nchini Kenya pamoja na misingi ya tathmini ya tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili.

Isitoshe, maswala ibuka katika Swahilihub yalijadiliwa ili kuonyesha namna Swahilihub ilivyochukua nafasi muhimu katika mazingira ya mtandaoni. Miongoni mwa masuala ibuka yaliyoshughulikiwa ni mjio wa vifaa vya kiteknolojia vinavyochangia katika kutoa tathmini mwafaka ya utendakazi wa tovuti mbalimbali katika kuyakidhi mahitaji ya watumiaji wake. Miongoni mwa vifaa hivyo ni Arhefs, Alexa na Similarweb ambavyo vilichangia pakubwa katika kutathmini mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Maandishi yaliyohakikiwa yalikuwa na uhusiano na malengo ya utafiti na yalilenga matumizi ya teknolojia katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili.

Kijumla, katika sehemu hii tumehakiki maandishi mbalimbali kwa kutambua mitazamo na maoni ya wataalamu mbalimbali kuhusu ukuzaji wa lugha kwa jumla na nafasi ya tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Kwa kushughulikia dhana na umuhimu wa ukuzaji wa lugha kwenye tovuti ya Swahilihub tumeonyesha kuwa tovuti ya Swahilihub ni muhimu kwa kubaini nafasi yake kwa ujenzi wa lugha ya Kiswahili, usambaaji wake na udumishaji wa hadhi na dhima yake miongoni mwa watumiaji wake mitandaoni. Isitoshe, uhakiki wa maandishi kuhusu mijadala ibuka kuhusu nafasi ya Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili nchini Kenya umeonyesha kuwa tovuti ya Swahilihub hutumika katika ujenzi wa Kiswahili, usambaaji wake na udumishaji wa hadhi na dhima yake kwa kujadili maswala ya kijamii na kitaaluma katika lugha ya Kiswahili mtandaoni. Kutokana na uhakiki wa maandishi hayo, imebainika kuwa kulikuwa na pengo lililofaa kuzibwa ambalo kwanza lilikuwa ni kubainisha viwango vya ukuzaji wa Kiswahili miongoni mwa watumiaji wa Swahilihub. Kisha kutathmini mchango wa tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili. Kadhalika, uhakiki wa maandishi umebaini historia ya tovuti ya Swahilihub, maendeleo, malengo, umuhimu na mustakabali wake na changamoto zinazokumba ukuzaji wa Kiswahili miongoni mwa watumiaji wake.

Sura ya tatu ilihusu muundo wa utafiti. Sura hii ilifafanua njia na mbinu zilizoshirikishwa katika utafiti. Utafiti huu ulitumia njia za utafiti maktabani na nyanjani. Mbinu zilizotumiwa katika utafiti huu ni pamoja na usaili, hojaji na uchunzaji. Isitoshe, sura hii imezungumzia mwelekeo changamano wa utafiti na eneo la utafiti, watafitiwa na uteuzi wa sampuli. Mambo mengine ambayo yalizingatiwa ni vifaa vya ukusanyaji data, majaribio ya vifaa vya utafiti, utafiti halisi, uthabiti na uaminifu wa vifaa. Mwongozo wa uchunzaji ulitumika kukusanya data katika matini zilizoandikwa kwa Kiswahili kwenye tovuti ya Swahilihub. Uchanganuzi wa kithamani ulifanywa kwa kuzingatia malengo mahsusi ya utafiti. Hatua nyingine muhimu katika tasnifu hii ilikuwa kupanga sawa data kuhusu mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili kwa minajili ya uchambuzi na uchanganuzi kwa njia rahisi.

Sura ya nne imejadili mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili. Data zilizotokana na usaili, uchunzaji na hojaji zilihaririwa ili kuhakikisha kwamba hakuna makosa yaliyofanywa au majibu kutotolewa. Uhariri ulilenga kuhakikisha kwamba data ni sahihi, kamilifu, na inayoweza kutumika na kukubalika katika maandishi. Ili kupata ripoti ambayo ina maana pana, data zilianishwa na kupangwa katika makundi kwa kutegemea madhumuni ya utafiti. Sura hii imeshughulikia kwa jumla mfumo wa Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili, Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili, tathmini ya Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili, changamoto na mustakabali wa Swahilihub pamoja na mkabala mpya wa tathmini ya tovuti katika ukuzaji wa lugha.

Katika sura ya tano, utafiti huu umetoa muhutasari, mahitimisho na mapendekezo yatakayoangazia masuluhisho yatakayopatikana miongoni mwa wadau wote wa elimu baada ya wao kuelewa umuhimu wa Swahilihub katika ukuzaji wa taaluma ya

Kiswahili. Hivyo basi kutokana na matokeo ya utafiti wetu, taaluma ya Kiswahili inaweza kukuzwa kupitia kwa matumizi mwafaka ya tovuti ya Swahilihub.

## 5.2 Hitimisho

Tasnifu hii inaibuliwa na ukweli kwamba Kiswahili ni lugha ya kimataifa inayosomwa kupitia kwa mtandao na ambayo ina nafasi katika kumudu teknolojia mpya zinazojiri kila uchao. Tovuti ya Swahilihub kwa upande mwingine ni teknolojia mpya inayohitaji lugha ya Kiswahili kuimarisha usambazaji na ukubalifu wake miongoni mwa mamilioni ya watumiaji wa lugha hii. Swahilihub ni mtandao wenye upekee mkubwa katika kuimarisha ukuzaji wa Kiswahili mitandaoni. Swahilihub ilichangia na inaendelea kuchangia kwa ujenzi, usambaaji na udumishaji wa hadhi na dhima ya Kiswahili na vivyo hivyo Kiswahili kilichangia na kinaendelea kuchangia kustawisha Swahilihub miongoni mwa wadau wa taaluma ya Kiswahili.

Matokeo na mapendekezo ya utafiti huu yalibaini mustakabali ya kuwa ni chimbuko na kichocheo cha kuanza kutafakari juu ya uundaji wa dira ya ukuzaji endelevu wa Kiswahili mtandaoni na ustawi endelevu wa Swahilihub katika karne ya 21. Kuzuka kwa teknolojia ya mawasiliano ya kimtandao ambayo imekuwa maarufu sana kumechangia pakubwa katika ukuzaji wa Kiswahili miongoni mwa watumiaji wa Swahilihub kote ulimwenguni. Utafiti huu unadahili kuwa Swahilihub inachukua jukumu muhimu sana katika ukuzaji wa Kiswahili kwani ndicho chombo kilicho na nafasi ya kikati katika kukusanya, kuhifadhi na kuhariri matini katika hali na viwango mbalimbali kwa wadau wa Kiswahili.

Kama mchango wa kitaaluma wa utafiti huu na kutokana na matokeo yake, tuliboresha nadharia ya Msambao wa Uvumbuzi kwa kubuni mkabala wa kinadharia. Hivyo basi, Swahilihub ilifanyiwa uchunguzi wa kina kubainisha mchango wake wa kinadharia katika

kuboresha mkabala wa tathmini ya tovuti na kujadili mustakabali wake katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Utafiti huu ulichochewa na makisio yetu kuwa maendeleo ya kiteknolojia huchangia mageuzi makubwa yanayoendana na urahisi wa tovuti kimatumizi na uamilifu wake kimatini. Teknolojia hii ya Swahilihub kwenye mitandao ya kijamii ni jambo geni sana ndiposa tovuti hii ilitathminiwa ili kubaini mchango wake katika ukuzaji wa Kiswahili.

Matokeo ya utafiti huu yalibainisha kwamba nafasi ya Swahilihub miongoni mwa tovuti nyingine ilikuwa duni kwa nafasi ya milioni mbili nukta nne kwa idadi ya bilioni moja nukta tisa. Idadi ya watumiaji wa tovuti ya Swahilihub ilitegemea kiwango cha ubora na utendakazi wake. Utendakazi huu wa tovuti ni dhana inayorejelea kasi au ule muda unaochukuliwa na tovuti kuwasilisha matini kwa mtumiaji. Huu ni muda unaokadiria ubora wa tovuti kwa kuonyesha wakati wa kuingia kwa mtumiaji kwa tovuti anapotafuta habari na wakati habari na matini muhimu anayoitafuta inapowasilishwa na kukabidhiwa mtumiaji huyu mtandaoni.

Tasnifu hii ilitoa mchango wa kuboresha nadharia ya Msambao wa Uvumbuzi wa Rodgers (2003). Mihimili ya nadharia ya msambao wa uvumbuzi ni pamoja na uvumbuzi, vyombo vya mawasiliano na mitagusano ya kijamii,muda wa msambao, na michakato ya msambao wa uvumbuzi imefanikisha tathmini ya mradi wa Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Mihimili hii imewezesha kujadili umuhimu wa tovuti ya Swahilihub kwa watumiaji wake. Kwa mfano, kuna baadhi ya watumiaji wa Swahilihub wanaotumia tovuti hii kupata habari huku wengine wakijinufaisha na burudani miongoni mwa faida zingine. Aidha, mihimili hii iliiwezesha sura hii vilevile kufafanua sababu ya watumiaji kuchagua na kutumia Swahilihub kutokana na narnna inavyokidhi mahitaji yao.

Hata hivyo nadharia hii ilikuwa na udhaifu wake ambao utafiti huu ulikusudia kuboresha kwa kubuni mkabala mpya. Kutokana na matokeo ya utafiti huu kuna haja ya kuangazia upya nadharia zinazohusu teknolojia katika Kiswahili. Hali hii inahitaji nadharia za kufanikisha ufafanuzi wa masuala muhimu ya kiusomi kwa kuzingatia utendakazi wa mihimili ya nadharia hizo kama ilivyo katika nyanja zingine za Kiswahili kama vile sarufi na fasihi. Kwa kufanya hivi, tutapunguza hali ya kutafsiri nadharia hizi kutoka kwa lugha za kigeni kabla ya kuzitumikiza. Hili litawezesha uchambuzi na uhakiki wa baadhi ya teknolojia zinazovumbuliwa kwa sasa na kwa siku za baadaye kwa urahisi.

Katika kuangazia mustakabali wa tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili, utafiti huu ulibuni mkabala bora wa tathmini ya tovuti za ukuzaji wa lugha ili kutoa mchango wake katika kukidhi haja ya kuboresha nadharia za kiteknolojia na Kiswahili. Hii ilitokana na changamoto zilizojitokeza katika utafiti huu kuhusu namna ya kuchanganua na kutathmini tovuti ya Swahilihub kwa misingi ya nadharia na mikabala iliyopo.

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, tulibuni na kuboresha mkabala wa kithamani. Utendakazi huu wa tovuti ni dhana inayorejelea kasi au ule muda unaochukuliwa na tovuti kuwasilisha matini kwa mtumiaji. Huu ni muda unaokadiria ubora wa tovuti kwa kuonyesha wakati wa kuingia kwa mtumiaji kwa tovuti anapotafuta habari na wakati habari na matini muhimu anayoitafuta inapowasilishwa na kukabidhiwa mtumiaji huyu mtandaoni.

Kuzuka kwa teknolojia ya mawasiliano ya kimtandao ambayo imekuwa maarufu sana kumechangia pakubwa katika ukuzaji wa Kiswahili miongoni mwa watumiaji wa Swahilihub kote ulimwenguni. Teknolojia hii ya mitandao ya kijamii ni jambo geni sana

kwa hivyo inastahili kutafitiwa. Kuna juhudi ambazo zimefanywa ili kuhusisha Kiswahili katika mitandao kama vile kuundwa kwa istilahi za Kiswahili katika kitandazi cha Facebook. Vilevile katika mwaka wa 2009 Facebook ilizinduliwa katika lugha ya Kiswahili na ikaitwa Sura Kitabu. Hivyo basi utafiti huu ulichochewa na haja ya kutathmini namna ambavyo tovuti ya Swahilihub inavyochangia ukuzaji wa Kiswahili mtandaoni nchini Kenya.

Pili, utafiti huu ulibaini namna mfumo wa tovuti ya Swahilihub unavyoathiri ukuzaji wa Kiswahili miongoni mwa watumiaji wake mtandaoni. Tathmini ya mchango wa tovuti ya Swahilihub ni suala muhimu katika makadirio ya manufaa yake kwa watumiaji wake. Mradi wa Swahilihub huenda ukakosa kutimiza malengo yake iwapo tathmini ya mchango wake haitapewa kipaumbele licha ya umuhimu wake mkubwa wa kuweka Kiswahili mtandaoni na kuwafikia watumiaji wengi kote duniani. Umuhimu huu hutegemea pakubwa kigezo cha urahisi wa kimatumizi pamoja na uamilifu wa tovuti husika. Maendeleo ya kiteknolojia huchangia mageuzi makubwa yanayoendana na urahisi wa tovuti kimatumizi na uamilifu wake kimatini.

Aidha utafiti huu umepambanua changamoto za matumizi ya Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili. Masuala mapya ya kiteknolojia kwenye tovuti huibuka, kuendelea na kubadilika kila kuchao. Mabadiliko haya huchangia changamoto za matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye tovuti ya Swahilihub miongoni mwa watumiaji wake. Changamoto hizi huathiri pakubwa uwezo wa tovuti ya Swahilihub kukusanya, kuhifadhi na kuimarisha upatikanaji wa matini ya Kiswahili mtandaoni kutokana na mabadiliko na maendeleo yanayojiri mtandaoni. Hali hii inalazimu mradi wa Swahilihub kuimarisha na hata kuongeza vipengee vya huduma kwa watumiaji wake ili kuendana na mabadiliko haya na

kuimarisha ukuzaji wa lugha ya Kiswahili katika majukwaa mbalimbali mtandaoni. Katika karne hii ya uvumbuzi, wataalamu na wanazuoni wanatumia mitandao katika shughuli zao hasa katika mawasiliano yao. Hivyo basi, kuna haja ya kupambanua changamoto za matumizi na makuzi ya lugha ya Kiswahili kwenye mradi wa Swahilihub ili kubaini ustahilifu wake kwa watumiaji wake kote ulimwenguni.

Hatimaye mustakabali wa Swahilihub katika ukuzaji wa Kiswahili ulijadiliwa kama msingi muhimu katika ukuzaji wa Kiswahili. Mustakabali wa tovuti ya Swahilihub ulitegemea vigezo vya urahisi wake kimatumizi na uamilifu wake kimatini. Vigezo hivi ni muhimu katika kudumisha na kuimarisha idadi ya watumiaji wa mradi wa Swahilihub. Uamilifu huu kimatini huhusu iwapo au la tovuti ya Swahilihub ina matini na kongoo inayokidhi mahitaji ya watumiaji wake. Aidha, vigezo hivi ni muhimu katika kuwapa motisha watumiaji wa tovuti ya Swahilihub ili watilie maanani matumizi yake kwa njia inayokuza Kiswahili mtandaoni. Hivyo basi, utafiti huu ulikuwa wa msingi katika kubainisha mchango wa tovuti ya Swahilihub kwa kujadili mustakabali wake katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili.

Utafiti huu ulijaza pengo lililoachwa na watafiti wa awali la kuikuza lugha ya Kiswahili mtandaoni kwa kupanua kanzi ya maandishi kuhusu Swahilihub na kuongeza maarifa kuhusu mchango wa Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Utafiti huu vile vile ulililiafikia lengo hilo kwa kubainisha mchakato wa usambaaji wa Swahilihub kuanzia uhamasisho, ushawishi, uamuzi, utekelezaji na udhibitisho miongoni mwa watumiaji wa Swahilihub nchini Kenya. Hatua hizi muhimu zilitumika kuweka wazi kiasi cha ubwiaji wa Swahilihub miongoni mwa wataalamu wa Kiswahili nchini Kenya.

Kuhusu matumizi ya vitengo mbalimbali vya Swahilihub, matokeo yalikuwa yafuatavyo: Habari asilimia 66(224), Jifunze kiswahili asilimia 63(214) Maktaba jisomee asilimia

58(197), Makala asilimia 56(190), Picha kwa asilimia 45(153), Mwanzo kwa asilimia 43(146), Video asilimia 32(108), na Blogu na ukumbi asilimia 31(106). Kwa jumla matokeo haya yalibaini kwamba kiwango cha ukubalifu cha mradi wa Swahilihub kilikuwa kwa asilimia 45(153) miongoni mwa watumiaji wake. Matumizi haya yalichangia usambaaji na ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kwa asilimia iyo hiyo ya 45(156) miongoni mwa watumiaji wake. Matokeo haya yanawiana na yale ya Kim na Wengine (2014) waliopata ukubalifu katika utafiti wao kuwa asilimia 46 pamoja na Owoche (2019) aliyepata ukubalifu wa tovuti za hoteli kuu nchini Kenya kwa asilimia 49. Ingawa matokeo haya yaliwiana na utafiti wa awali, matokeo ya utafiti huu yamebaini kiwango cha chini cha ukuzaji wa Kiswahili kwenye tovuti ya Swahilihub kwa asilimia 45(156).

Kutokana na matokeo haya utafiti huu umebainisha ya kwarnba Kiswahili kimekuzwa kwa kiasi kidogo katika tovuti ya Swahilihub. Hali hii ilitokana na watumiaji wengi kukiri kutumia facebook kwenye tovuti ya Swahilihub. Utafiti huu pia umedhihirisha kuwa jukwaa la facebook hutumiwa kwa wingi kupata habari, mwasiliano ya kujuliana hali na kupata picha na video mbalimbali miongoni mwa watumiaji wa mradi wa Swahilihub. Matokeo ya utafiti huu yalibaini kwamba licha ya nafasi yake muhimu katika tovuti ya Swahilihub jukwaa la wiikipedia halijahusishwa kwenye mradi wa Swahilihub. Matokeo haya yanawiana na yale ya (Jelimo, 2015) yaliyodhihirisha kwamba Kiswahili haikuzwi ipasavyo kwenye mitandao ya kijamii hususan facebook, twita na Wikipedia. Mtandao wa Wikipedia haujahusishwa katika tovuti ya Swahilihub.

Mtandao huu wa Wikipedia ndio maarufu sana kote ulimwenguni na ilibainika kuwa vifupisho ambavyo vinatumika pale ni vile ambavyo vimekubalika katika lugha ya Kiswahili na hata kuingizwa katika kamusi zetu. Kitandazi cha Facebook ndicho kinachoongoza katika matumizi ya vifupisho kikiwa na asilimia 60 ya vifupisho kutoka

lugha ya Kiswahili na Kiingereza kikifuatwa na Twitter na asimilia 30 na mwisho Wikipedia ambayo ni 10%. Katika mtandao wa Wikipedia ni dhahiri kuwa vifupisho ambavyo hutumika ni vile ambavyo vimekubaliwa na hata kuingizwa katika lugha ya Kiswahili. Wikipedia ni rmtandao wa watu maarufu na hutumiwa na wataalamu au wasomi kupitisha ujumbe ambao ni faafu. Mtandao wa Wikipedia ni tofauti na mitandao ya Facebook na Twita ambayo hutumiwa sana na vijana kwa shughuli zisizo rasmi.

Kwa hivyo mtandao wa Wikipedia unaweza kunufaisha lugha ya Kiswahili kupitia uhakiki wa makala mbalimbali yanayohifadhiwa pale. Jambo jingine tuliloweza kubainisha kupitia kwa mitandao hii ni kuwa, mitandao ya Facebook na Twita hutumiwa kwa ajili ya kutuma picha, habari na kuwasiliana na marafiki lakini mtandao wa Wikipedia hutumiwa kwa ajili ya kiakademia. Utafiti huu umebaini ya kwarnba Kiswahili kirnekuzwa kwa kiasi kidogo katika mradi wa Swahilihub.

Vile vile, utafiti huu ulikusudia kupambanua changamoto za matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye tovuti ya Swahilihub nchini Kenya. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa changamoto mbalimbali zinazokumba matumizi ya Swahilihub miongoni mwa wadau wa Kiswahili nchini Kenya zilikuwa ni; gharama, ugumu wa matumizi ya Swahilihub, ushindani mkubwa kutoka kwa tovuti wenza, tafsiri mbalimbali za dhana kwenye tovuti ya Swahilihub, ukosefu wa lugha ishara, ukosefu wa istilahi na tafsiri mwafaka, ukosefu wa matini faafu na braile, matini za wasiona uwezo wa kuona. Aidha, kutokana na changamoto hizi ilidhihirika kwamba Swahilihub haitumiki vyema na wadau kwani wengi wao huitumia kwa kusudi la kujiendeleza kibinafsi, kujulikana na kutambulika katika jamii badala ya kuitumia Swahilihub kuikuza taaluma ya Kiswahili.

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, masuala mengi yameibuka. Matokeo ya utafiti huu yanaakisi hali ya chini ya ukuzaji wa Kiswahili miongoni mwa watumiaji wa Swahilihub kwa asilimia 45%. Utafiti huu ulibainisha mchango wa vitengo vifuatavyo vya Swahilihub katika maendeleo ya taaluma ya Kiswahili: mwanzo, habari, video, picha, maktaba jisomee, jifunze Kiswahili, makala na blogu na ukumbi. Matokeo haya ni ya chini yakilinganishwa na motekeo ya ukubalifu wa tovuti zingine katika tafiti za awali (Taz. 2.4). Matokeo haya yanaonyesha kwamba wadau wengi hawaitumii tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili.

Aidha miongoni mwa wale walioitumia Swahilihub ilipatikana kuwa idadi kubwa ya watumiaji hao walitatizika kutokana na ugumu wa kimatumizi wa mfumo wa tovuti ya Swahilihub. Hali hii ilitokana na tovuti ya Swahilihub kuchukuliwa kama mradi, jambo au dhana mpya na wadau wa Kiswahili. Ingawa Swahilihub iliasisiwa miongo miwili iliyopita, uvumbuzi huu ungali unachukuliwa kuwa mpya miongoni mwa wataalam wa Kiswahili. Tashwishi kuhusu manufaa ya tovuti ya Swahilihub ndicho kizingiti kikubwa zaidi kwa msambao wake. Athari za tovuti ya Swahilihub kwa wadau wa Kiswahili ni miongoni mwa mambo yaliyowafanya wengi kuususia au kusita kuukubali kama uvumbuzi katika taaluma ya Kiswahili.

Isitoshe, tovuti ya Swahilihub ilikumbana na shinikizo kutoka kwa tovuti wenza kama vile mwananchi.com na mtanzania.com. Aidha, matumizi ya lugha zingine yalididimiza juhudi za kuendeleza taaluma ya Kiswahili kwenye mawanda marefu. Hali hii ilitinga kusudi la kuitumia tovuti ya Swahilihub katika ukuzwaji wa taaluma ya Kiswahili. Tatizo jingine kuhusu matumizi ya tovuti ya Swahilihub ni kuwa, uhamasishaji wake ulikuwa adimu mno huku watafitiwa wengi wakikariri kuwa hawakuwa na habari hata kidogo

kuhusu kuwepo kwa tovuti ya Swahilihub. Wadau wengi walidai kuwa sababu kuu inayowazuia kutumia tovuti ya Swahilihub ni ukosefu wa muda wa kutosha. Hawana muda wa kutosha wa maandalizi.

Utafiti huu ulifichua kwamba idadi kubwa ya wadau wa Kiswahili nchini Kenya hawatumii tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Aidha semina chache sana huandaliwa na mashirika ya kibinafsi na mada zinazoshughulikiwa ni finyu huku tovuti ya Swahilihub ikikosa kuhamasishwa ipasavyo. Aidha juhudi za wizara ya Elimu na kampuni ya Nation Media Group katika maandalizi ya seminaa kwa ajili ya uhamasisho wa tovuti ya Swahilihub na ukuzwaji wa taaluma ya Kiswahili nyanjani hazikubainika. Ingawaje utafiti huu umejaribu kuelezea suala la mchango wa tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili, ni muhimu kunga'mua kuwa si rahisi kuelezea masuala yote yanayohusu tovuti ya Swahilihub kwa kuwa hali ya teknolojia inakua na kubadilika kila uchao. Mambo mengi mapya yanazidi kuvumbuliwa na ni muhimu kuzidi kuyadhukuru katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili.

Taswira inayojitokeza kutokana na utafiti huu ni kwamba, wadau hawajaitendea haki taaluma ya Kiswahili katika kuweka mikakati ya ukuzaji wake. Utafiti uligundua kwamba wadau wengi, asilimia 55(187) ya watafitiwa hawajaikumbatia tovuti ya Swahilihub ipasavyo kama jukwaa linaloweza kukuza taaluma ya Kiswahili. Kutokana na utafiti huu ilibainika kwamba maandalizi ya wadau vyuoni pekee hayatoshi kuwatayarisha vyema hasa wanaposhughulikia maswala ibuka katika taaluma ya Kiswahili. Kuna uwezekano mkubwa kwamba huenda malengo ya kukuza taaluma ya Kiswahili kupitia tovuti ya Swahilihub yasitimizwe. Kila mwanafunzi, mwalimu na

wadau wote wanaohusika wanastahili kutekeleza wajibu wao kikamilifu na kwa dhati iwapo tunatarajia kuboresha taaluma ya Kiswahili nchini Kenya na ulimwenguni kwa jumla.

Ufafanuzi uliotolewa katika sura zilizotangulia umebaini kuwa tovuti ya Swahilihub imechangia katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kwa njia mbalimbali. Juhudi za kuitalii na kuisakura tovuti ya Swahilihub, majibu ya hojaji, mahojiano baina ya mtafiti na meneja pamoja na mratibu wa matini katika tovuti ya Swahilihub zimedhihirisha kuwa mradi huu ni muhimu. Wasomi, wanahabari na wadau wa Kiswahili wanafaidi kwa kiwango fulani kutokana na mradi huu. Kutokana na utafiti huu, inaweza kuhitimishwa kwamba ukuzaji wa Kiswahili mtandaoni kwenye tovuti ya Swahilihub hautimiziki ipasavyo nchini Kenya. Licha ya vikwazo vilivyomo, ukuzaji wa lugha ya Kiswahili unazingatiwa kiasi kwa sababu ya mielekeo chanya ya wadau. Swahilihub imetokea kuwa tovuti yenye manufaa kwa kiwango fulani katika kushughulikia maslahi ya watumiaji wake. Mahitaji haya ambayo ni ya kimawasiliano, kiuchumi, kiusomi miongoni mwa mengine yamefafanuliwa sambamba na malengo ya utafiti kwa kutumia mihimili ya nadharia ya msambao wa uvumbuzi.

## 5.3 Mapendekezo

Kutokana na utafiti uliofanywa na kwa kurejelea data iliyopatikana, utafiti huu unatoa mapendekezo yafuatayo: Ni muhimu kwa sera kuwekwa na mfumo wa Swahilihub kuboreshwa ili kuimarisha ushirikiano wake na asasi mbalimbali husika katika juhudi za ukuzaji wa Kiswahili mtandaoni. Ili kuboresha mfumo wa Swahilihub, wasimamizi wa tovuti ya Swahilihub wanastahili kuweka mikakati ya kutumia kikamilifu mitandao anuai

ya kijamii ili kupata data muhimu kuhusu hisia na maoni ya watumiaji walio wengi na wanaotumia kwa wingi mitandao ya kijamii.

Mitandao hii huchangia kupata mrejesho kutoka kwa watumiaji wa tovuti ya Swahilihub. Mrejesho huu ni muhimu katika uhariri wa matini ya tovuti ya Swahilihub na upangaji wa kurasa za tovuti ya Swahilihub kwa kuweka matini mbalimbali mahali zinapostahili kwa kutegemea sifa za mitandao hiyo ya kijamii. Utafiti huu unapendekekezea wasimamizi wa Swahilihub kuwa ni bora picha ziwekwe kwenye instagram huku video zikiwekwa kwenye yuotube na habari za kupashwa moja kwa moja kwenye 'twitter' na mijadala na mahojiano ya moja kwa moja kwenye 'facebook'. Hali hii itaimarisha mitagusano kati ya wasimamizi na watumiaji wa tovuti ya Swahilihub. Kwa kiwango kikubwa, ufanisi wa ruwaza ya 2030 ya Kenya katika kupata maendeleo endelevu inategemea sana ufanisi wa elimu husasan elimu ya lugha. Swahilihub ina nafasi ya kuikuza lugha ya Kiswahili mtandaoni na kuyaafikia malengo haya ya ruwaza ya 2030 ya Kenya.

Isitoshe, kituo cha kitaifa kuhusu maandalizi na uratibu wa tovuti ya Swahilihub kinafaa kistawishwe na kuimarishwa. Hatua hii itafidia juhudi za wadau wote ikiwemo kampuni ya Nation Media Group katika utafutaji na upataji wa miundo misingi inayohitajika kuipiga jeki tovuti ya Swahilihub.

Mtafiti hawezi kudai kuwa utafiti huu umechunguza mambo yote kuhusu matumizi ya tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili. Utafiti huu umeshughulikia tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili nchini Kenya. Kwa hivyo, utafiti huu unapendekeza mambo yafuatayo kwa utafiti zaidi: Kwanza, nadharia zinazohusu teknolojia katika Kiswahili zinafaa kufanyiwa utafiti wa kina kwa upesi kwani Kiswahili tayari sasa ni lugha ya kitandawazi. Hali hii inahitaji nadharia za kufanikisha ufafanuzi wa masuala muhimu ya kiusomi kwa kuzingatia utendakazi wa mihimili ya

nadharia hizo kama ilivyo katika nyanja zingine za Kiswahili kama vile sarufi na fasihi. Kwa kufanya hivi, tutapunguza hali ya kutafsiri nadharia hizi kutoka kwa lugha za kigeni kabla ya kuzitumikiza. Hili litawezesha uchambuzi na uhakiki wa baadhi ya teknolojia zinazovumbuliwa kwa sasa na kwa siku za baadaye kwa urahisi. Pia, pana haja ya kufanya utafiti kuhusu uwezekano wa tovuti ya Swahilihub kuchangia kudidimiza taaluma ya Kiswahili. Mbali na kuchunguza tovuti ya Swahilihub katika maendeleo ya Kiswahili, utafiti unaweza kufanywa kuchunguza tovuti zingine kwa kuhusisha majukwaa mengine ya kimtandao. Utafiti kama huu kuhusu matumizi ya tovuti ya Swahilihub katika ukuzaji wa taaluma ya Kiswahili kwa kulenga tovuti wenza unapaswa kufanywa ili kuweka msingi madhubuti wa kukuzia Kiswahili.

# MAREJELEO


Adormedia na wengine (2015). Backlink building blocks. Adormediafactory.

Aghaei, S., Nematbakhsh, M. A., & Farsani, H. K. (2012). Evolution of the world wide web: From WEB 1.0 TO WEB 4.0. International Journal of Web & Semantic Technology, 3(1), 1-10.

Alexa. (2017). Alexa about. Retrieved June 15, 2018, from https://www.alexa.com/about

Alexa. (2018, October 10). The top 500 sites on the web. Retrieved from https://www.alexa.

Anderson, T., Varnhagen, S., & Campbell, K. (1998). Faculty adoption of teaching and learning technologies: Contrasting earlier adopters and mainstream faculty. The Canadian Journal of Higher Education, 28(23),71-78.

Arvi Hurskainen (2004) “Helsinki Corpus of Swahili. Compilers”: Institute for Asian and African Studies (University of Helsinki) and CSC.

Arvi Hurskainen, (2004) “Swahili Language Manager: A Storehouse for Developing Multiple Computational Applications”. Nordic Journal of African Studies volume 13, 363-397.

Assegaff, S., Hendri, K., Sunoto, A., Yani, H., & Kisbiyanti, D. (2017). Social media success model for knowledge sharing (scale development and validation). Telkomnika (Telecommunication Computing Electronics and Control), 15(3), 1335-1343.

Ayot, H.O. & Wengine (1984*) Language for Learning.* Nairobi: Macmillan Kenya Ltd.

Baker, C. (1992) Attitudes and Language. Clevedon, England: Multilingual Matter Ltd.

BAKITA, (2004)" Makala ya siku ya Kiswahili na Utandawazi", Oar es salaamu.

Barnet, S. (1985) *A Short Guide to Writing about Literature*. HarperCollins Publishers.

Baron, N (2004) See you online: Gender Isuses in College Students Use of Instant TextingJournal of Language and Social Psychology

Beal, V. (2018, September 12). Quality backlink. Retrieved from https://www.webopedia.com/ TERM/Q/quality backlink.html

Bekavac, I., & Garbin Praničević, D. (2015). Web analytics tools and web metrics tools: An overview and comparative analysis. Croatian Operational Research Review, 6(2), 373-386.

Bennett, J., & Bennett, L. (2003). A review of factors that influence the diffusion of innovation when structuring a faculty training program. Internet and Higher Education ,6, 53-63.

Best & Khan, R. M. I. (2010). Use of mobile immersion in foreign language teaching to enhance target language vocabulary learning. MIER Journal of Educational Studies Trends and Practices, 66-82.

Bishop, G. (1986) *Innovation in Education.* Macmillan International College Edition.London.

Bitugi, M. (2004*) CHAKITA Kuandaa Mkutano katika Jiji.* Taifa Leo 2004, Agosti 30 Uk.10.

Blankenship, M. B., & Applegate, B. K. (1998). Public support for early intervention programs: Implications for a progressive policy agenda. Crime & Delinquency, 44(2), 187-204.

Blankenship, S.E. (1998). Factors related to computer use by teachers in classroom

instruction (Doctoral Dissertation, Virginia Polytechnic Institute and State University, 1998). ProQuest DigitalDissertations. (UMI No. AAT 9831651).

Borg, W. R. na M. D, Gall. (2003). Educational Research: An Introduction (Fifth Ed) New York: Longman.

Bakiza (2010): *Swahili grammar and workbook*. Routledge. Mpiranya, F. (2014).

Batul, F. (2009). Chatspeak; Linguistic Evolution or Devolution. New York: Pergamon Press

Braak, J.V. (2001). Individual characteristics influencing teachers' class use of computers. Journal of Educational Computing Research, 25(2), 141-157.

Brewer,J and A. Hunter (1989) Multimedia Research: A Synthesis of Style. Newbury Park

Brown, J na Wengine (1985) *AV Instruction Technology Media and Methods.*

Singapore: McGraw-Hill Book Lewis R.B.Co.

Bruner, J. (1962). The Process of Education, Cambridge: Harvard University Press. CA: Sage

Campbell, na wengine (2014) " The information content of mandatory risk factor disclosures in corporate filings," Production and Inventory Management, 20, 2 63-71.

Carter, C.W. (1998). An assessment of the status of the diffusion and adoption of computer-based technology in Appalachian College Association colleges and universities (Doctoral Dissertation, Virginia Polytechnic Institute and State University, 1998). ProQuest DigitalDissertations. (UMI No. AAT 9905169).

Casmar S.P. (2001). The adoption of computer technology by faculty in a college of

education: an analysis of administrative planning issues (Doctoral dissertation, Washington State University, 2001).Pro Quest Digital Dissertations. (UMI No. AAT 3025011).

Cater, C. I. (1998). Playing with risk? Participant perceptions of risk and management implications in adventure tourism. Tourism management, 27(2), 317325.

Chevalier, A., & Lanot, G. (2002). The relative effect of family characteristics and financial situation on educational achievement. Education Economics, 10(2), 165-181.Paukkeri, 2017

Chimera, R. (2000) *Kiswahili: Past, Present and Future Horizon*: Nairobi. Nairobi University Press. *Collins New Age Encyclopaedia* Vol. 14

Choudhury, N. (2014). World wide web and its journey from web 1.0 to web 4.0. International Journal of Computer Science and Information Technologies, 5(6), 8096–8100.

Clément, F. na wengine, (2010): Epistemic Vigilance . Mind & Language 25 (2010): 359-93.

Cooper, R na Robert, W. (1990) Information Technology Implementation Research: A Technological Diffusion Approach Stable URL: https://www.jstor.org/stable/2661451

Creswell, J. W., Plano Clark, V. L., Gutmann, M. L., & Hanson, W. E. (2003). Advanced mixed methods research designs. Handbook of mixed methods in social and behavioral research, 209, 240.

Creswell, J.W. (2003) Research Design. Thousand Oaks. C.A: Sage

Creswell, J.W. (2007) Educational Research Planning and Evaluation: Qualitative and

Creswell, J.W. na P.L.V Clark. (2011) Designing and Conducting Mixed Method

Creswell, J.W. na P.L.V Clark. (2011) Designing and Conducting Mixed Method Crowford, Administrative Uses of Microcomputers. Part III Evaluation and Selection. Nairobi, National Association of Secondary School Principals.

Crystal, D. (2001). A dictionary of language. University of Chicago Press.

Crystal, D. (2001). Language and the Internet. Cambridge: Cambridge University Press.

Crystal, D (2004). Language and the Internet. Cambridge: Cambridge University Press.

Crystal, D(2006). Language and the Internet. 2 nd ed. New York: Cambridge University.

Crystal, D ( 2008a). Text Messages. ELT Journal 62(1): 77-83.

Crystal, D (2008b). Txting: the gr8 db8. Oxford: Oxford University Press.

Dabale, W. P., Jagero, N., & Nyatoti, L. M. (2015). Client Satisfaction and Health Services Delivery in an African Public Clinics: The Case of Mutare, Zimbabwe. Management and organizational studies, 2(2).

Dean, B. (2018). Link building for seo: The definitive guide. Backlinko.

Designs‟. Education Evaluation and Policy Analysis 11 (3) 255 - 274 dialogic perspective. Information Development, 32(3), 718–727.

Diffily, S. (2006). The website manager’s handbook. Lulu. com.-, G.L. (1987) Microcomputers in Education: Elements of Computer-Based Curriculum in Eduction: U.S Government Printing Office. Washington.

Dooley, K.E. (1999). Towards a holistic model for the diffusion of educational technologies: An integrative review of educational innovation studies. Educational Technology & Society 2(4), 35-45.

Dorr, A. (1984) Television and Children. Calif. Newbury Park.

DoubleClick. (2016). The need for mobile speed. Google.

Eckler, P., Rodgers, S., & Everett, K. (2016). Characteristics of community newspaper coverage of tobacco control and its relationship to the passage of tobacco ordinances. Journal of community health, 41(5), 953-961.

Eurydice, B. (2003) ICT in Education Systems in Europe: Retrieved on 10th October 2008

Fang, Y., Liu18, C., Chang19, T. J., & Dinh, H. Q. (2007). Appalachian tycoon: an environmental

Fielding, N. na J. Fielding. (1986) Linking Data. Bevery Hills: Sage

Finley, T.R. (2003). A descriptive study of utilization of technology from a perspective of full-time faculty in Virginia’s higher education teacher-education programs (Doctoral dissertation, The George Washington University, 2003). ProQuest DigitalDissertations. (UMI No. AAT 3083800).

Fisher, R. (2003) Teaching Thinking: Philosophical Enquiry in the Classroom. London,

Continuum.

Fishman, J.A. (1991) Reversing Language Shift: Theoretical and Empirical Foudations

Fishman, J.A. (ed) (2001) Can Threatened Languages Be Saved? Reversing Language for New Partnership‟. In: Reichardt, C.F and S.F Rallis (eds) The Qualitative –

Frankel, J.R. & Wallen, N.E. (1990) How to Design and Evaluate Research in Education. New York: McGraw Hill.

Gakuru, Mucemi , Frederick K. Iraki, Roger Tucker, Ksenia Shalonova, Kamanda Ngugi, (2005)"Development of a Kiswahili text to speech system", In INTERSPEECH, pp1481-1484. game in second life. In Second life education workshop 2007(p. 72)

Gavalda, M. (2018). A begginer’s guide to website speed optimization. ” Akamai”

Gay,L.R. (1976) Educational Research: Competencies for Analysies and Application. Ohio: Charles E. Merril Publishing Company.

Gibbs, G., & Simpson, C. (2005). Conditions under which assessment supports students’ learning. Learning and teaching in higher education, (1), 3-31.

Gikambi, H. (2014). 'Mgeni Njoo Mwenyeji Atambe'-Athari Za Facebook, Twitter Na Youtube Katika Vyombo Vya Habari Vitumiavyo Kiswahili. Makala kwenye Kongarnano la Swakc. http://www.afrikanistik.uni-bayreuth.de/de/colloq/swahili_colloq/index.html.

Gilliespice, T (1986) *Integration of Media into the Curriculum*.London: Kogan Page.

Godwin, W. (1993). Political and philosophical writings of William Godwin.

Google. (2018a, October 10). Bounce rate. Retrieved from https : / / support . google . com / analytics/answer/1009409?hl=en

Google. (2018b). Improve Server Response Time. Retrieved July 26, 2018, from https : //

developers.google.com/speed/docs/insights/Server

Google. (2018c, September 30). *Transparency report.* Retrieved from https://transparencyreport. google.com/safe-browsing/overview

Google. (2019, January 21). From the garage to the googleplex. Retrieved from https://www. google.com/about/our-story/

Gotch, N. (2018, September 12). How to build backlinks in 2018. Retrieved from https://www. gotchseo.com/backlinks/

Gray, D.E. (2009) Doing Research in the Real World. Lodon: SAGE Publication Ltd.

Green, J.C. (1989) „Towards a Conceptual Framework for Mixed Methods Evaluation

Green, J.C. (2008) „Is Mixed Methods Social Inquiry a Distinctive Methodology?"

Guy De Pauw, Gilles-Maurice de Schryver and Peter Waiganjo Wagacha, (2009) " A Corpus-based Survey of Four Electronic Swahili–English Bilingual Dictionaries", Lexikos volume19 (AFRILEX- reeks/series 19:), pp: 340352 16.

Guy De Pauw1, Gilles-Maurice de Schryver, and Peter W. Wagacha (2006) "Data-Driven Part-of-Speech Tagging of Kiswahili" Petr Sojka, Ivan Kopeˇcek and Karel Pala (Eds.): TSD, LNAI volume 4188, Springer- Verlag Berlin Heidelberg 2006, pp. 197–204,

Hadrien Gelas, Laurent Besacier, F. Pellegrino, (2012) "Developments of Swahili resources for an automatic speech recognition system", SLTU - Workshop on Spoken Language Technologies for Under-Resourced Languages, Cape-Town, South Africa.

Harasim, L. (1993). Global Networks: Computer and International Communication. Cambridge: The MIT Press.

Harris, A. L., & Rea, A. (2009). Web 2.0 and virtual world technologies: A growing impact on is education. Journal of Information Systems Education,

20(2), 137 Has Come. Educational Reseacher 33(7) u.k 14-26.

Herman, J. Osmundson, E., and Pascal, J. (October,1996). Los Alamos National Laboratory Critical Issues Forum Final Evaluation Report, Center for the Study of Evaluation, UCLA Graduate School of Education.

Hidayat, R. S., & Zpalanzani, A. (2011). From novel into comic: a case of semiotic translation. TransCon Proceedings.

Hoerup, S.L. (2001). Diffusion of an innovation: computer technology integration and the role of collaboration (Doctoral dissertation, Virginia Polytechnic Institute and State University, 2001). ProQuest DigitalDissertations. (UMI No. AAT 3031436).

Hogan, A. (2014). Linked data & the semantic web standards.

Http://en.wikipedia.org/wiki/Languages_of_the_Democratic_Republic_of_the_Congo Accessed 27/06/2016

Ibrahim, M. (2016). Evaluating Hotel Websites as a marketing communication channel: A

Ilhebuzor, N.A. (1986) *Appropriate Instructional Media (AIMS): An Issue in Educational Technology in the Nigerian School System.* British Journal of Educational Technology, 17 (2).

Internet Live Stats. (2018). Internet Live Stats google search today. Retrieved June 30, 2018, from http://www.internetlivestats.com/

Internet Society. (2018). 2017-internet-society-global-internet-report-paths-to-our-digital-future. Internet Society.

Ip, C., Law, R., & Lee Ipara, I.O. (2001) Uwezekano *wa Kiswahili kuwa Lugha ya Kufundishia ya Pili Katika Kiwango cha Juu cha Shule za Msingi* Katika Shitemi;N.I. et al (ed). Kiswahili: A Tool for Development.

Eldoret, Moi University Press.

Isleem, M I. (2003). Relationships of selected factors and the level of computer use for instructional purposes by technology education teachers in Ohio public schools: a statewide survey (Doctoral dissertation, The Ohio State University, 2003). ProQuest Digital Dissertations. (UMI No. AAT 3124087).

Ismail, S. (2006) The Turkish Online Journal of Educational Technology – TOJET April 2006 ISSN: 1303-6521 volume 5 Issue 2 Article 323

Jacobsen, M. (1998). Adoption patterns and characteristics of faculty who integrate computer technology for teaching and learning in higher education. (Doctoral dissertation, The University of Calgary, 1998).ProQuest DigitalDissertations. (UMI No. AAT NQ34679).

Jager, A.K na A.H. Lokman (1999) *Critical Thinking Handbook*

Jagero, J. A. Mohochi, E. S. na Indede, F. (2013). "The Usage of Kiswahili in Blog, Discourse and the Effects on Its Development". International Journal of Humanities and Social Science. VOL. 3 NO. 14 (Special Issues- July 2013) 192-199.

James,T.(2004)Informationand Communication Technologies for Development in Africa.I.D.R.C.Ottawa.

Jelimo, (2015) Athari za Lugha za Tovuti katika Mustakabali wa Ufundishaji wa Kiswahili: Mount Kenya University.

Johnson na Onweugbuzie (2004) Mixed Method Research: A Research Pradigim Whose Time Has Come. Educational Reseacher 33(7) u.k 14-26.

Johnson, G. (2007). Strategy as practice: research directions and resources Journal of Mixed Methods Research 2(1). 7 – 22.

Kahigi, K. K. (2007). Ujanibishaji wa Office 2003 na Windows XP kwa Kiswahili Sanifu. Kioo cha Lugha, 5(1).

Kamusi ya Cambridge (2015) The Cambridge Dictionary of Psychology. *Reference Reviews*, *24*(3), 8-8.

Kaplan, M. & Heinlein, M. (2010). Users of the world, unite! The challenges of social media, Business Horizons, 53 (1), 59-68.

Khayesi, M. K. (2002) 'Kiswahili and Information Technology: Challenges In Public University Libraries in Kenya'. Kiswahili, Juzuu 65, u.k. 24 - 31. Dar es Salaam, T.U.K.I.

Khayesi, M., & Amekudzi, A. A. (2005). Kingdon’s multiple streams model and automobile dependence reversal path: the case of Curitiba, Brazil. Journal of Transport Geography, 19(6), 1547-1552.

Kimani, N. (1997) *Kiswahili na Elimu Nchini Kenya.* Nairobi, Twaweza Communications

Kimui, V.W. (1988) Availability and Use of Learning and Teaching Resources in Primary Teacher’s Colleges in Kenya. P.Hd Thesis.Nairobi, Kenyatta Unversity

King, A. (2008). Website optimization. ” O’Reilly Media, Inc.”.

King, C. (2010). Social media localization, April 28, retrieved on 30 June 2015 from http:// cindyking. biz/localizatio-of- socialmedia/

Kinsella, A. R. (2010). 10. Was recursion the key step in the evolution of the human

language faculty?. Recursion and human language, 104, 179.

Kothari, C.R. (2003) *Research Methodology: Methods and Techniques.* New Delhi: Vishwa Prakashan

Lacey, M.(2004) 'Using a new Language in Africa to save dying ones'. The Standard, 16th November 2004. p.10, Nairobi, Standard Limited.

Law, R., Qi, S., & Buhalis, D. (2010). Progress in tourism management: A review of website evaluation in tourism research. Tourism management, 31(3), 297–313.

Lee, H., & Law, R. (2012). Profiling the users of travel websites for planning and online experience sharing. Journal of Hospitality & Tourism Research, 36(3), 418-426.

Less, K.H. (2003). Faculty adoption of computer technology for instruction in the North Carolina Community College System (Doctoral dissertation, East Tennessee State University, 2003).ProQuest Digital Dissertations. (UMI No. AAT 3097072).

Leung, D., Law, R., & Lee, H. “. (2016). A modified model for hotel website functionality evaluation. Journal of Travel & Tourism Marketing, 33(9), 1268–1285.

Leung, X. Y., Bai, B., & Stahura, K. A. (2015). The marketing effectiveness of social media

Li, Y., Roth, S., Laser, M., Ma, J. X., & Crosson, C. E. (2003). Retinal preconditioning and the induction of heat-shock protein 27. Investigative ophthalmology & visual science, 44(3), 1299-1304.

Light, P.C. (1998). Sustaining innovation. San Francisco: Jossey-Bass.

Lu, M. T., & Yeung, W. L. (1998). A framework for effective commercial web application development. Internet Research, 8(2), 166-173.

Maina, (2016) http:www.mwananchi.co.tz/swahilihub/1597604-2779982;

Marie, S. (2003) Gold Rush Alice World,Grades 5 and 8 Available on http://www.timetrek.org/index2.htm. Accessed on 18/02/2016.

Martin, M.H. (2003). Factors influencing faculty adoption of Web-based courses in teacher education programs within the State University of New York (Doctoral dissertation, Virginia Polytechnic Institute &State University,2001).Pro Quest Digital Dissertations.(UMINo.AAT 3089087). Maseno: Kanezja Publishers.

Mazrui, A. A. (1995). The “Other” as the “Self” under Cultural Dependency: The Impact of the Postcolonial University. .

Mazrui, A. A. na Mazrui, A.M. (1995) Swahili State and Society. Nairobi, East Africa Educational Publishers.

Mbatiah, M. Iribe, M. P. & Michira, N. (2013). Ukuzaji wa Kiswahili: Dhima na majukumu ya asasi mbalimbali.

Mcfedries, P. (2004). *Word spy: the word lover’s guide to modern culture*. New York: Broad Books.

McKenzie, J. (2001). How teachers learn technology best. From Now On: The Educational Technology Journal, 10(6). Retrieved March 01, 2005, from http://www.fno.org/mar01/howlearn.html

media, *Business Horizons*, 53 (1), 59-68.

Medlin, B.D. (2001). The factors that may influence a faculty member's decision to adopt electronic technologies in instruction (Doctoral dissertation,

Virginia Polytechnic Institute and State University, 2001). ProQuestDigitalDissertations. (UMI No. AAT 3095210).

Mohochi, E. (2002). “Teknolojia ya Mawasiliano na nafasi ya Kiswahili Ulimwenguni in Utafiti wa Kiswahili I.K Simala (ed) Maseno: Maseno University.Milroy, L. (1987) Observing and Analyzing Natural Language. Oxford: Basil Blackwell Ltd.

Moogan, P. (2014). The beginner’s guide to link building.

Moraa, J.M. (2012). "Uzalishaji wa Msamiati katika Mradi wa Microsoft East Africa 2004-2009." Tasnifu ya M.A ya Chuo Kikuu cha Kenyatta. Haijachapishwa.

Morse, J.M. (1991) Approaches to Qualitative – Quantitative Methodological

Moz. (2018). Backlinks what are backlinks? Retrieved July 5, 2018, from https:// moz.com/

Msanjila, Y. P. (2002). Dhima ya Kiswahili katika Karne ya 21.

Mugenda, O. &Mugenda A. (2003) Qaulitative and Quantitative Approaches. Nairobi Acts Press

Murray, M., & Berwick, D. M. (2003). Advanced access: reducing waiting and delays in primary care. Jama, 289(8), 1035-1040.

Mutai, K.M. (2000) How to Write Quality Research Proposal: A Complete Simplified Recipe. New York Thellery Publications.

Mutembei, A. (2011). Kukitandawazisha Kiswahili kupitia simu za kiganjani: tafakari

Mutiso, K (2014). "Sexism in Forbidden Language: The case of Kiswahili and English." Journal of Oriental and African Studies. 2014; 23:353-379.kuhusu Isimujamii. SWAHILI FORUM 18: 198-210.

Milroy, L. (1987), Language and Social Networks. Blackwell Publishers: Oxford.

Nachmias, C.F. & Nachmias, D. (2003*) Research Methods in Social Sciences:* London: St. Martins Press Inc. Nairobi: Masola Publishers.

Nanehkaran, Y. A. (2013). An introduction to electronic commerce. International journal of scientific & technology research, 2(4), 190-193.

Nekesa, B. (2010). Language, mobile phones and internet: a study of SMS texting, email, IM and SNS chats in computer mediated communication (CMC) in Kenya. Netherlands Graduate School of Linguistics.

Nielson (2009, March). "Global Faces and networked places": A Nielson report on social Networking's new footprint. Retrieved 27/05/2014.118 http://blog.nielsen.com/n ielsenw ire/wpcontent/uploads/1009/n ielsen g loal facesmar09 .pd[

Njihia K. (2005). A digital divide: Kiswahili holds the key. Journal of Language, Technology & Entrepreneurship in Africa, 1(1), 133-143.

Njihia K. (2015). Taathira za Kiswahili na Lugha Nyingine kwa Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha za mama mijini Nairobi, Kiambu na Thika: Mfano wa Kikuyu.Chuo Kikuu cha Kenyatta (Tasnifu Isiyochapishwa)

O’brien, H. L., & Toms, E. G. (2013). Examining the generalizability of the User Engagement Scale (UES) in exploratory search. Information Processing & Management, 49(5), 1092-1107.

Onweugbuzie et al. (2004) Mixed Method Research: A Research Pradigim Whose Time

Orodho, A. J. (2003) Essentials of Educational and Social Sciences Research Method.

Orodho, A. J. (2009) Elements of Education and Social Science Research Method.

Orodho, J. A. (2004). Techniques of writing research proposals and reports in education and social sciences. Nairobi: Masola Publishers.

Owino A. (2011) Tathmini ya Matumizi ya TEKNOHAMA katika ufundishaji wa Riwaya ya Kiswahili katika shule za upili wilayani Kisumu Magharibi.Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro (Tasnifu ya uzamili isiyochapishwa)

Owoche P. (2019) Online Hotel Branding Based on the Dialogic Principles of Internet Communication (Doctoral dissertation, Kibabii University,Kenya 2019 Unpublished)

Pappert, S. (1987) Computer Criticism Vs Technocentric Thinking. British Journal of Education Technology. Vol.16No. 4. 2005.(Unpublished)

Parisot, A.H. (1995). Technology and teaching: The adoption and diffusion of technological innovationsby a community college faculty (Doctoral dissertation, Montana State University, 1995). ProQuestDigitalDissertations. (UMI No. AAT 9542260).

Parisot, A.H. (1997). Distance education as a catalyst for changing teaching in the community college:Implications for institutional policy. New Directions for Community Colleges, 99, 5-13.Peil, M. (1995) *Social Science Research Methods:* A Handbook for Africa. Nairobi: Lectern Publications.

Patrick, P. L. (2009) Sociolinguistic Methods. England: University of Essex

Piansoongnern, O., Anurit, P., & Kuiyawattananonta, S. (2011). Talent management in Thai cement companies: A study of strategies and factors influencing employee engagement. African Journal of Business Management, 5(5), 1578-1583.

Picciano, A.G. (2004) *Educational Research Premier*.London: Continuum. Quantitative debate:New Perspective uk 85-95. SanFrancisco: Josey Bass Quantitative Reserch (2 ed) Ohio: Prentice Hall, Inc.

R. Shah, B. Lin, A. Gershman, and R. Frederking, (2010) “Synergy: A named entity recognition system for resourcescarce languages such as swahili using online machine translation”, in Proceedings of the Second Workshop on African Language Technology (AfLaT 2010), , pp.21–26.

Rallis, S.F. (1994) „Qualitative and Quantitative Inquiries Are Not Incompatible: A Call Research. California U.S.A: Prentice Hall, Inc.
Research. California U.S.A: Prentice Hall, Inc.
Revisted: A 21st Century Perspective. Clevedon, England: Multilingual Matterseducation

Rodgers, N. (2003, July 3). 14 Stats that Show Why Video Marketing is Important for Hotels. Retrieved from https://www.e-marketingassociates.com/blog/14stats-that-show-whyvideo-marketing-is-important-for-hotels

Rodgers, E.M. (2003). Diffusion of innovations (5th ed.). New York: Free Press.Sampath, K. na Wenzake (1990) *Introduction to Educational Technology*. New Delhi: Sterling Publisher Private Ltd.

Ryan, B., & Gross, N. C. (1943). The diffusion of hybrid seed corn in two Iowa communities. Rural sociology, 8(1), 15.

Ryan, M. (2003). Public relations and the web: Organizational problems, gender, and institution type. Public Relations Review, 29(3), 335–349.

Schema.org. (2018). Schema.org welcome to schema.org. Retrieved July 7, 2018, from

https: //schema.org/

Schilling, N. (2013) Sociolinguistic Fieldwork. Cambridge: Cambridge University Press

Schmidt, D. (1995). Use and integration of computer-related technology in teaching by preservice teachereducation faculty (Doctoral dissertation, Iowa State University, 1995). ProQuest DigitalDissertations.(UMI No. AAT 9610982).

Seemann, K. (2003). Basic principles in holistic technology education. Journal of Technology Education, 14(2),28-39.

Seleman S. Sewangi, (2000) "Tapping the Neglected Resource in Kiswahili Terminology: Automatic Compilation of the Domain-Specific Terms from Corpus", Nordic Journal of African Studies, Vol. 9, issues 2, pp 60-84.

Shepard, C. (2015, July 15). Can you rank in google without links? new data says slim chance. Retrieved from https://moz.com/blog/backlinks-google-study

Sherry, L. (1997). The boulder valley internet project: Lessons learned. THE (Technological Horizons inEducation) Journal, 25(2), 68-73.

Silva, na wengine (2008). Web 3.0: A vision for bridging the gap between real and virtual. In Proceedings of the 1st acm international workshop on communicability design and evaluation in cultural and ecological multimedia system (pp. 9–14). ACM.

Simala, I. K.(2002) Utafiti wa Kiswahili. Maseno, Chuo Kikuu cha Maseno.

SimilarWeb. (2019, January 21). Hotels.com Traffic Sources. Retrieved from https : / / www.similarweb.com/website/hotels.com#overview

Simmons, E. (2005). The Impact of the Weblogs: A Case Study of The United States

and

Simmons, E. (2009). Iran, Unpublished Senior Thesis (Hons), The Ohio State University, Retrieved February 26, 2009, from http;//kb.osu.edu/dspace/bitstream/1811/371/1/BlogImpact.pdf

Singh, N. Lenhart, K. & Bostic, K. (2010). Global Social Media Usage and the Language factor. White paper: Lionbridge.

Slyke, C.V. (1998). Technology cluster innovations: impacts of adding a technology to an existing cluster (Doctoral dissertation, University of South Florida, 1998). ProQuest DigitalDissertations.(UMI No. AAT 9911522).

Spier, L. (1929). Problems arising from the cultural position of the Havasupai.

Spotts, T.H. (1999). Discriminating factors in faculty use of instructional technology in higher education. Educational Technology & Society, 2(4), 92-99.

Sprague, D., Kopfman, K., & Dorsey, S. (1999). Faculty development in the integration of technology in teacher education courses. Journal of Computing in Teacher Education, 14(2), 24-28.

Stuart, W.D. (2000). Influence of sources of communication, user characteristics and innovation characteristics on adoption of a communication technology (Doctoral dissertation, The University of Kansas, 2000).ProQuest DigitalDissertations. (UMI No. AAT 9998115).

Surendra, S.S. (2001). Acceptance of Web technology-based education by professors and administrators of a college of applied arts and technology in Ontario (Doctoral dissertation, University of Toronto, 2001). ProQuest Digital Dissertations. (UMI No. AAT NQ58603).

SWEOR, (2018). The Definitive Web Design Resource Guide: 2018 (Updated). (2019). Sweor.com. Retrieved 30 July 2019, from https://www.sweor.com/webdesignresources Tourism Research, 39(2), 147–169

TUKI (2001) Kamusi ya Kiswahili-Kiingereza, Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili, Chuo kikuu cha Dar-es-salaam.

TUKI (2004) kamusi ya Kiswahili sanifu (Toleo la pili). Nairobi. Oxford University Press.

TUKI (2006) Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili (3rd Ed), Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili, Chuo kikuu cha Dar-es-salaam.

Valente, T. W., & Rogers, E. M. (1995). The origins and development of the diffusion of innovations paradigm as an example of scientific growth. Science communication, 16(3), 242-273.

Van Dijk, T. A. (2001). 'Multidisciplinary CDA: A plea for diversity'. In R. Wodak, and M. Meyer, (eds.) *Methods of critical discourse analysis:Introducing qualitative Methods* (pp 95-120). London: Sage Publications.

Wagner, D. (2017, May). Towards evaluating the robustness of neural networks. In 2017 IEEE Symposium on Security and Privacy (SP) (pp. 39-57). IEEE.

Wamalwa.S. (2016) Tathmini ya Uwasilishaji na Upokezi wa Taarifa za Hadari za Kiswahili Katika Tovuti ya Swahilihub Chuo Kikuu cha Kenyatta (Tasnifu isiyochapishwa)

Weinberg, T. (2009). *The New Community Rules*. C.A.: O' Reilly Media Inc.

Werry, C. C. (1996). Linguistic and interactional features of Internet Relay Chat. *Pragmatics and beyond new series*, 47-64.

Williams na wengine. (2009). Unraveling the relationship between literacy, language proficiency, and patient–physician communication. Patient education and counseling, 75(3), 398-402.

Yun, Y. H., Wang, W. T., Deng, B. C., Lai, G. B., Liu, X. B., Ren, D. B., ... & Xu, Q. S. (2015). Using variable combination population analysis for variable selection in multivariate calibration. Analytica chimica acta, 862, 14-23.

Zakaria, Z. (2001). Factors related to information technology implementation in the Malaysian Ministry of Education Polytechnic. (Doctoral dissertation, Virginia Polytechnic Institute and State University, 2001

# VIAMBATISHO

## A. Kiambatisho I: Mwongozo wa Dodoso

15/10/2015

Kwa mtafitiwa,

Mimi ni mwanafunzi katika Idara ya Elimu ya Lugha na Fasihi katika Chuo kikuu Cha Sayansi na Teknolojia Cha Masinde Muliro anayesomea shahada ya uzamivu katika Kiswahili. Ninafanya utafiti kuhusu tathmini ya swahilihub katika uendelezwaji wa taaluma ya Kiswahili. Inatumainiwa kwamba utafiti huu utachangia katika kubainisha nafasi ya swahilihub katika uendelezwaji wa taaluma ya Kiswahili miongoni mwa wataalam wa kiswahili. Wewe ni kati ya watafitiwa waliotambuliwa kushiriki katika uchunguzi huu. Nakusihi unisaidie ili niweze kukusanya data. Maelezo yote yatakayotolewa yatahifadhiwa kwa siri wakati na baada ya utafiti.

Tafadhali usiandike jina lako kwenye hojaji utakayojibu maswali yake.

Wako mwaminifu,

OWINO ANTHONEY OLOO

### B. Kiambatisho II: Hojaji kwa wahadhiri wa Taaluma ya Kiswahili

**SEHEMU YA A: Maswali ya kimsingi.**

#### 5.3.1.1 Maagizo

Tafadhali jaza nafasi katika hojaji uliyopewa. Haina haja uandike jina. Maelezo utakayotoa yatatumiwa tu kwa kusudi la uchunguzi huu na yatahifadhiwa sana wakati na baada ya utafiti.

1. Ni kipi kiwango chako cha kuhitimu cha kitaaluma?

a. Digrii B.ED/B.A { }

b. M.ED/M.A { }

c. PhD { }

2. Umetumia swahilihub kwa miaka mingapi?

a. 1 { }

b. (2-5) { }

c. (Zaidi ya 5) { }

3. Umekuwa ukitumia swahilihub kufunza lugha ya Kiswahili kwa muda upi?

a. (1) { }

b. (2-5) { }

c. (Zaidi ya 5) { }

#### 5.3.1.2 SEHEMU YA B: Nafasi ya vitengo vya swahilihub Katika kuendeleza taaluma ya kiswahili.

4. Ifuatayo ni orodha ya vitengo mbalimbali vya swahilihub vinavyotumika kuendeleza taaluma ya Kiswahili. Weka alama (/) ama (X) kuonyesha iwapo umevitumia au haujavitumia mtandaoni.

| Kitengo cha swahilihub | Naitumia sana | Naitumia | Siitumii | Sijui |
|---|---|---|---|---|
| Mwanzo | | | | |
| Habari | | | | |
| Blogu na ukumbi | | | | |
| Jifunze Kiswahili | | | | |
| Video | | | | |
| Maktaba Jisomee | | | | |
| Picha | | | | |

5. Je, unatumia swahilihub kwa njia yo yote ambayo haijatajwa hapo juu?

a. Ndiyo { }

b. La { }

Kama jibu lako katika swali la 5 hapo juu ni ndiyo, tafadhali zitaje njia hizo.

…………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………

6. Je, wanafunzi wako wanatumia swahilihub kuendeleza taaluma ya Kiswahili?

a. Ndiyo { }

b. La { }

7. Je, tovuti ya swahilihub inatosheleza mahitaji ya kuendeleza taaluma ya Kiswahili?

a. Ndiyo { }

b. La { }

Kama jibu lako katika swali 7 hapo juu ni la, zitaje njia faafu za kuboresha tovuti ya swahilihub?

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

8. Je, unakumbana na changamoto zipi katika kuitumia tovuti ya swahilihub kuiendeleza taaluma ya Kiswahili?

.........................................................................................................................................

.........................................................................................................................

9. Je, unadhani matumizi ya tovuti ya swahilihub kuiendeleza taaluma ya Kiswahili yameenea kwa kiasi gani?

a) Yameenea sana { }

b) Yameenea { }

c) Hayajaenea { }

d) Sina uhakika { }

Eleza sababu za jibu lako katika swali la 9 hapo juu?

.....................................................................................................................................10

. Ni nini mustakabali wa swahilihub katika kuiendeleza taaluma ya kiswahili?

.....................................................................................................................................

## C. Kiambatisho III: Hojaji kwa wanafunzi wa Taaluma ya Kiswahili

**SEHEMU YA A: Maswali ya kimsingi.**

### 5.3.1.3 Maagizo

Tafadhali jaza nafasi katika hojaji uliyopewa. Haina haja uandike jina. Maelezo utakayotoa yatatumiwa tu kwa kusudi la uchunguzi huu na yatahifadhiwa sana wakati na baada ya utafiti.

1. (i)Je, Ulijua vipi kuwa kuna tovuti ya swahilihub ambayo inaeendeleza taaluma ya Kiswahili? a) Kutokana na ushawishi wa wahadhiri wangu wa kiswahili { }

b) Kupitia kwa vyomba vya habari { }

c) Kutokana na kushiriki kwenye makongamano ya kiswahili { }

b) Kutokana na ushawishi wa wanafunzi wenzangu wa kiswahili { }

2. Umetumia swahilihub kwa miaka mingapi?

a) 1 { }

b) (2-5) { }

c) (Zaidi ya 5) { }

3. Umekuwa ukitumia swahilihub kuendeleza taaluma ya Kiswahili kwa muda upi?

a) (1) { }

b) (2-5) { }

c) (Zaidi ya 5) { }

### 5.3.1.4 SEHEMU YA B: Nafasi ya vitengo vya swahilihub Katika kuendeleza taaluma ya kiswahili.

4. Ifuatayo ni orodha ya vitengo mbalimbali vya swahilihub vinavyotumika kuendeleza taaluma ya Kiswahili. Weka alama (/) ama (X) kuonyesha iwapo umevitumia au haujavitumia mtandaoni.

| **Kitengo cha swahilihub** | **Naitumia sana** | **Naitumia** | **Siitumii** | **Sijui** |
|---|---|---|---|---|
| Mwanzo | | | | |
| Habari | | | | |
| Blogu na ukumbi | | | | |
| Jifunze Kiswahili | | | | |
| Video | | | | |
| Maktaba Jisomee | | | | |
| Picha | | | | |

5. Je, unatumia swahilihub kwa njia yo yote ambayo haijatajwa hapo juu?

a) Ndiyo { }

b) La { }

Kama jibu lako katika swali la 5 hapo juu ni ndiyo, tafadhali zitaje njia hizo.

…………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………….

6. Je, walimu wako wanatumia swahilihub kuendeleza taaluma ya Kiswahili?

a. Ndiyo { }

b. La { }

7. Je, tovuti ya swahilihub inatosheleza mahitaji ya kuendeleza taaluma ya Kiswahili?

a. Ndiyo { }

b. La { }

Kama jibu lako katika swali la 7 hapo juu ni la, zitaje njia faafu za kuboresha tovuti ya swahilihub?

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

8. Je, unadhani matumizi ya tovuti ya swahilihub kuiendeleza taaluma ya Kiswahili yameenea kwa kiasi gani?

a) Yameenea sana { }

b)Yameenea { }

c) Hayajaenea { } d) Sina uhakika { }

Eleza sababu za jibu lako katika swali la 8 hapo juu?

...........................................................................................................................

9. Je, unakumbana na changamoto zipi katika kuitumia tovuti ya swahilihub kuiendeleza taaluma ya Kiswahili?

...........................................................................................................................10

. Ni nini mustakabali wa swahilihub katika kuiendeleza taaluma ya kiswahili?

...........................................................................................................................

**D. Kiambatisho IV: Hojaji kwa watumiaji wengine Swahilihub**

**SEHEMU YA A: Maswali ya kimsingi.**

**5.3.1.5 Maagizo**

Tafadhali jaza nafasi katika hojaji uliyopewa. Haina haja uandike jina. Maelezo utakayotoa yatatumiwa tu kwa kusudi la uchunguzi huu na yatahifadhiwa sana wakati na baada ya utafiti.

1. (i)Je, Ulijua vipi kuwa kuna tovuti ya swahilihub ambayo inaeendeleza taaluma ya Kiswahili?

a) Kutokana na ushawishi wa wahadhiri wangu wa kiswahili { }

b) Kupitia kwa vyomba vya habari { }

c) Kutokana na kushiriki kwenye makongamano ya kiswahili { }

b) Kutokana na ushawishi wa wanafunzi wenzangu wa kiswahili { }

2. Umetumia swahilihub kwa miaka mingapi?

a) 1 { }

b) (2-5) { }

c) (Zaidi ya 5) { }

3. Umekuwa ukitumia swahilihub kuendeleza taaluma ya Kiswahili kwa muda upi?

e) (1) { }

f) (2-5) { }

g) (Zaidi ya 5) { }

### 5.3.1.6 SEHEMU YA B: Nafasi ya vitengo vya swahilihub Katika kuendeleza taaluma ya kiswahili.

4. Ifuatayo ni orodha ya vitengo mbalimbali vya swahilihub vinavyotumika kuendeleza taaluma ya Kiswahili. Weka alama (/) ama (X) kuonyesha iwapo umevitumia au haujavitumia mtandaoni.

| **Kitengo cha swahilihub** | **Naitumia sana** | **Naitumia** | **Siitumii** | **Sijui** |
|---|---|---|---|---|
| Mwanzo | | | | |
| Habari | | | | |
| Blogu na ukumbi | | | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Jifunze Kiswahili | | | | |
| Video | | | | |
| Maktaba Jisomee | | | | |
| Picha | | | | |

5. Je, unatumia swahilihub kwa njia yo yote ambayo haijatajwa hapo juu?

c) Ndiyo { }

d) La { }

Kama jibu lako katika swali la 5 hapo juu ni ndiyo, tafadhali zitaje njia hizo.

…………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………

6. Je, tovuti ya swahilihub inatosheleza mahitaji ya kuendeleza taaluma ya Kiswahili?

a) Ndiyo { }

b) La { }

Kama jibu lako katika swali la 7 hapo juu ni la, zitaje njia faafu za kuboresha tovuti ya swahilihub?

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

8. Je, unadhani matumizi ya tovuti ya swahilihub kuiendeleza taaluma ya Kiswahili yameenea kwa kiasi gani?

e) Yameenea sana { }

f) Yameenea { }

g) Hayajaenea { }

h) Sina uhakika { }

Eleza sababu za jibu lako katika swali la 8 hapo juu?

..............................................................................................................................

..................................................................................................................

9. Je, unakumbana na changamoto zipi katika kuitumia tovuti ya swahilihub kuiendeleza taaluma ya Kiswahili?

..............................................................................................................................

..................................................................................................................

10. Ni nini mustakabali wa swahilihub katika kuiendeleza taaluma ya kiswahili?

..............................................................................................................................

..................................................................................................................

**E. Kiambatisho V: Dodoso kwa mahojiano kwa Meneja wa Swahilihub**

1. Je, mradi wa swahilihub ulianza lini na kwa nini?
2. Je, tovuti ya swahilihub hutumia mbinu zipi kuiendeleza taaluma ya kiswahili?
3. Kuna tovuti zingine za kiswahili, kwa nini ulichagua swahilihub iwe tovuti ya kiswahili?

4.Je, ni akina nani watumizi wa swahilihub?

5. Je, ni kwa kiwango kipi tovuti ya swahilihub imeenea?
6. Je, ni nini malengo ya tovuti ya swahilihub?
7. Je, swahilihub na mradi wa Helsinki zinahusiananje katika kuendeleza taaluma ya kiswahili?
8. Je, ni kongoo zipi zinazopatikana katika Helsinki na zinahusianaje na zile za swahilihub?

9. Je, unahisi kwamba swahilihub inachangia kuiendeleza taaluma ya Kiswahili? Kwa nini?
10. Je, tovuti ya swahilihub inatosheleza mahitaji ya kuendeleza taaluma ya Kiswahili?
11. Je, unakumbana na changamoto zipi katika kuimarisha mradi wa swahilihub?
12. Unakabiliana vipi na chamgamoto hizi?
13. Ni nini mustakabali wa swahilihub katika kuiendeleza taaluma ya kiswahili?

## F. Kiambatisho VI: Dodoso kwa mahojiano kwa Wahudumu wa Nation Media

1. Je, umewahi kutumia swahilihub kuiendeleza taaluma ya Kiswahili?
2. Je, tovuti ya swahilihub hutumia mbinu zipi kuiendeleza taaluma ya kiswahili?
3. Kuna tovuti zingine za kiswahili na kwa maoni yako zinahusianaje na swahilihub katika kuiendeleza taaluma ya kiswahili?

4.Je, mnadhibiti vipi matumizi ya swahilihub kuiendeleza taaluma ya kiswahili?

5. Je, kwa maoni yako swahilihub imeenea kwa kiwango kipi?
6. Je, ni nini malengo ya tovuti ya swahilihub?
7. Je, tovuti ya swahilihub inatosheleza mahitaji ya kuendeleza taaluma ya Kiswahili? 8. Je, kitengo cha ubora wa Kiswahili kimekumbana na changamoto zipi katika kuimarisha mradi wa swahilihub?

10. Unakabiliana vipi na chamgamoto hizi?
11. Ni nini mustakabali wa swahilihub katika kuiendeleza taaluma ya kiswahili?

## G. Kiambatisho VII: Kielelezo cha Uchunzaji

**Kikaomtandaoni..............................Muda**

**iliyotumiwa..................................................**

**Tarehe............................................ Wakati.....................................................................**

**Mada husika...........................................................................................**

| Matumizi | Kutokea baada ya kila dakika tano | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kitengo cha swahilihub** | 5 | 10 | 15 | 20 | 25 | 30 | 35 | 40 |
| Mwanzo | | | | | | | | |
| Habari | | | | | | | | |
| Blogu na ukumbi | | | | | | | | |
| Jifunze Kiswahili | | | | | | | | |
| Video | | | | | | | | |
| Maktaba Jisomee | | | | | | | | |
| Picha | | | | | | | | |

## H. Kiambatisho VIII: Idhini ya Utafiti

REPUBLIC OF KENYA


**NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION**

National Commision for Science, Technology and Innovation -

Ref No: **970534**

Date of Issue: **20/July/2020**

**RESEARCH LICENSE**



**This is to Certify that Mr.. ANTHONEY OLOO OWINO of Masinde Muliro University of Science and Technology, has been licensed to conduct research in Nairobi on the topic: TATHMINI YA MRADI WA SWAHILIHUB KATIKA UKUZAJI WA LUGHA YA KISWAHILI NCHINI KENYA for the period ending : 20/July/2021.**

License No: **NACOSTI/P/20/5847**

**970534**

Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

## I. Kiambatisho IX: Plagiarism Statement

**PLAGIARISM STATEMENT**

STUDENT DECLARATION

1. I hereby declare that I know that the incorporation of material from other works or a paraphrase of such material without acknowledgement will be treated as plagiarism according to the Rules and Regulations of Masinde Muliro University of Science and Technology.
2. I understand that this thesis must be my own work.
3. I know that plagiarism is academic dishonesty and wrong, and that if I commit any act of plagiarism, my thesis can be assigned a fail grade (“F”)
4. I further understand I may be suspended or expelled from the university for academic dishonesty

Name…Owino Anthoney Oloo ………Signature………………………………..

Reg. No………………………………….Date…………………………………….


**SUPERVISOR(S) DECLARARTION**

I/We hereby approve the examination of this thesis. The thesis has been subjected to plagiarism test and its similarity index is not above 20%.

1. Name………………………………….Signature…………………Date,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,

2. Name………………………………….Signature……………...…..Date,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,

## J. Kiambatisho X: Plagiarism Level




## K. Kiambatisho XI: Machapisho

i. Owino, A., na Simala, I., (2018). Tathmini ya Tovuti ya Swahilihub katika kuendeleza Kiswahili Kitaaluma kwenye jadida la CHAKAMA Chama cha Kiswahili cha Afrika Mashariki., 978997650587-0.

ii. Owino, A.,na Simala, I.,(2018). Changamoto za Kiteknohama katika Ufundishaji wa Riwaya ya Kiswahili katika shule za upili nchini Kenya kwenye jadida la CHAKAMA Chama cha Kiswahili cha Afrika Mashariki., 978997650587-7.

## L. Kiambatisho XII: Makongamano na Semina

i. Owino, A., na Simala, I., (2018). Tathmini ya Tovuti ya Swahilihub katika Kuendeleza Kiswahili Kitaaluma kwenye jarida la CHAKAMA Chama cha Kiswahili cha Afrika Mashariki., 978997650587-0.

ii. Owino, A.,na Simala, I.,(2018). Changamoto za Kiteknohama katika Ufundishaji wa Riwaya ya Kiswahili katika Shule za upili nchini Kenya kwenye jarida la CHAKAMAK Chama cha Kiswahili cha Afrika Mashariki., 978997650587-7.